Maarifa ya Uislamu

**Darsa la Watu Wazima**

**Juzuu 5**

# JAMII YA KIISLAMU



**Islamic Propagation Centre**

Jamii ya Kiislamu

Historia ya kushushwa Qur'an 96:1-5, inatukumbusha na kutufunza kuwa Mtume (s.a.w)alianza kushushiwa wahyi kwa kupewa amri ya kusoma. Hivyo, hapana shaka kabisa kuwa Elimu ndiyo Faradhi ya kwanza inayopaswa kutekelezwa na kila Muislamu tangu zama za Mtume (s.a.w) hadi sasa.

Kusoma au kutafuta Elimu kumefanywa kuwa Faradhi ya kwanza ili kumuwezesha mja kumju Mola wake na kumpatia ujuzi wa kutosha juu ya kanuni na sheria za Allah (s.w), ambazo zikifuatwa katika kila kipengele cha maisha ya kila siku, hupatikana uadilifu na amani ya kweli katika jamii.

Hii ni juzuu ya Tano ya Maarifa ya Uislamu katika mfululizo wa juzuu 7 za masomo kwa Darasa la Watu wazima unao kusudia kumuwezesha mja na jamii kufikia kilele hicho.

Mfululizo huu wa masomo katika juzuu 7 ni:
1. Lengo la Maisha ya Mwanadamu
2. Nguzo za Uislamu
3. Qur'an na Sunnah
4. Familia ya Kiislamu
5. Jamii ya Kiislamu
6. Historia ya Kuhuisha Uislamu
7. Kuhuisha Uislamu katika jamii

## Maarifa ya Uislamu

## Darsa la Watu Wazima

## Juzuu 5

# JAMII YA KIISLAMU

Islamic Propagation Centre

Toleo ya Kwanza 2004

Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.

© Hakimiliki 2005, 2004 na IPC

Maarifa ya Uislamu
Darasa la Watu Wazima
Juzuu ya Tano

Wachapaji/Wasambazaji
Islamic Propagation Centre (IPC)
S.L.P 55105, Dar es Salaam, Tanzania.
Chapisho la kwanza, 21, April, 2004
Nakala 1000
Chapisho la kwanza, 27, April, 2005
Nakala 1000

Kimetayarishwa na Islamic Propagation Centre
P.O.BOX 55105, simu 022-2450403

Usanifu wa kurasa na Jalada: Islamic Propagation Centre.

**Neno la Awali**

Shukurani zote njema zinamstahiki Allah(s.w) aliye Bwana na Mlezi wa walimwengu wote. Rehema na Amani ziwaendee Mitume wake wote pamoja na wale wanaofuata mwenendo wao katika kuhuisha Uislamu katika jamii.

Tunamshukuru Alla(s.w) kwa kutuwafikisha kutoa juzuu ya Tano ya Maarifa ya Uislamu kwa Darasa la Watu Wazima. Masomo haya ya Uislamu kwa watu wazima yamejikita katika Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad(s.a.w).

Juzuu hii ya Tano, imekusudiwa kuwawezesha wasomaji kuyafahamu vyema Maadili ya Kiislamu na tafauti yake kimsingi,ikilinganishwa na yale ya jamii za kitwaghuuti. Misingi hii ya Maadili imedhihirishwa kwa ufafanuzi wa kiutekelezaji, katika Utamaduni, sheria na hukumu, uchumi na kuchuma; na hatimaye katika Siasa na uendeshaji wa Dola.

Hivyo basi, baada ya wasomaji kuipitia juzuu hii kwa makini, inatarajiwa watakuwa mstari wa mbele kwenye harakati za kuhuisha Uislamu katika jamii, wakitumia neema ya mali, nguvu, vipawa na muda aliowajaalia Allah(s.w), kama walivyofanya Mitume na watu wema waliotangulia.

رَبَّنَآ ءَاتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾

*Mola wetu! Tupe rehema zinazotoka kwako*
*na tutengenezee uongofu*
*katika kila jambo letu*
*(18:10)*

## Yaliyomo

**Sura ya Kwanza**......................................................1
**Misingi ya Maadili**................................................1
Binadamu si mnyama..............................................1
Mtizamo wa Kikafiri juu ya Uadilifu...........................5
Mtizamo wa Uislamu juu ya Uadilifu..........................11
Zoezi la Kwanza.....................................................20

**Sura ya Pili**.........................................................21
**Utamaduni**...........................................................21
Utamaduni wa Muislamu........................................21
Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu...............25
Tabia njema.............................................25
Vazi la Kiislamu.......................................28
Miiko katika kula na kunywa.................37
Michezo na Burdani...............................54
Misiba na Maombolezo...........................65
Maombi na Dua.......................................69
Kumkumbuka Allah (s.w) Saa 24.............75
Zoezi la Pili..........................................................80

**Sura ya Tatu**.......................................................81
**Sheria**.................................................................81
Maana ya Sheria...................................................81
Kazi za sheria katika jamii....................................81
Chimbuko la sheria za Kitwaghuti............................83
Chimbuko la Sheria ya Kiislamu.......................89
Mahakama ya Kiislamu..................................98
Haki za Mshitakiwa ............................104
Mgawanyo wa Makosa.........................110
Haki za wasiokuwa Waislamu..............................118
Zoezi la Tatu.......................................................121

**Sura ya Nne**........................................................122
**Uchumi**........................................................122
Maana ya Uchumi..................................................122
Nadharia ya uchumi wa Kiislamu...........................123
Dhana ya mafanikio..................................124
Dhana ya umilikaji mali..........................125
Dhana ya bidhaa.......................................126
Dhana ya Matumizi...................................126
Milki ya Rasilimali....................................127
Umuhimu wa uchumi katika Uislamu...................134
Mazingatio muhimu katika uchumi wa Kiislamu......138
Sera ya uchumi katika Uislamu............................139
Haki ya Serikali kuzuia Dhulma...............140
Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu..........142
Biashara ................................................143
Haki ya kumiliki mali.............................157
Mipaka ya Umilikaji mali.........................159
Mgawanyo wa mali katika Uislamu.........................160

Zakat.................................................160
Sadakat..............................................161
Kodi (Jizya)..........................................166
Mikopo...............................................167
Mfumo wa benki (za riba) za kitwaghuti...................175
Madhara ya riba katika jamii....................177
Uharamu wa Riba katika Uislamu............179
Benki za Kiislamu............................................187
Mudharabah.......................................188
Musharikah........................................188
Ijara-Uara wa Iktina...............................189
Murabah...........................................189
Muqaradha........................................189
Uzuri wa benki za Kiislamu.....................190
Zoezi la Nne......................................................191

**Sura ya Tano**......................................................193
**Siasa**......................................................193
Maana ya Siasa......................................................193
Mifumo ya siasa za kitwaghutii..................................193
Ujima......................................................194
Utumwa......................................................194
Ukabaila......................................................195
Ubepari......................................................195
Ujamaa......................................................195
Udemokrasia......................................................196
Mfumo wa siasa ya Kiislamu......................................197
Dhana ya Dola......................................................198
Dola za Kitwaghutii......................................................199
Muundo na Uendeshaji wake..................199
Dosari za Dola za Kitwaghutii..................204
Dola ya Kiislamu......................................................204
Dhana ya Utawala..................................205
Vyombo vya Dola..................................206
Uraia katika Dola ya Kiislamu..................211
Msonge wa Uongozi..................................213
Masharti ya kuwatii viongozi (Ulul-amri)...219
Siza za anayestahiki kuwa kiongozi..........223
Wajibu wa kiongozi..................................230
Usimamishaji Haki katika dola ya Kiislamu..........243
Haki ya Kuishi......................................245
Haki ya Usalama wa Maisha....................246
Haki ya Heshima......................................247
Haki ya Uhuru......................................248
Haki ya Kuhukumiwa kwa Uadilifu............250
Haki ya Usawa wa Binaadamu..................251
Haki ya uhuru wa mahusiano..................252
Haki za raia......................................252
Haki za wasiokuwa Waislamu..................259
Zoezi la Tano......................................................269

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

# Utangulizi

Lengo la kuumbwa watu na kuwezeshwa kuishi hapa duniani ni kumuabudu Allah (sw). Qur'an, kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, kinabainisha kuwa Allah (sw) anasema:

وَمَا خَلَقْتُ ٱلْجِنَّ وَٱلْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥٦﴾

*Sikuwaumba majini na wanaadamu ila waniabudu (51:56)*

Ibada kwa msimamo wa Qur'an haiishii tu kwenye kusali, kufunga, kutoa zakat na sadaqat, kuhiji, kumsalia Mtume (saw), kumsifu na kumtukuza Allah (sw). Kila jambo analofanya mtu katika binafsi yake, kifamilia au kijamii, ni ibada. Na ndiyo maana Allah(sw) anaamuru kuwa:

قُلْ إِنَّ صَلَاتِى وَنُسُكِى وَمَحْيَاىَ وَمَمَاتِى لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَـٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾ لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

*Sema: hakika sala zangu, na shughuli zangu, na uhai wangu na umauti wangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Hana mshirika (6:162-163)*

Aidha, kuna aina mbili tu za ibada kwa mujibu wa Qur'an. Ibada wafanyayo watu kumuabudia Allah (sw) na ibada ambayo watu hufanya kumuabudu Shetani. Ushahidi uthibitishao kuwepo kwa ibada ya watu kumuabudu shetani ni ile kauli ya Allah (sw) alipowaonya wanadamu mbele, kuwa siku ya kiyama atawalaumu akisema:

أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَـٰبَنِىٓ ءَادَمَ أَن لَّا تَعْبُدُوا۟ ٱلشَّيْطَـٰنَ ۖ
إِنَّهُۥ لَكُمْ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴿٦٠﴾ وَأَنِ ٱعْبُدُونِى ۚ هَـٰذَا
صِرَٰطٌ مُّسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

*Je, sikukuagizeni, enyi wanadamu kuwa msimuabudu shetani? Hakika yeye kwenu ni adui aliye dhahiri . Na kwamba niabuduni mimi. Hii ndiyo njia iliyonyooka. (36:60-61)*

Hivyo, watu na watahadhari amali zao zisiwe za kumuabudu shetani kwa dhamira na matendo. Maana amali za mja, akiwa binafsi au kundi, huingia kwenye moja ya aina hizo za ibada. Qur'an inasema kuna madaftari mawili ya amali za waja:

كَلَّآ إِنَّ كِتَـٰبَ ٱلْفُجَّارِ لَفِى سِجِّينٍ ﴿٧﴾

*Kwa hakika maandishi (ya amali) za watu waovu yamo katika Sijjin.*

كِتَـٰبٌ مَّرْقُومٌ ﴿٩﴾

*(hilo)Ni daftari lililoandikwa (ndani yake amali za watu wabaya). (83:7,9)*

كَلَّآ إِنَّ كِتَـٰبَ ٱلۡأَبۡرَارِ لَفِى عِلِّيِّينَ ﴿١٨﴾

*Hakika maandishi ya watu wema yamo katika Iiyyin.*

كِتَـٰبٌ مَّرۡقُومٌ ﴿٢٠﴾

*(Hilo) ni daftari ambalo zinaandikwa humo (amali za watu wema). (83:18,20)*

Kutokana na ukweli huu, unapatikana ulazima kwa Waislamu kuishi katika jamii yenye kujenga mazingira mazuri ya kutomkwaza muumini kutenda mema na kumsaidia aweze kumuabudu Allah (sw) katika kila amali aitendayo. Jukumu hili la kujenga jamii bora, inayoongozwa kwa kanuni na sheria zenye adili (flaw-less), haki na uadilifu usio na doa la upogo, limewekwa mabegani mwa waumini, Waislamu! Anasema Allah (sw):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱدۡخُلُواْ فِى ٱلسِّلۡمِ كَآفَّةً وَلَا
تَتَّبِعُواْ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَـٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوٌّ مُّبِينٌ

*Enyi mlioamini! Ingieni katika hukumu zote za Uislamu, wala msifuate nyayo za shetani, kwa hakika yeye ni adui dhahiri (2:208)*

Kwahiyo, pamoja na kutekeleza zile nguzo za Uislamu kwa ukamilifu wake, yapasa zitujenge na tujengeke kuwa wakweli katika amali na kauli thaabiti katika kuusimamia na kuufuata mfumo wa maisha wa Kiislamu kijamii. Tusifuate nyayo za shetani, isipokuwa sheria za Allah (sw) katika kuhukumu na kuhukumiana. Tuchume kiislamu na kuuvaa utamaduni wake, tujenge maadili ya Kiislamu na kuifuata siasa yake safi, iliyotwahara.

Juzuu hii, kwahiyo, inakusudia kudhihirisha mawanda na msimamo wa Uislamu katika maisha ya kijamii katika sura zifuatazo:

1 Misingi ya maadili katika Uislamu
2 Utamaduni katika Uislamu
3 Sheria katika Uislamu
4 Uchumi katika Uislamu
5 Siasa na Uendeshaji wa Dola

## Sura ya Kwanza

## MISINGI YA MAADILI

**Binadamu si mnyama**

Mtu ni kiumbe tofauti na viumbe wengine, hata wale waliokaribiana kimaumbile katika kundi la mamalia (mammals).Pamoja na makafiri kudai kuwa asili ya mtu ni jamii ya masokwe kwa kuwa wanakaribia kufanana kimaumbile, wametafautiana mno.Tofauti hii inatokana na vipawa maalum alivyotunukiwa mtu ukilinganisha na vipawa vya wanyama. Vipawa hivi humfanya mwanadamu aunde au kufuata maadili fulani, jambo ambalo wanyama hawana.Vipawa hivi ni:

1.**Akili** yenye kumuwezesha kutafakari juu ya mambo mbali mbali.
2.**Kujitambua** (Self consciousness) kunakomuwezesha mtu kujua mahusiano yake na mazingira yake.
3.**Elimu** yenye kumuwezesha kuendesha maisha yake hapa ulimwenguni kwa wepesi na kwa ufanisi.
4.**Uhuru** wa kuchagua na kutenda alitakalo ndani ya kanuni za maumbile:

Vipawa hivi humfanya mtu mwenye akili timamu ajiulize maswali mengi ya msingi kama vile, nini chanzo cha ulimwengu na vyote vilivyomo, nini kusudio la kuwepo watu na maumbile yote yaliyowazunguka, ni ipi hatima ya ulimwengu na vyote vilivyomo, n.k. Mwenendo wa tabia ya mtu itategemeana na majibu atakayoyapata kutokana na maswali hayo ya msingi. Akipata majibu sahihi ataweza kuishi maisha mazuri yenye kulingana na lengo la kuumbwa kwake.Kwa hakika majibu sahihi atayapata

kutoka kwa yule aliyeMuumba yeye pamoja na maumbile yote yaliyomzunguka. Anapaswa kumtambua Muumba wake kwa kutumia vipawa hivi vya ziada alivyotunukiwa kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفِ
ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ لَءَايَٰتٍ لِّأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٠﴾

*Hakika katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonyesha kuwapo Mwenyezi Mungu mmoja), kwa wenye akili. (3:190)*

ٱلَّذِينَ يَذْكُرُونَ ٱللَّهَ قِيَٰمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ
وَيَتَفَكَّرُونَ فِى خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ رَبَّنَا مَا
خَلَقْتَ هَٰذَا بَٰطِلًا سُبْحَٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿١٩١﴾

*Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima na wakikaa na wakilala. Na hufikiri umbo la mbingu na ardhi (kisha) wakasema "Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya Moto." (3:191)*

Kwa mujibu wa aya hizi, kinachofuatia baada ya mtu kumtambua Muumba, ni kufuata mwongozo wake katika kila kipengele cha maisha.

Endapo binaadamu atatumia vipawa vyake vya akili, utambuzi wa ubinafsi, elimu na uhuria kwa kufuata msukumo wa matashi yake atapotea njia na kuishi maisha yasiyo na muelekeo na atakuwa na mwenendo na tabia

iliyochupa utu inayompelekea kufanya mambo maovu na duni kuliko yale yanayofanywa na wanyama. Juu ya hili Muumba wetu karimu anatutanabahisha:

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ ٱلْجِنِّ وَٱلْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا يَسْمَعُونَ بِهَآ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ كَٱلْأَنْعَـٰمِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْغَـٰفِلُونَ ﴿١٧٩﴾

*"Na bila shaka tumewaumbia Moto wa Jahannamu wengi katika majini na watu (kwa sababu hii): Nyoyo (akili) wanazo, lakini hawafahamu kwazo, na macho wanayo lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotofu zaidi. Hao ndio walioghafilika."(7:179)*

Inadhihirika bayana kuwa pamoja na maendeleo makubwa ya sayansi na tekinolojia, amani katika maisha ya hivi leo chini ya mfumo wa kitwaghutii (mfumo unaochupa mipaka ya utu aliyoiweka Muumba), imetoweka kabisa, na dhuluma imeshamiri. Kutoa na kupokea rushwa ndio mtindo wa maisha; ujambazi na uporaji umeongezeka kitaifa na kimataifa; familia zinavunjika na ufuska kustawi; vijana wengi wametumbukia katika unywaji pombe, uvutaji bangi, utumiaji wa madawa ya kulevya na kupoteza kabisa dira ya maisha yao; ukweli na uaminifu vimekuwa vitu adimu, ambapo fitina na propaganda za uwongo uliokithiri vimeshamiri katika vyombo vya habari kitaifa na kimataifa.

Ukatili wanaofanyiana binaadamu hivi leo ni wa kutisha kiasi ambacho mwanafalsafa mmoja wa Kiingereza aitwaye *Bertrand Russell* alifikia kusema kuwa si haki kabisa kumnasibisha binaadamu na mnyama kwa sababu mnyama anatabia nzuri sana kuliko binaadamu! Mara nyingi mnyama akiua, huua kwa haja ya chakula cha wakati huo huo na si kuzusha vita isiyo na maana yoyote na kuua mamilioni ya watu wasio na hatia.

Mauwaji ya halaiki yaliyofanywa na Majeshi ya Marekani na Washirika wake dhidi ya wananchi na raia wa Afghanistan na Iraq, pamoja na unyama wa Serikali ya Israil dhidi ya Wapalestina, ni ushahidi wa alichokisema *Russell* .

Akijadili juu ya maadili ya binaadamu yalivyo katika ulimwengu huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia, mwanafalsafa mwingine Harold H.Titus ameandika:

*"Mlolongo wa matukio katika miaka ya hivi karibuni umedhihirisha wazi kuwa kuna jambo lililokwenda kombo katika maisha ya binaadamu. Binaadamu amejipatia uwezo mkubwa mpya katika nyanja za sayansi na tekinolojia, lakini mara nyingi uwezo huo umetumika katika njia za uharibifu. Binaadamu amepanua upeo na ubora wa ujuzi wake, lakini amepiga hatua ndogo sana, kama basi amepiga hatua yoyote, katika kujileta furaha na amani".*

Aidha, mwanasaikologia aitwaye F.S.C. Northrop, naye anaishangaa hali hii ya maadili na kuandika:

*"Ulimwengu wetu ni wa kitendawili. Mafanikio ambayo ndio fahari yake yanatishia kuuangamiza... yaelekea kila tunapopiga hatua ya maendeleo ndivyo tunavyoshindwa kudumisha ustaarabu".*

Wanafalsafa hawa wangelikuwa Ulul-albaab (wenye akili) na kumtambua Muumba wao, wasingeliishangaa hali hii kwani imedhihirishwa na Muumba Karimu tangu karne ya sita (A.D.), pale Mtume Muhammad (s.a.w) aliposhushiwa wahyi wa Qur-an:

لَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ فِىٓ أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٤﴾ ثُمَّ
رَدَدْنَٰهُ أَسْفَلَ سَٰفِلِينَ ﴿٥﴾ إِلَّا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟
وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ فَلَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ ﴿٦﴾

*Bila shaka TumeMuumba mwanaadamu kwa umbo lililobora kabisa. Halafu tukamrudisha kuwa chini kuliko walio chini.Ila wale wenye kuamini na kutenda mema, watakuwa na ujira usiokwisha, (unaendelea maisha) (95:4-6)*

Aya hizi zinatukumbusha kuwa pamoja na binaadamu kuumbwa katika umbo bora na kutunukiwa vipaji alivyo navyo hawezi kuwa na mwenendo na tabia njema mpaka awe amemtambua na kumuamini Mola wake Muumba na kufuata mwongozo wake pekee katika kuendesha maisha yake ya kila siku ya kibinafsi na kijamii huku akitarajia kupata radhi zake na malipo kutoka kwake katika maisha ya hapa duniani na ya kesho akhera.

**Mtizamo wa Kikafiri juu ya Maadili**

Maadili ni mwenendo mwema unaombakisha binaadamu katika hadhi yake na kumfikisha katika lengo la kuumbwa kwake. Katika jitihada za kumfanya binaadamu awe na tabia ya kufanya mema na kuacha maovu ili kuleta furaha na amani katika jamii, baadhi ya wanafalsafa wa kikafiri wanauliza na kujaribu kutoa majibu ya maswali makuu manne yafuatayo:

1. Ni kitu gani ambacho ndicho lengo kuu la maisha?
2. Zipi chem chem, tunazozitegemea katika ujuzi wetu juu ya mema na maovu? Yaani tutajuaje kuwa jambo fulani ni baya au zuri? Tunapata kutoka wapi habari hizi za mema na maovu?
3. Ni nani msimamizi wa mwenendo wa tabia ya binaadamu? Yaani ni mamlaka ipi yenye kuhakikisha kuwa watu wanakuwa waadilifu?
4. Ni kitu gani kinachowasukuma watu wafuate mwenendo fulani wa tabia? Wanahamasishwa na nini?

Hebu tupitie majibu wanayotoa wanafalsafa na udhaifu wa majibu hayo:

**1. Lengo kuu la maisha kwa mtazamo wa makafiri**

Katika kujibu swali la kwanza "Ni lipi lengo kuu la maisha yetu", wanafalsafa wa kikafiri wamegawanyika katika makundi mengi miongoni mwa hayo ni haya matatu.

Kundi la kwanza linasema lengo kuu la maisha yetu hapa duniani ni kuishi maisha yenye furaha. Hivyo basi jambo lolote linalotuongezea furaha yetu ni jema na lolote lile linalotuletea machungu, huzuni, na majonzi ni ovu.

Kundi la pili linasema lengo kuu la maisha yetu hapa duniani ni kufikia utimilifu (perfection). Hivyo kitendo chochote kinachopelekea katika kukuza na kukamilisha vipawa vyetu ni kitendo chema na jambo lolote linalokwaza na kuviza vipawa vyetu visifikie kilele cha ukamilifu wake ni jambo ovu.

Kundi la tatu linasema lengo kuu la maisha haya ni kuwa kila mtu atimize wajibu wake kwa madhumuni ya kutimiza wajibu tu basi (duty for the sake of duty). Hivyo jambo lolote linalomfanya mtu atimize wajibu wake bila

ya kutarajia chochote ni jema na kila linalomzuia kutimiza wajibu wake kwa madhumuni tu ya kutimiza wajibu basi ni ovu.

**Udhaifu wa majibu hayo**

Tukichunguza majibu ya wanafalsafa wa kikafiri juu ya lengo la maisha, tunaona kuwa yanapwaya sana.

Tukianza na jibu la kwanza linalosema kuwa furaha ndio lengo kuu la maisha yetu hapa duniani, maswali kadhaa yanazuka. Ni furaha ya aina gani hiyo inayotafutwa? Ni furaha anayoihisi mtu baada ya kutosheleza matamanio yake ya kimwili au ni furaha inayotokana na kujifaharisha? Ni furaha itokanayo na kutathmini kazi za sanaa au furaha ya kiroho? Ni furaha ya nani inayotafutwa, ya mtu binafsi au ya jamii ambamo anaishi? Au furaha ya watu wote au ni furaha ya kikundi cha watu tu?

Tukichukua jibu la pili lisemalo kuwa lengo kuu ni kufikia utimilifu, pia yanajitokeza maswali kadhaa. Nini maana ya utimilifu? Ni kipi kipimo cha utimilifu? Ni utimilifu wa nani unaotafutwa wa tabaka au kikundi alicho mtu au wa mtu binafsi au wa jamii?

Vivyo hivyo tukichukua jibu la tatu lisemalo lengo kuu ni kutimiza wajibu kwa lengo tu la kutimiza wajibu, hatuwezi kuepuka maswali haya:. Lengo hili maana yake ni nini hasa? Nani aliyeliweka? Nini hekima ya kulifuata?

**2.Utambuzi wa Mema na Maovu kwa Mtizamo wa Makafiri**

Katika kujibu swali la pili, “zipi chem chem. (sources of knowledge) tunazozitegemea katika ujuzi wetu juu ya mema na maovu, wanafalsafa wamegawanyika makundi matatu vile vile.

Kundi la kwanza, linasema uzoefu wa binaadamu (human experience) ndio chem chem pekee ya hakika inayomuwezesha mtu kujua lipi jema na lipi ovu. Rai hii hujulikana kama "*empiricism*" katika lugha ya Kiingereza. Kwa mujibu wa rai hii tunajua kuwa jambo fulani ni baya kwa sababu katika maisha yetu ya kila siku uzoefu wetu umetuonyesha kuwa jambo hilo lina madhara fulani kwetu.

Kundi la pili, linasema kinachotujulisha kuwa jambo fulani ni zuri au baya ni silka zetu (*intuition*). Na rai hii hujulikana kama "*Intuitionism*" kwa lugha ya Kiingereza.

Kundi la tatu, linasema kuwa kinachotuwezesha kupambanua zuri na baya ni kipawa cha kufikiri na kuhoji au "*Rationalism*" kama rai hii inavyojulikana kwa Kiingereza.

**Udhaifu wa Makafiri juu ya Chem chem ya Ujuzi wa Wema na Uovu**

Iwapo tutazifanya rai hizo za makafiri kuwa ndio chem chem ya ujuzi wa mema na maovu, tutajikuta katika hali ya kutatanisha sana. Jema la asubuhi laweza kuwa ovu la jioni na kinyume chake.

Kasoro za rai kuwa, "chem chem ya ujuzi juu ya wema na ovu ni uzoefu" ni hizi zifuatazo:

Kwanza, inabidi watu wasubiri mpaka kiyama ndio wang'amue kuwa jambo fulani lilikuwa baya au zuri ili upatikane uzoefu wa watu wote na halafu uzoefu huo uchambuliwe na kutafsiriwa kwa ufasaha bila upendeleo wowote. Hii ina maana kuwa watu itabidi wasubiri mpaka siku ya kiyama kabla ya kujua kuwa jambo fulani ni baya au zuri. Na zaidi hakuna mtu anayeweza kuutafsiri uzoefu wa watu wote kwa usahihi bila ya upendeleo.

Pili, uzoefu wowote alionao binaadamu leo umegawanyika katika fani chungu nzima za Elimu na mabingwa wa kila fani wanautafsiri uzoefu wao kulingana na mwangaza wa taaluma zao. Tuchukue uzoefu wa nani katika kuamua lipi ni jema na lipi ovu? Na kama kila mtu afuate uzoefu wake basi hapatakuwa na jambo lolote ambalo tunaweza kusema ni jema au baya, kwa mfano, wizi ni jambo baya, mwizi atasema hapana, uzoefu wangu unanionesha kuwa nikiiba nakula na kustarehe bila ya kuhangaika huku na huko!

Halikadhalika kutegemea hoja, akili na silka kuna matatizo kama hayo.Hapana shaka yoyote kuwa kipaji cha akili ni hazina kubwa yenye manufaa mengi na kiongozi kikubwa katika maisha yetu na husaidia kuturekebisha katika namna mbali mbali. Lakini katika suala hili haitufikishi popote. Kwanza lina zuka swali lile lile: Je, tuitegemee akili ya nani? Akili yangu au yako au ya huyu au ya yule? Au tutegemee akili ya kikundi Fulani cha watu au ya watu wote au ya watu wa kizazi hiki au kilichopita au cha baadaye?

Tatu, swali zito zaidi ni kama akili ya binaadamu peke yake haiwezi kufanya kazi hiyo, kwa sababu lipo suala la upendeleo na chuki ambalo huipotosha akili. Athari za hisia, harara za maono, dhana za awali na sababu za kimakuzi au za kimazingira juu ya akili haziwezi kupuuzwa. Kutokana na udhaifu huu si busara kuifanya akili na silka kuwa chem chem za ujuzi juu ya mema na maovu.

### 3.Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Makafiri

Katika kujibu swali la tatu, “*Ni nani msimamizi wa tabia ya binaadamu?*”, wanafalsafa wa kikafiri wametofautiana pia.

Kundi la kwanza linasema kuwa maadili ya jamii yatasimamiwa na lengo tarajiwa. Yaani kama lengo kuu ni “furaha” basi ni kule kupatikana kwa furaha ndiko kutakako simamia maadili ya jamii.

Kundi la pili, linasema msimamizi ni kitu wanachokiita “law of practical reason”, yaani “kanuni zinazooana na hoja”. Rai hii inafanana na ile ya “Rationalism” ya kutumia akili.

Kundi la tatu, linasema msimamizi ni serikali kwa kutumia askari polisi, mahakama na magereza.

Kundi la nne, linasema msimamizi ni maoni ya watu katika jamii hiyo hiyo yaani “Social pressure”.

**4.Motisha wa Kufuata Maadili kwa Mtizamo wa Makafiri**

Katika kujibu swali la nne, “Ni kitu gani kinachowasukuma wawe na maadili wafuate maadili ya jamii, baadhi ya wanafalsafa wanasema ni katika maumbile ya binaadamu kutii na kuheshimu sheria. Lakini tunaona siku hizi watu wanavyoshindana kuvunja sheria!

Kundi la pili la wanafalsafa linadai kuwa kinachomsukuma mtu kufuata maadili ya jamii ni kutaka malipo na kuepukana na adhabu (Reward and Punishment). Swali linakuja: “Ni nani anayetoa malipo au adhabu hiyo?” Wengine wanasema ni dola au serikali na wengine wanasema ni jamii anamoishi mtu.

Itadhihirika wazi kuwa majibu yanayotolewa na wanafalsafa wanaojaribu kusimamisha maadili ya jamii kwa misingi ya kikafiri yanapwaya na hutatanisha sana. Hata hivyo haina maana kuwa yote yaliyosemwa na wanafalsafa hawa ni upuuzi usiokuwa na ukweli wowote. Zipo chembe chembe za ukweli hapa na pale lakini bila

kudhibitiwa na mfumo sahihi hoja zao zinaelea tu angani. Dosari kubwa kupita zote katika jitihada zao ni kule kumtaka binaadamu awe muadilifu bila kwanza kumuamini Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho.

**Mtizamo wa Uislamu juu ya Uadilifu**

Kosa kubwa walilolifanya wanafalsafa wa kikafiri katika jitihada za kuchunguza mwenendo wa tabia ya binaadamu ni kule kuanzia utafiti wao katikati badala ya kuanzia mwanzo. Kabla ya kuingia kwenye yale maswali manne, walitakiwa waulize na kuyatafutia majibu sahihi maswali mawili ya kwanza ya msingi yafuatayo:

1. Nini chanzo cha binaadamu? Yaani binaadamu ametokea wapi au "Nani aliyemfanya akawepo?
2. Ni ipi hadhi na nafasi ya binaadamu katika ulimwengu huu?

Katika kujibu swali la kwanza tunajifunza katika Qur-an kuwa binaadamu ni kiumbe wa Mwenyezi Mungu aliyetukuzwa:

وَلَقَدْ خَلَقْنَٰكُمْ ثُمَّ صَوَّرْنَٰكُمْ ثُمَّ قُلْنَا لِلْمَلَٰٓئِكَةِ ٱسْجُدُوا۟ لِءَادَمَ فَسَجَدُوٓا۟ إِلَّآ إِبْلِيسَ لَمْ يَكُن مِّنَ ٱلسَّٰجِدِينَ ﴿١١﴾

*"Na hakika tulikuumbeni, kisha tukakutieni sura, kisha tukawaambia malaika: "Msujudieni Adamu" Basi wakasujudu isipokuwa Ibilis hakuwa miongoni mwa waliosujudu." (7:11)*

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى خَٰلِقٌۢ بَشَرًا مِّن صَلْصَٰلٍ مِّنْ حَمَإٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٨﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُۥ وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِى فَقَعُوا۟ لَهُۥ سَٰجِدِينَ ﴿٢٩﴾ فَسَجَدَ ٱلْمَلَٰٓئِكَةُ كُلُّهُمْ أَجْمَعُونَ ﴿٣٠﴾

*"Na (kumbuka) Mola wako alipowaambia Malaika, hakika Mimi nitaMuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti; wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda.Basi nitakapomkamilisha na kumpulizia roho inayotokana na Mimi basi mumuangukie kwa sijida (kuonyesha utii wenu)" Basi Malaika wakamsujudia wote pamoja." (15:28-30)*

Kuhusu hadhi na nafasi ya binaadamu hapa ulimwenguni tunajifunza katika Qur-an kuwa yeye ni Khalifa au balozi (mwakilishi) wa Mwenyezi Mungu hapa ulimwenguni anayepaswa kuuongoza kwa uadilifu kwa kufuata mwongozo wa yule aliyemteua kuwa balozi hapa. Kuhusu nafasi hii ya mwanaadamu Qur-an inatukumbusha:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَٰٓئِكَةِ إِنِّى جَاعِلٌ فِى ٱلْأَرْضِ خَلِيفَةً ۖ

*"(Wakumbushe) wakati Mola wako alipowaambia Malaika: 'Mimi nitaleta Khalifa katika ardhi…" (2:30)*

Ili kumuwezesha binaadamu kuchukua nafasi yake hapa ardhini, Allah (s.w) amemtunuku elimu ya mazingira yake pamoja na mwongozo utokao kwake kupitia kwa

Mitume wake na vitabu vyake kama tulivyojifunza katika aya zifuatazo:

وَعَلَّمَ ءَادَمَ ٱلۡأَسۡمَآءَ كُلَّهَا

*"Na (Mwenyezi Mungu) akamfundisha Adamu majina ya vitu vyote..." (2:31)*

قُلۡنَا ٱهۡبِطُواْ مِنۡهَا جَمِيعٗاۖ فَإِمَّا يَأۡتِيَنَّكُم مِّنِّي هُدٗى

فَمَن تَبِعَ هُدَايَ فَلَا خَوۡفٌ عَلَيۡهِمۡ وَلَا هُمۡ يَحۡزَنُونَ

*"Tukasema "Shukeni humo nyote, na kama ukikufikieni uongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.(2:38)*

وَٱلَّذِينَ كَفَرُواْ وَكَذَّبُواْ بِـَٔايَٰتِنَآ أُوْلَٰٓئِكَ

أَصۡحَٰبُ ٱلنَّارِۖ هُمۡ فِيهَا خَٰلِدُونَ ٣٩

*Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakao kuwa watu wa motoni, humo watakaa milele." (2:39)*

Pamoja na kutunukiwa elimu na kupewa mwongozo wa maisha, binaadamu pia ametiishiwa viumbe vyote, ikiwa ni pamoja na Malaika. Qur-an inazidi kutukumbusha:

هُوَ ٱلَّذِي خَلَقَ لَكُم مَّا فِي ٱلۡأَرۡضِ

*"Yeye (Allah) ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi, ...." (2:29)*

Binaadamu kwa kupewa nafasi ya Ukhalifa na kutunukiwa elimu na vipawa vyote alivyonavyo, maisha yake hapa ulimwenguni yamekuwa mtihani.

تَبَٰرَكَ ٱلَّذِى بِيَدِهِ ٱلْمُلْكُ وَهُوَ عَلَىٰ كُلِّ شَىْءٍ
قَدِيرٌ ﴿١﴾ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلْمَوْتَ وَٱلْحَيَوٰةَ لِيَبْلُوَ
كُمْ أَيُّكُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلْغَفُورُ ﴿٢﴾

*Ametukuka yule ambaye Mkononi mwake umo ufalme (wote); Naye ni mwenye uweza juu ya kila kitu. Ambaye ameumba mauti na uhai ili kukujaribuni (kukufanyieni mtihani); ni nani miongoni mwenu mwenye amali nzuri. Naye ni Mwenye nguvu na Mwenye Msamaha. (67:1-2)*

إِنَّا خَلَقْنَا ٱلْإِنسَٰنَ مِن نُّطْفَةٍ أَمْشَاجٍ نَّبْتَلِيهِ
فَجَعَلْنَٰهُ سَمِيعًۢا بَصِيرًا ﴿٢﴾ إِنَّا هَدَيْنَٰهُ ٱلسَّبِيلَ
إِمَّا شَاكِرًا وَإِمَّا كَفُورًا ﴿٣﴾

*Kwa hakika tumemuumba mtu kutokana na mbegu ya uhai iliyochanganyika: (ya mwanamke na mwanaume), ili tumfanyie mtihani (kwa amri na makatazo); kwa hivyo tukamfanya ni Mwenye kusikia Mwenye kuona. (76:2-3)*

Binaadamu atafaulu mtihani huu kama ataishi hapa ulimwenguni kama mja na khalifa wa Allah (s.w) kwa kufuata na kusimamisha sheria ya Allah (s.w) ambayo itapelekea kusimamisha uadilifu katika jamii.

Mtu, atafeli mtihani huu kama ataishi hapa ulimwenguni kwa kufuata na kusimamisha sheria zilizotungwa na watu zinazopelekea ulimwengu kuwa uwanja wa fujo na vurugu.

Matokeo ya mtihani huu hayatatangazwa katika maisha yetu ya hapa duniani bali yatatolewa baada ya watu wote kumaliza makazi yao hapa duniani na baada ya mema na maovu yao kujidhihirisha kikamilifu. Ni katika wakati huo ambapo Allah (s.w) atamhesabu kila mtu na kuamua ni yupi alitimiza wajibu wake kama Khalifa wake hapa ulimwenguni na yupi ambaye hakutimiza. Hisabu hiyo haitahusu jambo moja maalumu au kipengele fulani tu bali itahusu maisha yote ya binaadamu ya kibinafsi na kijamii. Itahusu pia vipawa vyake vyote vya mwili na akili na amana yoyote aliyopewa juu ya watu au vitu.

Kwa mtizamo wa Uislamu, Ufalme ni wa Allah (s.w) peke yake na binaadamu ni khalifa wake tu, hivyo njia pekee ya uadilifu inayompasa binaadamu ni kutekeleza wajibu aliopewa na Allah (s.w). Hana uhuru wa kuamua apendavyo upi uwe mwenendo wake wa tabia, bali kipimo cha lipi jema na lipi ovu lazima kichukuliwe kutoka kwa Allah (s.w), wajibu wa binaadamu ni kutekeleza kwa ukamilifu na uaminifu wajibu aliokabidhiwa na Muumba wake.

Maadili ya jamii hayatabuniwa na binaadamu bali utachukuliwa kutoka kwa Allah (s.w) ambaye ndiye Muumba na mpangaji wa sheria. Binaadamu hanabudi kuishi na kutenda kulingana na maamrisho na sheria ya Allah (s.w). Uhusiano huu uliopo kati ya Allah (s.w) na binaadamu utakapo eleweka, yale maswali manne ya wanafalsafa wa kikafiri, kuhusiana na Maadili ya jamii, yatapata majibu yaliyowazi na yanayotua akilini.

**Majibu ya maswali manne yanavyotolewa na Uislamu**

Pindi mtu akiikubali nafasi ya **uja** na **ukhalifa** aliyopewa binaadamu na Muumba wake, maswali makuu manne ya wanafalsafa wa kikafiri, juu ya mwenendo wa tabia ya binaadamu, yanajibiwa na Uislamu kwa wepesi kama ifuatavyo:

**1.Lengo Kuu la Maisha kwa Mtizamo wa Uislamu**

Kufuzu mtihani wa Allah (s.w) na kupata radhi zake ndiyo lengo kuu la maisha ya binaadamu hapa duniani. Atafuzu mtihani wa Mola wake, endapo binaadamu atajitahidi kutii sheria za Allah (s.w) katika kila kipengele cha maisha yake binafsi na kujitahidi kusimamisha sheria hizo katika jamii. Yaani binaadamu atafuzu kwa kufanya biashara na Allah (s.w) kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ هَلۡ أَدُلُّكُمۡ عَلَىٰ تِجَٰرَةٖ
تُنجِيكُم مِّنۡ عَذَابٍ أَلِيمٖ ١٠ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ
وَرَسُولِهِۦ وَتُجَٰهِدُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ بِأَمۡوَٰلِكُمۡ
وَأَنفُسِكُمۡۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ١١

*Enyi mlioamini! Je! Nikujulisheni biashara itakayokuokoeni na adhabu iumizayo?(Biashara yenyewe ni hii):Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu, haya ni bora kwenu; ikiwa mnajua. (61:10-11)*

يَغۡفِرۡ لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡ وَيُدۡخِلۡكُمۡ جَنَّٰتٖ تَجۡرِى مِن
تَحۡتِهَا ٱلۡأَنۡهَٰرُ وَمَسَٰكِنَ طَيِّبَةٗ فِى جَنَّٰتِ عَدۡنٖۚ ذَٰلِكَ
ٱلۡفَوۡزُ ٱلۡعَظِيمُ ١٢

*(Mkifanya haya) atakusameheni dhambi zenu na atakuingizeni katika mabustani yapitayo mito mbele yake na (atakupeni) maskani mazuri mazuri katika Bustani za milele; Huku ndiko kufuzu kukubwa" (61:12)*

إِنَّ ٱللَّهَ ٱشْتَرَىٰ مِنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ أَنفُسَهُمْ وَأَمْوَٰلَهُم
بِأَنَّ لَهُمُ ٱلْجَنَّةَ ۚ يُقَٰتِلُونَ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ فَيَقْتُلُونَ
وَيُقْتَلُونَ ۖ وَعْدًا عَلَيْهِ حَقًّا فِى ٱلتَّوْرَىٰةِ وَٱلْإِنجِيلِ
وَٱلْقُرْءَانِ ۚ وَمَنْ أَوْفَىٰ بِعَهْدِهِۦ مِنَ ٱللَّهِ ۚ فَٱسْتَبْشِرُوا۟
بِبَيْعِكُمُ ٱلَّذِى بَايَعْتُم بِهِۦ ۚ وَذَٰلِكَ هُوَ ٱلْفَوْزُ
ٱلْعَظِيمُ ﴿١١١﴾

*"Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waislamu nafsi zao na mali zao ili naye awape Pepo. Wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu; wanaua na wanauawa. Hii ndiyo ahadi aliyojilazimisha (Mwenyezi Mungu) katika Taurati, Injili na Qur-an. Na ni nani atekelezaye zaidi ahadi yake kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyofanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa." (9:111)*

## 2.Chem chem ya Ujuzi wa Wema na Uovu kwa Mtizamo wa Uislamu

Chem chem za kweli anazoweza kuzitegemea binaadamu katika kutambua mema na maovu ni Allah (s.w) kupitia kwa Mitume na vitabu vyake.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنَاتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ
الْكِتَابَ وَالْمِيزَانَ لِيَقُومَ النَّاسُ بِالْقِسْطِ ۖ

*"Kwa hakika tumewapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu......" (57:25)*

**3.Msimamizi wa Maadili kwa Mtizamo wa Uislamu**

Msimamizi wa mwenendo wa tabia njema inayompeleka binaadamu kwenye kusimamisha uadilifu ni Imani thabiti juu ya Allah (s.w) na Siku ya mwisho (siku ya malipo) na juu ya vipengele vingine vya nguzo sita za imani ya Kiislamu. Muumini wa kweli hana hiari ya kwenda kinyume na maamrisho na makatazo ya Allah (s.w) na Mitume wake.

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلَا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللَّهُ وَرَسُولُهُ
أَمْرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ ۗ وَمَن يَعْصِ
اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَقَدْ ضَلَّ ضَلَالًا مُّبِينًا ﴿٣٦﴾

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao." (33:36)*

**4.Motisha inayowapelekea Waislamu kusimamisha Uadilifu katika jamii**

Kinachowachochea Waislamu kuwa na tabia ya kufanya mema na kuacha maovu, na kisha kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii ni matarajio ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kukhofia ghadhabu zake. Matokeo ya kupata radhi za Allah (s.w) na kuepuka ghadhabu zake

ni kuepukana na maisha ya huzuni na hofu hapa duniani na kupata maisha ya furaha na amani ya milele huko akhera.

Majibu haya yanayotolewa na Uislamu yanatanzua utatanishi wote uliokuwepo katika majibu yaliyotolewa na wanafalsafa wa kikafiri juu ya maadili.

## Zoezi la Kwanza

1. Taja vipawa alivyotunukiwa Mwanadamu vinavyomtafautisha na wanyama.

2. Bainisha makusudio ya Allah (sw) yanayotarajiwa kufikiwa na mwanadamu aliyetunukiwa vipawa hivi.

3. Ng'amua na kubainisha sababu kubwa mbili zilizopelekea makafiri wasiafikiane, wala kufaulu kudhihirisha lengo halisi la maisha ya mwanadamu hapa duniani.

4. Eleza kwa kutoa mifano hai, upogo na udhaifu uliopo katika dhana za makafiri juu ya maadili na uadilifu katika mawanda manne.

5. Ukiondoa suala la Qadar, taja misingi mitano iliyobainishwa ndani ya Qur'an ambayo ndiyo mihimili mikuu ya maadili mema ya Kiislamu.

6. Tumia Qur'an kujibu kwa ufasaha wa kukinaisha , maswali manne ya makafiri juu ya misingi ya Maadili na uadilifu.

7. (a) Nini maana ya Maadili?
   (b) Wakati wanyama huongozwa na silka, wanadamu wana Maadili, kwanini?

8. Kwanini mtu asiyemuamini Allah na siku ya mwisho, hawezi kufanya wema muda wote au kuacha maovu kabisa?

## Sura ya Pili

## UTAMADUNI

Uislamu ni utaratibu kamili wa maisha uliofumwa na Allah (s.w) unaoelekeza namna Muumini anavyoweza kukiendea kila kipengele cha maisha yake ya kila siku ili kumuwezesha kuishi kwa furaha na amani na kufikia lengo la maisha yake hapa ulimwenguni. Miongoni mwa vipengele muhimu vya maisha ambavyo jamii ya mwanaadamu haina budi kuviendea ni kipengele cha utamaduni au mila na desturi za jamii. Sio kila mila na desturi za jamii zinamfikisha mwanaadamu katika lengo la maisha yake hapa duniani kwa furaha na amani.

Ukichunguza tamaduni za jamii mbali mbali utagundua kuwa tamaduni hizo hazimuinui mwanaadamu na kumfikisha katika kilele cha hadhi yake, bali kinyume chake huiteremsha hadhi yake na kuifanya duni kuliko ile ya wanyama.Ni utamaduni wa Kiislamu pekee unaomuinua mwanaadamu na kumbakisha katika kilele cha hadhi yake tukufu ya Ukhalifa wa Allah (s.w), kwa vile utamaduni huu umefumwa na Mwenyewe Sub-haanahu Wata’aala, Mjuzi wa kila kitu, Mwenye hekima.

### Utamaduni wa Muislamu

Waislamu tumehimizwa katika Qur-an kuwa tusifuate utamaduni mwingine au mila nyingine isiyokuwa ile mila ya Nabii Ibrahim (a.s) kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

وَمَن يَرْغَبُ عَن مِّلَّةِ إِبْرَٰهِـۧمَ إِلَّا مَن سَفِهَ نَفْسَهُۥ ۚ وَلَقَدِ
ٱصْطَفَيْنَـٰهُ فِى ٱلدُّنْيَا ۖ وَإِنَّهُۥ فِى ٱلْـَٔاخِرَةِ لَمِنَ ٱلصَّـٰلِحِينَ

*Na nani atakayejitenga na mila ya Ibrahim isipokuwa anayeitia nafsi yake katika upumbavu. Na kwa yakini sisi tulimchagua (Ibrahimu) katika dunia, na kwa hakika yeye katika akhera atakuwa miongoni mwa watu wema kabisa. (2:130)*

وَمَنْ أَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ أَسْلَمَ وَجْهَهُۥ لِلَّهِ وَهُوَ مُحْسِنٌ
وَٱتَّبَعَ مِلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ حَنِيفًا ۗ وَٱتَّخَذَ ٱللَّهُ إِبْرَٰهِيمَ
خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾

*Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule ambaye ameuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahim (kuwa Muislamu kweli kweli).Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahim kuwa kipenzi chake. (4:125)*

Mila ya Ibrahim (a.s) iliyosisitizwa katika aya hizi si nyingine zaidi ya ile ya kumpwekesha Allah (s.w) na kujitupa kwake kwa utii na unyenyekevu.Yaani mila ya Ibrahimu (a.s) ni kuufuata Uislamu kwa ukamilifu kwa kutii kwa unyenyekevu maamrisho yote ya Allah (s.w) na kujitenga kwa utii na unyenyekevu na yale yote aliyoyakataza (s.w). Mwenendo huu wa Nabii Ibrahiim ambao tunasisitizwa tuufanye utamaduni wetu uko bayana katika Qur-an:

إِذْ قَالَ لَهُۥ رَبُّهُۥٓ أَسْلِمْ ۖ قَالَ أَسْلَمْتُ لِرَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٣١﴾

*(Kumbukeni) Mola wake (Ibrahim) alipomwambia Silimu (jisalimishe kwa unyenyekevu), akanena: "Nimejisalimisha kwa Mola wa Ulimwengu wote".(2:131)*

وَوَصَّىٰ بِهَآ إِبْرَٰهِـۧمُ بَنِيهِ وَيَعْقُوبُ يَٰبَنِىَّ إِنَّ ٱللَّهَ
ٱصْطَفَىٰ لَكُمُ ٱلدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسْلِمُونَ

*Na Ibrahim akawausia haya wanawe na Yaaqubu (pia akawausia wanawe): Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni dini hii, basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu (wanyenyekevu kwa Allah (s.w). (2:132).*

Tunajifunza katika aya hizi kuwa hatua ya kwanza ya kufuwata mila ya Ibrahim ni sisi wenyewe kujisalimisha kikweli kweli kwa Allah (s.w) kwa kufuata maamrisho yake yote na kuacha makatazo yake yote. Hatua ya pili ya kufuata mila ya Ibrahimu ni ile ya kuwahimiza ahali zetu kuwa Waislamu wa kweli wenye kufuata mwenendo wa maisha anaoridhia Allah (s.w) katika kuendea kila kipengele cha maisha yao ya kila siku.

Pia aya zifuatazo zinatubainishia kwa uwazi mwenendo wa Nabii Ibrahimu (a.s) ambao tunahimizwa tuuige na tuufanye ndio mila yetu:

إِنَّ إِبْرَٰهِيمَ كَانَ أُمَّةً قَانِتًا لِّلَّهِ حَنِيفًا وَلَمْ يَكُ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٢٠﴾

*Hakika Ibrahimu alikuwa kiongozi (mfano mzuri wa kuigwa) mnyenyekevu kwa Mwenyezi Mungu mtii kamili, wala hakuwa miongoni mwa washirikina.(Alikuwa) mwenye kushukuru neema zake (Allah).(Mwenyezi Mungu) akamchagua na kumuongoza katika njia iliyonyooka.(16:120)*

وَءَاتَيْنَٰهُ فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً ۖ وَإِنَّهُۥ فِى ٱلْءَاخِرَةِ لَمِنَ ٱلصَّٰلِحِينَ ﴿١٢٢﴾

*Na tukampa wema katika dunia; na hakika yeye katika akhera atakuwa miongoni mwa watu wema (pia). (16:122).*

Nabii Ibrahim (a.s) alikataa kata kata mila ya jamii yake na akawahakikishia kwa maneno na matendo kuwa yeye ni Muislamu na si miongoni mwa washirikina:

إِنِّي وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ
وَٱلْأَرْضَ حَنِيفًا ۖ وَمَآ أَنَا۠ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿٧٩﴾

*Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi. Hali ya kuwa nimeacha dini ya upotofu. Mimi (ni Muislamu) si miongoni mwa washirikina. (6:79).*

Vile vile Muislamu wa kweli anayefuata vilivyo mila ya Ibrahimu (a.s) hana budi kuuhakikishia ulimwengu kwa maneno na matendo kuwa yeye ni Muislamu katika hali zote na si miongoni mwa washirikina.Msimamo wa Muislamu wa kweli ni huu ufuatao:

قُلْ إِنَّنِي هَدَىٰنِي رَبِّيٓ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ
دِينًا قِيَمًا مِّلَّةَ إِبْرَٰهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ ٱلْمُشْرِ
كِينَ ﴿١٦١﴾

*Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka, katika dini iliyo sawa kabisa ambayo ndiyo mila ya Ibrahim aliyekuwa muongofu, wala (kabisa) hakuwa miongoni mwa washirikina."(6:161)*

قُلْ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ
ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾

*Sema: "Hakika swala yangu na Ibada zangu (nyingine zote) na maisha yangu na kufa kwangu (vyote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.Bwana (Rabii) wa walimwengu wote.(6:162)*

لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

*Hana mshirika wake. Na haya ndiyo niliyoamrishwa na mimi ni wakwanza wa waliojisalimisha". (6:163).*

Tumejifunza kutokana na aya hizi kuwa mila ya Muislamu ni Uislamu. Yaani Muislamu wa kweli hana mila nyingine isiyo kuwa ile ya kufuata vilivyo mwenendo wa kujisalimisha kwa Allah (s.w) kwa kila kipengele cha maisha.

**Vipengele vya Utamaduni wa Kiislamu**

Tumejifunza kuwa utamaduni wa Kiislamu ni mwendo wa maisha unaofuata bara bara misingi ya Uislamu kwa kuchunga vilivyo mipaka ya Allah (s.w) katika kukiendea kila kipengele cha maisha. Hivyo kila kipengele cha maisha ya jamii ya Kiislamu ni kipengele cha utamaduni wa Kiislamu.

**1.Tabia njema**

Muislamu wa kweli ni yule anayejitahidi kwa kadri ya uwezo wake kujipamba na tabia njema. Tabia njema ndio mwenendo wa Mitume wa Allah (s.w) ambao tumeamrishwa tuigize mwenendo wao hatua kwa hatua. Msisitizo wa kufuata mwenendo wa Nabii Ibrahim (a.s) tumeshauona na pia tusisahau msisitizo wa kuigiza mwenendo wa Mtume (s.a.w) unaobainishwa na aya ifuatayo:-

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ

يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلْيَوْمَ ٱلْءَاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*Bila shaka mnao mfano mwema (kiigizo chema) kwa Mtume wa Allah, kwa mwenye kumuogopa Allah (s.w) na siku ya mwisho na mwenye kumkumbuka Allah (s.w) kwa wingi. (33:21).*

Mtume (s.a.w) ambaye tunatakiwa tumuigize alikuwa ni mwenye tabia nzuri kweli kweli kama Mola wake anavyomsifu katika Qur-an:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*Na bila shaka unatabia njema kabisa (68:4).*

Mtume mwenyewe katika kuwasisitiza Waislamu kujivisha vazi zuri la tabia njema amesema:

*Aliye mbora kuliko wote miongoni mwenu ni yule aliye wazidi kwa tabia njema. (Bukhari na Muslimu).*

Pia Mtume (s.a.w) amebainisha ubaya wa mtu kuwa na tabia mbaya aliposema:

*Yule ambaye tabia yake ni mbaya na katili (harsh) hataingia Peponi. (Abu Daudi).*

Vipengele vya tabia njema ambavyo kila Muislamu anahimizwa ajivishe na kujipamba kwavyo vimebainishwa kwa uwazi katika Qur-an na Hadith (Rejea Juzuu ya 2 na 3) na kwa muhtasari Muislamu wa kweli anatakiwa afanye kila jambo kwa ajili ya Allah (s.w) na awe mwenye kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati awe mwema na mwenye kuwahurumia wanaadamu wenziwe na viumbe wengine, awe mwepesi wa kutoa msaada wa hali na mali, awe mwenye kumuheshimu kila mtu, awe mwenye kuongea maneno mazuri na kwa upole awe ni mwenye

kujizuia na hasira na kuwavumilia wengine, awe mwenye subira na mwepesi wa kusamehe wengine kwa ajili ya Allah (s.w), awe mwenye kutoa haki za wengine na awe jasiri na mwenye msimamo katika kutetea haki za wengine na katika kusimamisha haki katika jamii, awe tayari kutoa nafsi yake na mali yake kwa ajili ya kusimamisha Uislamu katika jamii, awe mwenye kukinai, awe mkarimu, awe mwenye kujitahidi kujipamba na tabia njema nyinginezo ambazo huzaa mahaba, furaha na amani katika jamii na awe mwenye kujiepusha na maneno na matendo yote maovu ambayo huzaa bugh-dha, chuki, uadui na vurugu katika jamii ya mwanaadamu.

Wazazi wa Kiislamu na wahusika na taasisi zote za Kiislamu zinazohusika na malezi ya watoto, wanayodhima kubwa ya kuwalea vijana wa katika maadili haya mema. Ni vyema tukumbushane Waislamu wote kuwa suala la kuwalea vijana wetu katika maadili ya Kiislamu ni suala la msingi na la muhimu kuliko shughuli nyingine yoyote ile tutakayowafanyia vijana hawa. Amesema kweli Mtume wa Allah aliposisitiza:

> *Hapana zawadi yoyote atakayoitoa baba kumpa kijana wake itakayozidi kumfunza tabia njema. (Tirmidh).*

Waislamu, tutakapoacha kuchukua dhima hii ya kuwalea vijana wetu katika mila ya Ibrahim na badala yake tukawaachia walelewe katika mila za kitwaaghuti tutakuwa tumewapoteza vijana wetu na tutakosa wa kuwarithisha katika uongozi wa kusimamisha Uislamu katika jamii. Tunawajibika kuwarithisha watoto wetu utamaduni wa Kiislamu kama alivyofanya Nabii Ibrahim(a.s)

وَوَصَّىٰ بِهَآ إِبۡرَٰهِـۧمُ بَنِيهِ وَيَعۡقُوبُ يَٰبَنِيَّ إِنَّ ٱللَّهَ
ٱصۡطَفَىٰ لَكُمُ ٱلدِّينَ فَلَا تَمُوتُنَّ إِلَّا وَأَنتُم مُّسۡلِمُونَ

*Na Ibrahimu akawausia haya wanawe na Yaaqubu (mjukuu wake na kuwaambia) Enyi wanangu! Hakika Mwenyezi Mungu amekuchagulieni dini hii; basi msife ila nanyi mmekuwa Waislamu". (2:132)*

Waislamu kamwe tusitarajie kuwa Uislamu utasisimama katika jamii yetu bila ya kuwalea vijana wetu katika maadili ya Kiislamu pamoja na kuomba msaada wa Allah(s.w) atuwezeshe kufanya kazi hii kama alivyotufundisha kuomba katika Qur-an:

رَبَّنَا هَبْ لَنَا مِنْ أَزْوَٰجِنَا وَذُرِّيَّـٰتِنَا قُرَّةَ أَعْيُنٍ وَٱجْعَلْنَا

لِلْمُتَّقِينَ إِمَامًا ﴿٧٤﴾

*Mola wetu! Tupe katika wake zetu na watoto wetu yatuburudishayo macho (yetu – nyoyo zetu) na utujaalie tuwe viongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu. (25:74).*

**2. Vazi la Kiislamu**

Vazi la Kiislamu ni sehemu ya utamaduni wa Kiislamu. Vazi la Kiislamu ni lile vazi linalositiri uchi kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Lengo la vazi kwa jamii ya mwanaadamu linabainishwa katika Qur-an:

يَـٰبَنِىٓ ءَادَمَ قَدْ أَنزَلْنَا عَلَيْكُمْ لِبَاسًا يُوَٰرِى سَوْءَٰتِكُمْ

وَرِيشًا ۖ وَلِبَاسُ ٱلتَّقْوَىٰ ذَٰلِكَ خَيْرٌ ۚ ذَٰلِكَ مِنْ ءَايَـٰتِ ٱللَّهِ

لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿٢٦﴾

*Enyi wanaadamu! Hakika tumekuteremshieni nguo zifichazo tupu zenu na nguo za pambo na nguo za ucha-Mungu ndizo bora. Hiyo ni katika ishara za Mwenyezi Mungu ili mpate kukumbuka. (7:26)*

Kama inavyobainishwa katika aya hii lengo kuu la vazi la Kiislamu ni kusitiri awrah (uchi). Vazi la Kiislamu ni lile linalotekeleza masharti yafuatayo:

**(a) Vazi lisitiri Awrah (uchi)**

**Awrah ya mwanamke** ni mwili mzima isipokuwa uso na viganja vya mikono kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w) aliposema:

> *Mwanamke atakapofikia baleghe hataacha wazi sehemu yoyote ya mwili wake isipokuwa uso na viganja (Abu Daud).*

Amri ya kujisitiri kwa wanawake inabainishwa katika aya zifuatazo:

وَقُل لِّلْمُؤْمِنَٰتِ يَغْضُضْنَ مِنْ أَبْصَٰرِهِنَّ
وَيَحْفَظْنَ فُرُوجَهُنَّ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ
إِلَّا مَا ظَهَرَ مِنْهَا ۖ وَلْيَضْرِبْنَ بِخُمُرِهِنَّ عَلَىٰ
جُيُوبِهِنَّ ۖ وَلَا يُبْدِينَ زِينَتَهُنَّ إِلَّا لِبُعُولَتِهِنَّ أَوْ
ءَابَآئِهِنَّ أَوْ ءَابَآءِ بُعُولَتِهِنَّ أَوْ أَبْنَآئِهِنَّ أَوْ أَبْنَآءِ
بُعُولَتِهِنَّ أَوْ إِخْوَٰنِهِنَّ أَوْ بَنِىٓ إِخْوَٰنِهِنَّ أَوْ بَنِىٓ
أَخَوَٰتِهِنَّ أَوْ نِسَآئِهِنَّ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَٰنُهُنَّ أَوِ
ٱلتَّٰبِعِينَ غَيْرِ أُوْلِى ٱلْإِرْبَةِ مِنَ ٱلرِّجَالِ أَوِ ٱلطِّفْلِ

ٱلَّذِينَ لَمْ يَظْهَرُوا۟ عَلَىٰ عَوْرَٰتِ ٱلنِّسَآءِ ۖ وَلَا يَضْرِبْنَ
بِأَرْجُلِهِنَّ لِيُعْلَمَ مَا يُخْفِينَ مِن زِينَتِهِنَّ ۚ وَتُوبُوٓا۟
إِلَى ٱللَّهِ جَمِيعًا أَيُّهَ ٱلْمُؤْمِنُونَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٣١﴾

*Na waambie Waislamu wanawake wainamishe macho yao, na wazilinde tupu zao, wala wasidhihirishe viungo vyao isipokuwa vinavyodhihirika (uso na viganja). Na waangushe shungi zao mpaka vifuani mwao na wasionyeshe mapambo yao ila kwa waume zao au baba zao, au baba za waume zao, au watoto wao, au watoto wa waume zao, au kaka zao, au wana wa kaka zao, au wana wa dada zao, au wanawake wenzi wao, au wale iliyowamiliki mikono yao ya kuume, au wafuasi wanaume wasio na matamanio au watoto ambao hawajajua mambo yaliyohusu uke. Wala wasipige miguu yao ili yajulikane wanayoyaficha katika mapambo yao. Na tubieni nyote kwa Mwenyezi Mungu, enyi Waislamu ili mpate kufaulu. (24:31).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ قُل لِّأَزْوَٰجِكَ وَبَنَاتِكَ وَنِسَآءِ ٱلْمُؤْمِنِينَ
يُدْنِينَ عَلَيْهِنَّ مِن جَلَٰبِيبِهِنَّ ۚ ذَٰلِكَ أَدْنَىٰٓ أَن يُعْرَفْنَ
فَلَا يُؤْذَيْنَ ۗ وَكَانَ ٱللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿٥٩﴾

*Ewe Mtume! Waambie wake zako na binti zako, na wanawake wa Kiislamu wajiteremshie uzuri nguo zao. Kufanya hivyo kutapelekea upesi wajulikane (kuwa ni watu wa heshima ili) wasiudhiwe. Na Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe (na) mwingi wa kurehemu. (33:59).*

Pamoja na mwanamke kuamrishwa kujifunika mwili mzima isipokuwa uso na viganja, pia katika aya hizi anaamrishwa:

- Ateremshe shungi mpaka kifuani. Shungi ni kitambaa (mtandio) kinachofunika kichwa, shingo na kifua.
- Asidhihirishe mapambo yake na
- Asitingishe miguu yake na viungo vyake vingine kiasi cha kujulisha aliyoyaficha katika mapambo.

**Awrah ya mwanaume** ni sehemu yote iliyo kati ya kitovu na magoti kwa mujibu wa kauli ya Mtume (s.a.w) aliposema:

*Sehemu yoyote iliyo juu ya magoti haina budi kufunikwa na sehemu yoyote iliyo chini ya kitovu haina budi kufunikwa. (Darqutny).*

*Mwanamume hana budi kufunika ile sehemu ya mwili wake iliyo kati ya kitovu na magoti. (Al-Mabsuut).*

Ni haram kwa Muislamu mwanamume kuvaa bukta au kaptura nje ya chumbani kwake.

**(b) Vazi lisibane**

Vazi la mwanamke au mwanamume lisibane kiasi cha kuonyesha mchoro wa sehemu za mwili zinazotakiwa zisitiriwe.

**(c) Vazi lisiwe lenye Kuonyesha (transparent)**

Mwenye kuvaa vazi linaloonyesha rangi ya mwili anahesabika kuwa yuko uchi kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Hafsa bint Abdur-Rahman, alikuja kwa Aysha (r.a) akiwa amevaa shungi inayoonyesha kichwa chake na mabega. Aysha aliichana chana na kumfunika shungi nzito. (Imam Malik)*

Mtume (s.a.w) amesema: Allah amewalaani wanawake waliovaa nguo na huku bado wako uchi.

**(d) Vazi Lisiwe Lenye Kuvutia**

Wanawake wameamrishwa kufunika mwili mzima ili kuficha uzuri wao wa asili (natural beuty) na mapambo yao ili wasiyavute matamanio ya wanaume. Ni katika msingi huu pia wanawake wa Kiislamu hawaruhusiwi kuvaa vazi linalovutia sana nje ya nyumbani kwake. Ni katika msingi huu pia wanawake wa Kiislamu hawaruhusiwi kutoka majumbani mwao ila kwa dharura kama inavyosisitizwa katika Qur-an:

Ni mwenendo wa kitwaghuti kwa wanawake kutokatoka majumbani mwao ovyo na kuonyesha ovyo mapambo yao ikiwa ni pamoja na mavazi yanayovutia.

**(e) Vazi la mwanamke lisifanane na la mwanamume na kinyume chake**

Ni haramu kwa mwanamume kuvaa mavazi ya wanawake na pia ni haramu kwa wanawake kuvaa mavazi ya wanaume. Katika Hadith iliyosimuliwa na Ibn Abbas, Mtume (s.a.w) amewalaani wanaume wanaoigiza mavazi na tabia za kike na wanawake wanaoigiza mavazi na tabia za kiume.

**(f) Vazi lisiwe kiigizo cha vazi la wasiokuwa Waislamu**

Ni haramu kwa Muislamu kuigiza mavazi ya wasiokuwa

Waislamu. Hii ni kwa sababu Waislamu wanao utamaduni wao ambao ni tofauti na wa watu wengine. Muislamu anatakiwa atambulikane, ili kwa mfano aweze kusalimiwa na Waislamu wenziwe kwa "*Assalaam Alaykum*" maamkizi ya Kiislamu waliyoyatumia mitume wote na wafuasi wao na ndiyo yatakayo kuwa maamkizi ya Peponi. Kuamkiana huko hakutawezekana kwa mfano iwapo Waislamu wanaona haya kuvaa vazi litakalowatambulisha kuwa ni Waislamu.

Matokeo yake ni kwamba utamaduni wao utapotea na wao kumezwa katika utamaduni wa kijahili. Muislam anatakiwa ajirekebishe haraka iwapo kwa mavazi yake watu wanashindwa kumtofautisha na kafiri au mtu wa utamaduni mwingine. Ni aibu ilioje kwa Muislamu kujikuta anaambiwa na mtu mwingine: "Mimi siku zote hizi sikujua kama wewe ni Muislamu". Tunafahamishwa katika Hadithi iliyosimuliwa na Ibn Umar kuwa Mtume (s.a.w) amesema:

> *Atakaye waigiza watu, atahusikana nao(atakuwa pamoja nao). (Ahmad, Abu-Daud).*

**(g) Vazi lisiwe la majivuno na kujifaharisha**

Vazi linalompelekea mtu kwenye majivuno na kujifaharisha ni vazi haram, na limekemewa vikali na Mtume (s.a.w) kama tunavyojifunza katika Hadithi zifuatazo:

> *Ibn Umar ameeleza kuwa atakaye ning'iniza suruali yake kwa kujifaharisha, Allah (s.w) hatamwangalia siku ya kiyama. (Bukhari na Muslim).*

> *Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Avaaye vaa vazi la fahari katika ulimwengu huu, Allah (s.w) atamvisha vazi la huzuni(hizya) siku ya kufufuliwa". (Tirmidh, Ahmed, Abu Daud, Ibn Majah).*

**(h) Vazi lisiwe chafu na la kudhalilisha**

Kinyume cha kujifaharisha ni kujidhalilisha. Ni haram kwa Muislamu kuvaa vazi linalo mdhalilisha. Muislamu anatakiwa ale vizuri na kuvaa vizuri ila tu asijifaharishe wala asifanye israfu. Allah (s.w) ametuamrisha kutangaza neema zake:

وَأَمَّا بِنِعْمَةِ رَبِّكَ فَحَدِّثْ ﴿١١﴾

*"Na neema za Mola wako zisimulie" (93:11).*

Ni katika kushukuru na kutangaza neema za Allah (s.w) kwa mtu kuvaa vizuri na kula vizuri na kwa kadri ya uwezo wake. Pia tunajifunza hili katika Hadith ifuatayo:

*Amr bin Shuaib amesimulia kutoka kwa baba yake, kutoka kwa babu yake kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika Allah anapenda kuona matokeo ya neema zake kwa mja wake". (Tirmidh).*

Yaani Allah (s.w) hampendi mtu ambaye ingawa amemneemesha bado anaendelea kuishi katika hali ile ile duni kama kwamba hakuneemeshwa neema yoyote. Pia Waislamu wanahimizwa wajenge tabia ya usafi na umaridadi wa miili yao na nguo zao kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَثِيَابَكَ فَطَهِّرْ ﴿٤﴾

*Na nguo zako uzitakase. (74:4).*

وَٱللَّهُ يُحِبُّ ٱلْمُطَّهِّرِينَ ﴿١٠٨﴾

*"Na Mwenyezi Mungu anawapenda wajitakasao". (9:108)*

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلتَّوَّٰبِينَ وَيُحِبُّ ٱلْمُتَطَهِّرِينَ ﴿٢٢٢﴾

*"Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaotubu na huwapenda wanojitakasa". (2:222).*

Kujitakasa katika aya hizi, hakuishii kwenye kujitakasa nafsi tu bali ni pamoja na kujitakasa mwili, nguo na matendo.

*Jabir anasimulia: Mtume (s.a.w) alipokuja kutuona alimkuta mtu mwenye nywele nyingi zisizochanwa, kisha Mtume akasema: Huyu mtu hajapata kitu cha kuchania kichwa chake! Na alimuona mtu aliyevaa nguo chafu, kisha akasema: Huyu mtu hajapata kitu (maji) cha kufulia nguo zake! (Ahmad, Nisai)*

Unadhifu ni katika utamaduni wa Kiislamu. Mtume (s.a.w) amehimiza:

*"Uislamu ni nadhifu, basi jinadhifisheni".*

Kwa ajili ya unadhifu Mtume (s.a.w) alipendelea sana vazi jeupe kama inavyobainika katika Hadith zifuatazo:

*Abu Dard'a amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: Hakika vazi bora ambalo waweza kuwa nalo katika kukutana na Mola wako kaburini au msikitini ni vazi jeupe. (Ibn Majah).*

*Samurah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Vaa vazi jeupe kwa sababu ni safi na linapendeza, na lifanyeni sanda kwa ajili ya maiti wenu. (Ahmad, Tirmidh, Nisai).*

**(i) Vazi la hariri limeharamishwa kwa wanaume**

Ni haramu kwa wanaume kuvaa nguo za hariri au mapambo ya dhahabu na fedha kwa mujibu wa Hadith zifuatazo:

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hakika anayevaa nguo za hariri katika ulimwengu huu hatakuwa na kitu katika siku ya Malipo".(Bukhari na Muslim).*

*Hudhaifa amesimulia "Mtume wa Allah ametukataza kutumia vyombo vya dhahabu na fedha na pia ametukataza vazi la hariri hata kukaa juu yake". (Bukhari na Muslim).*

Bali wanawake wameruhusiwa kuvaa nguo za hariri na kuvaa mapambo ya dhahabu na fedha ila tu wachunge mipaka iliyowekwa:

*Abu Mussa anaeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Dhahabu na hariri vimefanywa halali kwa wafuasi wangu wanawake na wamefanywa halali kwa wafuasi wangu wanaume" (Tirmidh, Nisai)*

Pia vazi jekundu (sio lenye mistari au michirizi myekundu)limeharamishwa kwa wanaume. Tunafahamishwa katika Hadith kuwa:

*Abdullah bin Amr amesimulia:"Mwanamume mmoja aliyevalia vipande viwili vya nguo nyekundu alipita na akamsalimia Mtume, lakini Mtume hakuitikia salam hiyo" (Tirmidh, Abu Daud).*

**(j) Wanaume wamekokotezwa kuvaa kofia**

Wanaume wamehimizwa sana kuvaa kitu cha kufunika kichwa iwe kofia au kilemba. Katika Hadith iliyo nukuliwa na Baihaq na Tirmidh, Mtume (s.a.w) amesema kuwa kufunika kichwa kwa kilemba ni katika mwenendo wa Malaika. Ikumbukwe kuwa kwa wanawake kufunika kichwa si jambo la kupendeza tu bali ni wajibu. Mwanamke akiacha kichwa wazi hatakama amefunika sehemu nyingine yote ya mwili atahesabika kuwa yuko uchi na akitembea hivyo mbele ya wanaume wasio maharimu wake, laana ya Allah (s.w) itakuwa juu yake.

Huu ndio utamaduni wa Kiislamu ambao kila Muislamu wa kweli analazimika kujiambatanisha nao. Utamaduni

mwingine wowote utakaompelekea Muislamu kuvaa kinyume na vazi la Kiislamu utakuwa ni utamaduni wa Kijahili au wa shetani. Allah (s.w) anatuhadharisha na Shetani katika aya ifuatayo:

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ لَا يَفۡتِنَنَّكُمُ ٱلشَّيۡطَٰنُ كَمَآ أَخۡرَجَ أَبَوَيۡكُم
مِّنَ ٱلۡجَنَّةِ يَنزِعُ عَنۡهُمَا لِبَاسَهُمَا لِيُرِيَهُمَا سَوۡءَٰتِهِمَآۚ إِنَّهُۥ
يَرَىٰكُمۡ هُوَ وَقَبِيلُهُۥ مِنۡ حَيۡثُ لَا تَرَوۡنَهُمۡۗ إِنَّا جَعَلۡنَا
ٱلشَّيَٰطِينَ أَوۡلِيَآءَ لِلَّذِينَ لَا يُؤۡمِنُونَ ﴿٢٧﴾

*Enyi wanaadamu! Shetani asikutieni katika matata, kama alivyowatoa wazee wenu katika pepo akawavua nguo zao ili kuwaonyesha tupu zao. Hakika yeye pamoja na kabila yake wanakuoneni, na hali ya kuwa nyinyi hamuwaoni. Bila shaka sisi tumejaalia mashetani kuwa marafiki wa wale wasioamini. (7:27).*

**3. Miiko katika kula na kunywa**

Hata kula na kunywa katika Uislamu kuna miiko yake. Muislamu wa kweli hatakula na kunywa tu bila kuchunga miiko na kufuate utaratibu uliowekwa. Mwongozo wa kula na kunywa uko bayana katika Qur-an. Hebu turejee aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ كُلُواْ مِمَّا فِي ٱلۡأَرۡضِ حَلَٰلٗا طَيِّبٗا وَلَا
تَتَّبِعُواْ خُطُوَٰتِ ٱلشَّيۡطَٰنِۚ إِنَّهُۥ لَكُمۡ عَدُوّٞ مُّبِينٌ ﴿١٦٨﴾

*Enyi watu! Kuleni vilivyomo katika ardhi, halali na vizuri wala msifuate nyayo za shetani, bila shaka yeye kwenu ni adui dhahiri. (2:168).*

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُلُوا۟ مِن طَيِّبَـٰتِ مَا رَزَقْنَـٰكُمْ
وَٱشْكُرُوا۟ لِلَّهِ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿١٧٢﴾

*Enyi mlioamini! Kuleni vizuri tulivyokuruzukuni, na mumshukuru Mwenyezi Mungu, ikiwa mnamuabudu yeye peke yake. (2:172).*

وَكُلُوا۟ وَٱشْرَبُوا۟ وَلَا تُسْرِفُوٓا۟ ۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلْمُسْرِفِينَ

*"… Na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu.Hakika yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao kiasi". (7:31).*

Katika aya hizi Allah (s.w) anatuagiza kuwa:

(i) Tule vilivyo halali na vilivyopatikana kwa chumo halali.
(ii) Tule vizuri tuvipendavyo kwa kadiri ya uwezo wetu.
(iii) Tusifanye ubadhirifu katika kula na kunywa.
(iv) Tumshukuru Yeye kwa vile alivyotuneemesha, kwa kufuata maamrisho yake kwa utii na kuchunga mipaka yake kwa unyenyekevu katika maisha yetu ya kila siku.

Wanaokula na kunywa bila kufuata mazingatio haya wanakuwa hawatofautiani kabisa na wanyama.Qur-an inasema:

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ ٱلْأَنْعَـٰمُ
وَٱلنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ﴿١٢﴾

*Lakini waliokufuru hujifurahisha (hapa duniani) na kula kama walavyo wanyama, na moto ndio makazi yao. (47:12)*

**Vyakula vilivyo haramishwa**

Vyakula vyote visivyo haramishwa katika Qur-an na Hadith ni halali. Vyakula vilivyoharamishwa katika Qur-an:

حُرِّمَتْ عَلَيْكُمُ ٱلْمَيْتَةُ وَٱلدَّمُ وَلَحْمُ ٱلْخِنزِيرِ وَمَآ أُهِلَّ لِغَيْرِ ٱللَّهِ بِهِۦ وَٱلْمُنْخَنِقَةُ وَٱلْمَوْقُوذَةُ وَٱلْمُتَرَدِّيَةُ وَٱلنَّطِيحَةُ وَمَآ أَكَلَ ٱلسَّبُعُ إِلَّا مَا ذَكَّيْتُمْ وَمَا ذُبِحَ عَلَى ٱلنُّصُبِ وَأَن تَسْتَقْسِمُوا۟ بِٱلْأَزْلَـٰمِ

*Mnaharamishiwa nyamafu na damu na nyama ya nguruwe na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Allah, na kilichokufa kwa kusongeka koo, na kilichokufa kwa kupigwa, na kilichokufa kwa kuanguka, na kilichokufa kwa kupigwa pembe (na wanyama wengine), na alichokila mnyama ila mkiwahi kukichinja. Na (pia mmeharamishiwa) kilichochinjwa panapo fanyiwa Ibada isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu (kama mizimu)… (5:3).*

Aya hizi za Qur-an pamoja na *(6:145)* zinatupatia mafunzo yafuatayo juu ya vyakula vilivyoharamishwa:

1. Mnyama aliye kufa bila ya kuchinjwa kwa sababu yoyote iwayo (mzoga).

2. Mnyama asiyechinjwa kwa jina la Allah – Tumeamrishwa katika Qur-an:

فَصَلِّ لِرَبِّكَ وَٱنْحَرْ ﴿٢﴾

*Basi swali kwa ajili ya Mola wako na uchinje (kwa ajili ya Mola wako). (108:2).*

Kutokana na amri hii si halali kula nyama ya mnyama aliyechinjwa na Kafiri, Mshirikina au yeyote asiye Muamini Allah (s.w) na Upweke wake. Nyama itakuwa halali iwapo mchinjaji ni Muislamu atakaye chinja kwa jina la Allah – Bismillah Allahu Akbar na atakayezingatia masharti ya kuchinja ya kumkata mnyama koo (shingo) kwa kisu kikali au kitu chochote cha kukatia kilicho kikali.

Muislamu yeyote awe mtoto, mwanamume au mwanamke katika hali yoyote anaruhusiwa kuchinja. Wala hapana suala la kupewa kisu na Sheikh.

3. Mnyama aliyechinjwa kwa ajili ya matambiko, mashindano, n.k. mnyama huyo maadam kusudio la kuchinjwa kwake ni kumshirikisha Allah (s.w) nyama yake ni haramu kuila hata kama mwenye kuchinja anajiita Muislamu na ametaja jina la Allah wakati wa kuchinja.

4. Nyama ya nguruwe.

5. Damu inayomwagika – damu inayobakia kwenye nyama si haramu.

**Vyakula vilivyoharamishwa katika Hadith**

6. Wanyama na ndege wote wanaowinda wengine kwa makucha na meno au midomo yao ni haramu kula nyama yao kwa mnasaba wa Hadith zifuatazo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema:"Kila mnyama awindae kwa meno ni haramu kuliwa" (Muslim)*

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume wa Allah aliharamisha kila mnyama awindaye kwa meno na kila ndege anayewinda wengine kwa kucha. (Muslim)*

Wanyama wanaowinda kwa meno na kucha ni kama simba, chui, paka, fisi, vicheche, mbwa mwitu, n.k.

Ndege wanao winda kwa makucha ni kama tai, mwewe, kipanga, n.k.

7. Nyama ya punda wa nyumbani, farasi na nyumbu ni haramu kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo

*Khalid bin Walid ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha nyama ya farasi, nyumbu na punda wa nyumbani. (Abu Daud, Nisai).*

Bali nyama ya punda milia ni halali kama tunavyofunzwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Watadah ameeleza kuwa alimchinja pundamilia (punda wa porini). Mtume (s.a.w) akamuuliza: Unachochote katika nyama yake?" Alijibu: Tuna miguu miwili ya nyuma. Kisha alichukua na kula. (Bukhari na Muslim).*

8. Nyama ya wanyama wachafu wenye kuathiri mwili na utu kama nguruwe, mbwa, paka, n.k.

*Ibn Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah ameharamisha nyama na maziwa ya wanyama wachafu. (Tirmidh).*

9. Ni haramu kula nyama ya mjusi na jamii yote ya mijusi:

*Abdul-Rahman bin Shibl amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) ameharamisha nyama ya mijusi. (Abu Daud).*

10.Nyama ya paka ni haramu:
*Jabir amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) ameharamisha nyama ya paka na kumpiga bei.*

11.Nyama ya kiungo cha mnyama kilichokatwa mwenyewe akiwa yungali hai kama vile mkia wa kondoo, mguu wa mnyama uliokatika kwa ajali, n.k. ni haramu kwa mnasaba wa Hadith ifuatayo:

*Abu Waqidil Laysi ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alikuja Madina akawakuta wanapenda nundu za ngamia na kukata mikia ya kondoo. Mtume (s.a.w) akasema: "Kile kilichokatwa kwa wanyama wakingali hai ni mzoga. Ni haramu kuliwa". (Tirmidh, Abu Daud).*

12. Ni haramu kula wadudu isipokuwa nzige kwa mujibu wa Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mizoga ya aina mbili na damu za aina mbili, vimefanywa halali kwetu: Mizoga ya samaki na nzige na damu ya maini na wengu. (Ahmad, Ibn Majah, Darqutni).*

Hivi ndivyo vyakula vilivyo haramishwa katika Qur-an na Hadith lakini Muislamu atakaposongwa na njaa ya kufa na kupona na pakawa hapana njia yoyote ya kupata chakula, ameruhusiwa kula haramu kiasi kidogo cha kumuwezesha kuishi na wala asile kwa kufurahia kama tunavyojifunza katika Qur-an:

فَمَنِ ٱضْطُرَّ غَيْرَ بَاغٍ وَلَا عَادٍ فَإِنَّ رَبَّكَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

*"... Lakini aliyelazimika (kula kwa ajili ya njaa, n.k.) pasipokupenda wala kwa kuvuka mipaka, basi, Mwenyezi Mungu ni mwingi wa kusamehe na mwingi wa kurehemu. (6:145)*


42

**Vinywaji vilivyoharamishwa**

Vinywaji vyote vinavyolevya (intoxicants) vimeharamishwa hata kuonja.

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِنَّمَا ٱلْخَمْرُ وَٱلْمَيْسِرُ وَٱلْأَنصَابُ
وَٱلْأَزْلَٰمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ ٱلشَّيْطَٰنِ فَٱجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ
تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa). (5:90)*

Ulevi, kamari, kumshirikisha Allah na kutazamia ni matendo yanayoivuruga jamii na kuifarikisha:

إِنَّمَا يُرِيدُ ٱلشَّيْطَٰنُ أَن يُوقِعَ بَيْنَكُمُ ٱلْعَدَٰوَةَ
وَٱلْبَغْضَآءَ فِى ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ وَيَصُدَّكُمْ عَن ذِكْرِ ٱللَّهِ
وَعَنِ ٱلصَّلَوٰةِ ۖ فَهَلْ أَنتُم مُّنتَهُونَ ﴿٩١﴾

*Hakika shetani anataka kukutieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi je, hamtaacha haya)? (5:91).*

Vinywaji vyote vinavyolevya na vilivyo najsi kama vile damu, mkojo, n.k. vimeharamishwa kunywewa hata kwa dawa kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Waili al-Hadhrami ameeleza: Tariqa bin Suwaid alimuuliza Mtume (s.a.w) juu ya ulevi. Mtume (s.a.w) aliuharamisha. (Tariqa) akasema hakika natengeneza ulevi kwa ajili ya dawa. Mtume (s.a.w) alijibu: Huo si dawa bali ni ugonjwa. (Muslim).*

Ulevi ni haramu ukinywewa kwa wingi au kwa uchache kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kinacholevya ni haramu kikiwa kingi au kidogo. (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

**Vyakula na vinywaji Halali**

Vyakula na vinywaji vyote vilivyo patikana kwa njia ya halali au kutokana na chumo la halali na visivyo haramishwa katika Qur-an na Snnah, ni halali kwa Waislamu. Ni haramu mtu kuharamisha alivyovihalalisha Allah (s.w).

Mtume (s.a.w) alipoapa kutokula "asali" kwa sababu tu ya kutaka kuwaridhisha wake zake, Mola wake alimuonya na kwa hiyo tunaonywa Waislamu wote:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلنَّبِىُّ لِمَ تُحَرِّمُ مَآ أَحَلَّ ٱللَّهُ لَكَ ۖ تَبْتَغِى مَرْضَاتَ أَزْوَٰجِكَ ۚ وَٱللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١﴾

*Ewe Mtume: Mbona unaharamisha alichokuhalalishia Mwenyezi Mungu? Unatafuta radhi za wake zako? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu. (66:1).*

Kama mtu chakula fulani kinamdhuru au hakipendi atakuwa na udhuru wa kutokila lakini asikiharamishe.

**Adabu za kula**

Kula kwa Muislamu ni Ibada, kwani wakati anapokula anatakiwa azikumbuke neema za Allah (s.w) na azishukuru kwa kumuabudu Mola wake ipasavyo. Mtu anayemkufuru Allah (s.w) na kuona kuwa lengo la kuwepo kwake hapa ulimwenguni ni kula na kustarehe, mbele ya Allah (s.w) anawekwa katika kundi la wanyama kama tunavyojifunza katika aya ifuatavyo:

إِنَّ ٱللَّهَ يُدْخِلُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ جَنَّٰتٍ تَجْرِى مِن تَحْتِهَا ٱلْأَنْهَٰرُ ۖ وَٱلَّذِينَ كَفَرُوا۟ يَتَمَتَّعُونَ وَيَأْكُلُونَ كَمَا تَأْكُلُ ٱلْأَنْعَٰمُ وَٱلنَّارُ مَثْوًى لَّهُمْ ﴿١٢﴾

*Kwa hakika Mwenyezi Mungu atawaingiza walioamini na kufanya mema katika mabustani yapitayo mito mbele yake. Lakini waliokufuru hujifurahisha (hapa duniani) na kula kama walavyo wanyama, na moto ndio makazi yao. (47:12)*

Muislamu hatarajiwi ale kama walavyo wanyama, bali anatarajiwa ale kwa heshima na adabu iliyobainishwa na Uislamu kama tunavyojifunza katika kipengele hiki. Adabu za kula hapa tutazigawanya katika mbeya nne zifuatazo:

(a) kabla ya kuanza kula.
(b) Wakati wa kula.
(c) Baada ya kula.
(d) Kula katika kundi.

**(a) Kabla ya kuanza kula**

(i) Kuhakikisha kuwa chakula Muislamu anacho kwenda kula ni halali kwani tonge moja la chakula haramu linamfanya mtu asikubaliwe Ibada zake kwa siku 40.Pia tunafahamishwa kuwa mwili

uliojengwa na chakula haramu umeharamishiwa pepo na mahali unapojuzu kuingia ni motoni.

(ii) Kuosha mikono kabla ya kuanza kula ili kutoa uchafu kwa ajili ya afya. Pia kufanya hivyo kuna baraka ndani yake kama tunavyofahamishwa katika Hadith ifuatayo:

*Salman ameeleza; Nimesoma katika Taurati kuwa baraka za chakula zinapatikana kwa kuosha mikono baada ya kula. Nilipolieleza hili kwa Mtume (s.a.w) alisema: Baraka za chakula zinapatikana kwa kuosha mikono kabla ya kuanza kula na baada ya kumaliza kula. (Tirmidh).*

(iii) Meza au mahali pa kulia patandikwe kitambaa safi, vyema kiwe cheupe ili chakula kitakachodondoka humo kiokotwe na kuliwa kama alivyosisitiza Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) hakuwahi kulia kwenye meza kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Anas (r.a) amesimulia: Kwa kadri nijuavyo, Mtume (s.a.w) kamwe hakuwahi kula chakula kwenye trei kubwa, wala hakuwahi kula silesi za mkate zilizokaushwa, wala hakuwahi kula mezani. (Bukhari).*

(iv) Wakati wa kula mtu akae vizuri, asiwe amejiegemeza wala asile huku amelala. Akae mkao ambao utamuwezesha kula kwa starehe:

*Abdullah bin Amr amesimulia kuwa Mtume wa Allah hakuwahi kuonekana akila huku ameegemea mahali…" (Abu Daud)*

(v) Kuweka nia ya kula ili kupata nguvu za kumtumikia (kumuabudu) Allah (s.w) inavyostahiki na kuzingatia aya ifuatayo:

ثُمَّ لَتُسْـَٔلُنَّ يَوْمَئِذٍ عَنِ ٱلنَّعِيمِ ﴿٨﴾

*Kisha kwa hakika mtaulizwa siku hiyo juu ya neema (mlizopewa mlizitumiaje). (102:8)*

(vi) Mgeni atosheke na chakula kilichotayarishwa na wenyeji wake, badala ya kuwasumbua wenyeji wake wamtayarishie chakula kingine. Ila ikiwa chakula hicho ni kigeni kwake na hawezi kula, basi itakuwa hapana budi atafutiwe chakula kingine.

(vii) Ni vyema kula chakula pamoja kuliko kula mmoja mmoja kwani chakula kinacholiwa kwa pamoja kina baraka kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Umar bin Khattab ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kula pamoja na sio kwa kutengana kwani baraka ziko kwa walio pamoja na wengi. (ibn Majah).*

Pia kuwakaribisha chakula wageni, fukara, maskini, yatima na wote wenye kuhitajia ni jambo lililosisitizwa sana katika Uislamu.Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa mtu asiyejihimiza kuwalisha maskini na kuwaangalia vyema yatima amekadhibisha siku ya malipo hata kama atajiita Muislamu:

أَرَءَيْتَ ٱلَّذِى يُكَذِّبُ بِٱلدِّينِ ﴿١﴾ فَذَٰلِكَ ٱلَّذِى يَدُعُّ
ٱلْيَتِيمَ ﴿٢﴾ وَلَا يَحُضُّ عَلَىٰ طَعَامِ ٱلْمِسْكِينِ ﴿٣﴾

*Je, umemuona yule anayekadhibisha dini (asiyeamini akhera)? Huyo ni yule anayemsukuma yatima, wala hajihimizi kuwalisha maskini. (107:1-3).*

Katika Hadith iliyosimuliwa na Ibn Abbas, Mtume (s.a.w) amesema:

*Baraka zinashuka haraka haraka katika nyumba ambamo chakula hutolewa kuliko kisu kinavyopita katika nundu ya ngamia(Ibn Majah)*

**(b) Wakati wa kula**

(i) Kuanza kula kwa jina la Allah kwa kusema: "Bismillahir rahmanir Rahiim". Muislamu kuanza kula bila ya kulitaja jina la Allah (s.w) ni kumkaribisha Shetani katika chakula chake. Katika Hadith iliyosimuliwa na Hudhaifah Mtume wa Allah amesema:

*Hakika Shetani anakifanya chakula kiwe halali kwake pale ambapo jina la Allah halikutajwa. (Muslim)*

Kama Muislamu amesahau kuanza kwa jina la Allah wakati wa kula atakapokumbuka asema:

*"Bismillahi awwalahu wa aakhirahuu" yaani "Naanza kwa jina la Allah mwanzoni mwake na mwishoni mwake". (Tirmidh, Abu Daudi).*

(ii) Kula kwa mkono wa kulia. Mtume (s.a.w) amesema: "Mmmoja wenu atakapokuwa ana kula, na ale kwa mkono wa kulia na atakapokuwa anakunywa, na anywe kwa mkono wa kulia". (Muslim).

(iii) Kumega chakula sehemu iliyo mbele yako, ukianzia chini na wala sio juu kama inavyosisitizwa katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) aliletewa chakula kisha akasema:Anza kumega pembani mwake*

*na wala isiwe katikati kwa sababu baraka zinamiminika kwenda chini kupitia katikati. (Tirmidh, Ibn Majah na Darimi).*

Katika riwaya ya Abu Daud, alisema: "Wakati mmoja wenu anakula, asile kutokea sehemu ya juu ya chakula bali amege kuanzia sehemu ya chini pembeni mwa sahani kwa sababu baraka zinashuka kutokea sehemu ya juu.

Pia tunakatazwa kuyumbayumba kwenye sahani wakati wa kula kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Amir bin Salamah ameHadithia: Nilikuwa kijana mdogo chini ya malezi ya Mtume wa Allah na mkono wangu ulikuwa unayumba yumba katika sahani kwa hiyo alinionya: "Kula kwa mkono wako wa kulia na mega pale palipo karibu yako" (Bukhari na Muslim)*

(iv) Muislamu akila anatakiwa amege tonge ndogo ndogo na atafune vizuri ili kurahisisha usagaji wa chakula tumboni.

(v) Ni vizuri kukata nyama kwa meno kuliko kutumia kisu kama Mtume (s.a.w) anavyotuhimiza katika Hadith ifuatayo:

*Aysha ameeleza kuwa Mtume wa Allah anasema: "Usikate nyama kwa kisu kwa sababu ni jambo la wageni, lakini ichane kwa meno kwani huleta utamu zaidi na ni wepesi zaidi kufanya hivyo." (Abu Daud, Darimi).*

(vi) Kama chakula ni cha moto ni vizuri kusubiri kipoe na sivizuri kupoozesha chakula kwa kupuliza.

(vii) Kula kwa kiasi. Si vizuri Muislamu kujaza sana tumbo. Hiyo ni israfu na inamadhara yake kiafya na kiroho:

*Miqdam bin Maadi amesimulia: "Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: "Hapana mtu kujaza sana tumbo lake kiasi cha kuchukiza. Hapana budi pawe na kipimo cha kujaza tumbo kwa mwanaadamu kiasi cha kuubakisha uti wake wa mgongo katika hali ya kunyooka. Kama hawezi kuweka kipimo hicho, basi theluthi (1/3) ya tumbo lake aijaze chakula, theluthi (1/3) iliyobakia kwa ajili ya hewa. (Tirmidh, Ibn Majah).*

(viii) Kuokota tonge la chakula lililoanguka kwa bahati mbaya na kula kama liliangukia kwenye kitambaa maalum kilichotayarishwa kwa ajili hiyo. Kama tonge hilo litakuwa limeanguka chini, utaondoa sehemu iliyoshika chini na kula sehemu safi iliyobakia.Jitihada zote hizi ni ili kuepukana na israfu ambayo ni njia ya Shetani. Tunajifunza hili katika Hadith ifuatayo:

*Jabir ameeleza kuwa alimsikia Mtume wa Allah akisema: Hakika Shetani anamuhudhuria kila mtu katika kila kitu anachokifanya hata wakati wa chakula. Tonge la chakula litakapomponyoka mmoja wenu na atupe sehemu iliyo shika vumbi na ale kilichobakia na asimwachie shetani. Na atakapo maliza chakula chake na alambe vidole vyake kwani hajui ni wapi katika chakula chake kuna baraka. (muslim).*

(ix) Kulamba sahani na vidole ili kuhakikisha kuwa hakuna hata chembe ya chakula inayotupwa, ni miongoni mwa adabu za kula kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Kaab bin Malik ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akila kwa vidole vitatu na alikuwa akilamba mkono wake kabla hajanawa. (Muslim).*

*Jabir amesimulia kuwa Mtume (s.a.w) alikuwa akilamba vidole vyake na sahani na akisema: Hujui ni wapi katika chakula kuna baraka. (Muslim)*

*Ibn Abbas ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Mmoja wenu anapokula chakula hatanawa bila ya kulamba mkono wake. (Bukhari na Muslim).*

**(c) Baada ya chakula**

(i) Baada ya Kulamba vidole, na sahani tunanawa mikono kwa ajili ya unadhifu na kutunza afya zetu. Mtume (s.a.w) ametusisitiza kunawa baada ya kula kama inavyobainishwa katika Hadith:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Atakayepitisha usiku na uchafu mkononi mwake kwa sababu ya kutonawa (baada ya kula) ikatokea kudhurika kutokana na uchafu huo, asimlaumu yeyote ila yeye mwenyewe. (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

(ii) Kumshukuru Allah (s.w). Baada ya Muislamu kula au kunywa kitu chochote humshukuru Allah (s.w) kwa kusema:"Al-hamdulillaahi Rabbila-aalamiin" yaani shukrani zote anastahiki Bwana mlezi wa viumbe vyote". Amesimulia Abu Sayyid Al-Kudriyyi kuwa Mtume (s.a.w) alipomaliza kula alizoea kushukuru hivi:

*Al-hamdulillaahil-ladhii atwa-amanaa wasaqaanaa wajaalnaa minal muslimiina.*

Yaani:

*Sifa zote njema zinamstahiki Allah aliyetulisha, akatunywesha na akatufanya kuwa Waislamu. (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Muislamu atatakiwa akiweke kila kitendo anachokifanya katika Ibada kwa kukianza kwa jina la Allah, kuchunga mipaka ya Allah wakati wa kukifanya na kumaliza kwa kumshukuru Allah (s.w).

Hivyo, kula kutakuwa Ibada endapo Muislamu ataanza kula kwa jina la Allah, kisha akawa anamkumbuka Allah (s.w). Faida zaidi ya kumshukuru Allah (s.w) baada ya kula inabainishwa katika Hadith ifuatayo:

*Anas ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Hakika Allah anamfurahia mja anayekula chakula kisha akamshukuru baada yake au anayekunywa kisha akamshukuru baada yake. (Muslim).*

(iii) Kumshukuru mwenyeji au mtayarishaji wa chakula kwa kumwambia "*Ahsante*" au "*Shukran*" kwani asiye mshukuru mwanaadam aliyemtendea wema, hawezi kumshukuru Allah (s.w):

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mlaji mwenye shukrani ni sawa na mfungaji mwenye subira. (Tirmidh, Ibn Majah).*

Kulinganishwa mlaji na mfungaji ni kielelezo kingine kuwa kula ni Ibada kama ilivyo kufunga kama utaratibu wa kula utafuatwa kama unavyofuatwa katika kufunga.

Pamoja na kutoa shukrani kwa mtayarishaji wa chakula, ni vyema pia kumuombea dua kwa kusema: "*Jazakallahu khair*" akiwa mwanamume, na akiwa mwanamke utamuombea kheria kwa kusema: "*Jazakillahi khair*" yaani "Allah akujazie kheri".

**(d) Adabu za kula katika Kundi**

(i) Mtu asianze kula kabla ya wengine.
(ii) Asifanye haraka, ale kwa kasi inayolingana na wengine na awafikirie wengine ili asiwapunje.
(iii) Kama kila mmoja anajiwekea chakula katika sahani yake kutoka kwenye dish kubwa, hana budi kuchukua kiasi kidogo kwanza mpaka wote

waenee, kisha akihitaji baadaye ataongeza lakini vile vile awafikirie wengine nao watakaotaka kuongeza.

(iv) Asiwang'ang'anize wengine kula aina ya chakula asichokipenda, badala yake awapendelee wengine kile anachokipenda.

(v) Asiwaangalie wengine wanavyokula wala sahani zao.

(vi) Awapendelee wengine kupata kitu kama vile maji kabla ya yeye mwenyewe kupata.

(vii) Vile vile awe tayari kuwahudumia wengine kabla yeye hajahudumiwa.

(viii) Asiache kula na kunawa kabla ya wengine. Hata kama ameanza kushiba, itabidi aendelee kidogo kidogo mpaka wote washibe kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Nguo ya chakula inapotandikwa, hapana mtu atakayesimama mpaka nguo hiyo iondolewe wala hapana mtu atakayetoa mkono wake kwenye chakula hata kama ameshiba mpaka watu wote wamemaliza kula. Ikibidi aache kula kabla ya wengine, na awatake radhi kwani bila ya kufanya hivyo atawavunja moyo (atawanyima raha) wenzake… (Ibn Majah).*

(ix) Asikosoe chakula au kinywaji mbele ya wengine.

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) hakuwahi kubainisha ubaya wa chakula (au kukiadhiri chakula) chochote kama alikipenda chakula alikila na akama hakukipenda chakula aliacha kula. (Bukhari na Muslim).*

### 4. Michezo na Burdani

Uislamu ni utaratibu wa maisha uliokamilika. Umebainisha namna ya kuliendea kila jambo linalohitajika katika kuendesha maisha ya mwanaadam ya kila siku katika kila uwanja ili kumuinua mwanaadamu kimwili, kiutu na kijamii. Michezo ni miongoni mwa vipengele hivi. Uislamu unawataka watu wacheze na kufurahia lakini kwa kuchunga mipaka iliyowekwa na kuzingatia lengo la maisha ya mwanaadamu hapa ulimwenguni.

#### *Michezo iliyoruhusiwa katika Uislamu*

Michezo yote ambayo humfanya mchezaji kupata uwezo zaidi wa kiafya na kiakili wa kumuabudu Allah (s.w) inasisitizwa kufanywa na Uislamu. Mtume (s.a.w) amesema: "Afya kwa mtu anayemwogopa Allah (s.w) ni bora kuliko utajiri". Mara kwa mara Mtume (s.a.w) katika kusisitiza afya njema ya mwili na akili amesema: "Waumini (wacha Mungu) wote mbele ya Allah ni sawa lakini aliyebora zaidi ni yule mwenye siha nzuri zaidi". Hivyo, michezo yote isiyochupa mipaka ya Allah (s.w) itakayochezwa kwa lengo la kujenga afya ya mwili na akili haikukatazwa katika Uislamu.

Aidha, michezo yote ya mazoezi ya kivita kama vile kulenga shabaha, kutupa mkuki, kareti, mieleka, mbio za farasi, imesisitizwa na Uislamu. Ikumbukwe kuwa Waislamu ni askari wa Allah (s.w) ambao daima wanatakiwa wawe tayari kupigana na maadui wa Uislamu na Waislamu mara watakapoanza kuwachokoza. Kazi ya kupigania dini ya Allah (s.w) haikupachikwa kwa jeshi maalum lililoandaliwa kwa kazi hiyo, bali hiyo ni Ibada inayomuhusu kila Muislamu.

*Utbah bin Amir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kila mchezo atakaocheza mtu ni haramu ila kutupa mishale, kumfunza farasi wake na kucheza na mkewe. Hakika hii ndio michezo ya kweli (yenye faida).*

Pamoja na kwamba michezo yote hii iliyotajwa katika Hadith hii inatoa mazoezi ya mwili na kuituliza akili bado kuna faida za ziada zinazopatikana. Ambapo michezo miwili ya kwanza inampa Muislamu mazoezi ya kijeshi, mchezo wa kucheza mtu na mkewe chumbani au katika mazingira ya nyumbani kwao, huimarisha furaha na upendo katika familia.

**Michezo iliyoharamishwa katika Uislamu**

Michezo iliyoharamishwa katika Uislamu tunaweza kuigawa katika mafungu mawili:

**Kwanza**, uharamu unaotokana na kuchupa mipaka ya Allah (s.w). Hata kama atacheza michezo iliyoruhusiwa kwa nia nzuri ya kuupa mwili mazoezi, kujipa mazoezi ya kijeshi n.k. itakuwa ni haramu michezo hiyo endapo atachupa miapaka ya Allah (s.w) katika uchezaji wake kama vile kucheza na bukta hadharani, kupita wakati wa swala, kutumia lugha chafu, n.k.

**Pili**, kucheza michezo yote iliyoharamishwa katika Qur-an na inayofanana na hiyo. Michezo yote ya kamari au ya kibahati nasibu (games of chance) na yenye mfano wa hiyo imekatazwa katika Qur-an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ إِنَّمَا ٱلْخَمْرُ وَٱلْمَيْسِرُ وَٱلْأَنصَابُ وَٱلْأَزْلَـٰمُ رِجْسٌ مِّنْ عَمَلِ ٱلشَّيْطَـٰنِ فَٱجْتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (au kuombwa) asiye kuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia (kupiga ramli, utabiri, n.k.) ni uchafu na ni kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufaulu. (5:90).*

Michezo yote ya kibahati nasibu kama vile michezo yote ya pata-potea, karata, dama, bao, chess na michezo yote ya mashindano kama vile mpira riyadha, ndondi, n.k. imeharamishwa kwa sababu inaleta madhara makubwa katika jamii.Pamoja na faida inayotazamiwa katika michezo hiyo, madhara yake ni makubwa zaidi. Hili anatuhakikishia Allah (s.w) katika Qur-an:

يَسْـَٔلُونَكَ عَنِ ٱلْخَمْرِ وَٱلْمَيْسِرِ ۖ قُلْ فِيهِمَآ إِثْمٌ كَبِيرٌ وَمَنَـٰفِعُ لِلنَّاسِ وَإِثْمُهُمَآ أَكْبَرُ مِن نَّفْعِهِمَا ۗ

*Wanakuuliza juu ya ulevi na kamari, Sema: Katika hivyo mna madhara makubwa na manufaa kwa (baadhi ya) watu. Lakini madhara yake ni makubwa zaidi kuliko manufaa yake.... (2:219).*

Pamoja na madhara mengine mengi madogo na makubwa yanayotokana na michezo ya kikamari (kibahati nasibu), madhara makuu yamebainishwa katika Qur-an kama ifuatayo:

*Hakika Shetani anataka kukutilieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali. Basi, je hamtaacha (mabaya hayo)?*

Madhara maku bwa ya michezo yote ya kikamari kama yalivyobainishwa katika aya hii ni:

(a) Kusababisha uadui na bughudha.
(b) Kuwazuilia waumini kumkumbuka Allah (s.w)
(c) Kuwazuilia waumini kuswali (kwa wakati).

Hebu tuangalie madhara haya kwa kuzingatia hali halisi ya michezo ambayo imepewa nafasi kubwa na kuundiwa wizara katika jamii za kitwaghuti.

**(a) Michezo ya Kikamari Husababsha Uadui na Bughudha**

Wale wote wanaojihusisha au waliowahi kujihusisha na michezo hii watakuwa mashahidi wa ukweli huu. Ilivyo kawaida ni kwamba anayepata ushindi katika michezo hiyo hufurahia na kujiona na yule anayeshindwa huchukia na huwa na hisia za kutaka kulipiza kisasi. Kwa ujumla katika michezo ni furaha na ufakhari kwa mshindi na ni huzuni na chuki kwa aliyeshindwa. Ukichanganya hali hizi mbili unachotarajia ni nini kama sio uadui na bughudha baina ya wachezaji wa pande mbili. Kuteta, kusengenya, matusi na utani ni lugha ya kawaida ya michezo. Uadui kati ya timu mbili za mpira na washabiki wake si jambo geni kwetu. Watu kuuana kutokana na kudhulumiana katika michezo ya kamari si jambo geni.

Utashangaa vipi dola za kitwaghuti zinaipa michezo hii kipaumbele! Kisingizio chao kikubwa ni kwamba inaleta ushirikiano na kujenga udugu. Hii ni kauli ya uongo inayopingana na hali halisi. Tumeelezwa kuwa michezo ya kikamari na ya mashindano ni kazi ya Shetani. Ni muhali kutokea ushirikiano na upendo katika uwanja wa michezo ambapo Shetani ndiye mgeni rasmi.

**(b) Michezo ya Kikamari (Games of chance) huwazuilia Waumini kumkumbuka Allah (s.w)**

Kila mchezaji au aliyeshuhudia michezo ya karata, bao, chess, gudugudu, na michezo mingine yote ya kibahati nasibu (games of chance),pamoja na mchezo wa mpira, anafahamu vyema jinsi michezo hii inavyopoteza muda na kumsahaulisha mtu na majukumu muhimu ya maisha

yake binafsi, familia na jamii kwa ujumla. Ni mara ngapi tunawaona watu wazima na akili zao na wenye majukumu mengi mbele yao, wakishinda kutwa wanacheza bao bila hata kula.

Ni mara ngapi tunaona wakati umetangazwa mchezo kati ya timu mbili maarufu za mpira, watazamaji wakihudhuria uwanjani saa mbili asubuhi na kungojea humo uwanjani mpaka saa kumi alasiri, mechi itakapoanza?

Ni jambo la kawaida vile vile kuwakuta watu wazima na nguvu zao na akili zao timamu wakitumia muda mrefu katika michezo ya karata na mingineyo kama hiyo. Michezo yote hii hupumbaza wachezaji na watazamaji wasiweze kufikiri mambo ya msingi ya maisha yao. Utashangaa kwa nini michezo ya aina hii inapewa kipaumbele katika jamii za kitwaghuti hasa kwa vijana wa mashuleni na mitaani. Bila shaka huu ni mpango wa kuwapumbaza vijana ili watawala madhalimu waendelee kuiendesha jamii watakavyo kwa maslahi yao binafsi.

Katika Uislamu michezo yote inayompumbaza mtu asitekeleze majukumu yake na kuliendea lengo lake la kuwepo hapa ulimwenguni imeharamishwa na atakayejitumbukiza humo atakuwa miongoni mwa watu wa motoni kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ ﴿٣٨﴾ إِلَّآ أَصْحَٰبَ ٱلْيَمِينِ
﴿٣٩﴾ فِى جَنَّٰتٍ يَتَسَآءَلُونَ ﴿٤٠﴾ عَنِ ٱلْمُجْرِمِينَ ﴿٤١﴾ مَا
سَلَكَكُمْ فِى سَقَرَ ﴿٤٢﴾ قَالُوا۟ لَمْ نَكُ مِنَ ٱلْمُصَلِّينَ ﴿٤٣﴾ وَلَمْ
نَكُ نُطْعِمُ ٱلْمِسْكِينَ ﴿٤٤﴾ وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ ٱلْخَآئِضِينَ

*Kila nafsi itafungika (motoni) kwa amali (mbovu) ilizozichuma. Isipokuwa watu wa kuliani, wanaulizana juu ya watu wabaya: Ni kipi kilichokupelekeni motoni? Waseme:Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakisali, wala hatukuwa tunalisha maskini. Na tulikuwa tukizama (katika upuuzi) pamoja na waliokuwa wakizama.(74:38-45).*

Lengo la maisha ya mwanaadamu ni kumtumikia Allah (s.w) kwa kusimamisha Ufalme wake katika jamii kwa kuhakikisha kwa hali na mali kuwa utaratibu wa maisha unaofuatwa na jamii ni ule aliouweka Yeye. Ili kufikia lengo hili kuu, kila wakati mwanaadamu anatakiwa akumbuke uhusiano wake na Allah (s.w) na daima akumbuke kuwa yeye hapa ulimwenguni ni Khalifa wa Allah (s.w).Mtu aliyezama kwenye michezo ya upuuzi inayopoteza muda na kupumbaza ni muhali kuwa na kumbukumbu hizi hata kama atajiita Muislamu. Waislamu hasa waliofuzu mbele ya Allah (s.w) ni wale wanaojiepusha na michezo yote ya upuuzi (laghwi) kama tunavyojifunza katika Qur-an:

قَدْ أَفْلَحَ ٱلْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ ٱلَّذِينَ هُمْ فِى صَلَاتِهِمْ

خَٰشِعُونَ ﴿٢﴾ وَٱلَّذِينَ هُمْ عَنِ ٱللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾

*Hakika wamefuzu Waislamu, ambao katika swala zao huwa ni wanyenyekevu. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi. (23:1-3).*

Katika suratul Furqaan tunafahamishwa kuwa miongoni mwa sifa za waja wa Rahman ni pamoja na wale ambao hawajihusishi na mambo ya upuuzi, hata tu kuwa watazamaji:

وَٱلَّذِينَ لَا يَشْهَدُونَ ٱلزُّورَ وَإِذَا مَرُّوا۟ بِٱللَّغْوِ مَرُّوا۟ كِرَامًا

*Na wale ambao hawashuhudii shahada za uwongo, na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima (zao) (25:72)*

**(c) Michezo ya Upuuzi huwazuilia Waumini kuswali**

Michezo ya upuuzi kama vile mpira, bao, karata, n.k huwapumbaza wachezaji na wasikilizaji kiasi cha kujenga tabia ya kupuuza swala.Tumeyashuhudia haya katika magenge ya mabao.Ni jambo la kushangaza kuwakuta Waislamu wakiendelea na bao kuanzia asubuhi mpaka jioni na kupitwa na swala zote za kutwa kisha huziswali kadha wakati wa isha, jambo ambalo halimo kabisa katika utaratibu wa kusimamisha swala tano. Swala ni faradhi kuswali katika wakati wake maalumu

إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ كَانَتْ عَلَى ٱلْمُؤْمِنِينَ كِتَـٰبًا مَّوْقُوتًا

*"... Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhususi". (4:103).*

Swala ndio zana ya kumuwezesha Muislamu kumuabudu Mola wake ipasavyo na humuwezesha kuishi kwa nidhamu katika jamii kama Khalifa wa Allah (s.w). Nidhamu katika jamii haipatikani pale ambapo swala imepuuzwa.

Hivyo michezo yote inayomtoa mtu katika lengo la kuumbwa kwake ni michezo ya upuuzi na Muumini wa kweli hana budi kujiepushia mbali na michezo hiyo.

**(iv) Sherehe na Burdani**

Maisha ya mwanaadamu yamezungukwa na furaha na majonzi penye furaha watu hushereheka na penye msiba watu huomboleza. Katika kipengele hiki tutazingatia sherehe na burdani katika jamii ya Kiislamu ukilinganisha na jamii za kitwaghuti.Katika jamii ya kitwaghuti

iliyozunguka tunawaona watu wakijiburudisha na kujitumbuiza katika sherhe zao kwa ngoma, disco, nyimbo, mashairi, ngonjera n.k. Je, Uislamu unamtazamo upi juu ya sherehe na burdani na kushereheka kwa Waislamu kunatofautianaje na kushereheka kwa majahili?

Majahili hawajui halali wala haramu katika sherehe zao na katika kusherehekea kwao. Kwa maana nyingine majahili hawajali kuona nafsi ya sherehe iliyo mbele yao kuwa ni yenye kumridhisha Allah (s.w) au ni yenye kumchukiza na katika kushereheka kwao hawana habari na mipaka ya Allah (s.w) aliyoiweka.

Sherehe ya Kiislamu ni tofauti sana na hizi za kitwaghuti.

Kwanza katika Uislamu, sherehe yoyote ile inayopingana na hukumu za Allah (s.w) ni haramu na hivyo si ruhusa Waislamu kushiriki. Kwa mfano ni haramu kwa Waislamu kuitika mwito wa harusi ya kumuoza binti wa Kiislamu kwa Mkristo au kwa yeyote asiyekuwa Muislamu.Halikadhalika ni haramu kwa Waislamu kujiunga na sherhe zozote zile za kidini minghairi ya Uislamu. Kwa mfano, kama ilivyo haramu kwa Waislamu kujitumbukiza katika sherehe za matambiko ya aina yote ndivyo ilivyo haramu kwa Waislamu kusherehekea Krismas, Mwaka mpya na Pasaka.

Jambo la pili linalozingatiwa na Waislamu katika sherehe zao ni uchungaji wa mipaka ya Allah (s.w) katika kushereheka kwenyewe. Vyakula na vinywaji vitakavyotumika katika sherehe havina budi kuwa halali, vitolewe bila ya kufanya israfu na pasiwe na ubaguzi wowote katika kuvigawanya.

*Imesimuliwa na Abu Hurairah kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Karamu ya harusi iliyo mbaya kuliko zote ni ile ambayo wamealikwa matajiri wakaachwa maskini" (Bukhari na Muslim).*

Kwa ujumla sherehe za Kiislamu zinatakiwa ziambatanishwe na kutoa sadaqa ili kuwafurahisha majirani na wenye matatizo. Maendelezo ya sherehe za Kiislamu kuanzia hatua ya mwanzo hadi ya mwisho hayanabudi kuzingatia mipaka yote ya Allah (s.w). Kilele cha sherehe za Kiislamu kinafikiwa kwa kumtaja Allah (s.w) na kumtaka maghfira. Qur-an inatuongoza kuwa:

إِذَا جَآءَ نَصۡرُ ٱللَّهِ وَٱلۡفَتۡحُ ﴿١﴾ وَرَأَيۡتَ ٱلنَّاسَ يَدۡخُلُونَ
فِي دِينِ ٱللَّهِ أَفۡوَاجٗا ﴿٢﴾ فَسَبِّحۡ بِحَمۡدِ رَبِّكَ وَٱسۡتَغۡفِرۡهُۚ
إِنَّهُۥ كَانَ تَوَّابَۢا ﴿٣﴾

*Itakapofika nusra ya Mwenyezi Mungu na kushinda. Na ukawaona watu wakiingia katika dini ya Mwenyezi Mungu makundi makundi. Basi hapo mtakase Mola wako pamoja na kumsifu, umuombe maghufira (msamaha) hakika yeye ndiye apokeaye toba. (110:1-3).*

Katika aya hizi tunakumbushwa kuwa hatuna budi kukumbuka daima kuwa ushindi au furaha ya aina yoyote anaileta Allah (s.w). Hivyo, katika hali hiyo ya furaha hatuna budi kumshukuru Allah na kumsifu kwa sifa zake na kumuomba msamaha kwa makosa yetu ili furaha hiyo tuliyoipata hapa duniani iwe yenye kuendelea katika maisha ya akhera, Muislamu kamwe hatathubutu kujihasirisha na kujitumbukiza katika huzuni ya milele katika maisha yake ya akhera kwa sababu ya furaha zidanganyazo za hapa duniani.

Furaha ya kweli kwa Muislamu ni ile iliyoambatana na Radhi za Allah (s.w). Na lolote lile linalomghadhibisha Allah (s.w) ni msiba na huzuni kubwa kwa Muislamu hata kama limesherehekewa na walimwengu wote.

Hebu sasa tuanglie mtazamo wa Uislamu juu ya matumizi ya ngoma, "disco", nyimbo na mashairi kama burdani na kama sehemu ya sherehe.

**Ngoma na "Disco".**

Michezo yote ya ngoma, disco, dansi, n.k. kama tuionavyo katika utamaduni wa jamii hizi za kijahili, ni haramu kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, ni laghwi yaani michezo ya upuuzi kwani huwafanya watu wapoteze muda mwingi nje ya lengo la kuumbwa kwao hapa ulimwenguni. Yaani michezo hii ya ngoma na "disco" huwasahaulisha wachezaji na watazamaji kumkumbuka na kumtukuza Allah (s.w). Kwa hiyo michezo hii ya ngoma ni miongoni mwa kazi ya shetani na Allah (s.w) ametukataza kushiriki katika shughuli zote za Shetani.

Pili, michezo mingi ya ngoma na "madisco" huchezwa katika mchanganyiko wa wanawake na wanaume na huwa ni vichocheo vikubwa sana vya zinaa. Katika Uislamu ni haramu kushiriki katika shughuli yoyote inayochochea zinaa.

وَلَا تَقْرَبُوا۟ ٱلزِّنَىٰٓ ۖ إِنَّهُۥ كَانَ فَـٰحِشَةً وَسَآءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu mkubwa) na njia mbaya (kabisa).(17:32)*

Katika sherehe za harusi wanawake wameruhusiwa kupiga dufu na kuimba nyimbo ambazo hazichupi mipaka ya Allah (s.w) kama tunavyojifunza sunnah. Hapana kamwe katika mafundisho ya Mtume (s.a.w) ambapo dufu limetiliwa mkazo kama Waislamu wanavyolitilia leo hii.

**Nyimbo na mashairi**

Nyimbo na mashairi huwa halali au haramu kutegemeana na madhumuni ya nyimbo au mashairi hayo. Ni wazi kuwa nyimbo au mashairi ya kimapenzi ambayo ni vichochezi vya zinaa ni haramu moja kwa moja. Pia mashairi au nyimbo ambazo ndani yake kuna lugha mbaya, au kuna kuitukana au kuipinga dini ya Allah (s.w), basi mashairi hayo au nyimbo hizo zitakuwa ni haramu. Hali kadhalika mashairi na nyimbo ambazo ziko pale kumpotezea mtu muda wake ni laghwi na ni haramu.

Nyimbo na mashairi ambayo ndani yake kuna hekima na mafunzo ya aina mbali mbali ambayo hayaambatani na sauti na midundo ya ngoma za miziki, yanakubalika katika Uislamu. Nyimbo na mashairi ya Kiislamu hayana budi kumuelekeza Muislamu katika kumcha Mwenyezi Mungu zaidi na katika kumpa nguvu na hamasa ya kupigania dini ya Allah (s.w). Tunajifunza katika Hadith ya Bukhari na Muslim iliyosimuliwa na Jundub kuwa Mtume wa Allah (s.w) alijipooza kishairi alipoumia vidole vyake katika vita vya Uhud.

Alijiliwaza katika shairi hilo kuwa kutokwa na damu kwake si kwa sababu nyingine ila ni kwa ajili ya Allah (s.w) na kwa ajili ya dini yake. Pia katika Hadith nyingine ya Bukhari na Muslim iliyosimuliwa na Barasi, tunajifunza kuwa Mtume (s.a.w) aliimba wimbo wa kuwatia nguvu Waislamu walipokuwa katika kazi ngumu sana ya kuchimba handaki katika vita vya Handaki wakati Waislamu wapatao alfu mbili (2,000) tu walipovamiwa mjini

mwao na jeshi la watu wapatao alfu ishirini na nne (24,000) mnamo 5 A.H. Wimbo huu umesheheni na maneno ya hekima na kuwapelekea Waislamu kuwa imara kwa kumtegemea Allah (s.w).Hakika Allah (s.w) aliwanusuru Waislamu katika vita hivyo.

**5. Misiba na Maombolezo**

Misiba na maombolezo ni miongoni mwa vipengele vya utamaduni wa jamii. Kila jamii ina namna yake ya kupokea misiba na kuomboleza. Katika jamii za kijahili misiba yote imeambatanishwa na mkono wa mwanaadamu au nguvu zinazotokana na maumbile asili yaliyomzingira mwanaadamu.

Maombolezo ya misiba, kama vile maombolezo ya vifo, katika jamii za kijahili huambatana na malalamiko, lawama, masononeko.Wengine, katika kupunguza msononeko hulewa sana, huchezesha ngoma na hufanya kila jambo lingine litakalowapumbaza ili wasahau kifo.

Mtazamo wa Uislamu juu ya misiba na maombolezo yake ni tofauti kabisa na mitazamo ya kijahili, Waislamu wanamini kuwa kila jambo hutokea kwa Qadar ya Allah (s.w) pamoja na kwamba kila jambo linalotokea limeambatanishwa na sababu za kimaumbile. Kwa mfano ni kawaida kuwa ukimkata mtu shingo kwa kisu kilichokikali atachinjika na atakufa lakini haitatokea hivyo iwapo kitendo hicho hakikulandana na Qadar ya Allah (s.w). Nabii Ismail (a.s) hakuchinjika pamoja na jitihada za baba yake – Ibrahimu (a.s) za kumchinja kwa kisu kikali sana.Mwenyewe Nabii Ibrahiim (a.s) hakuungua moto alipotumbukizwa kwenye moto mkubwa na mkali kwa kuwa kitendo hicho cha kumuua kwa kumchoma moto hakikulandana na Qadar ya Allah (s.w). Kutokana na mifano hii miwili tunaona wazi kuwa hautokei msiba wowote ila uko mikononi mwa Allah (s.w):

مَآ أَصَابَ مِن مُّصِيبَةٍ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا فِىٓ أَنفُسِكُمْ إِلَّا
فِى كِتَٰبٍ مِّن قَبْلِ أَن نَّبْرَأَهَآ إِنَّ ذَٰلِكَ عَلَى ٱللَّهِ
يَسِيرٌ ﴿٢٢﴾ لِّكَيْلَا تَأْسَوْا۟ عَلَىٰ مَا فَاتَكُمْ وَلَا تَفْرَحُوا۟
بِمَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ وَٱللَّهُ لَا يُحِبُّ كُلَّ مُخْتَالٍ فَخُورٍ ﴿٢٣﴾

*Haitokei msiba katika ardhi wala katika nafsi zenu ila umekwisha andikwa katika kitabu kabla hatujaumba; hakika jambo hilo ni jepesi kwa Allah.Ili msihuzunike sana juu ya kitu kilichokupoteeni wala msifurahi sana kwa alichokupeni. Na Mwenyezi Mungu hampendi kila ajivunaye, ajifaharishaye. (57:22-23).*

Kwa mtazamo wa Uislamu, furaha na huzuni ndio hali halisi ya mazingira ya ulimwengu na yote ni mitihani kwa mwanaadamu. Mwanaadamu mwenye akili atakayefaulu vizuri mtihani huu wa furaha ni yule anayefahamu fika kuwa furaha zote anazozipata katika ulimwengu huu zimetoka kwa Allah (s.w) ili kumjaribu kuwa atakuwa ni mwenye shukurani na kutumia furaha hizo kwa kumtukuza Allah (s.w) na kumuabudu inavyostahiki ikiwa ni pamoja na kumuomba msamaha kutokana na udhaifu wake wote uliompelekea kumkosea Bwana Mlezi (Rabb) wake.

Atakayefurahia maisha yake hapa ulimwenguni kama kwamba yeye mwenyewe binafsi au wengine katika wanaadamu ndio chanzo cha furaha hizo na kwa hiyo akafurahia atakavyo bila ya kujali mipaka aliyoweka Allah (s.w), basi atakuwa ni mwenye kubunda katika mtihani wa furaha.

Na mwanaadamu mwenye akili atakayestahiki kufaulu mtihani wa misiba ni yule anayefahamu vyema kuwa mtu hawezi kufikwa na msiba wowote ila Allah (s.w) apende; kuwa hapana mtu yeyote awezaye kumletea mtu msiba iwapo Allah (s.w) hakumwandikia msiba huo na wala hapana yeyote awezaye kumuondolea mtu msiba iwapo Allah (s.w) amemuandikia msiba huo.

Atafaulu mbele ya Allah (s.w) yule ambaye anapofikwa na msiba hapapatiki, hanung'uniki na kulalama bali huupokea msiba huo kwa moyo mkunjufu na kuridhia kuwa huo ni utaratibu wa Allah (s.w) usio na makosa na kwamba kila alilolipanga Allah (s.w) ni lenye kumnufaisha mwanaadamu. Namna Waislamu wanavyotakiwa waipokee misiba imebainishwa katika aya zifuatazo:

وَلَنَبۡلُوَنَّكُم بِشَيۡءٖ مِّنَ ٱلۡخَوۡفِ وَٱلۡجُوعِ وَنَقۡصٖ
مِّنَ ٱلۡأَمۡوَٰلِ وَٱلۡأَنفُسِ وَٱلثَّمَرَٰتِۗ وَبَشِّرِ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٥٥
ٱلَّذِينَ إِذَآ أَصَٰبَتۡهُم مُّصِيبَةٞ قَالُوٓاْ إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّآ إِلَيۡهِ
رَٰجِعُونَ ١٥٦ أُوْلَٰٓئِكَ عَلَيۡهِمۡ صَلَوَٰتٞ مِّن رَّبِّهِمۡ
وَرَحۡمَةٞۖ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡمُهۡتَدُونَ ١٥٧

*Na tutakutieni katika msukosuko wa (baadhi ya mambo haya); khofu na njaa na upungufu wa mali na wa watu na matunda. Na wapashe habari njema wanaosubiri. Ambao uwapatapo msiba husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na kwake yeye tutarejea (atatupa jaza yake)". Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola wao na Rehema, na ndio wenye kuongoka. (2:155-157).*

Waislamu wanapopatwa na misiba wanatakiwa wasubiri kama iliyobainishwa katika aya hizi na pia wanatakiwa wamuombe Allah (s.w) awawezeshe kuwa miongoni mwa wenye subira na awabariki na kiuwarehemu kutokana na misiba hiyo. Katika Hadith iliyosimuliwa na Abu Hurairah, Mtume (s.a.w) amesema:

> *Allah (s.w) atasema: "Hapana zawadi mbele yangu ila Pepo kwa mja wangu ambaye ninapomfisha kipenzi chake miongoni mwa watu katika dunia huomba ujira mwema kutokana na msiba huo." (Bukhari).*

Waislamu wanawajibika kuwapa mkono wa pole na kuwaliwaza wale waliopatwa na msiba kwa maneno yafuatayo aliyotufunza mtume (s.a.w): *"Hakika kila alichokichukua Allah (s.w) ni chake na kile alichokitoa ni chake na kila kitu kitarejea kwake kwa muda maalum". Kwa hiyo kuwa mwenye subira na tarajia kupata malipo*". (Bukhari na Muslim). Tunajifunza vile vile katika Hadith kuwa, mwenye kumliwaza aliyepatwa na msiba amepata malipo sawa na yule aliyesubiri katika msiba:

> *Abdullah bin Masud ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema "Anaye mliwaza yule aliyekuwa na msiba, kuna kwake malipo sawa na yule aliyefikwa na msiba". (Tirmidh, Ibn Majah)*

Iwapo kwa njia moja au nyingine Muislamu ataona kuwa msiba uliomtokea ni matokeo ya matendo yake maovu au kupuuza kwake mwongozo wa Allah (sw), hana budi kujitupa kwa Allah (s.w) kwa toba ya kweli na kusubiri na sio kukata tamaa. Kwani pamoja na kukosea kwake, Allah (s.w) ameahidi kumsamehe kama tunavyojifunza katika Qur-an:

وَمَآ أَصَـٰبَكُم مِّن مُّصِيبَةٍ فَبِمَا كَسَبَتْ أَيْدِيكُمْ
وَيَعْفُوا۟ عَن كَثِيرٍ ﴿٣٠﴾

*Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya vitendo vya mikono yenu, na (juu ya hivi Mwenyezi Mungu) anasamehe mengi. (42:30).*

**6.Maombi na Dua**

Ni katika utamaduni wa Kiislamu Muislamu kumtegemea Allah (s.w) kwa kila jambo. Muislamu wa kweli anafahamu vyema kuwa mafanikio yote hutokana na Allah (s.w). Hivyo anapopatwa na tatizo lolote hana budi kwanza kabisa kumuelekea Mola wake na kumuomba msaada kabla hajamuelekea mtu yeyote kwa msaada. Hii ndio ahadi tunayoitoa kila mara tusomapo suratul-Fatiha:

إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥

*Wewe tu ndiye tunayekuabudu na wewe tu ndiye tunayekuomba msaada. (1:5).*

Hatuna budi kukumbuka kuwa matatizo na shida mbali mbali zinazotufika ni mtihani kwetu kuwa tutakuwa ni wenye kusubiri na kuomba msaada wa Allah (s.w) au tutapapatika na kutafuta misaada kwa wengine minghairi ya Allah (s.w). anatuita Allah (s.w) katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ ٱسۡتَعِينُواْ بِٱلصَّبۡرِ وَٱلصَّلَوٰةِۚ إِنَّ ٱللَّهَ

مَعَ ٱلصَّٰبِرِينَ ١٥٣

*Enyi mlioamini! Jisaidieni (katika mambo yenu) kwa subira na swala bila ya shaka Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaosubiri. (2:153).*

Pia Waislamu hatuna budi kuwa na hakika, mia kwa mia, kuwa Allah (s.w) ni muweza wa kila kitu na


69

halishindikani kwake jambo na kwamba ni mwenye kusikia maombi yetu na yukaribu zaidi kuliko tulivyo karibu na mshipa mkuu wa damu wa shingoni (jangular vain) mwetu:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِۦ نَفْسُهُۥ ۖ
وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ ٱلْوَرِيدِ ﴿١٦﴾

*Na bila shaka tumemuumba mtu nasi tunajua yanayopita katika nafsi yake, nasi tukokaribu naye zaidi kuliko mshipa wa shingo (yake). (50:16)*

Baada ya kuwa na uhakika wa namna hii hatuna budi kuyaelekeza maombi yetu moja kwa moja kwa Allah (s.w) kwa matumaini makubwa ya kupata kila tunachokiomba. Tunajifunza katika aya zifuatazo namna ya kumuomba Allah (s.w):

وَإِذَا سَأَلَكَ عِبَادِى عَنِّى فَإِنِّى قَرِيبٌ ۖ أُجِيبُ دَعْوَةَ
ٱلدَّاعِ إِذَا دَعَانِ ۖ فَلْيَسْتَجِيبُوا۟ لِى وَلْيُؤْمِنُوا۟ بِى لَعَلَّهُمْ
يَرْشُدُونَ ﴿١٨٦﴾

*Na waja wangu watakapokuuliza hakika yangu (waambie kuwa) mimi niko karibu nao. Naitikia maombi ya mwombaji anaponiomba. Basi na waniitikie na waniamini, ili wapate kuongoka. (2:186).*

ٱدْعُوا۟ رَبَّكُمْ تَضَرُّعًا وَخُفْيَةً ۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلْمُعْتَدِينَ

*Mwombeni Mola wenu kwa unyenyekevu na kwa siri (kwa suati ndogo bila ya kufanya kelele). Yeye (Mwenyezi Mungu) hawapendi wapitao mipaka(7:55).*

Katika aya hizi tunajifunza yafuatayo:

**Kwanza**, tunatakiwa tumuombe Allah (s.w) moja kwa moja bila ya kupitishia maombi yetu kwa yeyote yule na wala tusiombe kwa baraka za yoyote yule. Kumuomba Allah kwa baraka za yeyote au kupitia kwa yeyote ni kumdunisha Allah (s.w) na kukanusha Qur-an (2:186). Tunaamrishwa tumuombe Allah (s.w) na kwa baraka zake na majina yake matukufu:

وَلِلَّهِ ٱلۡأَسۡمَآءُ ٱلۡحُسۡنَىٰ فَٱدۡعُوهُ بِهَاۖ وَذَرُواْ ٱلَّذِينَ
يُلۡحِدُونَ فِيٓ أَسۡمَٰٓئِهِۦۚ سَيُجۡزَوۡنَ مَا كَانُواْ يَعۡمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

*Na Mwenyezi Mungu ana majina (sifa) mazuri mazuri, muombeni kwayo, na waacheni wale wanaoharibu utukufu wa majina yake. Karibuni hivi watalipwa yale waliyokuwa wakitenda. (7:180).*

**Pili**, tunatakiwa pia tumuombe Allah (s.w)a kwa unyenyekevu, na kwa siri sio kwa kupiga makelele. Ili tuwe wanyenyekevu kwa Allah (s.w) wakati wa kuomba hatuna budi kuomba kwa lugha tunayoifahamu vyema. Tukiwa ndani ya swala tutaomba kwa lugha ya Kiarabu lakini hatuna budi kufahamu tafsiri au maana ya yale tunayoyaomba.

**Tatu**, vile vile tunatakiwa wakati wa kumuomba Allah (s.w) tuwe na khofu kwa kuzingatia Hadhi yake na Utukufu wake na papo hapo tuwe na yakini kuwa ameyasikia maombi yetu na atatujibu kulingana na ahadi yake, kwani yeye ni muweza wa kutujibu na si mwenye kukhalifu miadi yake.

**Nne**, sharti kubwa tunalotakiwa tulitekeleze ili maombi yetu yajibiwe ni kumuitikia Allah (s.w). Kumuitikia Allah (s.w) ni kumuamini Allah (s.w) inavyostahiki na kumuabudu ipasavyo kwa kumtii kwa unyenyekevu katika kukiendea kila kipengele cha maisha yetu ya kila siku. Kuchunga mipaka yote ya Allah (s.w) kwa kutekeleza maamrisho yake yote na kujiepusha mbali na makatazo yake yote ni katika kumuitikia Allah (s.w). Hivyo ili yajibiwe maombi yetu mbali mbali tunayomuomba Allah (s.w), hatuna budi kujitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kufuata utaratibu wa maisha aliotufunulia Allah (s.w) katika kuendesha maisha yetu ya kila siku.

Waislamu hatupaswi kumuomba Allah (s.w) tukiwa na shida au tunapohitajia msaada tu wa maisha ya dunia, bali tunatakiwa tumuombe Allah (s.w) nyakati zote, tukiwa katika furaha au tukiwa katika matatizo. Tukiwa katika furaha tunatakiwa tumuombe Allah (s.w) aijaalie furaha hiyo iwe yenye kheri. Tukiwa katika matatizo tunamuomba Allah (s.w) atuondolee matatizo hayo na atulipe ujira mwema kutokana na kusubiri kwetu juu ya matatizo hayo na iwe ni sababu ya kutusamehe makosa yetu. Kwa mtazamo huu Muislamu katika nyakati zote na katika hali zote yuko katika Ibada ya Allah (s.w) na hupata thawabu (ujira mwema mbele ya Allah (s.w)) akiwa katika dhiki au katika furaha. Kwa ujumla tunatakiwa katika maombi yetu, tumuombe Allah (s.w) atupe mema ya hapa duniani na huko akhera na atuondolee dhiki ya hapa duniani na adhabu kali ya huko akhera.

رَبَّنَآ ءَاتِنَا فِى ٱلدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِى ٱلْءَاخِرَةِ حَسَنَةً وَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿٢٠١﴾

*Mola wetu! Tupe mema duniani na (tupe) mema akhera, na utulinde na dhabu ya moto. (2:201)*

Dua mashuhuri ambazo tunaweza kuzitumia katika kumuomba Allah (s.w) ni zile zilizoombwa na waja wake mbali mbali kama zilivyobainishwa katika Qur-an na zile alizozitumia Mtume Muhammad (s.a.w) katika kumuomba Mola wake katika hali na nyakati mbali mbali kama zinavyobainika katika Hadith mbali mbali. Hapa tumejaribu kubainisha aya za Qur-an mnamopatikana dua mbali mbali walizoomba waja wa Allah (s.w).

Dua ya Adam (a.s) na Hawa ya kuomba msamaha baada ya kumkosea Mola wao kwa kula tunda walilokatazwa: (7:23)

Dua alizoomba Nabii Nuhu (a.s):
*(23:26), (26:117-118), (54:10), (71:26-28), (11:41), (11:45), (11:47), (23:29).*

Dua ya Nabii Swaleh (a.s): (23:39)

Maombi ya Nabii Ibrahim (a.s)
*(2:126-129), (14:35-41), (26:83-89), (37:99-100), (60:4-5).*

Maombi ya Nabii Lut (a.s):
*(26:169), (29:26), (29:30).*

Maombi ya Nabii Ayyub (a.s)
(21:83), (38:41).

Maombi ya Nabii Yusuf (a.s)
(12:33), (12:101).

Dua ya Nabii Shuayb (a.s)
(7:89).
Maombi ya Nabii Mussa (a.s)
*(28:16), (28:17), (28:21), (28:24), (7:148), (20:25-35), (7:151), (10:88), (7:155-156), (2:67), (5:25).*

Maombi ya wafuasi wa Nabii Mussa (a.s):
(10:85-86), (7:126).

Dua ya Bi Asia, Mkewe Firaun: (66:11).

Maombi ya watu wa Talut wakati walipokuwa wakipambana na Jaluti (Mfalme wa Maadui): (2:250).

Dua ya Nabii Sulaiman (a.s): (27:19), (38:35).

Dua ya Malkia wa Sheba – Bibi Bilqis: (27:44).

Dua ya Nabii Yunus (a.s) - (21:87).

Maombi ya Nabii Zakaria (a.s) – Mlezi wa Bibi Mariam:
(3:38), (19:4-6), (21:89).

Maombi ya Hannah – Mama wa Bibi Maryam – (3:35-36).

Maombi ya wafuasi wa Nabii Issa (a.s): (3:53).

Dua ya Vijana wa pangoni: (18:10).

Dua ya mwenye Bustani: (68:29).

Dua ya Mume na mke kabla ya mtoto kuzaliwa – (7:189).

Dua za Malaika: (11:73), (40:7-9).

Dua ya watu wema: (7:47)

Dua za Mtume Muhammad (s.a.w) na wafuasi wake:

*(1:1-7), (2:156), (2:201), (2:286), (3:8-9), (3:16), (3:26-27), (3:191-194), (4:45), (5:83), (6:161-163), (9:59), (17:24), (20:114), (21:112), (23:93-94), (23:97-98), (23:109), (23:118), (25:65-66), (25:74), (39:46), (46:15), (59:10), (66:8), (113:1-5), (114:1-6).*

### (vii) Kumkumbuka Allah (s.w) Saa 24

Kumkumbuka Allah (s.w) muda wote wa maisha ndio lengo lililombele ya kila Muislamu wa kweli.Lengo la kuletwa kwetu hapa ulimwenguni ni kumuabudu Allah (s.w), yaani kumtumikia Allah (s.w) kwa unyenyekevu kwa muda wote wa maisha yetu. Kumtumikia Allah (s.w) kwa muda wote wa maisha yetu kunawezekana tu endeapo tutaendesha maisha yetu yote ya saa 24 kwa kuchunga barabara mipaka ya Allah (s.w) aliyotuwekea katika kukiendea kila kipengele cha maisha yetu katika kila fani ya mtu binafsi, familia, uchumi, siasa, utamaduni, sheria na fani nyinginezo za maisha ya jamii. Kuchunga mipaka ya Allah (s.w) kwa muda wote wa saa 24 katika kila kipengele na kila fani ya maisha ni jambo linalowezekana pale Muislamu atakapoibakisha akilini mwake kumbukumbu ya Allah (s.w) kila wakati.Ni vipi Muislamu ataweza kumkumbuka Allah (s.w) kila wakati?

**Kwanza**, Muislamu ataweza kumbukumbuka Allah (s.w) na utukufu wake kila wakati, endapo kila mara atazichunguza neema zote zilizomzunguka alizotunukiwa na Mola wake kisha akawa ni mwenye shukurani kwake kwa kumtii na kumtukuza ipasavyo. Pia Muislamu atazidi kukuza yakini juu ya uwezo na utukufu wa Allah (s.w) endapo atatafakari kwa makini umbile la mbingu na ardhi na vyote vilivyomo. Allah (s.w) anatuhakikishia kuwa watu wenye kushukuru neema zake na kutumia akili zao vilivyo katika kutafakari maumbile yaliyowazunguka ndio pekee wanaoweza kumkumbuka na kuuona utukufu wake kwa muda wote wa saa 24.

إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفِ
ٱلَّيْلِ وَٱلنَّهَارِ لَءَايَٰتٍ لِّأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٠﴾

*Katika kuumbwa kwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana, ziko hoja (za kuonyesha kuwepo Allah (s.w) na utukufu wake) kwa wenye akili.(3:190)*

ٱلَّذِينَ يَذْكُرُونَ ٱللَّهَ قِيَـٰمًا وَقُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِهِمْ
وَيَتَفَكَّرُونَ فِى خَلْقِ ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ رَبَّنَا مَا
خَلَقْتَ هَـٰذَا بَـٰطِلًا سُبْحَـٰنَكَ فَقِنَا عَذَابَ ٱلنَّارِ ﴿١٩١﴾

*Ambao humkumbuka Mwenyezi Mungu wakiwa wima, na wakiwa wamekaa na wakiwa wamelala.Na hutafakari juu ya umbile la mbingu na ardhi (kisha husema): Mola wetu! Hukuviumba hivi bure. Utukufu ni wako. Basi tuepushe na adhabu ya moto. (3:191).*

**Pili**, Muislamu ataweza kubakia katika kumkumbuka Allah (s.w) endapo atajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kusimamisha swala tano za faradhi kama ipasavyo na pia akajitahidi kwa kadri iwezekanavyo kufuatilizia swala za Sunnah na hasa zile zilizokokotezwa. Kazi ya swala iliyosimamishwa vilivyo katika kumuwezesha Muislamu aweze kumkumbuka Mola wake kwa nyakati zote imebainishwa wazi katika aya ifuatayo:

ٱتْلُ مَآ أُوحِىَ إِلَيْكَ مِنَ ٱلْكِتَـٰبِ وَأَقِمِ ٱلصَّلَوٰةَ ۖ
إِنَّ ٱلصَّلَوٰةَ تَنْهَىٰ عَنِ ٱلْفَحْشَآءِ وَٱلْمُنكَرِ ۗ وَلَذِكْرُ ٱللَّهِ
أَكْبَرُ ۗ وَٱللَّهُ يَعْلَمُ مَا تَصْنَعُونَ ﴿٤٥﴾

*Soma uliyoletewa wahyi katika kitabu (hiki ulicholetewa) na usimamishe swala. Bila shaka swala (ikiswaliwa vilivyo) humzuilia (huyo mwenye kuswali na) mambo machafu na maovu, na kwa yakini (ndani ya swala) kuna kumkumbuka Mwenyezi Mungu kukubwa. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayotenda. (29:45).*

**Tatu**, Muislamu ataweza kubakia katika kumkumbuka Allah (s.w) nyakati zote iwapo atajitahidi kwa kadri ya uwezo wake kutekeleza nguzo ya Zakat na kuwa mwepesi wa kutoa mali yake na kujitolea nafsi yake kwa ajili ya Allah (s.w) katika kusaidia na kutoa huduma mbali mbali za kijamii.

Pia Muislamu atabakia katika kumkumbuka Allah s.w) na utukufu wake kila wakati endapo atakamilisha nguzo ya funga ya Ramadhani na kuiambatanisha na funga za Sunnah kwa kadri ya uwezo wake kisha akatekeleza nguzo ya Hija iwapo anauwezo. Tukumbuke kuwa, lengo la nguzo tano za Uislamu ni kumtayarisha mja aweze kumtumikia Mola wake ipasavyo katika kila kipengele cha maisha yake.

**Nne**, kumsafia nia Allah (s.w) na kumtanguliza katika kila kitendo tunachokifanya. Kabla hatujafanya kitendo chochote kile hatuna budi kukichunguza kitendo hicho kuwa kitatupelekea kupata radhi za Allah (s.w) au ghadhabu zake. Endapo kitendo hicho ni chema na chenye kutupelekea kupata radhi za Allah (s.w) tukifanye. Endapo kitendo hicho chema kitawaudhi makafiri, washirikina, wanafiki na maadui wengine wa Allah (s.w) tusisite kukifanya maadam matarajio yetu ni radhi za Allah (s.w) tu. Endapo kitendo hicho ni kiovu na chenye kutupelekea kughadhibikiwa na Allah (s.w) tukiache na kujiepusha mbali nacho hata kama kufanya hivyo kutawakasirisha walimwengu wote. Hii ndiyo tabia ya Waislamu wa kweli kama inavyobainishwa katika aya zifuatazo:

مَن جَآءَ بِٱلْحَسَنَةِ فَلَهُۥ عَشْرُ أَمْثَالِهَا ۖ وَمَن جَآءَ
بِٱلسَّيِّئَةِ فَلَا يُجْزَىٰٓ إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿١٦٠﴾

*Afanyaye kitendo kizuri (kila kitendo kilichofanywa kwa ajili ya Allah ni kitendo kizuri) atalipwa (mbele ya Allah ) mfano wake mara kumi. Na afanyaye kitendo kibaya hatalipwa ila sawa nacho tu. Nao (wote hao) hawata dhulumiwa.(6:160)*

قُلْ إِنَّنِى هَدَىٰنِى رَبِّىٓ إِلَىٰ صِرَٰطٍ مُّسْتَقِيمٍ دِينًا قِيَمًا مِّلَّةَ
إِبْرَٰهِيمَ حَنِيفًا ۚ وَمَا كَانَ مِنَ ٱلْمُشْرِكِينَ ﴿١٦١﴾

*Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu ameniongoza katika njia iliyonyooka, (katika) dini iliyosawa sawa kabisa ambayo ndiyo dini ya Ibrahim aliyekuwa mwongofu, wala kabisa hakuwa miongoni mwa washirikina. (6:161)*

قُلْ إِنَّ صَلَاتِى وَنُسُكِى وَمَحْيَاىَ وَمَمَاتِى لِلَّهِ
رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿١٦٢﴾

*Sema: Hakika swala yangu, matendo yangu yote mengine, na uzima wangu, na kufa kwangu (yote) ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Muumba Mlezi wa walimwengu wote.(6:162)*

لَا شَرِيكَ لَهُۥ ۖ وَبِذَٰلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَا۠ أَوَّلُ ٱلْمُسْلِمِينَ ﴿١٦٣﴾

*Na haya ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha kwa Mwenyezi Mungu (6:163).*

Tunajifunza katika aya hizi kuwa jambo lolote atakalolifanya Muislamu kwa ajili ya Allah (s.w) ni jambo jema (amali swalihi), na kila jambo jema analolifanya mja hulipwa ujira mwema (thawabu) kutokana na kitendo hicho mara kumi. Tunahimizwa kuwa katika Ibada ya Allah (s.w) katika kila kitendo chetu. Muda tutakao kuwa nje ya Ibada ya Allah (s.w) tutakuwa katika Ibada (utumishi wa) ya wengine minghairi ya Allah (s.w) na bila shaka wakati huo tutakuwa ni washirikina. Jambo lingine ambalo ni la msaada kwetu litakalotupelekea kuyafanya matendo yetu yote yawe Ibada ni kuanza kila jambo kwa jina la Allah, yaani kuanza kila jambo kwa *"Bismillahir Rahmaanir Rahiim – "Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema Mwenye kurehemu*". Muislamu anatakiwa ajenge tabia ya kuanza kila jambo jema kwa "*Bismillah*". Miongoni mwa faida kubwa zinazopatikana kwa Muislamu kwa kuanza kila jambo lake kwa *"Bismillahir Rahmaanir Rahiim"* huku akiwa anazingatia maana yake ni hizi zifuatazo:

(1) Mtu anapoanza na "*Bismillah*" anatanguliza maombi yake ya kutaka msaada wa Allah (s.w), ili alifanikishe jambo hilo analotaka kulifanya kwa ajili yake.

(2) Kuanza kila jambo kwa "*Bismillah*" kutamkinga kufanya mambo machafu na maovu kwani kama ni Muislamu wa kweli atamuonea haya Allah (s.w) na hatathubutu kufanya jambo ovu kwa jina lake.

(3) Kitendo cha kuanza kwa "*Bismillah*" ni kitendo kinachompelekea Muislamu kuwa hadhiri na kile anachoanza kukifanya na humkumbusha kutia nia yake ya kufanya kitendo hicho kwa ajili tu ya kutafuta radhi za Allah (s.w).

## Zoezi la Pili

1. (a) Eleza maana ya utamaduni
    (b) Msingi wa Utamaduni wa Kiislamu ni Mila ya nani?

2. Kwanini ni muhimu kwa jamii kufuata Mila ya nabii Ibrahiim (a.s)

3. Orodhesha masharti ya vazi la Kiislamu

4. Taja mambo manne muhimu ambayo Qur'an inamtaka kila Muislamu ayazingatie katika kula na kunywa.

5. Orodhesha
    (a) Vyakula vilivyoharamishwa kwa Muislamu.
    (b) Vinywaji vilivyoharamishwa kwa Muislamu.

6. Eleza kwa muhtasari adabu anazotakiwa kuzitekeleza Muislamu katika kula.

7. (a) Michezo ina umuhimu gani kwa Muislamu.
    (b) Ni michezo ipi isiyoruhusiwa kwa Waislamu, na kwanini?

8. Taja mambo ya Msingi yanayohitajika kuyafanya na kuyasimamia ili sherehe na burdani za Waislamu zisikiuke Qur'an na Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w), kama zilivyo sherehe na burdani za wasiokuwa Waislamu.

9. Muislamu anapofikwa na msiba, anatafautianaje na asiyekuwa Muislamu katika kuomboleza?

10. Soma kwa makini sura 3:190-192. Kisha onesha vipengele na mkakati wa namna ya kutekeleza maudhui yake, na ushikamane nayo kila siku.

## Sura ya Tatu

## SHERIA

### Maana ya sheria

Katika lugha ya Kiarabu, neno Shariah lina maana ya njia ya kufuatwa. Kiistilahi neno sheria linakusanya katika maana yake, taratibu, sharti, kanuni (principles) na amri (rules) ambazo huwekwa ili kuongoza mahusiano ya watu katika jamii inayohusika.

Sheria ni fani muhimu mno katika maisha ya jamii. Haijatokea jamii yoyote ile katika kipindi cha historia ya mwanaadamu isiyo na sheria. Kazi ya sheria ni kuiweka jamii katika nidhamu na kulinda haki za raia ili ipatikane furaha na amani katika jamii hiyo.

Sheria ni kanuni au amri ambazo si tu hupasa kutiiwa, bali pia zinapovunjwa, mvunjaji hudhibitiwa baada ya kugundulika na kuadhibiwa na vyombo vinavyohusika na usimamiaji wa hiyo sheria. Kwahiyo, ili pawepo na sheria ni lazima pia pawepo na vyombo vyenye mamlaka na nguvu ya kusimamia ili kuhakikisha kuwa hiyo sheria inafuatwa na iwapo itavunjwa basi hatua zitachukuliwa dhidi ya mvunjaji.

### Kazi ya Sheria katika Jamii

**Kwanza** sheria humlinda binaadamu binafsi dhidi ya madhara mbali mbali yanayoweza kusababishwa na mwenendo wake mbaya. Kwa mfano sheria ya kulazimishwa watu kufanya kazi ina lengo la kuwaepusha watu na umaskini wa kujitakia. Sheria ya kumkataza mtu kuvuta bangi na kutumia madawa ya kulevya ina lengo la kulinda afya yake. Sheria ya barabarani ina lengo la

kumuepusha mtu na ajali. Uzoefu unaonesha kuwa sheria zinapokuwa madhubuti mwenendo na hulka ya watu hubadilika na hivyo hujiepusha na maovu.

**Pili**, sheria hulinda watu na mali zao. Kwa mfano sheria zinazokataza kuua (bila ya sababu inayokubalika kisheria), kumjeruhi mtu, kuiba, kunyang'anya, kulaghai, kupunja vipimo, n.k. ziko pale ili kulinda uhai na mali za watu. Bila ya kuwepo sheria kama hizi watu watadhulumiana na kuliana mali kwa batili.

**Tatu**, sheria ni muhimu ili kuhifadhi amani na usalama katika jamii, ili jamii iweze kuishi bila ya migongano na vurugu. Bila ya kuwepo amani na usalama jamii haiwezi kupiga hatua za kimaendeleo bali maisha hujaa hofu na vitisho.

**Nne**, sheria huhifadhi maadili ya jamii. Inafahamika kuwa maadili ni moja ya misingi mikuu ya mwenendo wa jamii. Hivyo moja ya malengo makuu ya sheria kwa kawaida huwa ni kulinda maadili ili kuhakikisha kuwa jamii inaendeshwa katika mwenendo mwema.

**Tano**, sheria inapanga utaratibu juu ya namna ya kuendesha shughuli mbali mbali zenye maingiliano ya kijamii. Mfano sheria ya ujenzi wa makazi mijini, matumizi ya barabara, taratibu za uendeshaji serikali na vyombo vyake, uendeshaji wa masoko, uendeshaji wa biashara, utunzaji wa mazingira, ulinzi na usalama wa raia na taifa, n.k.

Kwa ujumla, kazi kuu ya sheria ni kuiweka jamii katika nidhamu na kulinda haki za raia ili ipatikane amani na furaha katika maisha ya mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Pamoja na ukweli huu, swali linakuja: "kama kazi ya sheria nikuiweka jamii katika nidhamu na kuleta furaha

na amani, mbona hivi leo, pamoja na jamii za kitaifa na kimataifa kujiwekea sheria, hatuoni dalili ya furaha na amani isipokuwa vurugu, vita, mauaji ya halaiki, ukandamizaji na unyanyasaji wa kila aina?”

Hatuna budi kufahamu kuwa si kila sheria ya jamii inaleta furaha na amani kwa raia wote. Sheria nyingi zilizotungwa na wanaadamu zina udhaifu mkubwa kama tutakavyoona. Kwa hiyo pamoja na nia njema inayokuwepo wakati wa kuzitunga, katika matumizi yake hazifikii kabisa lengo linalokusudiwa. Ni sheria za Allah (s.w) pekee zinazoweza kuiweka jamii ya mwanaadamu katika nidhamu inayotakikana na kuiwezesha kuishi kwa furaha na amani. Sheria ya Kiislamu inaweza kuifikisha jamii kwenye lengo hilo kwa kuwa imewekwa na Muumba mwenyewe ambaye anamjua vyema mwanaadamu, matashi yake, matatizo yake, ujanja wake na udhaifu wake kwa ujumla kama Qur-an inavyotutanabahisha:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا ٱلْإِنسَـٰنَ وَنَعْلَمُ مَا تُوَسْوِسُ بِهِۦ نَفْسُهُۥ ۖ
وَنَحْنُ أَقْرَبُ إِلَيْهِ مِنْ حَبْلِ ٱلْوَرِيدِ ﴿١٦﴾

*Bila shaka tumemuumba mtu, nasi tunajua yanayopita katika nafsi yake; nasi tu karibu naye zaidi; kuliko mshipa wa shingo (yake).” (50:16)*

**Chimbuko la sheria za Kitwaghuti**

Chimbuko la sheria zilizotungwa na wanaadamu ni vipawa vya wanaadamu vya kufikiri na kuhoji (reason) na mila na desturi zilizozoeleka. Hivyo sheria hizo ni zao la akili ya mwanaadamu na mazingira yake. Hata hivyo, pamoja na kuwa vipawa hivyo vya kuhoji, miiko na desturi hizo ni nyenzo za muhimu, lakini zenyewe tu bila ya ufunuo (revelation) kutoka kwa Mwenyezi Mungu hutoa ujumbe wa kubahatisha na usio na uhakika wa kudumu. Hata

hivyo wale wakanao ufunuo hushikilia kuwa ndizo chemchem za hakika katika utunzi wa sheria na kanuni mbali mbali. Kwa jitihada hizo za akili (bila ya ufunuo), jamii, nchi na mataifa yote ya kitwaghuti hujitungia sheria mbali mbali ambazo nazo hutokana na chimbuko kuu, ambalo ni Katiba. Katiba za nchi ndizo msingi wa sheria zote.

**Udhaifu wa sheria zilizotungwa na binadamu**

Ni wazi kuwa kutumia akili na kufikiri ni jambo muhimu sana kwa mwanaadamu, lakini je akili ya mwanaadamu au fikra zinaweza kutoa sheria ambazo ndio mwongozo wa maisha? Wanaadamu hutofautiana sana katika kufikiri na huathiriwa sana na mazingira, wakati na matashi. Ni nani mwenye fikra za kutoa sheria sahihi zenye kuweza kuwaongoza wanaadamu hapa ulimwenguni zisizoathiriwa na mazingira yake; wakati na matashi yake. Ukweli ni kwamba uamuzi unaotokana na fikra ya mwanaadamu hutegemea mazingira yake ambayo yako katika upeo wa milango ya fahamu ambayo tayari ina udhaifu mkubwa. Kama taarifa iliyopatikana kutokana na milango ya fahamu itakuwa na kasoro, pia uamuzi utakaotegemea taarifa hiyo nao utakuwa na kasoro.

Hali kadhalika, ujuzi na uwezo wa kufahamu wa mwanaadamu haumtoshi kuweza kuyazingatia mazingira yote yanayopasa kuzingatiwa katika kumpangia mwanaadamu sheria, au utaratibu unaofaa wa maisha. Watafiti wa mambo ya uwezo wa akili ya mwanaadamu wameonesha kuwa akili ya binaadamu siku zote uwezo wake umefungika katika mazingira aliyomo na upeo wa maendeleo ya sayansi ambao jamii yake imeufikia. Ni ukweli unaokubaliwa na watu wote kuwa, mambo yote anayoyajua mwanaadamu kuhusu nafsi na mwili wake yeye mwenyewe na kuhusu mazingira yake ni machache ikilinganishwa na yale yote anayohitajia kuyajua ili kujitosheleza katika ujuzi alionao.

Udhaifu huu umepelekea mwanaadamu kutegemea zaidi dhana na ujuzi usiotosheleza katika kutoa maamuzi ya lipi baya na lipi zuri. Hii imepelekea mwanaadamu kujipangia taratibu zisizomfaa kwa dhana ya kuwa hizo ndizo zifaazo.Hivyo, mara nyingi hata mwanaadamu anapokusudia kujipangia taratibu nzuri zifaazo ameishia

kutunga sheria zisizofaa, na pengine zenye madhara kwake mwenyewe.Hii ndio imekuwa moja ya sababu kubwa za kubadilishwa mara kwa mara kwa sheria za kutungwa na mwanaadamu. Ukizichambua vyema sheria hizo utakuta kuwa mara nyingi badala ya kutimiza malengo ya kuwepo kwake katika jamii, zenyewe huenda kinyume chake. Matokeo yake, kwa mfano badala ya kumkinga mwanaadamu na maovu na madhara yake, zenyewe huyachochea. Na badala ya kulinda maadili zenyewe husaidia kuyabomoa. Na huchochea dhulma badala ya kuzuia. Bali katika jamii nyingine, sheria huwa ndio chimbuko la ukandamizaji na uonevu wa kila hali.

Sheria kama zile zinazounga mkono mifumo ya utumwa katika jamii, ubaguzi wa rangi n.k., ni mifano ya udhaifu mwingi uliopo katika mifumo ya sheria zilizotungwa na binaadamu.

Jambo lingine ni kuwa, moyo wa mwanadamu nao umetawaliwa na matashi ambayo mara nyingi huwapelekea watungaji wa sheria wasiofuata mwongozo wa Muumba kujipendelea katika sheria wanazozitunga. Hili linadhihiri katika kila kaumu ya watu wafuatao sheria zilizowekwa na wanaadamu.

Mfano wakati wa Firauni yeye mwenyewe alijikweza na kujifanya Mungu. Sheria ziliwapendelea na kuwakweza jamaa na watu wa kabila lake (yaani Wamisri):

إِنَّ فِرْعَوْنَ عَلَا فِي ٱلْأَرْضِ وَجَعَلَ أَهْلَهَا شِيَعًا يَسْتَضْعِفُ طَآئِفَةً مِّنْهُمْ يُذَبِّحُ أَبْنَآءَهُمْ وَيَسْتَحْيِۦ نِسَآءَهُمْ ۚ إِنَّهُۥ كَانَ مِنَ ٱلْمُفْسِدِينَ ﴿٤﴾

*"Hakika Firauni alitakabari (alijitukuza) katika ardhi na akawafanya watu wa huko makundi mbali mbali. Akalidhoofisha kundi moja miongoni mwao, akiwachinja watoto wao wanaume na kuwawacha hai watoto wao wanawake.Hakika yeye alikuwa miongoni mwa waharibifu (kabisa)." (28:4).*

Mifano ya namna hii ni mingi. Wagiriki wa zamani pamoja na kusifiwa kwao kuwa chimbuko la dhana ya demokrasia na falsafa za kuigwa za kina Socrates, Plato, Aristotle n.k, walijitungia sheria zilizowagawa watu kati ya mabwana na watumwa. Katika jamii hiyo, watumwa, wanawake na wale ambao hawakuwa wazawa walikuwa hawana haki yoyote, na zaidi watumwa walikuwa ni sawa na bidhaa zinazoweza kuuzwa na kununuliwa, bali hata na kuuawa na mabwana zao kama njia ya kujifurahisha!

Katika wakati huu tulionao pia udhaifu huu wa matashi ya watu umetawala utunzi wa sheria. Katika sheria za kimataifa, mataifa makubwa ya Ulaya na Marekani yamelaumiwa kwa kujipendelea. Huko Marekani, watu weusi wanakandamizwa na kubanwa sana. Hivyo sheria zilizotungwa na mwanaadamu mara nyingi haziafikiani na misingi ya haki na usawa.

Pia mara nyingi sheria hizo hushindwa kuyazingatia na kuyasimamia sawasawa maslahi ya kweli ya mwanaadamu. Hii inatokana na zile sifa za udhaifu alizonazo huyo mwanaadamu mwenye kuzitunga hizo sheria. Sifa zile tulizo zitaja juu pamoja na nyingine nyingi kama vile za uongo, wivu, husuda, hila na ulaghai, ubinafsi, uchoyo, hasira, kiburi, n.k., pamoja na ile sifa ya ufinyu na uwezo wa kujua mambo. Ni kwa msingi huu Allah (s.w) ametutanabahisha:

وَإِن تُطِعْ أَكْثَرَ مَن فِى ٱلْأَرْضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِ ۚ إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّ وَإِنْ هُمْ إِلَّا يَخْرُصُونَ ﴿١١٦﴾

*"Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu hawafuati ila dhana tu na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi)." (6:116)*

Hivyo ni makosa makubwa akili ya mwanaadamu kubeba dhima ya utunzi wa sheria. Matokeo yake, badala ya sheria hizo kutimiza malengo ya kuwepo kwake katika jamii, zinakiuka na kuchochea madhara. Haweki haki na uadilifu, ila dhuluma. Na kwahivyo sheria huwa ndio chimbuko la ukandamizaji na uonevu wa kila namna. Sheria kama zile zinazoruhusu ulevi, uzinifu, utumwa, ubaguzi wa rangi, ukoloni , riba, kamari (n.k.) ni mifano ya udhaifu mwingi uliopo katika mifumo ya sheria zilizotungwa na mwanaadamu.

Matokeo ya sheria hizo kuyaruhusu mambo hayo imekuwa ni ya maafa na maangamizi makubwa kwa watu wa dunia nzima. Ulevi umekuwa ndio sababu inayoongoza kwa kusababisha maafa ya ajali barabar ani na matatizo mengi ya kiafya. Zinaa imesababisha magonjwa mbali mbali kama vile Kaswende, Kisonono na Ukimwi. Riba na Kamari navyo vimekuwa ndio sababu kubwa ya umaskini katika nchi za ulimwengu wa tatu. Sehemu kubwa ya mzigo wa madeni ya mataifa maskini inatokana na riba. Na hali ya uchumi ilivyo kwa sasa ni kuwa nchi maskini kamwe hazitaweza kujivua mzigo wa madeni ambayo huongezeka siku zote kutokana na kukua kwa riba. Kwa ujumla sheria zilizotungwa na mwanaadamu zimeshindwa

kabisa kuiongoza jamii katika misingi ya haki na usawa.

**Udhaifu katika Usimamizi wa sheria za kitwaghuti**

Pamoja na udhaifu katika utunzi wa sheria, upo pia udhaifu katika usimamiaji wa sheria hizo. Hii inatokana na ukweli kwamba kila anachoweza kukipanga mwanaadamu, mwanaadamu anaweza kukipangua. Sheria zilizotungwa na binaadamu hazimjengei mja ile fikra muhimu sana ya utii kwa yule aliyemwekea sheria, mwenye uwezo wa kubaini pindi tu mja huyo atakapozikiuka. Vile vile watunzi wa sheria hujiweka juu ya sheria daraja ambayo mwanaadamu hastahiki kuwa nayo.

Sheria za kibinaadamu pamoja na kuwepo vyombo vya dola vya kusimamia kama vile polisi, vikosi vya kuzuia fujo, kamisheni za kuzuia rushwa, magereza, idara za usalama wa taifa, na kadhalika, bado inashindikana kuhakikisha kuwa zinatekelezwa. Sababu ni kuwa ni vigumu binaadamu kumchunga binaadamu mwenzake kama awezavyo kumchunga mbuzi au kondoo. Ni rahisi mwanaadamu kujificha mwanaadamu mwenzake asimuone, na hivyo kufanya maovu bila taabu. Pia wakiukaji sheria waweza kushirikiana na wasimamizi wake kwa kutumia rushwa, udugu, ukabila, urafiki na kadhalika.

**Chimbuko la Sheria ya Kiislamu**

Msingi wa kwanza wa sheria ya Kiislamu ni Qur-an. Qur-an ni mwongozo utokao moja kwa moja kwa Allah (s.w) kupitia kwa Mtume Muhammad (s.a.w). Allah (s.w) ndiye Muumba wa binaadamu na vyote vilivyomzunguka katika mbingu na ardhi. Amekiumba kila kitu kwa lengo na Ndiye pekee Mwenye kustahiki kutoa mwongozo, kuweka taratibu, na kanuni zitakazokiwezesha kila kiumbe kuwa na nidhamu itakayokipelekea kufikia lengo lake.

Hivyo, Allah (s.w) ndiye chimbuko la sheria zote zinazomiliki maumbile yake (natural laws) zinazoyawezesha maumbile hayo yabakie katika nidhamu inayoyawezesha kufikia lengo lake. Pia Allah (s.w) ndiye pekee anayestahiki kumuwekea binaadamu sheria (social laws) itakayomuwezesha kuwa na nidhamu itakayompelekea kuishi kama mja na khalifa wa Allah (s.w) hapa ulimwenguni.

Msingi wa pili wa sheria ya Kiislamu ni Sunnah ya Mtume Muhammad (s.a.w) Mtume Muhammad (s.a.w) pamoja na Mitume wengine, wameteuliwa na Allah (s.w) ili kuwa Waalimu katika jamii zao wanaoupokea na kuufundisha ujumbe kutoka kwa Allah (s.w) kinadharia na kimatendo. Si ujumbe wote kutoka kwa Allah (s.w) kupitia kwa mitume ulioandikwa na kuhifadhiwa katika vitabu vyake bali sehemu kubwa ya ujumbe wa Allah (s.w) unadhihiri katika maelekezo na utendaji wa Mitume kama Qur-an inavyotuthibitishia juu ya Mtume (s.a.w):

وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ۝٣ إِنْ هُوَ إِلَّا وَحْىٌ يُوحَىٰ ۝٤

*Wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi yake). Hayakuwa haya (anayosema) ila ni wahyi uliofunuliwa (kwake).(53:3-4)*

Hivyo ni wajibu kwa Waislamu kumtii Mtume (s.a.w) kwa kufuata vilivyo mafundisho yake na kumuigiza tabia yake.

**Vyanzo vingine vya sheria ya Kiislamu**

Tumeona kuwa vyanzo vikuu vya sheria ya Kiislamu ni Qur-an na Sunnah. Vyanzo vya aina ya pili vya sheria ya Kiislamu ni vile vinavyopatikana kwa kutumia vigezo vya Qur-an na Sunnah. Vyanzo hivi ni Al-Ijmaa, Al-Qiyaas na Al-Ijtihaad.

**Al-Ijmaa'**

Al-Ijmaa ni makubaliano ya kongamano la wanazuoni (shura ya wataalamu) wa jamii, baada ya kufariki Mtume (s.a.w). Makubaliano hayo yanafikiwa kwa kuzingatia mipaka ya Qur-an na Sunnah na maslahi ya jamii. Ijmaa, haitakubalika pale itakapokwenda kinyume na Qur-an na Sunnah. Allah (s.w) mwenyewe anatuhimiza kushauriana katika mambo mbali mbali ambayo hatuyapati moja kwa moja kutoka kwake katika aya zifuatazo:

فَبِمَا رَحْمَةٍ مِّنَ ٱللَّهِ لِنتَ لَهُمْۖ وَلَوْ كُنتَ فَظًّا غَلِيظَ
ٱلْقَلْبِ لَٱنفَضُّواْ مِنْ حَوْلِكَۖ فَٱعْفُ عَنْهُمْ وَٱسْتَغْفِرْ لَهُمْ
وَشَاوِرْهُمْ فِى ٱلْأَمْرِۖ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِۚ إِنَّ
ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلْمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

*Basi kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao (Ewe Muhammad). Na kama ungekuwa mkali na mwenye moyo mgumu bila shaka wangalikukimbia. Basi wasamehe wewe na uwaombee msamaha (kwa Mwenyezi Mungu) na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (tu ufanye hili uliloazimia). Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao. (3:159)*

وَٱلَّذِينَ ٱسْتَجَابُواْ لِرَبِّهِمْ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَمْرُهُمْ
شُورَىٰ بَيْنَهُمْ وَمِمَّا رَزَقْنَٰهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri Zake) na wakasimamisha Sala, na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38)*

Pia Ijmaa inasisitizwa katika aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ
ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ فَإِن تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي
شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمۡ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ
وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِۚ ذَٰلِكَ خَيۡرٞ وَأَحۡسَنُ تَأۡوِيلًا ٥٩

*Enyi mlioamini! Mtiini Allah na mtiini mtume na wenye mamlaka juu yenu walio katika nyie. Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Allah na Mtume wake ikiwa mnamwamini Allah na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo heri nayo ina matokeo bora kabisa. (4:59)*

وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِنۢ بَعۡدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ ٱلۡهُدَىٰ
وَيَتَّبِعۡ غَيۡرَ سَبِيلِ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ نُوَلِّهِۦ مَا تَوَلَّىٰ وَنُصۡلِهِۦ
جَهَنَّمَۖ وَسَآءَتۡ مَصِيرًا ١١٥

*Na atakayemuasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya Waislamu, tutamgeuza aliko geukia mwenyewe na tutamwingiza katika Jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia." (4:115)*

Aya hizi zinasisitiza kuwa shura ya wataalamu na viongozi wa jamii ya Kiislamu itakapopitisha maamuzi ambayo hayapingani na Qur-an na Sunnah, Waislamu wanalazimika kutii vinginevyo watakuwa wamemuasi Allah (s.w) na Mtume wake.

Naye Mtume (s.a.w) katika kusisitiza Ijmaa, amesema katika Hadith:

*"Watu wangu (waumini wa kweli wa umma wake) hawatakubaliana na yeyote anayewapoteza na njia ya haki"*

Mifano mingi ya Ijmaa inapatikana katika kipindi cha Maswahaba, baada ya kufariki Mtume (s.a.w). Kwa mfano, katika Qur-an na katika Sunnah ya Mtume (s.a.w), adhabu ya mlevi haikubainishwa. Lakini shura ya maswahaba ilikaa na kuweka adhabu ya viboko thamanini kwa mlevi kutokana na ushauri 'Ali bin Abuu Taalib aliyesema: "Anayekunywa pombe analewa; mlevi huongea ovyo (kama kichaa); anayeongea ovyo huwazulia watu uovu; na anayewazulia watu uovu adhabu yake ni viboko thamanini kwa mujibu wa Qur-an:

وَٱلَّذِينَ يَرْمُونَ ٱلْمُحْصَنَٰتِ ثُمَّ لَمْ يَأْتُوا۟ بِأَرْبَعَةِ
شُهَدَآءَ فَٱجْلِدُوهُمْ ثَمَٰنِينَ جَلْدَةً وَلَا تَقْبَلُوا۟ لَهُمْ
شَهَٰدَةً أَبَدًا ۚ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ ﴿٤﴾

*"Na wale wanaowasingizia wanawake watahirifu (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wane, basi wapigeni mijeledi thamanini, na msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki". (24:4)*

**Al-Qiyaas (analogical Deduction)**

Al-Qiyaas ni maamuzi(fat-wa)anatoa mwanachuoni (mjuzi wa Qur-an na Sunnah) kulingana na mazingira na kwa maslahi ya jamii, pale ambapo hapana fat'wa iliyotolewa na Qur-an au Hadith au Ijmaa. Suala la kutumia akili limesisitizwa mno katika Uislamu kama tunavyojifunza katika aya zifuatazo:

إِنَّ فِي خَلْقِ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَٱخْتِلَٰفِ ٱلَّيْلِ
وَٱلنَّهَارِ لَءَايَٰتٍ لِّأُوْلِي ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿١٩٠﴾

*"Hakika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko hoja (za kuonyesha kuwepo Allah (s.w) kwa **wenye akili**." (3:190)*

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ ٱلْجِنِّ وَٱلْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ
لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا وَلَهُمْ ءَاذَانٌ لَّا
يَسْمَعُونَ بِهَآ ۚ أُوْلَٰٓئِكَ كَٱلْأَنْعَٰمِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ أُوْلَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلْغَٰفِلُونَ ﴿١٧٩﴾

*"Na bila shaka tumewaumbia Moto wa Jahannam wengi katika majini na watu (kwa sababu hii). Nyoyo (akili) wanazo lakini hawafahamukwazo na macho wanayo lakini hawaoni kwayo na masikio wanayo lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama, bali wao ni wapotevu zaidi. Hao ndio walioghafilika." (7:179)'*

Suala la kutoa maamuzi kwa kutumia akili pale ambapo hapana fat-wa ya Qur-an na Sunnah ameliridhia Mtume (s.a.w) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*"Mtume (s.a.w) alimtuma Mu'aadh bin Jabal Yemen kwenda kuwa Kadh (Jaji) na mkuu wa Jimbo (Governor). Kabla hajaondoka, Mtume (s.a.w) alimuuliza kuwa kama atafikwa na tatizo atalitatua kwa kutumia kigezo gani. Mu'aadh alijibu kuwa atatoa maamuzi kutokana na Qur-an. Mtume (s.a.w) akamuuliza: Jaalia kuwa*

*hukupata ufumbuzi wa tatizo hilo katika Qur-an, utafanyaje katika kutoa uamuzi?" Mu'aadh akajibu kuwa atatafuta ufumbuzi kutokana na Sunnah ya Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) akaendelea kumuuliza: "Jaalia hukupata jibu kwenye Qur-an wala Sunnah utafanyaje?" Mu'aadh bin Jabal alijibu kuwa atatoa uamuzi kutokana na* ***akili*** *yake. Mtume (s.a.w) alifurahi kusikia jibu hili."*

Pia tunajifunza katika Hadith kuwa Mtume (s.a.w) alimtuma Abuu Musa al Ash-a'ri kwenda Yemen na kumuagiza kuwa ahukumu kwa mujibu wa Qur-an, na kama hakupata uamuzi kutoka kwenye Qur-an, atumie Hadith za Mtume (s.a.w) na akikosa kupata uamuzi kutokana na Hadith, basi atoe maamuzi kutokana na akili yake.

**Al-Ijtihaad**

Ijtihaad ni neno la Kiarabu lenye maana ya kufanya jitihada ili kufikia maamuzi binafsi. Katika masuala ya kisheria, **Ijtihaad**, ni kutumia jitihada za kuchambua na kutoa ufafanuzi juu ya sheria.

Imamu Shafii, ameunga mkono suala la Ijitihaad, kwa kurejea aya ya Qur-an ifuatayo:

وَمِنْ حَيْثُ خَرَجْتَ فَوَلِّ وَجْهَكَ شَطْرَ ٱلْمَسْجِدِ ٱلْحَرَامِ ۚ
وَحَيْثُ مَا كُنتُمْ فَوَلُّوا۟ وُجُوهَكُمْ شَطْرَهُۥ

*"Na po pote wendako geuza uso wako kwenye msikiti mtakatifu. Na popote mlipo geuzeni nyuso zenu upande uliko (msikiti huo) ..." (2:150).*

Imamu Shafii kutokana na agizo la aya hii, anasisitiza kuwa si rahisi mtu kujua upande ilipo Ka'abah bila kutumia jitihada binafsi, kwa kutumia jua, ramani, dira, n.k.

Ijtihaad inakubalika kwa kuzingatia misingi ya Qur-an, Sunnah, Ijmaa na Qiyas. **Mujtahidi** hanabudi kuwa na ujuzi wa kina juu ya Qur-an, Sunnah, Ijmaa na Qiyas. Pamoja na ujuzi wa kutosha juu ya vyanzo hivi vinne vya sheria, Mujtahidi pia hanabudi kuwa na sifa zifuatazo:

(a) Awe Muislamu mzuri wa vitendo.
(b) Awe mcha-Mungu mwenye kushikamana na Qur-an na Sunnah.
(c) Asiwe mwenye kuathiriwa na misimamo ya vikundi.
(d) Awe muadilifu na muaminifu na awe ameepukana kabisa na matendo machafu.

**Halali na Haramu Katika Sheria ya Kiislamu**

Uislamu umepambanua na kuliweka wazi kila jambo. Uislamu pamoja na kuwataka watu wafanye mema na kuacha maovu umeainisha wazi wazi yepi mema (*Ma'arufaat*).

Na yepi maovu (Munkaraat). Allah (s.w) peke yake ndiye mwenye mamlaka ya kuhalalisha na kuharamisha. Kuhalalisha alicho kiharamisha Allah (s.w) au kufanya kinyume chake ni kuchukua nafasi ya Allah (s.w) katika mamlaka yake na hiyo ni shirk kubwa.

Yale yote aliyohalalisha Allah (s.w) yana manufaa kwa binaadamu kibinafsi na kijamii. Katika sheria ya Kiislamu mambo halali yamewekwa katika daraja tatu zifuatazo:

(i) Faradh. (iii) Mustahabu. (iii) Mubaha.

(i) **Faradh** ni mambo ambayo ni halali lakini kutokana na umuhimu wake, Allah (s.w) amewaamrisha watu kuyatekeleza pasina hiari. Mwenye kuacha kufanya haya kwa makusudi atakuwa amevunja amri au sheria ya Allah (s.w), na atastahiki **kughadhibikiwa** na Mola wake na kustahiki adhabu yake iwapo hataleta **toba ya kweli**.

(ii) **Mustahabu** ni mambo ambayo sio tu kuwa ni halali kuyafanya, bali pia watu wanahimizwa sana wajitahidi kuyafanya kwa ajili ya manufaa binafsi na jamii kwa ujumla. Mambo hayo yanaweza kuwa yale yanayohusiana na Ibada maalumu, siasa, uchumi, utamaduni, n.k.

(iii) **Mubaha**, katika sheria ya Kiislamu ni jambo lolote ambalo ni halali kulifanya lakini sio lazima kulifanya. Kwa mfano, iwapo mtu anapenda bustani ya maua anaruhusiwa na sheria kuwa nayo lakini sheria haimlazimishi mtu kuwa na bustani ya maua.

Yale yote aliyoyaharamisha Allah (s.w) yana madhara kwa binaadamu kibinafsi na kijamii. Kufanya mambo yaliyoharamishwa ni kuvunja sheria ya Allah(s.w) na kustahiki **ghadhabu** zake na **adhabu** yake.

Kuna mambo ambayo japo sheria haijatamka waziwazi kuwa ni haramu lakini uzoefu unaonesha kuwa yana madhara kwa binaadamu kibinafsi na kijamii. Mambo ya aina hii katika sheria ya Kiislamu huitwa **makruhu** Muislamu analazimika kujiepusha na mambo haya.

Ukichunguza makatazo yote katika sheria ya Kiislamu utaona kuwa yamewekwa kwa manufaa ya binaadamu na yamegawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo:

(i) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **imani**.
(ii) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **maisha** na **uhai** wa binaadamu.
(iii) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **akili** ya binaadamu.
(iv) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **heshima** na **hadhi** ya binaadamu.
(v) Makatazo yenye lengo la kulinda na kuhifadhi **mali**.

## Mahakama ya Kiislamu

Uislamu huyaratibu maisha ya jamii na hivyo kuweka sheria zinazolinda maslahi ya mtu yasiharibiwe na mtu mwingine. Sheria pia inamhakikishia usalama wake raia anayetuhumiwa kuwa ametenda kosa fulani. Sheria ya Kiislamu husimamisha haki kwa kuzingatia; maslahi ya dola ya kuzuia uhalifu na kwa kuyalinda maslahi ya raia ili haki zake zidumishwe:

1. Kanuni ya uwajibikaji wa mhalifu.
2. Kanuni ya uwiano wa kosa na adhabu, na
3. Kanuni ya kutosogeza nyuma hukumu zinazotolewa kwa wahalifu.

### 1. Kanuni ya uwajibikaji kwa mhalifu

Raia hawezi kuwa salama iwapo atalazimika kujibu mashtaka ya makosa ya mtu mwingine. Hivyo kanuni hii ni msingi wa usalama wa raia.

Kanuni hii ina maana kuwa ni yule mtendaji wa kosa tu ndiye ashitakiwe, na si mtu mwingine yeyote. Yaani ikiwa Juma ndiye aliyeteka nyara ndege basi yeye peke yake (kama alikuwa peke yake) ndiye ashitakiwe. Asichukuliwe baba yake mtu au mkewe n.k.

Kanuni hii pia maana yake ni kuwa ikiwa mtoto wa Rais ameiba pesa, basi asiachwe kwa sababu ni mtoto wa mtu mkubwa. Kanuni hii pia ina maana kuwa mtu aliyeshiriki katika kutenda kosa kama mtendaji mkuu au kama msaidizi hana budi kushitakiwa kwa mujibu wa kushiriki kwake. Qur-an imebainisha katika sehemu mbali mbali juu ya kanuni hii ya uwajibikaji wa mtu binafsi:

وَأَن لَّيْسَ لِلْإِنسَانِ إِلَّا مَا سَعَىٰ ﴿٣٩﴾

*Na kwamba mtu hatapata ila yale aliyoyafanya. (53:39)*

مَّنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا ۗ وَمَا رَبُّكَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٤٦﴾

*Anayefanya mema anajifanyia (mwenyewe) nafsi yake, na mwenye kutenda ubaya ni juu (ya nafsi) yake (vile vile). Na Mola wako si dhalimu kwa waja wake (41:46)*

وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا ۚ

*Wala nafsi yoyote haichumi (ubaya) ila ni juu yake. (6:164)*

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۚ

*Wala hatabeba mzigo wa mwingine. (35:18)*

مَن يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ

*Atakayefanya ubaya atalipwa kwa (ubaya) huo. (4:123)*

Hadith za Mtume (s.a.w) pia zinaithibitisha kanuni hii. Mtume (s.a.w) amesema:

*"Nafsi haitaulizwa kwa makosa ya baba, au ndugu yake.*

Huko Ulaya kanuni hii ilitambuliwa baada ya Mapinduzi ya Ufaransa. Kanuni hii ilipitishwa katika sheria ya Januari 21, 1790, na kuingizwa katika katiba 1791. Kabla ya hapo mtu aliwajibika siyo tu kwa makosa yake bali pia kwa makosa yaliyotendwa na wengine.

Kwa mfano sheria moja ya Kifaransa ya zama hizo ilikuwa inasema kuwa kusema maneno yasiyopendeza dhidi ya Mfalme ni kosa ambalo adhabu yake ni kifo kwa huyo msemaji na kufilisiwa mali ya familia ya mtu huyo.

**2. Kanuni ya uwiano wa kosa na adhabu**

(a) Kanuni hii ina maana kuwa hakuna mtu anayeweza kushitakiwa au kuadhibiwa isipokuwa kama ilivyobainishwa na sheria. Kanuni hii ina maana kuwa makosa na adhabu zake lazima zitolewe na serikali.

Kanuni ya uhalali wa kosa na adhabu inalinda usalama wa raia kwa kuhakikisha kuwa mtu hanyanyaswi na dola. Kanuni hii pia inadhibiti mamlaka na uwezo wa hakimu kwani hawezi kutoa adhabu isipokuwa tu kama ilivyowekwa katika sheria, hata kama kosa hili limeudhi watu namna gani.

Hivyo basi sheria ndiyo inayogawa baina ya lipi halali na lipi haramu. Hakuna mtu atakayeadhibiwa au kushitakiwa kwa jambo ambalo halikubainishwa wazi kuwa ni kosa kabla ya kutendwa:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾

*Na si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka tuwapelekee Mtume. (17:15)*

رُّسُلًا مُّبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ لِئَلَّا يَكُونَ لِلنَّاسِ عَلَى
ٱللَّهِ حُجَّةٌۢ بَعْدَ ٱلرُّسُلِۚ وَكَانَ ٱللَّهُ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿١٦٥﴾

*(Hao ni) Mitume waliotoa khabari (kwa watu wema) wakawaonya (wabaya) ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya (kuletwa hawa) Mitume. Allah ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hikima. (4:165).*

وَمَا كَانَ رَبُّكَ مُهْلِكَ ٱلْقُرَىٰ حَتَّىٰ يَبْعَثَ فِىٓ
أُمِّهَا رَسُولًا يَتْلُوا۟ عَلَيْهِمْ ءَايَٰتِنَاۚ

*Na Mola wako haangamizi miji mpaka ampeleke Mtume katika mji wao mkuu, awasomee aya zetu. (28:59)*

وَأُوحِىَ إِلَىَّ هَٰذَا ٱلْقُرْءَانُ لِأُنذِرَكُم بِهِۦ وَمَنۢ بَلَغَۚ

*Na Qur-an hii imefunuliwa kwangu ili kwa hiyo nikuonyeni nyinyi na kila imfikiayo. (6:19).*

وَإِن مِّنْ أُمَّةٍ إِلَّا خَلَا فِيهَا نَذِيرٌ ﴿٢٤﴾

*Na hakuna taifa lolote ila alipita humo muonyaji (Mtume). (35:24).*

Hivyo Qur-an ambayo ndio chimbuko kuu la sheria ya Kiislamu imeweka kanuni kuwa mshitakiwa hawezi kuadhibiwa mpaka kwanza awe ametaarifiwa juu ya kuwa jambo hili ni kosa. Haki ya kuarifiwa kosa na adhabu yake ndio lengo la kanuni hii ya uhalali wa kosa na adhabu.

### 3. Kanuni ya Kutosogeza nyuma hukumu zinazotolewa

Raia hawawezi kuzitumia haki zao kwa usalama iwapo wanaweza kushitakiwa kwa makosa ambayo hayakuwa makosa wakati yalipotendwa. Kwa sababu hiyo Uislamu unatambua kanuni hii na kuitumia katika sheria zake. Kanuni hii ina maana kuwa sheria huanza kutumika baada ya kutangazwa na siyo kabla. Umuhimu wa kanuni hii ni kulinda usalama wa raia na pia inazuia matumizi mabaya ya madaraka.

Hii ni taafauti na mifumo yaa sheria za kitwaghuti ambapo mtu anakamatwa kisha sheria inafuatia. Kama ilivyotokea hapa nchini miaka ya themanini watu walikamatwa kwa madai ya kuhujumu uchumi wa nchi wakati hakukuwa na sheria ya uhujumu uchumi. Baada ya watu kukamatwa ndipo ikatungwa sheria! Qur-an imetaja kanuni hii katika Aya mbali mbali. Allah alikataza riba lakini hakuwaadhibu wale waliotoa au kula riba kabla ya kushuka katazo hilo *(taz:Qur-an 2:275).* Allah pia anakataza kuwaoa ndugu wawili wakati mmoja, lakini hakuwaadhibu wale waliofanya hivyo kabla ya kulidhihirisha kuwa ni kosa. *(taz: Qur-an, 4:23)*

Hali kadhalika, makatazo ya zinaa, wizi, ulevi na makosa mengine hayakutolewa adhabu iwapo yalifanywa kabla ya kubainishwa wazi katika Qur-an.

Lengo la kanuni hii ni kutoa muda wa kutosha kwa watu juu ya makatazo ya Allah ili kuwapa fursa ya kujirekebisha.

### Taratibu za Mashtaka katika Sheria ya Kiislamu

Miongoni mwa mambo muhimu sana yanayohakikisha usalama wa raia ni taratibu zinazotawala mwenendo wa mashitaka. Taratibu hizi zina lengo la kuleta mizani ya

haki kati ya haki ya dola ya kusimamia sheria na haki ya raia ya kuishi kwa amani bila usumbufu na kunyanyaswa kinyume cha sheria.

Katika sheria ya Kiislamu watu wote ni sawa mbele ya Sheria. Taratibu zake za mashitaka zaweza kugawanywa katika vipengele vikuu vinne:

1. Raia kudhaniwa kuwa hana hatia.
2. Upepelezi na kuhojiwa.
3. Haki za mshtakiwa wakati wa kusikiliza kesi.
4. Haki za mfungwa.

**Raia kudhaniwa kuwa hana hatia**

Kuhusu kanuni hii Mtume (s.a.w) amesema: *"Kila mtoto huzaliwa bila doa; ni wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi, Mkristo au Mmajusi."* (Bukhari) Mtume (s.a.w) pia amesema: *"Msitoe adhabu ikiwa mna shaka".*

Hivyo chini ya sheria ya Kiislamu hadhi ya mshtakiwa ni ile ya mtu asiye na hatia. Hii ina maana kuwa jukumu la kuthibitisha kosa linakuwa mikononi mwa mtu anayeshtaki. Mshatakiwa hatakiwi kutoa ushahidi wa kukanusha kosa (negative evidence). Kumtaka mshtaki (mlalamikaji) atoe ushahidi wa kuthibitisha kutendeka kwa kosa (positive proof) kunatokana na Hadithi ya Mtume (s.a.w) aliposema:

> *Lau watu wangeaminiwa kwa madai yao tu, baadhi ya watu wangedai damu na mali ya watu wengine, lakini mshtaki anawajibika kutoa uthibitisho wa madai yake. (Bukhari, Muslim, Ahmad).*

Aidha matokeo mengine ya kanuni hii ni kuwa shaka (shubha) inamsaidia mshtakiwa. Katika sheria ya Kiislamu ili kumtia mtu hatiani (conviction) inategemea uhakika kuwa mshtakiwa alitenda kosa na siyo uwezekano kuwa

alitenda kosa. Ikiwa kutokana na ushahidi uliotolewa hakimu bado ana wasi wasi basi itambidi aamue kuwa mshtakiwa hana hatia.

Hii ni kutokana na Hadithi ya Mtume (s.a.w) aliposema:

*"Msitoe adhabu ikiwa mna shaka. Mwacheni huru mshitakiwa, kwani bora kufanya kosa la kumsamehe kuliko kosa la kumwadhibu."*

## Haki za Mshitakiwa Wakati wa Upelelezi

Kumvamia mtu nyumbani kwake na kumpekua ni kitendo kinachowaondoshea uhuru raia na cha kumdhalilisha mtuhumiwa, hivyo sheria ya Kiislamu imeweka taratibu za kulidhibiti hili. Ikumbukwe kuwa jamii itanufaika iwapo ukweli utajulikana kutokana na upelelezi utakaofanywa. Hivyo sheria ya Kiislamu imeweka kanuni ya kuyaweka katika mizani yote mawili.

Sheria ya Kiislamu inazuia upekuzi wa nyumba za watu pasi na sababu za kimsingi kisheria. Haki ya kila mtu kuwa faragha imebainishwa katika Qur-an aliposema Al-lah (s.w):

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَدْخُلُوا۟ بُيُوتًا غَيْرَ بُيُوتِكُمْ
حَتَّىٰ تَسْتَأْنِسُوا۟ وَتُسَلِّمُوا۟ عَلَىٰٓ أَهْلِهَا ۚ ذَٰلِكُمْ خَيْرٌ لَّكُمْ
لَعَلَّكُمْ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾

*Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa na muwatolee Salaam waliomo humo.Hayo ni bora kwenu; huenda mtakumbuka.(24:27)*

فَإِن لَّمْ تَجِدُوا۟ فِيهَآ أَحَدًا فَلَا تَدْخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤْذَنَ لَكُمْ ۖ
وَإِن قِيلَ لَكُمُ ٱرْجِعُوا۟ فَٱرْجِعُوا۟ ۖ هُوَ أَزْكَىٰ لَكُمْ ۚ وَٱللَّهُ
بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٢٨﴾

*Na kama hamtamkuta humo yoyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkiambiwa "rudini", basi rudini; hili ni takaso kwenu. Na Allah anajua mnayoyatenda. (24:28).*

Hivyo kwa mujibu wa aya hizi kuingia katika nyumba za watu kumekatazwa isipokuwa kwa idhini ya mwenye nyumba. Katazo hili halikomei katika nyumba tu, bali linahusu pia mali ya mwenye nyumba mwenyewe asipokuwapo. Mtume (s.a.w) amesema:

*Mambo matatu hayaruhusiwi kwa mtu yeyote; mtu anayeongoza kundi katika swala asijiombee dua peke yake, kwani akifanya hivyo atakuwa amewasaliti. Mtu asiangalie ndani ya nyumba ya mtu ila akipewa ruhusa. Na mtu asiswali hali amebanwa na haja hadi ajisaidie kwanza. (Muslim).*

Mtume (s.a.w) pia ametumia lugha ya ishara ili kusisitiza haki ya mtu kuwa huru kutokana na kubughudhiwa faragha katika Hadithi ifuatayo:

*Ikiwa mtu anakutazama (anakukodoleo macho) bila ridhaa yako na ukampiga kwa jiwe hadi ukalipofua jicho lake huna hatia.*

Haki hii pia inazihusu nguo zake mtu. Hakuna mtu mwenye haki ya kumfunua mwingine nguo ili kuangalia kitu alichokificha bila ya idhini na bila sababu ya msingi.

Aidha, kuilinda nyumba hakutakuwa na maana bila kumlinda mmilikaji pia. Barua zake mtu pia lazima zihifadhiwe. Hivyo ni haramu kuzisoma barua za mtu za kibinafsi baada ya kuzichukua kwa siri. Mtume (s.a.w) amesema: Mtu anayeisoma barua ya nduguye bila ruhusa yake, ataisoma barua hiyo motoni.

Hata hivyo, chini ya sheria ya Kiislamu haki ya kuwa na faragha na haki ya kutobughudhiwa yaweza kukiukwa ikibidi ili kudumisha amani na usalama wa jamii. Vyombo vya dola vyaweza kumpekua mtu kwa maslahi ya jamii. Lakini haki hiyo ya kupekua inatawaliwa na masharti yanayohakikisha kuwa raia hanyanyaswi ovyo. Masharti hayo ni:

1. Mtoaji wa amri ya kupekuwa ni mkuu anayehusika na malalamiko (Wali-al-Muzahim). Kwa mujibu wa kanuni za mahakama za Kiislamu, hakimu hana haki ya kutoa amri ya upekuzi (search-warrant) wala si juu yake kutafuta ushahidi. Kazi yake ni kumwambia mlalamikaji kuleta ushahidi wa uthibitisho wa madai yake.

2. Hati ya kupekua haiwezi kutolewa hadi kwanza upatikane ushahidi wa kutosha unaoonesha kuwa upo uwezekano mkubwa kuwa kosa limetendwa na mshitakiwa. Kwa mfano ikiwa mtu mwadilifu anatoa taarifa kuwa amemwona mtu anaingia faraghani na mwanamke au kama mtu anapita nje ya nyumba na akasikia harufu ya pombe yatoka ndani na kelele za watu waliolewa.

3. Kosa ligunduliwe kihalali, kuwa ikiwa limegunduliwa kwa njia za haramu kama ujasusi (kwa mfano kwa kutoboa tundu ukutani na kuchungulia ndani aukusikliza kwa siri na kwa kuvizia. Ushahidi wa kijasusi hauwezi kutumika kumtia mtu hatiani.

Allah amesema:

*"Wala msipeleleze" (49:12)* وَلَا تَجَسَّسُوا۟

**Haki za Mtuhumiwa wakati wa Kuhojiwa**

Katika sheria ya Kiislamu mahojiano siyo maana yake mtuhumiwa kujibu maswali tu la. Bali ni fursa ya kumwambia mtuhumiwa makosa yake na ushahidi uliopatikana dhidi yake, ili akiri au aukanushe ushahidi huo.

Vile vile katika sheria ya Kiislamu hakuna mtu atakayeadhibiwa mpaka kwanza mahakama ya wazi (yenye kushuhudiwa na watu) ithibitishe kosa lake. Kesi za faragha ni haramu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu pia ni haramu kumkamata mtu kwa kumshuku tu na kumsukumiza jela bila ya kufuata utaratibu wa mahakama na bila ya kumpa fursa ya kujitetea. Aidha ni haramu kumtesa mtuhumiwa "ili aisaidie polisi" kuhusiana na uovu uliotendeka. Uadilifu katika kutoa hukumu, bila ya ubaguzi wa aina yoyote ni jambo lililosisitizwa katika misingi ya sheria ya Kiislamu:

وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ ٱلنَّاسِ أَن تَحْكُمُوا۟ بِٱلْعَدْلِ ۚ

*"Na mnapohukumu baina ya watu hukumuni kwa uadilifu". (4:58)*

Pia Mtume (s.a.w) amesisitiza:

*"Nimeamrishwa kuhukumu kwa uadilifu".*

Katika sheria ya Kiislamu hairuhusiwi mtu kuwekwa ndani mpaka ahukumiwe kwa uadilifu, wala hapana yoyote asiye na hatia kuadhibiwa au kutiwa ndani kwa makosa ya mwingine au kwa niaba ya mwingine.

Tofauti na sheria za kijahili ambazo humuona mtuhumiwa kuwa ana makosa kwanza mpaka aithibitishie mahakama kuwa hana makosa, sheria ya Kiislamu humuona mtuhumiwa hana makosa mpaka mahakama ithibitishe kuwa ana makosa.

**Haki za mtuhumiwa zinavyohifadhiwa**

1. Wanaohoji wawe wawili:
   (i) Mkuu wa Malalamiko.
   (ii) Mwendesha mashtaka (Muhtasib).

2. Mtuhumiwa katika makosa ya Hudud na Qisas ana haki ya kutoapa.

3. Katika uchunguzi wa makosa ya Hudud anayo haki ya kukataa kuhojiwa, na anayo haki ya kukaa kimya.

4. Kimya chake hakiwezi kuwa ushahidi dhidi yake.

5. Mtuhumiwa asiteswe (au kufanyiwa ukatili).
   Mtume (s.a.w) amesema: Allah atawatesa siku ya malipo wale waliowatesa wenzao duniani. Bwana Audi ibn Artana alimwandikia Umar barua kumwomba ruhusa ya kuwatesa watu wanaokataa kutuo Zaka. Umar akamkatalia.

6. Mahojiano yawe ya kibinaadamu, ili mtuhumiwa akiri kosa lake kwa hiari bila kulazimishwa. Mtume (s.a.w) alimwambia mtu aliyeletwa kwake kwa tuhuma za wizi: *"Sidhani kama uliiba; Je, uliiba? Au Bwana Maaz alipokiri kuwa kazini, Mtume (s.a.w) alimpa fursa ya kubatilisha ungamo lake, akamwambia, "Labda ulimbusu tu, au pengine ulimpapasa tu?"* Aidha mwanamke mmoja alituhumiwa wizi, Mtume (s.a.w) akamwambia, "*Je, uliiba? Sidhani kama uliiba. Sema hapana*" Hivyo kumpa fursa ya kufuta ungamo lake.

7. Chini ya sheria ya Kiislamu mtuhumiwa aweza kukana ungamo lake wakati wowote kabla ya kutolewa adhabu. Bwana Maaz, alikana ungamo lake baada ya kuanza kupigwa mawe, lakini wapigaji hawakumwacha. Alipoambiwa Mtume (s.a.w) akasema, "Kwa nini hamkumwacha atubie? Allah angepokea toba yake".

**Haki za mshtakiwa wakati wa kusikilizwa kesi**

(1) Afunguliwe mashtaka haraka na ahukumiwe.

(2) Ushahidi katika makosa ya Hudud ni wa kisheria na si wa rai.

(3) Anayohaki ya kulipwa fidia ikiwa atahukumiwa kimakosa.

(4) Ashitakiwe katika mahakama yenye mahakimu wenye ujuzi na waadilifu.

(5) Mtu yeyote pamoja na kiongozi wa nchi anaweza kujibu mashitaka mahakamani.

(6) Mshitaki na mshitakiwa wote wana haki ya kumteua mtu wa kuwawakilisha mahakamani (wakili).

**Haki ya Kuhukumiwa kwa Uadilifu**

Sheria ya Kiislamu ipo pale kusimamia uadilifu na lengo lake si kuadhibu wala kukomoa bali kujenga jamii bora. Kila mtu bila ya kujali dini yake, rangi, taifa lake, uraia wake, (n.k.), anastahiki kuhukumiwa kwa uadilifu. Uadilifu katika kutoa hukumu umesisitizwa na ndio msingi mkuu wa sheria ya Kiislamu:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ

*Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi (wa kupitisha haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa ushahidi kwa uadilifu… (5:8).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ
لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَٰلِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ
غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا فَٱللَّهُ أَوْلَىٰ بِهِمَا ۖ فَلَا تَتَّبِعُوا۟ ٱلْهَوَىٰٓ
أَن تَعْدِلُوا۟ ۚ

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au maskini… basi msifuate matamanio mkaacha uadilifu… (4:135).*

## Mgawanyo wa Makosa

Sheria imeyagawanya makosa katika makundi makubwa matatu:

(i) Makosa ya Hudud
(ii) Makosa ya Qisasi
(iii) Makosa ya Ta'azir

## Makosa ya Hudud

Makosa ya Hudud ni yale ambayo yamekatazwa na Allah na hukumu zake kutajwa katika Qur-an au Sunnah. Makosa hayo ni haya yafuatayo:

### (1) Kuritadi (Ridda)

Kuritadi ni Muislamu kuukanusha Uislamu kwa maneno aya yoyote ya Qur-an. Au kuukataa Uislamu kwa vitendo kama vile kwa kuzini au kuyawacha

maamrisho ya Qur-an kama vile swala na zaka. Mtu anahesabiwa amekanusha Uislamu kwa makusudi na hali yakuwa anajua adhabu ya kufanya hivyo.

Mtu aliyeritadi anapewa muda wa kutubia kosa lake. Ukipita muda wa kutosha na hajatubia basi hukumu yake ni kuuliwa:Hukumu imetolewa katika Qur-an:

فَٱقْتُلُوا۟ ٱلْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدتُّمُوهُمْ وَخُذُوهُمْ
وَٱحْصُرُوهُمْ وَٱقْعُدُوا۟ لَهُمْ كُلَّ مَرْصَدٍ ۚ فَإِن
تَابُوا۟ وَأَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ فَخَلُّوا۟ سَبِيلَهُمْ ۚ
إِنَّ ٱللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٥﴾

*Basi wauweni washirikina popote muwakutapo na wakamateni mateka, na wazungukeni na wakalieni katika kila njia. Lakini wakitubu na wakasimamisha swala na wakatoa zaka, basi iacheni njia yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kurehemu. (9:5).*

**(2) Uasi (Baghi)**

Baghi ni uasi dhidi ya kiongozi halali wa Kiislamu. Uasi huo waweza kuwa hauna msingi wowote au waweza kuwa umetegemezwa katika kipengele fulani maalum ambacho hao wapiganaji Waislamu wamekitegemea katika uasi wao. Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awasihi waache uasi huo na ayajue madai yao ili ipatikane suluhu. Wakikataa ana haki ya kupigana nao. Hata hivyo iwapo madai yao ni ya haki na Imam ndiye aliyekwenda kinyume

na Uislamu basi huyo kiongozi ndiye mwasi na wale wanaopigana naye hawataadhibiwa. Kuhusiana na Uasi Allah amesema katika Qur-an:

وَإِن طَآئِفَتَانِ مِنَ ٱلۡمُؤۡمِنِينَ ٱقۡتَتَلُواْ فَأَصۡلِحُواْ بَيۡنَهُمَاۖ فَإِنۢ
بَغَتۡ إِحۡدَىٰهُمَا عَلَى ٱلۡأُخۡرَىٰ فَقَٰتِلُواْ ٱلَّتِي تَبۡغِي حَتَّىٰ
تَفِيٓءَ إِلَىٰٓ أَمۡرِ ٱللَّهِۚ فَإِن فَآءَتۡ فَأَصۡلِحُواْ بَيۡنَهُمَا بِٱلۡعَدۡلِ
وَأَقۡسِطُوٓاْۖ إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُقۡسِطِينَ ٩

*Na ikiwa makundi mawili katika Waislamu wanapigana, basi fanyeni suluhu baina yao; na likiwa mojawapo linamdhulumu mwenziwe, basi lipigeni lile linaloonea mpaka lirudie katika amri ya Mwenyezi Mungu. Na kama likirudi basi yapatanisheni baina yao kwa uadilifu. Na hukumuni kwa haki. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanaohukumu kwa haki. (49:9)*

**(3) Wizi**

Kuhusiana na wizi Allah anasema:

وَٱلسَّارِقُ وَٱلسَّارِقَةُ فَٱقۡطَعُوٓاْ أَيۡدِيَهُمَا جَزَآءَۢ بِمَا كَسَبَا
نَكَٰلٗا مِّنَ ٱللَّهِۗ وَٱللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٞ ٣٨

*Na mwizi mwanamume au mwizi mwanamke, ikateni mikono yao; malipo ya yale waliyoyachuma. Ndiyo adhabu, itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye nguvu na mwenye hikima. (5:38)*

Hukumu ya mwizi ni kukatwa mkono wake wa kulia iwapo yatatimia masharti yafuatayo:

(a) Awe amekusudia kuchukua mali ya wizi pasi na idhini ya mwenye mali.

(b) Awe ameiondosha mali hiyo kutoka mahala inapowekwa.

(c) Awe amevunja sefu au kasha au kibweta cha fedha.

(d) Mali iliyoibiwa iwe ni halali katika Uislamu, isiwe mfano pombe, au nyama ya nguruwe au bangi n.k.

(e) Mali iliyoibiwa iwe imefikia angalau thamani ya kima cha chini Nisab yaani angalau tu ifikie thamani iliyo sawa kifedha na mizani moja. Juu ya hili Mtume (s.a.w) analifahamisha: Mkono wa mwizi usikatwe ila kama thamani ya mali iliyoibiwa ni sawa na thamani ya mizani.

Zipo kauli tofauti juu ya thamani ya Mizani, wengine wanasema ni robo ($^1/_4$) ya dinar ya dhahabu au dinar tatu za fedha. Wengine wanasema ni dirham kumi za fedha.

(f) Isiwepo "*shubha*", yaani mazingira yatakayoruhusu kutendeka kosa hilo.

**Tahadhari**

Adhabu ya mtu ambaye imethibitika kwa haki ya sheria kuwa kaiba ni kukakwa mkono. Ndivyo Allah (s.w) alivyoamuru! Basi ole wao wale wanaochukuwa sheria mkononi kwa kuwapiga watu, kuwajeruhi, kuwachoma moto, na pengine kuwauwa kwa ajili ya kuwatuhumu uwizi. Ni vyema ikaeleweka kuwa mwenye haki ya kuhukumiwa kifo, ni mtu aliyeuwa nafsi yenye haki ya kuwa hai kisheria. Vinginevyo Qur-an inakataza!

وَلَا تَقْتُلُوا۟ ٱلنَّفْسَ ٱلَّتِى حَرَّمَ ٱللَّهُ إِلَّا بِٱلْحَقِّ

*Wala usiuwe nafsi ambayo Mwenyezi Mungu amekataza (kuiuwa) isipokuwa kwa haki (17:33).*

أَنَّهُۥ مَن قَتَلَ نَفْسًۢا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِى ٱلْأَرْضِ
فَكَأَنَّمَا قَتَلَ ٱلنَّاسَ جَمِيعًا

*Atakayemuuwa mtu bila ya yeye kuuwa mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewauwa watu wote (5:32)*

**(4) Ujambazi (Haraba)**

Adhabu ya ujambazi imefafanuliwa katika Qur-an kama ifuatavyo:

إِنَّمَا جَزَٰٓؤُا۟ ٱلَّذِينَ يُحَارِبُونَ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ وَيَسْعَوْنَ
فِى ٱلْأَرْضِ فَسَادًا أَن يُقَتَّلُوٓا۟ أَوْ يُصَلَّبُوٓا۟ أَوْ تُقَطَّعَ
أَيْدِيهِمْ وَأَرْجُلُهُم مِّنْ خِلَٰفٍ أَوْ يُنفَوْا۟ مِنَ ٱلْأَرْضِ ۚ
ذَٰلِكَ لَهُمْ خِزْىٌ فِى ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَهُمْ فِى ٱلْءَاخِرَةِ عَذَابٌ
عَظِيمٌ ﴿٣٣﴾

*Basi malipo ya wale wanaopigana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kufanya uovu katika nchi ni kuuawa na kusulubiwa au kukatwa mikono yao na miguu yao kwa mabadilisho, au kuhamishwa katika nchi. Hii ndiyo fedheha yao katika dunia; na Akhera watapata adhabu kubwa. (5:33)*

Aya hii inawahusu wale wote wanaoifisidi jamii iwe kijeshi au kwa kuvuruga amani na usalama wa watu na mali zao, wanyama, mimea n.k. hivyo majambazi wanaotumia silaha wanaangukia chini ya sheria hii.

Hukumu hii itatumika iwapo jambazi atakuwa amesababisha kifo au la Yaani katika hali zote nne:

(a) Iwapo raia atavamiwa bila kuporwa mali yake.
(b) Iwapo raia atanyang'anywa mali yake kwa nguvu lakini bila ya kuuliwa.
(c) Iwapo raia atauliwa bila kuporwa mali.
(d) Iwapo raia atauliwa na kuporwa mali.

**(5) Uzinzi (zinaa)**

Adhabu ya zinaa ni kupigwa fimbo 100 hadharani, Allah (s.w) anasema:

ٱلزَّانِيَةُ وَٱلزَّانِى فَٱجْلِدُوا۟ كُلَّ وَٰحِدٍ مِّنْهُمَا مِا۟ئَةَ جَلْدَةٍ ۖ
وَلَا تَأْخُذْكُم بِهِمَا رَأْفَةٌ فِى دِينِ ٱللَّهِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ
بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْءَاخِرِ ۖ وَلْيَشْهَدْ عَذَابَهُمَا طَآئِفَةٌ مِّنَ ٱلْمُؤْمِنِينَ

*Mzinifu mwanamke na mzinifu mwanamume, mpigeni kila mmoja katika wao mijeledi mia. Wala isiwashikeni kwa ajili yao huruma katika (kupitisha) hukumu hii ya Mwenyezi Mungu ikiwa nyinyi mnamuamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Na lishuhudie adhabu yao (hii) kundi la Waislamu. (24:2).*

Sharti la kutolewa adhabu ya zinaa ni kupatikana kwa mashahidi wanne walioshuhudia kitendo hicho au kukiri kosa kwa mzinzi mwenyewe.

**(6) Kashfa (Badhf)**

Kashfa (defamalion) yawezekana ikawa ni msemo (slander) vijembe (innuendo) au maandiko na machapisho (libel) yenye lengo la kutoa kejeli dhidi ya, kutusi au kushusha hadhi ya mtu. Kuhusiana na kosa hili Qur-an imetoa adhabu ifuatayo:

وَٱلَّذِينَ يَرۡمُونَ ٱلۡمُحۡصَنَٰتِ ثُمَّ لَمۡ يَأۡتُواْ بِأَرۡبَعَةِ
شُهَدَآءَ فَٱجۡلِدُوهُمۡ ثَمَٰنِينَ جَلۡدَةٗ وَلَا تَقۡبَلُواْ لَهُمۡ
شَهَٰدَةً أَبَدٗاۚ وَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ ﴿٤﴾

*Na wale wanaowasingizia wanawake wataharifu (kuwa wamezini) kisha hawaleti mashahidi wanne, basi wapigeni mijeledi thamanini na Msiwakubalie ushahidi wao tena, na hao ndio mafasiki. (24:4).*

Kashfa katika sheria ya Kiislamu ni kumzulia mtu kuwa kazini au kulawiti au kulawitiwa au kumkashifu mtu muadilifu, mwenye akili timamu na uwezo wa kimwili wa kutenda kosa alilozuliwa.

**(7) Kunywa ulevi**

Qur-an imeharamisha ulevi pale aliposema Allah (s.w):

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ
وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٞ مِّنۡ عَمَلِ ٱلشَّيۡطَٰنِ فَٱجۡتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمۡ
تُفۡلِحُونَ ﴿٩٠﴾

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli ni uchafu (ni) katika kazi za shetani. Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu. (5:90).*

Hivyo ilipoteremka aya hii ya 90 na 91 Waislamu waliitiii amri ya Allah kwa kumwaga ulevi wote waliokuwa nao. Mtume (s.a.w) alitoa adhabu kwa mlevi kuwa ni kutandikwa viboko 40 kama alivyo amuru:

*"Yule anywaye ulevi mpigeni bakora"*

Imesimuliwa na Anas bin Malik (r.a) kuwa:

*Mtume (s.a.w) alimpiga mlevi kwa matawi (majani) ya mtende na kwa viatu. Na Abu Bakr alimwadhibu (mlevi) kwa fimbo arobaini. (Bukhari).*

**Makosa ya Qisas**

Baada ya makosa ya Hudud, kundi la pili ni lile la makosa ya Qisas.

Neno qisasi lina maana ya "usawa" au "kufanana". Lina maana kuwa mtu aliyetenda kosa fulani ataadhibiwa vile vile na kwa namna ile ile aliyotumia katika kumdhulumu mwenzake (kulipiziwa).

Haki ya Qisasi imewekwa na Allah (s.w) katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُتِبَ عَلَيۡكُمُ ٱلۡقِصَاصُ
فِي ٱلۡقَتۡلَىۖ ٱلۡحُرُّ بِٱلۡحُرِّ وَٱلۡعَبۡدُ بِٱلۡعَبۡدِ وَٱلۡأُنثَىٰ
بِٱلۡأُنثَىٰۚ فَمَنۡ عُفِيَ لَهُۥ مِنۡ أَخِيهِ شَيۡءٞ فَٱتِّبَاعُۢ
بِٱلۡمَعۡرُوفِ وَأَدَآءٌ إِلَيۡهِ بِإِحۡسَٰنٖۗ ذَٰلِكَ تَخۡفِيفٞ
مِّن رَّبِّكُمۡ وَرَحۡمَةٞۗ فَمَنِ ٱعۡتَدَىٰ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَلَهُۥ
عَذَابٌ أَلِيمٞ ١٧٨

*Enyi mlioamini! Mmepewa ruhusa kulipa kisasi katika waliouawa – Muungwana kwa muungwana na mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke.Na anayesamehewa na ndugu yake chochote basi ashikwe kulipa kwa wema; na yeye alipe kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola wenu na ni rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya haya, basi yeye atapata adhabu iumizayo. (2:178)*

Kimsingi makosa ya kisasi ni ya namna mbili: Makosa ya kuua na makosa ya kujeruhi. Makosa ya kisasi yanahesabiwa kuwa ni kukiuka haki ya mtu binafsi na hivyo sheria inampa fursa mtu au ndugu zake kulipa kisasi au kulipwa fidia. Kuhusu fidia tazama Qur-an 4:92. Haya ni maelezo ya jumla tu. Hata hivyo kabla ya kutekelezwa kwa kisasi au fidia yapo mambo kadhaa ya kuzingatia kuhusiana na ushahidi wa kosa, na adhabu.

**Makosa ya Ta'azir**

Makosa ya Ta'azir ni yale yote ambayo Qur-an na Sunnah havijaweka adhabu fulani maalum. Adhabu za makosa ya aina hii hutolewa na Jaji kwa idhini ya kiongozi wa Kiislamu. Neno **Ta'azir** lina maana ya adhabu. Kisheria Ta'azir lina maana ya adhabu ambayo haijawekwa moja kwa moja katika Qur-an bali hutegemea maamuzi ya Jaji au hakimu kwa kulinganisha kosa, mazingira ya kosa na adhabu.

**Haki za wasiokuwa Waislamu (Dhimmi)**

Sheria ya Kiislamu imewapa haki wasiokuwa Waislamu kama ifuatavyo:

**(i) *Haki ya ulinzi wa maisha na mali***

Damu ya Dhimmi ni haramu kumwagwa pasipo sababu kama ilivyo damu ya Muislamu. Muislamu akimuua

Dhimmi adhabu yake ni sawa na ile ya kumuua Muislamu. Mtume (s.a.w) amesema:

*“Ni jukumu langu kusimamia haki za wanyonge”.*

Vile vile mali ya Dhimmi katika sheria ya Kiislamu inathaminiwa kama ilivyo mali ya Muislamu. Muislamu akiiba mali ya Dhimmi kwa kiwango kile kilichotajwa na Mtume atahukumiwa kukatwa mkono kama kawaida.

Khalifa wa nne wa Mtume (s.a.w.) baada ya kumuhukumu Muislamu mmoja
kuuawa na warithi wa Dhimmi aliyemuua, alisisitiza:

*Yeyote aliye Dhimmi wetu damu yake ni takatifu kama damu yetu na mali yake ni takatifu kama mali yetu.*

**(ii) Haki katika sheria ya jinai**

Katika sheria ya Kiislamu hukumu za makosa ya jinai *(penal laws)* zinawahusu wadhimmi sawa na zinavyowahusu Waislamu. Makosa ya jinai ni makosa yanayoathiri jamii nzima na mhalifu atakuwa anaidhulumu jamii nzima. Kwa hivyo Dhimmi akiiba atakatwa kiganja chake cha mkono wa kulia, akizini atatandikwa viboko 100.

Ila Dhimmi hataadhibiwa kwa kosa la ulevi kama atakavyoadhibiwa akilewa Muislamu kwa kutandikwa viboko 40,

**(iii) Haki katika sheria za Madai (Civil Laws)**

Katika sheria ya Kiislamu hukumu za madai ni sawa sawa kwa Waislamu na wasio kuwa Waislamu. Kila mwenye kudaiwa atahukumiwa na sheria kutoa haki ya mdai bila ya ubaguzi wa dini. Pia yale yaliyo haramishwa kwa Waislamu katika uchumi pia sheria inayakataza kwa

madhimmi. Kwa mfano riba na kamari ni haramu kwa Waislamu na imekatazwa pia kwa wasiokuwa Waislamu kwani riba na kamari huiathiri jamii nzima.

**(iv) Haki ya heshima ya Dhimmi**

Kumvunjia heshima dhimmi kwa kumtukana, kumuita jina baya, kumdhuru, kumuadhiri, kumteta, n.k. ni makosa makubwa sana mbele ya Allah (s.w) kama ilivyo makosa makubwa kumfanyia Muislamu. Heshima ni haki inayomstahiki kila mwanadamu pasi na ubaguzi wa aina yoyote. Ni dhima ya serikali ya Kiislamu kulinda heshima ya kila mtu.

**(v) Sheria ya Mtu binafsi**

Katika sheria ya Kiislamu, mambo yote yanayohusu imani ya mtu binafsi huhukumiwa kulingana na imani ya dini yake. Kama jambo lililoharamishwa kwa Waislamu si haramu kulingana na imani ya Dhimmi, sheria itaendelea kumruhusu kulitenda jambo hilo.

## Zoezi la Tatu

1. Eleza maana ya sheria kilugha na kisheria.
2. Taja na kufafanua kwa muhtasari kazi za sheria katika jamii na manufaa yake.

3. Sheria zilizotungwa na wanadamu hazizingatii umbile halisi la mwanadamu, hivyo huzidisha matatizo badala ya kutatua. Jadili kwa kutoa mifano hai toka katika jamii yako.

4. Bainisha udhaifu uliopo kwenye chimbuko la sheria zilizotungwa na wanadamu kwa msukumo wa matashi na mahitaji, uzoefu, sayansi, akili na fikra zao.

5. (a) Taja misingi mikubwa miwili ya sheria za Kiislamu.
(b) Eleza maana ya **Al-Qiyaas** na **Al-Ijima'a**; na tafauti zake.

6. Eleza kwa muhtasari, kwanini sheria za Allah (sw) ndizo zenye uwezo wa kuondoa dhulma na ukandamizaji, na kusimamisha haki na uadilifu katika jamii.

7. (a) Taja makundi mawili ya amali za waja kwa mujibu wa Qur'an.
(b) Orodhesha daraja tatu za matendo mema.

8. Kazi ya Sheria za Kiislamu, ni kumnufaisha na kumhifadhi mwanaadamu.Thibitisha kwa dondoo tano zenye maelezo mafupi.

9. Bainisha
(a)Kanuni tatu zenye kumtwika au kumvua mja dhima ya kuhukumu au kuhukumiwa katika sheria ya Kiislamu.
(b) Utaratibu wa mashitaka wa Kiislamu.
(c) Tanzu za makosa katika sheria ya Kiislamu.

10. Uislamu ni mfumo wa maisha wa kiadilifu, hivyo, haunyimi wala kukandamiza haki za wasiokuwa Waislamu. Dhihirisha ukweli huu kwa kurejea Qur'an na Sunnah.

## Sura ya Nne

## UCHUMI

### Maana ya Uchumi

Mfumo wa maisha wa Kiislamu humuelekeza binaadamu kujenga na kudumisha uhusiano wake na Allah (s.w), uhusiano wake na binaadamu wenziwe na uhusiano wake na vinavyomzunguka katika ulimwengu huu. Aidha mfumo wa Kiislamu una lengo la kuelekeza namna ya kukiendea kila kipengele muhimu cha maisha ya binaadamu **uchumi** ukiwa miongoni.

Uchumi hujumuisha uzalishaji, usambazaji na utumiaji wa mali na huduma. Uislamu umelipa suala la uchumi nafasi muhimu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَا تُؤْتُوا۟ ٱلسُّفَهَآءَ أَمْوَٰلَكُمُ ٱلَّتِى جَعَلَ ٱللَّهُ لَكُمْ قِيَٰمًا

*"Wala msiwape wapumbavu mali zenu ambazo Allah amezijaalia kuwa msingi wa maisha yenu..." (4:5)*

Uislamu umeweka utaratibu wa kiuchumi unaohakikisha kuwa haki inatendeka kwa wote ili kudumisha amani, utulivu na mshikamano wa kweli katika jamii. Katika sura hii tutaangalia uchumi katika Uislamu kwa kuzingatia maeneo yafuatayo:

1. Nadharia ya uchumi wa Kiislamu.
2. Umuhimu wa uchumi katika Uislamu.
3. Mazingatio muhimu katika uchumi wa Kiislamu.
4. Sera ya uchumi katika Uislamu.
5. Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu.
6. Mgawanyo wa mali katika Uislamu.
7. Umuhimu wa Benki katika Uchumi.
8. Tatizo la Riba.

***1.Nadharia ya uchumi wa Kiislamu***

Mfumo wa uchumi katika Uislamu ni utaratibu utokanao na Qur-an na Sunnah juu ya uzalishaji, umilikaji, usambazaji, na utumiaji wa mali na huduma pamoja na miiko yake. Kwa msingi huo, uchumi huo umejengwa juu ya fikra ya ukati na kati (Iqtisaad), hivyo umetofautiana na mifumo mingine iliyobuniwa na watu. Dhana (concept) ya ukati (Iqtisaad) katika shughuli za kiuchumi ni kule kutoa uhuru kwa mtu binafsi (sekta binafsi) kuchuma na kumiliki mali ili iwe motisha kwake ya kuchapa kazi wakati huo huo serikali ikisimamia na kutoa miongozo katika uzalishaji na ugawaji, na vile vile kuwa na sekta zake (sekta za umma) ili kila mwana jamii apate haki za kimsingi. Mifumo iliyobuniwa na watu imeathiriwa na udhaifu wa kibinaadamu wa kuelemea upande huu au ule.

Ipo mifumo ya kiuchumi kama vile ubepari ambao umeelemea mno katika ubinafsi kiasi ambacho umepuuza kabisa haki za kijamii. Katika mfumo huu (ubepari) umma hauna chake; mali, huduma na shughuli mbali mbali hubinafsishwa. Wachache chini ya mfumo huu ndio hunufaika na rasilimali za Taifa. Hujilimbikizia mali, na motisha yao ya uzalishaji ni ile faida waipatayo. Serikali kuu ya mfumo huu wa kibepari hushirikiana na wachache hao waliohodhi mali, kuwanyonya walio wengi.

Pia, kuna mfumo wa uchumi wa Kikomunist au Kijamaa ambao nadharia yake imeelemea mno katika “**usawa**” wa sare kiasi cha kudhoofisha mno motisha ya watu binafsi na hivyo kupelekea kukosekana kwa ufanisi katika uzalishaji. Katika mfumo huu mali na shughuli mbali mbali hutaifishwa (toka milki ya watu binafsi kuwa milki ya taifa). Ukweli ni kwamba huwa si mali ya taifa kama inavyotangazwa bali mbiu ya “usawa”, na “mali ya umma”, chini ya mfumo huu, ni mwavuli tu uliokinga kikundi cha

watu kilichojipa mamlaka ya uendeshaji wa nchi kwa sura ya chama au serikali kwa maslahi ya kikundi hicho. Kikundi hicho ndicho humiliki na kutafuna mali huku wananchi wengi wakiendelea kudhulumiwa kwa sababu mbali mbali. Hivyo hakuna usawa ulio chini ya mfumo huu bali ni ubinafsi ule ule ambao huhamishwa toka kwa mtu binafsi kwenda kwenye kikundi fulani.

## Tofauti kati ya mfumo wa uchumi wa Kiislamu na ile ya Kitwaghuti

### (i) Dhana ya mafanikio

Katika mtazamo wa uchumi wa Kiislamu mafanikio yanatazamwa kwa kuzingatia hatima ya ama mtu kupata radhi za Mwenyezi Mungu au kubeba laana ya Mwenyezi Mungu.Mafanikio hayapimwi kwa mali. Katika uchumi wa Kitwaghuti mafanikio maana yake ni mafanikio ya kiuchumi. Ni kiasi gani cha mali mtu amefanikiwa kukipata.Jinsi atakavyojilimbikizia mali ndivyo itakavyoonesha "**mafanikio**" yake. Katika Uislamu kufuzu kwa kweli ni kupata radhi za Mwenyezi Mungu na kufeli kukubwa ni kule kukosa radhi hizo. Hivyo ili binaadamu afanikiwe hana budi kuishi kwa uadilifu.

Mtazamo huu unaathiri pia mizani yake ya wakati. Muislamu anapozitumia rasilimali zilizomo katika ardhi hafikirii tu mahitaji yake ya binafsi ya sasa bali pia matokeo ya vitendo vyake kwa vizazi vijavyo.

Kwa mtazamo huu mtu anakuwa hana haki ya kufuja mali au rasilimali za ardhi, kwa vile anazingatia maslahi yake katika maisha haya, huko akhera na maslahi ya viazazi vijavyo. Mafanikio katika Uislamu ni kule kulijua lengo la maisha hapa ulimwenguni, kuwa na kumbukizi ya kisimamo mbele ya Mola siku ya hesabu, kukinai

moyoni na kuona kila kitu cha ulimwengu huu kuwa ni cha kawaida. Kujitahidi kuyaendea mambo mema bila ya kuchelea chochote na kujiepusha na yale yote yanayoweza kumtoa mtu au kumkhasirisha katika maisha yajayo hata kama yana "manufaa" kwa mtazamo wa wengi katika maisha haya. Kujali shida na matatizo ya wengine na kuweza kutoa kwa ajili ya kuwasaidia wengine kwa kadiri ya wasaa uliopo.

Kuwa na huruma, mapenzi na bashasha isiyobagua taifa, kabila, nasabu wala ukoo wa mtu. Kutokuwa na chuki, majivuno, kibri, utesi, usengenyi, ulimbukeni, kujiona, kujitukuza au kujidhalilisha na kujitweza kwa yeyote yule anayemulikwa na jua iwe kihali au kimali.

Aliyetajiri wa Nafsi ni yule ambaye fursa yoyote aliyonayo haiwi kero na huzuni kwa wengine bali huitumia mwisho wa uwezo wake kupambana na taratibu potofu na kandamizi zinazotawala jamii yake. Hii ndiyo Dhana ya mafanikio katika Uislamu.

**(ii) Dhana ya umilikaji mali**

Katika Uislamu mmiliki wa hakika wa mali ni Mwenyezi Mungu, mwanaadamu kama Khalifa wa Allah hapa duniani anamiliki mali kwa dhamana tu siyo kwa hakika na kwa sababu hiyo ataulizwa jinsi alivyotumia hiyo mali.

Pamoja na hivyo mali katika Uislamu si kitu kiovu bali kinachosisitizwa ni kuwa ichumwe na kutumiwa kwa kuzingatia maelekezo ya Mwenyezi Mungu.

Kuhusu kutafuta mali Qur-an inatueleza kama ifuatavyo:

وَٱبْتَغِ فِيمَآ ءَاتَىٰكَ ٱللَّهُ ٱلدَّارَ ٱلْأَخِرَةَ ۖ وَلَا تَنسَ
نَصِيبَكَ مِنَ ٱلدُّنْيَا ۖ

*"Na utafute – kwa yale aliyokupa Mwenyezi Mungu makazi mazuri ya akhera wala usisahau sehemu yako ya dunia". (28:77)*

**(iii)Dhana ya bidhaa**

Katika uchumi wa kitwaghuti kitu chochote chaweza kuwa ni bidhaa maadamu kinaweza kutumiwa na mtu. Kwa mfano pombe pamoja na madhara yake huitwa bidhaa kwa kuwa hutumiwa na baadhi ya watu.

Katika uchumi wa Kiislamu "*bidhaa*" huitwa ama "*Atwayyibaati*" au "*Rizk*". Atwayyibaat ni kitu kizuri, safi, Twahara. Rizk ni neema, au hidaya itokayo kwa Allah (s.w). Hivyo katika uchumi wa Kiislamu bidhaa ni vile vitu halali tu kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Kisichokuwa halali si bidhaa. Kwa mfano pombe ni haramu hivyo si bidhaa.

**(iv)Dhana ya Matumizi**

Kwa kuwa Allah ndiye Muumba wa watu na rasilimali zote katika ulimwengu, sera ya uchumi wa Kiislamu haimpi mtu fursa ya kufuja mali apendayo pamoja na uhalali atakaokuwa nao katika dhamana ya milki ya mali hiyo. Kinyume chake, katika uchumi wa Kitwaghuti mtu anayo fursa ya kufuja mali apendavyo maadam ni mmiliki wa mali hiyo.

**(v) Mizani ya wakati katika tabia ya mtumiaji**

Mtu anapofanya maamuzi yoyote hujiuliza nini matokeo au matazamio ya kitendo hiki au uamuzi huu baada ya

saa moja au wiki moja au mwezi mmoja au mwaka mmoja au miaka mitano au kumi n.k. Kipimo cha wakati katika uchumi wa Kitwaghuti na ule wa Kiislamu ni tofauti. Katika ujahili mtu hujiuliza mali kiasi gani awe amepata atakapofikia umri fulani, kinyume chake Muislamu anapofikiria jambo lolote, pamoja na masuala ya uchumi, kipimo chake cha wakati hukipa upeo mpana sana. Hujiuliza, je hiki kitendo ninachofanya kitakuwa na matokeo gani siyo tu kwa wiki hii au mwezi huu au mwaka huu au ujao bali kina matokeo gani siku ya kiyama. Muislamu anaamini kuwa ipo siku ya malipo na kwamba kuna pepo na moto. Watu watahesabiwa na kulipwa kwa mujibu wa matendo yao. Kila mtu binafsi atasimamishwa peke yake mbele ya Mwenyezi Mungu na kupewa hisabu yake. Imani hii ina athari kubwa kwa Muislamu na maamuzi yake anayochukuwa.

**Milki ya Rasilimali**

Ili kujipatia maendeleo ya kiuchumi katika zama zote mwanaadamu anahitaji rasilimali za kumwezesha kufikia azma hiyo. Miongoni mwa rasilimali kuu (natural resources) ni zile zinazohusiana na ardhi, maji na wanyama. Kwa mujibu wa Uislamu rasilimali hizo ni neema za Allah (s.w).

**(a) Rasilimali za Ardhi**

وَفِى ٱلْأَرْضِ قِطَعٌ مُّتَجَـٰوِرَٰتٌ وَجَنَّـٰتٌ مِّنْ أَعْنَـٰبٍ
وَزَرْعٌ وَنَخِيلٌ صِنْوَانٌ وَغَيْرُ صِنْوَانٍ يُسْقَىٰ بِمَآءٍ وَٰحِدٍ
وَنُفَضِّلُ بَعْضَهَا عَلَىٰ بَعْضٍ فِى ٱلْأُكُلِ ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ لَـَٔايَـٰتٍ
لِّقَوْمٍ يَعْقِلُونَ ﴿٤﴾

*"Na katika ardhi mna vipande vinavyoungana (na kuzaa kwake namna mbali mbali) na mna mabustani ya mizabibu, na mimea mingine, na mitende ichipuayo katika shina moja na isiyochipua katika shina moja. Vyote vinavyonyweshelezwa (vinamiminiwa) maji yale yale; na tunavifanya bora baadhi yake vyengine katika kula (katika utamu). Hakika katika haya zimo ishara kwa watu wanaotia mambo akilini". (13:4)*

**(b) Rasilimali za maji na mvua**

وَتَرَى ٱلْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَآ أَنزَلْنَا عَلَيْهَا ٱلْمَآءَ ٱهْتَزَّتْ
وَرَبَتْ وَأَنۢبَتَتْ مِن كُلِّ زَوْجٍۭ بَهِيجٍ ﴿٥﴾

*"... Na unaiona ardhi imetulia kimya lakini anapoyateremsha maji juu yake, inataharaki na kukuwa na kuotesha kila namna ya mimea mizuri." (22:5)*

أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ أَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً فَسَلَكَهُۥ يَنَٰبِيعَ
فِى ٱلْأَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهِۦ زَرْعًا مُّخْتَلِفًا أَلْوَٰنُهُۥ ثُمَّ
يَهِيجُ فَتَرَىٰهُ مُصْفَرًّا ثُمَّ يَجْعَلُهُۥ حُطَٰمًا ۚ إِنَّ فِى ذَٰلِكَ
لَذِكْرَىٰ لِأُو۟لِى ٱلْأَلْبَٰبِ ﴿٢١﴾

*"Je! Huoni kwamba Mwenyezi Mungu ameteremsha maji kutoka mawinguni. Kisha akayapitisha (chini kwa chini) yakawa chemchem katika ardhi, tena akaotesha kwayo mimea ya rangi mbali mbali (na sura mbali mbali)..." (39:21).*

**(c) Rasilimali za bahari na samaki**

ٱللَّهُ ٱلَّذِى سَخَّرَ لَكُمُ ٱلْبَحْرَ لِتَجْرِىَ ٱلْفُلْكُ
فِيهِ بِأَمْرِهِۦ وَلِتَبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِهِۦ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

*"Mwenyezi Mungu ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite merikebu kwa amri yake, na ili mtafute fadhila yake na mpate kushukuru". (45:12)*

وَهُوَ ٱلَّذِى سَخَّرَ ٱلْبَحْرَ لِتَأْكُلُوا۟ مِنْهُ لَحْمًا طَرِيًّا
وَتَسْتَخْرِجُوا۟ مِنْهُ حِلْيَةً تَلْبَسُونَهَا وَتَرَى ٱلْفُلْكَ
مَوَاخِرَ فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِهِۦ وَلَعَلَّكُمْ
تَشْكُرُونَ ﴿١٤﴾

*"Na yeye ndiye aliyeitiisha bahari ili humo mule daima kitoweo kipya (samaki) na mtoe humo mapambo mnayoyavaa. Na utaona merikebu zikipasua humo, ili mtafute fadhila zake (kwa kufanya biashara) na ili mpate kushukuru." (16:14)*

**(d) Rasilimali za wanyama**

وَٱلْأَنْعَٰمَ خَلَقَهَا ۗ لَكُمْ فِيهَا دِفْءٌ وَمَنَٰفِعُ وَمِنْهَا
تَأْكُلُونَ ﴿٥﴾

*"Na (pia) amewaumba wanyama. Katika hao mnapata (vifaa vitiavyo) joto na manufaa; na wengine mnawala(16:5).*

وَلَكُمْ فِيهَا جَمَالٌ حِينَ تُرِيحُونَ وَحِينَ تَسْرَحُونَ ﴿٦﴾

*Na mnaona raha mnapowarudisha jioni na mnapowapeleka malishoni asubuhi.(16:6)*

وَتَحْمِلُ أَثْقَالَكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَّمْ تَكُونُوا۟ بَٰلِغِيهِ
إِلَّا بِشِقِّ ٱلْأَنفُسِ ۚ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ ﴿٧﴾

*Na (wanyama hao pia) hubeba mizigo yenu kupeleka katika miji msiyoweza kuifikia isipokuwa kwa mashaka na taabu. Hakika Mola wenu ni Mpole sana (na) Mwenye rehema nyingi".(16:7)*

وَٱلْخَيْلَ وَٱلْبِغَالَ وَٱلْحَمِيرَ لِتَرْكَبُوهَا وَزِينَةً ۚ وَيَخْلُقُ
مَا لَا تَعْلَمُونَ ﴿٨﴾

*Na (amewaumba) farasi na nyumbu na punda ili muwapande na (wawe) mapambo. Na ataumba (vipando vyingine) msivyovijua". (16:8).*

**(e) Rasilimali za madini**

Muhutasari wa aya hizo juu ya rasilimali unapatikana katika aya ifuatayo:

هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا

*"Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi." (2:29).*

**Wajibu wa Kufanyakazi**

Uislamu siyo tu unawahimiza watu kufanya kazi na kutokuwa wavivu bali kufanya kazi ni Ibada. Kila jambo lenye manufaa kwa watu binafsi, familia, jamii (n.k) laweza kuhesabiwa kuwa ni Ibada kwa Allah yakitimia masharti mawili; usafi wa nia (Ikhlasi) na kutenda jambo kwa kuzingatia mipaka ya sheria ya Kiislamu. Hivyo kazi ni Ibada. Kufanya kazi ni wajibu alionao mtu mbele ya Allah.Qur-an inawahimiza Waislamu kutenda kazi nzuri zenye manufaa katika eneo lolote lile.

وَقُلِ ٱعْمَلُوا۟ فَسَيَرَى ٱللَّهُ عَمَلَكُمْ وَرَسُولُهُۥ وَٱلْمُؤْمِنُونَ ۗ
وَسَتُرَدُّونَ إِلَىٰ عَٰلِمِ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَٰدَةِ فَيُنَبِّئُكُم بِمَا
كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٠٥﴾

*Na sema: Tendeni mambo (mazuri). Mwenyezi Mungu atayaona mambo yenu hayo na Mtume wake na Waislamu. Na mtarudishwa kwa mjuzi wa siri na dhahiri; naye atakwambieni (yote) mliyokuwa mkiyatenda." (9:105)*

Katika aya hii Mwenyezi Mungu amefungua milango kwa watu kutenda mambo yote mema katika eneo lolote la uchumi au siasa na yeye ataliona na atalilipa.

**Uchaguzi wa kazi**

Uislamu umempa mtu uhuru wa kuchagua kazi yoyote aipendayo maadamu kazi hiyo ni ya halali kwa mujibu wa sheria ya Kiislamu. Na ni wajibu wa serikali ya Kiislamu kuhakikisha kuwa watu wanapata fursa ya kufanya kazi wazipendazo. Watu watafanya kazi kwa mujibu wa vipaji vyao, kwani Mwenyezi Mungu amewajaalia watu vipawa mbali mbali:

وَهُوَ ٱلَّذِى جَعَلَكُمْ خَلَٰٓئِفَ ٱلْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ
فَوْقَ بَعْضٍ دَرَجَٰتٍ لِّيَبْلُوَكُمْ فِى مَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ

*"Na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni." (6:165).*

Kila mtu anafanyiwa mtihani kwa neema au kipawa alichopewa. Katika maisha yetu ya kila siku wanaadamu ni viumbe wanaotegemeana kila mmoja ananufaika kwa kazi ya mwenzake. Daktari atamhitaji Muashi kumjengea nyumba yake na Muashi atamhitaji Daktari kumtibu maradhi yake n.k. Katika Uislamu kazi hutegemea uwezo tu hakuna kazi zilizotengwa kwa ajili ya watu wa ukoo au kabila au nasaba fulani.

**Tofauti ya malipo**

Tofauti ya mapato au malipo ipo kwa sababu ya utendaji, uwingi au ubora wa bidhaa zilizozalishwa. Ni halali kwa fundi aliyetengeneza mashati kumi, hasa amzidi kipato yule aliyetengeneza matano. Au yule aliyetengeneza kitu bora lazima amzidi yule aliyetengeneza kitu duni. Aidha tafauti ya mapato pia ni halali iwepo kutokana na muda mrefu wa mafunzo baadhi ya kazi zikilinganishwa na nyingine. Kwa mfano ikiwa mtu ataajiriwa kufuta mavumbi katika madirisha ya ofisi atahitajia siku moja tu ya kuelekezwa namna ya kuifanya kazi hiyo. Lakini mtu akiajiriwa kutengeneza madirisha hayo atahitajia muda mrefu zaidi katika kujifunza useremala hawezi kuelekezwa kwa siku moja tu halafu akaweza kuunda dirisha. Hivyo malipo ya mfutaji na mtengenezaji wa madirisha hayawezi kuwa sawa. Malipo yao yakiwa sawa basi watu wanaweza

kuzikwepa kazi zinazohitaji mafunzo ya muda mrefu kama udaktari, usanifu majengo uhandisi (n.k.) na kukimbilia zile zenye mafunzo ya muda mfupi kama utarishi, uhudumu, kufagia ofisi n.k.

Aidha malipo hayatakuwa halali iwapo shughuli anayoifanya Muislamu ni faradhi. Kwa mfano; si halali kwa Imamu kupokea mshahara kwa ajili ya kusalisha swala za faradhi, si halali kupokea malipo kutokana na kumhudumia maskini, n.k.

**Hifadhi ya Wafanyakazi**

Uislamu pia umeweka taratibu za kuhifadhi haki na maslahi ya Wafanyakazi. Kwanza kila mfanyakazi lazima awe na mkataba na mwajiri wake. Mkataba huo uweke wazi malipo yake na kazi yake na makubaliano yao mengine. Mkataba huo ni bora uwe kwa maandishi lakini waweza pia kuwa kwa mdomo.

Mwenyezi Mungu ameagiza katika Qur-an kuwa watu watekeleze kikamilifu ahadi zao za halali.

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓا۟ أَوْفُوا۟ بِٱلْعُقُودِ ۚ

*"Enyi mlioamini tekelezeni wajibu ..." (5:1)*

Katika Hadith iliyosimuliwa na Bukhari, Mtume (s.a.w) amesema kuwa miongoni mwa watu watatu ambao Mtume (s.a.w) atawakataa siku ya Kiyama ni yule anayemwajiri mfanyakazi halafu asimpe haki zake.Katika Hadith nyingine amesema;Mlipeni mtu mliyemuajiri kabla ya jasho lake halijakauka. Mradi wa Hadith hii ni kuwa mtu asicheleweshewe malipo yake. Kama mapatano ni kila wiki au kila mwezi n.k. basi muda huo ukifika tu mtu alipwe.Vivyo hivyo kwa mfanyakazi malipo ya kazi yatakuwa

ni halali iwapo atatimiza kipimo walichoafikiana na mwajiri kwa mshahara huo. Kutegea kazi humfanya mtu achukue sehemu ya malipo isiyo haki yake. Kwa hiyo, kipato kinachotokana na kazi iliyotegewa kimechanganyika na kipato cha haramu. Uislamu unamtaka kila muumini awe mwaminifu na muadilifu katika kazi baada ya kupatana na kukubaliana na muajiri.

## 2. Umuhimu wa uchumi katika Uislamu

Mwanaadamu ameumbwa na mahitajio mengi ambayo hana budi kuyapata ili aweze kuishi kwa furaha na amani hapa ulimwenguni. Kwa kuwa mwanaadamu ni mchanganyiko wa mwili na roho, pia mahitajio yake yamegawanyika, ana mahitajio ya kiroho na kimwili. Mahitajio ya kiroho ambayo humuwezesha mwanaadamu kuishi maisha ya utulivu yenye furaha na amani, hupatikana kwa kufuata kwa utii na unyenyekevu mwongozo wa Allah (s.w).

Mahitajio ya kimwili kama vile chakula, mavazi, vipando na njia ya uchumi hupatikana kwa kuchapakazi chini ya mazingira yatokanayo na itikadi sahihi yenye kusimamiwa na viongozi wanaozingatia haki itokayo kwa Muumba. Katika Qur-an tunafahamishwa kuwa Allah (s.w) amejaalia mali anayoichuma mwanaadamu iwe ndiyo inayoboresha maisha yake:

وَلَا تُؤْتُوا۟ ٱلسُّفَهَآءَ أَمْوَٰلَكُمُ ٱلَّتِى جَعَلَ ٱللَّهُ لَكُمْ قِيَمًا

*"Wala msiwape wapumbavu mali zenu ambazo Mwenyezi Mungu amezijaalia kwa ajili ya maisha yenu ..." (4:5)*

Kutokana na aya hii, kuchuma mali si jambo la hiari kwa mwanaadamu kwani kwa namna Allah (s.w) alivyokadiria, maisha ya mwanaadamu kwa hapa ulimwenguni hayawezekani pasi na kuchuma.

Ni kweli kwamba vitu vyote vilivyomzunguka mwanaadamu katika ulimwengu huu vimeumbwa kwa ajili yake kwa ushahidi wa Qur-an:

هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا

*"Yeye ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi..." (2:29).*

Lakini mara nyingi vitu hivi haviko katika hali ya kutumiwa na mwanaadamu moja kwa moja. Bali mwanaadamu analazimika kutumia elimu yake, Maarifa yake, juhudi zake na vipawa vyake vingine ili ayabadilishe mazingira yake yaweze kumtumikia na kukidhi haja zake.

Kwa mtazamo huu Uislamu unatuamrisha kuchuma kama unavyotuamrisha kusimamisha Swala, kutoa Zakat na kutekeleza Ibada nyingine maalumu kama hizi:

فَإِذَا قُضِيَتِ ٱلصَّلَوٰةُ فَٱنتَشِرُوا۟ فِى ٱلْأَرْضِ وَٱبْتَغُوا۟ مِن
فَضْلِ ٱللَّهِ وَٱذْكُرُوا۟ ٱللَّهَ كَثِيرًا لَّعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ١٠

*Na itakapokwisha swala, tawanyikeni katika ardhi mtafute fadhila za Mwenyezi Mungu na mkumbukeni Mwenyezi Mungu kwa wingi, ili mpate kufaulu. (62:10)*

Tunajifunza kutokana na aya hii kuwa, kuchuma ni wajibu unaompasa Muislamu mara tu baada ya kutekeleza

Ibada maalum. Hili linabainishwa katika Hadithi ifuatayo:

> *"Abdullah bin Mus'ud ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: Kutafuta chumo la halali ni faradhi baada ya kutekeleza faradhi nyingine." (Baihaqi).*

Pia Mtume (s.a.w) amebainisha wazi ubora wa kujizatiti katika kutafuta chumo la halali kwenye Hadith ifuatayo:

> *"Miqdam bin Ma'ad Yakrab ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Hapana mmoja wenu aliyekula chakula kizuri kuliko kile alichokula kutokana na kazi ya mkono wake mwenyewe. Na Daud, Mtume wa Allah, alikuwa anakula kutokana na kazi ya mikono yake." (Bukhari)*

Kwa upande mwingine Uislamu unalaani uvivu na kuwategemea wengine pasi na sababu au dharura maalum kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

> *"Jubair bin Awam ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Mmoja wenu kuchukua kamba na kisha akaja na mzigo wa kuni akiwa amebeba mgongoni mwake na akauuza, na kwakufanya hivyo Allah akailinda hadhi yake, ni bora kwake kuliko kuomba omba watu, wakimpa chochote au wasimpe (Bukhari.)*

Mpaka hapo tumejifunza kuwa kwa mtazamo wa Uislamu, uchumi ndio msingi wa maisha ya mwanadamu hapa ulimwenguni na Uislamu umewajibisha kuchuma kwa kila mwenye uwezo.

Ni makosa katika Uislamu mtu mwenye uwezo na afya kubweteka na kuwategemea wengine katika kukidhi mahitaji yake.

**3.Mazingatio muhimu katika uchumi wa Kiislamu**

Kanuni kuu za uchumi katika Uislamu ni:

(i) Kumwamini Allah kuwa ndiye Muumba na mfalme wa ulimwengu huu yaani kumtii Allah katika mambo yote.

(ii) Binaadamu ni Khalifa wa Allah hapa duniani, hivyo wajibu wake ni kusimamisha amri ya Allah.

(iii) Ili kumsaidia mwanaadamu kutimiza wajibu wake kama Khalifa, Allah amemdhalilishia kila kitu katika ulimwengu huu:

ٱللَّهُ ٱلَّذِى سَخَّرَ لَكُمُ ٱلْبَحْرَ لِتَجْرِىَ ٱلْفُلْكُ فِيهِ بِأَمْرِهِۦ وَلِتَبْتَغُوا۟ مِن فَضْلِهِۦ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿١٢﴾

*"Mwenyezi Mungu ndiye aliyekutiishieni bahari ili humo zipite merikebu kwa amri yake ili mtafute fadhila yake na mpate kushukuru". (45:12).*

أَلَمْ تَرَ أَنَّ ٱللَّهَ سَخَّرَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ

*"Je, Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu amevitiisha kwa ajili yenu vilivyomo ardhini…" (22:65)*

أَلَمْ تَرَوْا۟ أَنَّ ٱللَّهَ سَخَّرَ لَكُم مَّا فِى ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَمَا فِى ٱلْأَرْضِ وَأَسْبَغَ عَلَيْكُمْ نِعَمَهُۥ ظَٰهِرَةً وَبَاطِنَةً ۗ

*"Je, Hukuona kwamba Mwenyezi Mungu amekutiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini na anakukamilishieni neema zake zilizo dhahiri na za siri? …" (31:20).*

هُوَ ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ ٱلْأَرْضَ ذَلُولًا فَٱمْشُوا۟ فِى مَنَاكِبِهَا وَكُلُوا۟ مِن رِّزْقِهِۦ ۖ وَإِلَيْهِ ٱلنُّشُورُ ﴿١٥﴾

*"Yeye ndiye aliyefanya ardhi iweze kutumika kwa ajili yenu. Basi nendeni katika pande zake zote na kuleni katika rizki zake na kwake ndiyo marejeo." (67:15).*

Hivyo kuzitumia neema hizo za Allah si dhambi bali ni katika kushukuru.

(iv) Kutokana na wajibu wa Ukhalifa wa Allah, mwanaadamu ataulizwa kwa neema alizompatia na atahesabiwa kwazo, ikiwa ni pamoja na namna alivyochuma na kutumia mali.

(v) Kuwa na mali au kutokuwa na mali nyingi au kidogo si dalili ya ubora au udhalili wa mtu. Hali zote mbili ni mtihani. Anachotazama Allah ni nyoyo za watu.

Misingi au kanuni hizo zikithibiti katika moyo wa mtu zinakuwa na athari kubwa sana katika shughuli za kiuchumi za Muislamu.

Kanuni ya **kwanza** kwa mfano humfanya mtu afuate maamrisho ya Allah na hivyo atafanya kila njia ajiepushe na makatazo yake.

**Pili**, kwa kujua kuwa yeye ni Khalifa tu atajua yeye si mmilikaji wa hakika, hivyo atafuata maagizo ya huyo aliyempa ukhalifa yaani Allah.

**Tatu**, atajua kuwa utajiri si kitu cha kukipigania, bali

mtu apiganie maisha bora na afya katika kutafuta radhi za Allah (s.w).

**Nne**, kwa kujua kuwa atahesabiwa na Allah anayeshuhudia kila kitu ataendesha shughuli zake za kiuchumi kwa kumcha Allah.

### 4. Sera ya uchumi katika Uislamu

**Kwanza**, katika Uislamu utekelezaji wa mambo yote hutegemea zaidi ucha-Mungu wa mtu binafsi na kuogopa kwake kusimamishwa mbele ya Allah na kuhisabiwa, kuliko usimamizi wa vyombo vya dola kama sheria, mahakama, na askari polisi. Hii ni kwa sababu hisabu siku ya kiyama itakuwa kwa kila mtu binafsi. Hapana shaka vyombo vya dola vipo katika Uislamu na vinafanya kazi lakini msisitizo wa utekelezaji wa mambo yote upo katika uadilifu na taqwa kuliko katika kuogopa polisi na mahakama.

**Pili**, uhuru wa watu binafsi kufanya wanalolitaka ndio sera inayofuatwa katika Uislamu. Yaani katika masuala ya uchumi Uislamu umempa uhuru kila mtu afanye lile analoliona linafaa. Na serikali ya Kiislamu haitaingilia uhuru wake huo isipokuwa tu pale ambapo haki haitatendeka iwapo uhuru huo hautaingiliwa. Mtume (s.a.w) amelielezea kwa ufasaha sana suala hili pale alipoyapigia mfano maisha ya watu katika jamii na wasafiri waliomo chomboni baharini:

> *"Hebu tuchukue mfano wa meli inayosafiri baharini ikiwa imejaza abiria ambao wamekaa katika sehemu zote za chini na juu. Sasa iwapo abiria mmoja aliyekaa katika sakafu hiyo ataamua kujipatia maji kirahisi kwa kutoboa pale alipoketi na iwapo abiria wengine watamzuia kufanya hivyo (na ni wajibu wa abiria wote walio juu na chini kumzuia) watamnusuru yeye na wao wenyewe na*

*kufa maji. Iwapo watamwacha atoboe basi watazama wote waliochini na juu ya meli." (Bukhari).*

Mfano huu unatuonesha kuwa japo Uislamu unampa kila mtu uhuru wa kufanya alitakalo lakini uhuru huo una mipaka. Iwapo mtu atafanya jambo lisilo la haki basi serikali ya Kiislamu lazima iingilie kati kwa maslahi ya jamii nzima.

**Tatu**, wajibu mkubwa wa serikali ya Kiislamu ni kusimamia haki na kuzuia dhulma katika maisha ya jamii.

**Haki ya Serikali kuzuia Dhulma**

**Kwanza**, serikali ya Kiislamu inao wajibu wa kuandaa mazingira mazuri ya kihuduma na kimawasiliano kuwawezesha raia kujiletea maendeleo na inao wajibu wa kuingilia kati ili kusimamia haki na kuzuia dhulma. Ni wakati gani kwa mfano ambapo serikali inaweza kuingilia kati. Allah ndiye aliyeziumba rasilimali zilizopo duniani na hivyo ni wajibu wa binaadamu kuzitumia rasilimali hizo kwa manufaa ya watu na kwa ufanisi. Hivyo serikali yaweza kuingilia kati iwapo rasilimali hizo zitatumiwa kuwadhulumu watu au hazitatumika kwa ufanisi.

**Pili**, baadhi ya kazi ni haramu katika Uislamu kwa sababu zimefungamana na mambo ya haramu, kama vile kamari, umalaya, uchawi, ulevi n.k. Ni wajibu wa serikali kuona kuwa mambo hayo hayapewi nafasi katika jamii.

**Tatu**, ni wajibu wa serikali pia kutoa fursa sawa kwa watu wote ya kuendeleza na kuvikuza vipaji vyao kwa kuwapa fursa sawa za elimu na mafunzo. Ni wajibu wa serikali kugharamia elimu kwa ajili ya manufaa ya watu wote. Elimu ni haki ya msingi kwa wanadamu wote.

**Nne**, ni wajibu pia wa serikali kuhakikisha kuwa hata

katika zile kazi za halali kisheria zinafanywa kwa uadilifu pasi na dhulma yoyote. Yaani Serikali ihakikishe mathalani kuwa bidhaa zinazotolewa zimefikia ubora kwa wanaoizalisha, kuona kuwa uadilifu wa kitaalamu unadumishwa, kuona kuwa Wafanyakazi wanalipwa mishahara kwa haki.

Hata hivyo, Uislamu hauelemei upande mmoja tu wa kumtetea mfanyakazi peke yake wala kumtetea mwajiri peke yake. Wafanyakazi pia wakileta madai yasiyo ya haki ni juu ya serikali kuingilia kati.

**Tano**, ni wajibu wa serikali pia kuzuia mambo yanayoweza kudhuru watu, kwa mfano kama mtu akijenga kiwanda cha hatari katika makazi wanamoishi watu. Au hata mambo yanayoweza kuwatesa wanyama, kama kuwabebesha mizigo mizito sana hadi wanaanguka na kuvunjika miguu au kufa, au kuwafanyisha kazi kwa mateso makubwa na kutowapa chakula cha kutosha. Hali kadhalika serikali inaweza kwa mfano kuzuia magari au meli iliyopakia abiria au mizigo kuliko uwezo wake.

**Sita**, katika suala la usambazaji wa bidhaa, serikali inaweza kuingilia kati iwapo watu watahodhi vyakula na bidhaa nyingine muhimu kwa lengo la kupandisha bei.

**Saba**, ni wajibu wa serikali kujenga miundo mbinu (infrastructures) na kuidhibiti, kwa mfano kujenga barabara, madaraja, reli, kusambaza maji ya bomba, kujenga mitambo ya umeme, simu n.k.

Wakati wa Ukhalifa wake, Ali (r.a) alimwambia Nahri, ambaye alikuwa mkuu wa jimbo la Misri; “Usifanye ukusanyaji wa kodi ya ardhi kuwa ndiyo kazi yako kubwa; kazi yako kubwa ni kuindeleza ardhi hiyo.”

**Nafasi ya serikali katika ugawaji**

Katika suala la ugawaji, wajibu wa serikali ya Kiislamu upo katika maeneo makuu yafuatayo:

(i) Kusimamia utoaji na ukusanyaji wa zaka. Serikali ndiyo yenye wajibu wa kuhakikisha kuwa kila anayepaswa kutoa Zaka anatoa na serikali inasimamia ukusanyaji wake.

(ii) Kutoza na kukusanya kodi iwapo zaka haikutosha.

(iii) Kutoza na kukusanya Jizya (aina ya kodi) kutoka kwa wasiokuwa Waislamu (dhimmi) wanaoishi katika dola ya Kiislamu.

(iv) Serikali ya Kiislamu pia inao wajibu wa kuchukua hatua za kupunguza tafauti kati ya maskini na matajiri, kwa kugawa Zakat na kutoa huduma muhimu bure kwa maskini.

**5. Haki na Uhuru wa kuchuma katika Uislamu**

Kwa kuwa kuchuma kwa njia za halali ni wajibu kwa kila mwenye uwezo wa kufanya kazi, hapana budi kila mtu kupewa uhuru kamili wa kutumia juhudi yake na vipawa vyake katika kuchuma kwa njia za halali. Katika Uislamu ni kosa kubwa kwa serikali au Dola kuweka vikwazo vya kuwazuia watu wasitumie vipaji vyao na uwezo wao wote katika kuchuma kwa njia za halali. Kinyume chake, serikali au dola ya Kiislamu ina wajibu wa kuondoa vikwazo vyote vinavyowazuia watu kutumia vipawa vyao vyote katika kuchuma na inawajibu pia wa kutoa motisha na vishawishi vya kuwavutia watu binafsi au watu waliojiunga katika vikundi wajiingize katika sekta mbali mbali za uchumi kwa juhudi kubwa na maarifa.

Pamoja na uhuru kamili uliotolewa na Uislamu wa kuchuma kwa njia za halali kwa kadri ya uwezo wa kila mtu, pia unampa kila mtu haki ya kumiliki kila alichokichuma kwa njia za halali kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَلَا تَتَمَنَّوْاْ مَا فَضَّلَ ٱللَّهُ بِهِۦ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ
بَعْضٍ ۚ لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا ٱكْتَسَبُواْ ۖ وَلِلنِّسَآءِ نَصِيبٌ
مِّمَّا ٱكْتَسَبْنَ ۚ وَسْـَٔلُواْ ٱللَّهَ مِن فَضْلِهِۦٓ ۗ إِنَّ ٱللَّهَ كَانَ
بِكُلِّ شَىْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

*"Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu kuliko wengine wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma, na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma. Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu. (4:32)*

**Biashara**

Biashara imepewa hadhi ya juu katika Qur-an na katika Hadith za Mtume (s.a.w) kwa sababu ya umuhimu wake katika kuwaunganisha wanaadamu na kuharakisha maendeleo yao.

Kihistoria, maendeleo ya ulimwengu yalianza pale biashara ilipopanuka na kuufanya utajiri wa ulimwengu ufike katika kila kona ya dunia.

Tunafahamu kilimo na viwanda ni shughuli muhimu

sana kwa maisha ya binaadamu, lakini mazao ya shambani na bidhaa za viwandani bila ya kusambazwa kwa watu wanaozihitaji, binaadamu bado watabakia katika hali duni. Inatokea hivyo kwa sababu binaadamu hakuumbwa kujitegemea kwa kila kitu. Vipaji, bahati na fursa havikugawanywa sawa sawa kwa kila mtu au kwa kila nchi ya ulimwengu katika nyanja zote za maisha.

Kiungo kikubwa cha ushirikiano huu ni biashara kati ya watu wa jamii moja au nchi moja na nyingine. Hivyo biashara ina umuhimu wake katika maisha ya binaadamu na maendeleo yake. Uhalali na msisitizo wa biashara uko bayana katika Qur-an:

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمۡ قَالُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡبَيۡعُ مِثۡلُ ٱلرِّبَوٰاْۗ وَأَحَلَّ
ٱللَّهُ ٱلۡبَيۡعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْۚ

*"... Haya ni kwa sababu wanasema: "biashara ni kama Riba" hali Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na kuiharamisha riba..." (2:275)*

Katika aya hii tunafahamishwa wazi kuwa Allah ameihalalisha biashara na kuiharamisha riba. Hivyo biashara yoyote itakayoambatana na riba. Kuuza kwa mkopo wa riba itakuwa ni biashara haramu. Katika kuonesha ubora wa biashara Mtume wa Allah amesema:

*"Mfanya biashara mkweli na mwaminifu (mcha Mungu) atakuwa pamoja na Mitume, Masadiq na Mashahidi". (Tirmidh, Ibn Majah)*

Malipo haya kwa mfanyabiashara yatapatikana tu iwapo atakuwa mkweli na mwaminifu katika biashara yake. Akiwa kinyume cha hivyo atakuwa pamoja na maasi katika

siku ya Kiyama kama tunavyofahamishwa katika Hadith nyingine inayosema:

*"Ubaid bin Rafa'a kutoka kwa baba yake ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) amesema: "Wafanyabiashara watakusanywa pamoja na wakosaji ila wenye kumuogopa Allah, wacha Mungu na wakweli." (Ibn Majah na Tirmidh).*

Kwa hiyo ili biashara iweze kuleta mafanikio kwa mfanyabiashara na kwa jamii kwa ujumla, hapana budi kufuata miiko na taratibu zilizowekwa na Uislamu.

**Kwanza**, pasiwe na udanganyifu wowote katika uuzaji na ununuzi. Kila mmoja kati ya muuzaji na mnunuzi anatakiwa awe mkweli na mwaminifu kwa mwenzake. Hebu tuzingatie Hadith ifuatayo:

*Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Allah amrehemu yule ambaye ana mahusiano mema wakati akiuza, akinunua na wakati wa kutoa uamuzi." (Bukhari).*

Jambo muhimu la kuangalia, katika biashara ni uaminifu katika upimaji kwa vipimo vya uzito, urefu, na ujazo. Wafanyibiashara walio wengi huanguka kwenye mtihani huu wa vipimo na huishia katika laana ya Allah (s.w). Qur-an imesisitiza mno kuchunga haki katika vipimo:

وَأَوْفُوا۟ ٱلْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنُوا۟ بِٱلْقِسْطَاسِ ٱلْمُسْتَقِيمِ ۚ

ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾

*"Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni." (17:35)*

أَوْفُوا الْكَيْلَ وَلَا تَكُونُوا مِنَ الْمُخْسِرِينَ ﴿١٨١﴾ وَزِنُوا
بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ﴿١٨٢﴾ وَلَا تَبْخَسُوا النَّاسَ
أَشْيَاءَهُمْ وَلَا تَعْثَوْا فِي الْأَرْضِ مُفْسِدِينَ ﴿١٨٣﴾

*"Kijazeni kipimo cha pishi sawa sawa wakati mnapopima; (msidhulumiane) wala msiwe miongoni mwa wapunguzao. Na pimeni kwa mizani iliyo sawa (pia). Wala msiwapunguzie watu vitu vyao, wala msitembee katika ardhi mkifisidi." (26:181-183).*

Pamoja na msisitizo huu Allah (s.w) anatufahamisha katika Qur-an kuwa aliiangamiza kaumu ya Nabii Shuayb (a.s) kwa sababu ya kukithiri kwao katika kuwapunja watu katika vipimo katika biashara. Maangamizi hayakuishia kwenye kaumu ya Shuayb (a.s) tu bali Allah (s.w) ameahidi maangamizi kwa kila mwenye kupunja katika vipimo kama inavyodhihirishwa katika aya zifuatazo:

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١﴾ الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ
يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَو وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾
أَلَا يَظُنُّ أُولَٰئِكَ أَنَّهُم مَّبْعُوثُونَ ﴿٤﴾

*"Maangamizi yatawathibitikia wapunjao wenziwao. Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili. Lakini wanapowapimia kwa kipimo cha vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza. Je! Wao hawafikiri ya kwamba watafufuliwa? (83:1-4)*

Waislamu hatuna budi kuwa macho sana katika vipimo vya uzito, ujazo na urefu tunavyotumia katika biashara zetu. Kutokana na msisitizo uliopo katika Qur-an mtu hata ajiite Muislamu mwenye kusali swala zote, akatoa zakat na sadaqa, akafunga, na akahiji, ataangamia na kuishia Jahannam iwapo katika biashara yake atakuwa anawapimia watu kwa ujanja ujanja.

Ugongaji wa vipimo vya ujazo na kuuza bei ya kipimo kizima, utegesheaji wa mizani, ugongaji wa mizani ili ishuke kabla ya kipimo kukamilika, uchanganyaji wa bidhaa mbovu na nzuri na kuiuza kwa bei nzuri (n.k.) ni miongoni mwa udanganyifu katika biashara. Mfanyabiashara wa namna hii ndiye yule Mtume (s.a.w) aliyesema atafufuliwa pamoja na waovu watakaoingia motoni. Pia tumefahamishwa katika Hadithi kuwa:

> *Wasikh bin Asqa'a ameeleza: Nimesikia Mtume wa Allah akisema: Anayeuza bidhaa mbovu bila kuonesha ubovu wake ataendelea kuwa katika laana ya Allah na malaika wataendelea kumlaani." (Ibn Majah).*

**Pili**, katika biashara pasiwe na viapo kwani hii ni miongoni mwa kuuza kwa ujanja-ujanja. Bidhaa iliyoapiwa sana na mwenye kuuza, inaweza imhadae mnunuzi aidhanie kuwa ni nzuri zaidi kuliko hali halisi. Mnunuzi atakapogundua baadaye ataona kuwa amedanganywa kwa viapo. Hivyo viapo vingi kwenye biashara, kwa muuzaji au mnunuzi vimekatazwa kwa sababu vina hila ndani yake. Mtume (s.a.w) ameonya katika Hadith ifuatayo:

> *Abu Qatada ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema, "Kuwa muangalifu na viapo vingi katika uuzaji, kwa sababu japo kuwa kunarahisisha uuzaji, kuna punguza baraka. (Muslim).*

Kuapa sana katika biashara kuna hadaa, kwa sababu wanunuzi wanapogundua kuwa wamedanganywa kwa viapo, na kumbe bidhaa hiyo haikuwa nzuri kiasi walichotarajia, hawatapendelea tena kununua kwa mfanya biashara huyo.

**Tatu**, katika biashara pawe na uhuru kamili kwa mnunuzi wa kuikataa au kuikubali bidhaa baada ya kuiangalia. Uhuru wa kuikataa bidhaa unaendelea kwa mnunuzi hata baada ya kununua, iwapo atagundua dosari yoyote katika bidhaa hiyo kabla ya kuanza kuitumia bidhaa hiyo. Vile vile muuzaji anayohaki ya kukataa au kukubali kuuza bidhaa yake kwa bei anayoridhika nayo kabla ya mkataba wa kununua hauja kamilika. Muuzaji hana uhuru wa kuitaka bidhaa irudishwe baada ya mkataba wa kuuza na kununua kukamilika labda kwa mapatano yaliyofanywa katika mkataba wa kuuziana. Kuhusu jambo hili la uhuru wa uamuzi wa muuzaji na mnunuzi katika kuuza na kununua bidhaa, tunafahamishwa katika Hadith ifuatayo kuwa:

> *Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Mnunuzi na muuzaji kila mmoja katika wao ana uhuru wa mapatano na mwenzake ili mradi tu hawajaachana ila kwa uhuru wa uamuzi wa ununuzi (anaweza akakataa bidhaa hata baada ya kuelewana)." (Bukhari na Muslim).*

Katika maelezo ya Muslim – wakati mnunuzi na muuzaji wanauziana kila mmoja katika wao ana uhuru wa uamuzi kutokana na mauzo au manunuzi yake, ili mradi tu wawe hawajaachana au wameuziana kwa mapatano. Kama kuuziana kwao ni kwa mapatano basi kila mmoja atafungika (kulingana na mapatano hayo).

Biashara yoyote itakayoendeshwa kwa kumnyima uhuru muuzaji au mnunuzi ni biashara haramu ambayo

haimnufaishi mnunuzi wala muuzaji. Kutokana na uzoefu wetu tunayaona haya katika mazingira yetu. Ni mara ngapi tumeona watu wakilazimishwa kununua bidhaa wasizozipenda wala kuzihitaji? Kwa mfano utaona mtu akilazimishwa kununua kilo ya unga wa muhogo usiofaa kula kabisa, ili apatiwe kilo ya sukari anayohitajia. Huu ni uuzaji wa hila na ni uuzaji wa haramu. Kuna mifano mingi kama hii, Uislamu umetoa uhuru kwa muuzaji na mnunuzi.

Kwa ujumla utaona biashara itakayoendeshwa kwa misingi ya Kiislamu iliyoelezwa hapa kwa ufupi, ndio pekee biashara halali na ndio pekee yenye kutumainiwa kuleta ushirikiano, umoja, ustawi na amani ya kweli ulimwenguni. Kisiasa na kiuchumi inafahamika wazi kuwa matatizo mengi yanayoukabili ulimwengu katika nyakati zote za historia yanasababishwa na kukiuka misingi ya haki ya biashara na ya uchumi, kwa ujumla aliyoiweka Allah (s.w).

Kwa hiyo Waislamu hatuna budi kujua kuwa utatuzi wa matatizo yanayoukabili ulimwengu ni kusimamisha misingi ya Uislamu katika nyanja zote za maisha, hasa katika nyanja za uongozi na uchumi ambazo ndizo roho ya jamii.

**Biashara haramu**

Biashara inaweza kuwa haramu kwa namna mbili: kwanza kwa kutofuata misingi ya halali iliyowekwa na Allah (s.w). Pili, kuna biashara ambayo moja kwa moja imeharamishwa hata kama misingi ya halali itafuatwa. Kwa maana nyingine kuna biashara ambazo zimeharamishwa katika nafsi yake yenyewe. Katika kipengele hiki tutaorodhesha biashara ambazo zimeharamishwa moja kwa moja katika nafsi yake na Hadithi mbali mbali za Mtume (s.a.w).

**(i) Muzabanah**

Ni kunufaika kibiashara kutokana na matatizo ya watu wengine. Ni haramu kufaidi shida ya mwengine katika biashara. Uislamu unataka mwenye shida asaidiwe na wala asikandamizwe kutokana na shida yake. Biashara ya Muzabanah imeharamishwa kwa muuzaji na mnunuzi. Uislamu unasisitiza kuwa kinachouzwa na kinachobadilishwa nacho ni lazima kifahamike kwa mnunuzi na muuzaji.

**(ii) Mu'awamah**

Huu ni uuzaji wa matunda, nafaka, na mazao mengine ya shambani kabla ya kukomaa kiasi cha kufaa kuliwa; na ni haramu kama inavyosisitizwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Umar ameeleza kuwa Mtume (s.a.w) ameharamisha kuuza matunda shambani mpaka yaive. Ameharamisha kwa muuzaji na mnunuzi (wamekubaliana Bukhari na Muslim). Na katika maelezo ya Muslim: (Mtume) aliharamisha kuuza tende mpaka ziive na nafaka mpaka ziwe nyeupe na zisiwe zenye kudhuriwa tena na madhara mbali mbali.*

*Jabir ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kuuza (kwa matunda yangali mtini) kwa kipindi cha miaka, na ameamrisha kungojea kwanza yawe tayari (kiasi cha kutoweza kudhuriwa na chochote). (Muslim).*

**(iii) Hablul-Habalah**

Kuuza kilichotumboni kabla hakijazaliwa. Kwa mfano kuuza mimba ya ng'ombe, mbuzi, kondoo, ngamia, n.k ni haramu. Tunafahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Umar ameeleza kuwa Mtume Mtukufu ameharamisha mauzo ya Habalul-Habalah; na ni uuzaji waliokuwa wakiufanya watu majahili. Mtu alikuwa akinunua ngamia*

*mpaka ngamia jike lishike mimba na mpaka hicho nacho katika tumbo la uzazi kiwe na mimba. (Bukhari na Muslim).*

Jambo linalosisitizwa katika Hadithi hii ni kwamba imeharamishwa kuuza mimba kwani ni jambo ambalo halina uhakika kabisa. Ajuaye na mwenye uhakika wa kuzaliwa au kutozaliwa kilichomo tumboni ni Allah (s.w) peke yake. Kwa hiyo uuzaji wa mimba ni uuzaji wa patapotea (uuzaji hewa).

**(iv) Uuzaji wa bidhaa kabla hazijamfikia mnunuzi ni haram**,

Ununuzi au uuzaji hauhusiki mpaka mnunuzi ashuhudie bidhaa anazouziwa. Hivyo ndivyo tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Ibn Abbas ameeleza: "Katika mauzo aliyoyaharamisha Mtume (s.a.w) ni mauzo ya chakula mpaka yawe mikononi mwa mnunuzi..." (Bukhari na Muslim).*

Msisitizo wa Hadithi hii ni kwamba mtu asiuze kitu ambacho hajakishuhudia machoni mwake au machoni mwa mwakilishi wake.

**(v) Uuzaji wa bidhaa njiani kabla ya wauzaji kufikisha bidhaa sokoni**.

Wakati mwingine wafanya biashara hufanya ujanja kwa kuteka nyara bidhaa njiani kabla hazijaingia sokoni ili kuwaghilibu na kuwapumbaza wauzaji ambao hawajajua bei halisi ya bidhaa ile sokoni.

Ununuzi wa namna hii ni ulanguzi na umeharamishwa katika Uislamu kama inavyosisitizwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Usimfuate mfanya biashara wa nafaka mkakutana naye njiani kabla (ya kuingia sokoni). Na endapo atanunua kutoka kwake-atakapoingia sokoni na kujua hali halisi ya soko ana haki ya kukataa mauziano ya awali. (Muslim, Bukhari).*

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Usikutane (usiteke nyara) bidhaa njiani mpaka zitakapofikishwa sokoni." (Bukhari na Muslim)*

Kununua bidhaa iliyonunuliwa na mwingine kwa kulipa bei kubwa zaidi au kwa sababu nyinginezo ni haramu kama inavyobainishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Hapana mapatano ya atakayenunua kitu yatayofanyika baada ya mwenzake kununua na hapana atakayemchumbia ambaye ameshachumbiwa na mwenzake (ndugu yake) mpaka apate ruhusa kutoka kwake (huyo) aliyeanza na kupatana bei au aliyeanza kuchumbia." (Muslim).*

Kinachosisitizwa katika Hadithi hii ni kwamba, Muislamu haruhusiwi kununua bidhaa iliyonunuliwa na mwingine. Mara nyingine kwa sababu ya husuda au uroho matajiri huweza kuwashawishi watu wenye uroho kama wao wakaamua kuvunja mkataba wa mauzo uliofanyika hapo awali ili apate bei kubwa kwa huyu mteja aliyejitokeza baada ya mauzo kwa yule mteja wa kwanza.

(vi) Kuuza maji au majani ambayo mtu hakuyagharamikia chochote imekatazwa katika Hadithi zifuatazo:

*Jabir amesimulia kuwa Mtume wa Allah amekataza (ameharamisha) kuuza maji ya asili. (Muslim).*

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Majani ya asili hayatauzwa ili kununua malisho yaliyomo. (Bukhari na Muslim).*

Hadithi hizi zinatufundisha kuwa mali asili kama maji, majani, miti ya porini (n.k.) ni haki ya kila mwanaadamu kwa hiyo hapana mwenye haki ya kuzuia mali ya asili na kuifanya yake na kuwauzia watu wengie. Bali kama mali asili imeshughulikiwa ndio ifae kutumika, itajuzu mwenye kuishughulikia awe na haki ya kudai arudishiwe gharama alizozitoa katika shughuli hiyo. Kama gharama za bomba, na mashine ya kusukumia maji na kadhalika.

Lakini kuyauza maji ya chemchem ya asili au mto ni haramu.

(vii) Uuzaji wa samaki aliyeko majini, uuzaji wa ndege anayeruka angani (ambaye hafugwi), uuzaji wa maziwa ambayo hayajakamuliwa na uuzaji wa manyoya ya mnyama yangali mwilini mwake ni uuzaji haramu. Ni wazi kuwa mauzo yote haya yameharamishwa kwa sababu bidhaa hizo hazina uhakika wa kuzipata. Ili pawe na haki kati ya muuzaji na mnunuzi bidhaa hizo hazina budi kupatikana kwanza mkononi ndio ziuzwe.

(viii) Uuzaji wa damu na uuzaji wa uhuru wa mtu (utumwa) uuzaji wa nywele na maziwa ya binaadamu ni biashara haramu. Vitu vyote hivi si haki ya mwanaadamu na havipatikani kutokana na jasho lake. Hivyo hana haki ya kuviuza na wala hana hata uwezo wa kukadiria thamani yake halisi. Kama hatuwezi kukadiria thamani ya mvuto mmoja wa hewa au thamani ya tone moja la maji, tunaweza kukadiria thamani ya damu, achilia mbali thamani ya maisha yetu?

(ix) Mauzo ya mbwa, nguruwe, pombe, damu na mzoga ni biashara haramu. Pia ni haramu kuuza picha na sanamu kama tunavyofahamishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kipato kilichotokana na kuuza damu, mbwa, na kipato cha Malaya. Na amelaani mwenye kupokea na mwenye kutoa riba, na mwenye kuchora mwili kwa chale na mwenye kuchorwa mwili kwa chale na mchoraji wa picha (za wanyama) na watu. (Bukhari).*

*Jabir ameeleza kuwa amemsikia Mtume wa Allah akisema katika mwaka wa ushindi (wa kuiteka Makka) wakati alipokuwa Makka.Hakika Allah na Mtume wake wameharamisha mauzo ya pombe; mizoga, nguruwe na masanamu. (Bukhari na Muslim).*

**(x) Ulanguzi (Kuhodhi bidhaa)**

Hili ni neno pana linalotumiwa kwa maana mbali mbali; lakini katika kipengele hiki tutalitumia neno hili kuwakilisha kitendo cha kuteka nyara bidhaa muhimu sokoni kwa kuinunua kwa wingi labda kwa bei ya juu kidogo kwa madhumuni ya kuilundika (kuihodhi) na kuifanya iwe adimu ili hapo baadaye itakapokosekana sokoni iuzwe kwa bei ya juu sana na kutoa faida kubwa sana.

Biashara ya namna hii ni biashara haram kama tunavyofahamishwa katika Hadithi kadhaa zifuatazo:

*Umar amesimulia kutoka kwa Mtume wa Allah aliyesema: "Mwenye kuleta nafaka (mjini) anazidishiwa rizki na mkusanyaji na mfichaji wa bidhaa hizo amelaaniwa." (Ibn Majah, Dirimi).*

*Umar amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Anayelundika na kuzuia bidhaa za chakula kwa siku 4 kwa nia ya kupata bei kubwa zaidi, anajitenga na Allah na Allah anajitenga naye." (Razin).*

Hadithi zote hizi zimedhihirisha ubaya wa kuzuia bidhaa, hasa bidhaa muhimu kama vile chakula, na kuzifanya ziwe adimu ili kuuza kwa bei kubwa itakayotoa faida kubwa sana. Biashara ya namna hii ni biahara haramu na laana ya Allah iko juu ya walanguzi hawa:

*Mu'az amesimulia: Nimemsikia Mtume wa Allah akisema: "Mbaya ni yule anayelundika bidhaa na kuifanya iwe adimu. Kama Allah akifanya bidhaa kuwa rahisi, yeye anachukia na kama Allah akifanya kuwa ghali, anafurahi. (Razin, Baihaqi).*

Hadithi hii inatueleza sura hasa ya mlanguzi. Ama mtu kuweka bidhaa alizozilima na alizotengeneza mwenyewe au kuuza bidhaa alizozinunua kutoka masafa ya mbali si haramu. Lililoharamishwa ni kule kununua bidhaa katika soko la kawaida na kuzificha ili baadaye aziuze kwa bei kubwa baada ya bidhaa hiyo kuwa adimu katika soko.

Pamoja na Uislamu kulaani ulanguzi, hauruhusu kumkangandamiza mfanyabiashara kwa kumuwekea bei ya bidhaa yake. Bei inatakiwa ijiweke yenyewe kulingana na hali halisi ya soko. Bidhaa zikiwa nyingi bei itakuwa chini na bidhaa zikiwa chache itakuwa juu. Tunajifunza kutokana na Hadithi ifuatayo:

*Anas amesimulia kuwa wakati mmoja katika wakati wa Mtume wa Allah bei ya vitu ilikuwa ghali. Wakamuomba Mtume: Ewe Mtume wa Allah panga bei kwa nafuu yetu. Mtume wa Allah akajibu: Hakika Allah ndiye anayemiliki*

*bidhaa, anapunguza, anatoa kwa wingi, anatoa rizki, na ananipendelea sana nikutane na Bwana wangu katika hali ambayo hapana yeyote kati yenu atakayenifanya niwe na dhima juu ya damu (iliyomwagika kwa sababu yangu) au mali (aliyopunjwa kwa sababu yangu)! (Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Uislamu kama usivyoruhusu kukandamizwa na kudhulumiwa mnunuzi ndivyo hivyo hivyo usivyoruhusu kukandamizwa kwa mchuuzi au muuzaji. Mtume (s.a.w) akiwa kiongozi mkuu wa serikali ya Kiislamu, hakuthubutu kutumia madaraka hayo kuingilia haki za wafanyabiashara walizopewa na Allah (s.w). Jibu lake kwa namna nyingine lilikuwa “anayepanga bei ni Allah (s.w).

Kutokana na Hadithi hii hapana yeyote aliyojitokeza mwenye haki ya kukaa chini na kumpangia mfanyabiashara bei iliyo kinyume na ile iliyojitokeza yenyewe sokoni. Kinachotakiwa kifanywe na nguvu za dola ni kutokomeza njama zote za ulanguzi na vikwazo vyote vya uchumi. Kisha kuwaacha huru wafanyabiashara wauze bidhaa zao kwa bei halisi inayokubaliwa katika soko huru.

(xi) Kupunguza kipimo cha ujazo au kilo kwa kuharibu mizani au kugonga vipimo vya ujazo ni haramu. Allah (sw) anasema :

وَيْلٌ لِّلْمُطَفِّفِينَ ﴿١﴾ الَّذِينَ إِذَا اكْتَالُوا عَلَى النَّاسِ
يَسْتَوْفُونَ ﴿٢﴾ وَإِذَا كَالُوهُمْ أَو وَّزَنُوهُمْ يُخْسِرُونَ ﴿٣﴾

*Maangamizo yatawathubutikia wapunjao (wenzao). Ambao wanapojipimia kwa watu hupokea (kipimo) kamili, lakini wanapowapimia kwa (kipimo cha) vibaba au mizani (au vinginevyo), wao hupunguza. (83:1-3)*

وَأَوۡفُواْ ٱلۡكَيۡلَ إِذَا كِلۡتُمۡ وَزِنُواْ بِٱلۡقِسۡطَاسِ ٱلۡمُسۡتَقِيمِۚ ذَٰلِكَ خَيۡرٞ وَأَحۡسَنُ تَأۡوِيلٗا ﴿٣٥﴾

*Na timizeni kipimo mpimapo; na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na bora mwishoni (kwake). (17:35).*

(xii) Kuficha ila (dosari) ya bidhaa inayouzwa ni haramu. Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhari, Baihaq na Al-Hakim, Mtume (s.a.w) amesema: Muuzaji na mnunuzi kila mmoja lazima atimize makubaliano. Na muuzaji akitoa habari zote juu ya bidhaa anayoiuza pamoja na mfano, kama unauza maharage makavu mwambie mnunuzi mathalan, uzuri wa maharage haya ni kuwa hayajatoboka lakini yana ila moja ya kuchelewa sana kuiva. Mwache mnunuzi apime hiari ya kununua au kuwacha.

Kutokana na maelezo yote haya; juu ya vipengele mbali mbali vilivyo haramishwa katika biashara, tunaona kuwa biashara japo ni kazi halali yenye hadhi kubwa mbele ya Allah, haitamnufaisha mwanaadamu iwapo mipaka ya Allah (s.w) haitachungwa wakati wa kufanya shughuli hiyo.

**Haki ya kumiliki mali**

Kumiliki mali ni suala la kimaumbile na limeshikamana na silka ya kujihami (self presevation).Katika historia ya binaadamu suala la kumiliki mali limekuwa likiandamana na itikadi au falsafa inayotawala mahali.

Kwa mfano katika baadhi ya jamii za kitwaghuti umilikaji wa mali uko chini ya familia au huwa chini ya "watu wote" (mali ya umma) au huwa chini ya mtu au watu binafsi. Katika Uislamu kila kitu kipo chini ya miliki ya Mwenyezi Mungu:

قُلِ ٱللَّهُمَّ مَـٰلِكَ ٱلۡمُلۡكِ تُؤۡتِي ٱلۡمُلۡكَ مَن تَشَآءُ وَتَنزِعُ
ٱلۡمُلۡكَ مِمَّن تَشَآءُ وَتُعِزُّ مَن تَشَآءُ وَتُذِلُّ مَن تَشَآءُۖ بِيَدِكَ
ٱلۡخَيۡرُۖ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيۡءٖ قَدِيرٞ ٢٦

*"Sema Ee Mola uliyemiliki Ufalme wote! Humpa ufalme umtakaye na humuondolea ufalme umtakaye na humtukuza umtakaye na humdhalilisha umtakaye, kheri imo mikononi mwako. Bila shaka wewe ni Mwenye Uwezo juu ya kila kitu". (3:26).*

Hivyo ni dhahiri kuwa Mwenyezi Mungu ndiye mmilikaji wa hakika wa vitu vyote. Binaadamu anamiliki mali kwa dhamana tu siyo kwa hakika na kwa sababu hiyo ataulizwa jinsi alivyotumia. Katika Qur-an Allah (s.w) ameruhusu watu binafsi au kwa vikundi kumiliki mali pale aliposema:

خُذۡ مِنۡ أَمۡوَٰلِهِمۡ صَدَقَةٗ تُطَهِّرُهُمۡ وَتُزَكِّيهِم بِهَا وَصَلِّ
عَلَيۡهِمۡۖ إِنَّ صَلَوٰتَكَ سَكَنٞ لَّهُمۡۗ وَٱللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ١٠٣

*"Chukua sadaka katika mali zao, uwasafishe kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (mbele yangu) na uwaombee dua. Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe); na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye." (9:103)*

Hivyo Uislamu unakubali na kuheshimu haki ya mtu au watu binafsi kumiliki mali.

**Mipaka ya Umilikaji mali**

(i) Mali hiyo iwe imechumwa kwa njia ya halali. Uislamu unaitambua haki ya kumiliki mali na haki ya kuilinda mali hiyo, lakini mali yenyewe iwe ya halali.

(ii) Mtu anaweza kuiuza au kuitumia mali yake apendavyo maadamu ana akili timamu. Iwapo hana akili timamu, itabidi apatikane mdhamini wa kuingalia mali hiyo kwa niaba na manufaa yake na manufaa ya jamii.

(iii) Maadamu mtu anayo mali basi anao pia wajibu wa kutekeleza majukumu yanayohusiana na mali aliyo nayo.

(iv) Uislamu unakataza ubakhili na israfu (ubadhirifu) katika matumizi. Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ ٱلْبَسْطِ
فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٩﴾

*Wala usifanye mkono wako (kama) uliofungwa shingoni mwako, wala usikunjue ovyo ovyo, utakuwa ni mwenye kulaumiwa na kufilisika. (17:29).*

يَٰبَنِيٓ ءَادَمَ خُذُواْ زِينَتَكُمْ عِندَ كُلِّ مَسْجِدٖ وَكُلُواْ
وَٱشْرَبُواْ وَلَا تُسْرِفُوٓاْۚ إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلْمُسْرِفِينَ ﴿٣١﴾

*Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila sala; na kuleni (vizuri) na kunyweni (vizuri). Lakini msipite kiasi tu. Hakika Yeye hawapendi wapitao kiasi. (7:31).*

Ubadhilifu ni kufanya mojawapo ya mambo matatu

**Kwanza**, kununua kitu usichokihitaji. Au kununua kitu unachokihitaji lakini kwa kiasi kingi kuliko unavyoweza kutumia. Kwa mfano kutengeneza chapati tano ilihali uwezo wako ni wa kula chapati mbili tu, halafu zile tatu ukazitupa jalalani. **Pili** ni ubadhilifu kununua kitu chochote kile cha haramu, hata ikiwa kwa thamani ndogo namna gani. Kwa mfano hata kama masanduku laki moja ya bia yanauzwa kwa shilingi hamsini ukiitoa shilingi hamsini hiyo kununua pombe hiyo unaandikiwa madhambi ya ubadhilifu. **Tatu** kutoa sadaka kwa ajili ya kujionesha kwa watu, badala ya kuandikiwa thawabu unaandikiwa madhambi ya israfu.

(v) Uislamu unakataza rasilimali zilizo katika jamii kuachwa bila kutumiwa Mtume (s.a.w) amesema mtu akiendeleza ardhi ana haki ya kuimiliki. Lakini akiiwacha kwa miaka mitatu bila kuitumia mtu mwingine ana haki ya kuiendeleza na kuimiliki.

### *6. Mgawanyo wa mali katika Uislamu*

Uislamu unasisitiza kuwa zaidi ya kuchuma, kumiliki na kusambaza mali, mgawanyo pia uwe wa haki katika jamii ili kujenga udugu, amani na utulivu wa kweli. Na katika kuhakikisha hilo mfumo wa uchumi wa Kiislamu (Iqtisad) unatumia njia zifuatazo:

**1. Zakat**

(i) Kilugha, neno zakat lina maana mbili: (a) Utakaso na (b) Ustawi. Hivyo zaka ni Ibada inayochangia sana katika kuleta uadilifu na ustawi wa jamii kiuchumi na hata kisiasa.

(ii) Zakat katika Uislamu ni taasisi maalumu na imesisitizwa katika Qur-an. Aya zipatazo 80 zimeitaja Zakat pamoja na Swala Zakat ina upeo mpana sana na ina husisha vipengele vingi kama vile:

(a) Kijamii – Zakat ni kama bima ya jamii inayowahakikishia wakazi hifadhi ya kiuchumi endapo watapata matatizo kama ya umaskini au maafa. Zaka pia huondosha chuki na migogoro ya kitabaka na kujenga hisia za kuwa wamoja.

(b) Kisaikilojia, Zakat inawalea watu katika moyo wa kuhurumiana na kusaidiana. Inawapa wanyonge na masikini moyo wa kujiamini na kujiona sawa na wengine.

(c) Kiuchumi – Zakat ni njia mojawapo ya kupambana na tatizo la umaskini. Tatizo hili linazikabili nchi zote na Uislamu unalenga katika kuondoa umaskini pasi na jitihada za watu binafsi. Uislamu haupiganii usawa bandia na kuwa kipato cha kila mtu kiwe sawa na mwingine wala Uislamu hauinyamazii hali ya wengine watumie na kusaza wakati wengine wanaendelea kutaabika kwa kushindwa kujipatia mahitaji muhimu. Tofauti za kimapato, vipaji na uwezo zitakuwepo katika jamii, lakini pengo la tofauti hiyo lisiwe kubwa sana.

(d) Kwa maumbile yake, Zakat huwahimiza watu kuweka vitega uchumi na kuzalisha mali na kupiga vita tabia ya kuhodhi mali. Hii ni kwa sababu Zakat hutozwa kwa kipato kilichokaa mwaka mzima bila kutumika.Kila mtu hanabudi kupata mahitaji ya msingi.

**2. Sadakat**

Hisia za kuhurumiana na moyo wa kusaidiana kama ndugu zinazomsukuma mtu kutoa Zakat kwa kutaraji kupata radhi za Allah ndizo hizo hizo zinazomsukuma mtu kutoa sadaka. Hivyo tofauti kati ya Zakat na sadaka haipo

katika lengo la kutoa bali katika wajibu wa kutoa. Zakat ni wajibu kutoa na sadaka ni amali iliyokokotezwa sana japo haikuwekewa kiwango na muda wa kutoa. Hutolewa kulingana na haja. Misingi ya kutoa sadaka ni ile ile ya kuhurumiana na kusaidiana kama Allah alivyoagiza katika Qur'an:

وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى
ٱلْإِثْمِ وَٱلْعُدْوَٰنِ ۚ

*Na saidianeni katika wema na ucha-Mungu, wala msisaidiane katika dhambi na uadui" (5:2).*

مَّثَلُ ٱلَّذِينَ يُنفِقُونَ أَمْوَٰلَهُمْ فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ كَمَثَلِ
حَبَّةٍ أَنۢبَتَتْ سَبْعَ سَنَابِلَ فِى كُلِّ سُنۢبُلَةٍ مِّا۟ئَةُ حَبَّةٍ ۗ
وَٱللَّهُ يُضَٰعِفُ لِمَن يَشَآءُ ۗ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٦١﴾

*Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyotoa mashuke saba; ikawa katika kila shuke pana punje mia., Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa mkubwa na Mwenye kujua." (2:261).*

Aidha, Mtume (s.a.w.) amesisitiza katika Hadithi nyingi sana umuhimu wa kutoa sadaka. Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhari, Muslim, Ahmad na At-Tirmidh, Mtume (s.a.w.) amesema mtu asiyewahurumia watu hatahurumiwa na Allah. Na katika Hadithi iliyosimuliwa na Attabarani na Baihaqi, Mtume (s.a.w.) amesema: Naapa

kwa Allah si muumini yule anayelala akiwa kashiba na ilhali jirani yake kalala na njaa.

Na katika Hadithi iliyosimuliwa na Al-Hakim, Mtume (s.a.w.) amesema ikiwa wakazi wa eneo fulani (kama vile mtaa) wakiamka asubuhi na ilhali mmoja wao ana njaa basi Allah hujitenga nao.

**Matukio maalum ya kutolewa kwa sadaka**

Baada ya kumaliza mfungo wa Ramadhani kutoa Zakatul Fitr ni lazima. Zakatul Fitr kiwango chake ni kilo 2½ za chakula kilichozoeleka katika mji huo kama vile mchele au ngano.

Na mtu hutoa kiasi hicho kwa ajili yake mwenyewe na hutoa tena kiasi hicho hicho kwa kila mtu anayemtegemea katika familia yake. Hivyo atamtoleo pia mkewe, na wanawe wote na wazazi wake iwapo anakaa nao na hawana uwezo.

Tukio la pili ni siku ya kuvuna mazao shambani, Mwenyezi Mungu ameagiza siku hiyo mtu atoe baadhi ya mazao yake na awape maskini, jamaa na majirani zake aliposema katika Qur'an:

وَهُوَ ٱلَّذِيٓ أَنشَأَ جَنَّٰتٖ مَّعۡرُوشَٰتٖ وَغَيۡرَ
مَعۡرُوشَٰتٖ وَٱلنَّخۡلَ وَٱلزَّرۡعَ مُخۡتَلِفًا أُكُلُهُۥ وَٱلزَّيۡتُونَ
وَٱلرُّمَّانَ مُتَشَٰبِهٗا وَغَيۡرَ مُتَشَٰبِهٖۚ كُلُواْ مِن ثَمَرِهِۦٓ
إِذَآ أَثۡمَرَ وَءَاتُواْ حَقَّهُۥ يَوۡمَ حَصَادِهِۦۖ وَلَا تُسۡرِفُوٓاْۚ
إِنَّهُۥ لَا يُحِبُّ ٱلۡمُسۡرِفِينَ ١٤١

*Naye (Allah) ndiye aliyeumba miti inayoegemezwa (katika chanja) katika kuota kwake na isiyoegemezwa na (akaumba) mitende na mimea ya matunda mbali mbali, na (akaumba) mizaituni na mikomamanga inayofanana na isiyofanana. Kuleni matunda yake inapotoa matunda; na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake (kwa kuwapa maskini na jamaa na majirani na wengineo) Wala msitumie kwa fujo, hakika Yeye (Allah hawapendi watumiao kwa fujo.” (6:141).*

Tukio la tatu ni wakati wa ndoa, Kuoana ni jambo lililohimizwa sana katika Uislamu. Hivyo Uislamu unasisitiza kuwa watu wasaidiane sana katika jambo hili. Wanazuoni wengi wanasema kuwa iwapo mtu anao uwezo wa kuoa lakini hapa mwanzo anakabiliwa na matatizo ya kifedha Hazina ya serikali ya Kiislamu *(Baitul Maal)* itumike kumsaidia. Wakati wa Ukhalifa wa Umar vijana kama hao walikuwa wakisaidiwa. Katika kuonesha ubora wa ndoa Allah amesema:

وَأَنكِحُوا الْأَيَامَىٰ مِنكُمْ وَالصَّالِحِينَ مِنْ عِبَادِكُمْ
وَإِمَائِكُمْ ۚ إِن يَكُونُوا فُقَرَاءَ يُغْنِهِمُ اللَّهُ مِن
فَضْلِهِ ۗ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٣٢﴾

*Na waozeni wajane miongoni mwenu (waungwana) na walio wema katika watumwa wenu (wanaume) na wajakazi wenu, kama watakuwa mafakiri Allah atawatajirisha katika fadhila zake; na Allah ni Mwenye wasaa” (24:32).*

Tukio la nne ni iwapo mtu atapata wageni. Uislamu unamtaka mtu awakirimu wageni wake. Katika Hadithi

iliyosimuliwa na Bukhari na Muslim, Mtume (s.a.w.) amesema: Yule anayemwamini Allah na siku ya mwisho awe mkarimu kwa wageni wake. Kwa mchana mmoja na usiku afanye takrima maalum. Kwa siku tatu zinazofuata afanye takrima ya kawaida na zaidi ya hapo ni sadaka ya hiari.

Tukio la tano ni wakati wa kugawa urithi, iwapo watakuwepo watu mafakiri wakati huo wa kugawa basi wapewe chochote, kwani Allah anasema:

وَإِذَا حَضَرَ ٱلْقِسْمَةَ أُوْلُوا۟ ٱلْقُرْبَىٰ وَٱلْيَتَٰمَىٰ وَٱلْمَسَٰكِينُ فَٱرْزُقُوهُم مِّنْهُ وَقُولُوا۟ لَهُمْ قَوْلًا مَّعْرُوفًا ﴿٨﴾

*"Na wakati wa kugawanya wakihudhuria jamaa na mayatima na maskini, wapeni kitu katika hayo (mali ya urithi) na waambieni kauli njema." (4:8).*

Tukio la sita ni agizo la Allah la kusaidiana kwa hali mbali mbali hasa majirani.

Tukio la saba ni wakati wa uzazi. Kama ambavyo Uislamu unahimiza ndoa ndivyo pia unavyothamini malezi ya watoto. Kihistoria Uislamu ndio ulioanzisha utaratibu wa kutoa malipo fulani maalum kwa familia zenye watoto wachanga.

Hivi leo ziko baadhi ya serikali duniani ambazo hutoa msaada wa pesa kwa familia zenye watoto wachanga. Huko Canada kwa mfano upo utaratibu wa kutoa msaada wa pesa kwa kila mtoto aliyezaliwa na kama watoto wakifikia umri wa miaka 18 na bado wanasoma kiwango cha pesa wanachopewa huongezwa.

Utaratibu huu ulianza katika karne ya 7 wakati wa ukhalifa wa Umar. Umar alianzisha mfumo wa kutoa dirham 100 kwa kila mtoto aliyezaliwa na kiwango hicho kiliongezwa kadiri mtoto alivyokua. Hivyo mfumo wa kutoa ruzuku kwa familia ni moja ya sadaqa zitolewazo katika mfumo wa uchumi wa Kiislamu.

**Sadaka wakati wa dharura**

Katika Hadithi iliyosimuliwa na Bukhari na Muslim, Mtume (s.a.w.) aliwasifu sana Al-Afariyyin (watu wa ukoo wa Abu Musa). Akasema watu hao walipokuwa vitani au safarini na chakula kikapungua basi walikikusanya pamoja chakula chote kilichosalia na kukigawa tena sawa sawa miongoni mwao.

Au nchi ikiingia njaa - ilitokea njaa kubwa kwa mfano wakati wa Ukhalifa wa Umar. Alichokifanya ni kutoa taarifa kwa viongozi wa majimbo mbalimbali na kuwataka walete chakula cha ziada. Na kilipokuja alikigawa bila ya kujali cheo, madaraka au ukoo wa mtu bali kwa kujali mahitaji tu. Kwa bahati njema njaa hiyo ilikwisha mapema. Lakini miongoni mwa maneno aliyoyasema Umar ni kuwa lau njaa hiyo isingekwisha mapema, basi angewakusanya watu wote wenye njaa na angewagawa kwa familia zenye chakula. Akasema hii ni kwa sababu watu hawatakufa wakila chakula hata kama hawatashiba.

**3. Kodi (Jizya)**

Ni njia nyingine itumiwayo na Uislamu katika kuigawanya mali katika jamii. Tafauti na Zakat na Sadaqa ambazo hupasa kutolewa na Waislamu, Jizya hutolewa na wasiokuwa Waislamu (Dhimmi), wanaoishi chini ya dola ya Kiislamu, kwa ajili ya kupata hifadhi na huduma mbalimbali.

**4. Mikopo**

Mikopo kama njia mojawapo ya kugawa mali kwa watu wote, Uislamu unaruhusu watu kukopeshana. Mtu anaweza kumkopesha mwingine fedha ama kwa kutumia (matumizi ya kawaida katika maisha) au kwa kumsaidia mtaji kufanya biashara.

**Njia za uchumi zilizoharamishwa**

Vipengele vya biashara haramu vilivyoorodheshwa nyuma ni miongoni mwa hizo. Njia nyingine za uchumi zilizoharamishwa ni hizi zifuatazo:

***(i) Wizi***

Wizi wa aina yoyote ni kitendo cha dhulma ni haramu katika Uislamu.

***(ii) Ulevi***

Ulevi wa aina yoyote kwa kiwango chochote ni haramu. Uharamu wa ulevi hauishii kwa mnywaji tu; bali pia ni haramu kushiriki katika hatua yoyote ile ya utengenezaji, uuzaji na uandazi.

> *Anas ameeleza kuwa Mtume (s.a.w.) amewalaani (watu) kumi kuhusiana na pombe-yule anayeikamua, yule aliyehusishwa katika kuikamua, yule anayeinywa, yule anayeibeba, yule anayepelekewa, yule anayeiandaa, yule anayeiuza, yule anayepanga bei yake, yule anayeinunua na yule anayemnunulia. (Tirmidh, Ibn Majah).*

Kutokana na Hadithi hii, inatuwia wazi kuwa aina yoyote ile ya utengenezaji, uuzaji na unywaji imeharamishwa. Pato lolote mtu atakalolipata kama malipo ya kushiriki katika hatua yoyote ya matayarisho na unywaji wa ulevi, litakuwa ni pato la haramu. Hebu tuangalie hali halisi. Je, hatuwaoni Waislamu wakishiriki kwa ukamilifu

katika viwanda vya pombe kama mameneja, makarani, wakemia, madereva, n.k.? Je, hawa wataridhika kuendelea kujiita Waislamu na ili hali kila saa wako katika laana ya Allah na Mtume wake na ibada zao zote hazikubaliwi maadam miili yao imerutubishwa na kipato cha haramu; kivazi chao ni haramu na kila walicho nacho katika mazingira yao kimepatikana kwa pato la haramu?

### *(iii)* ***Kamari***

Kamari imeharamishwa pamoja na pombe kama ilivyo katika aya ya (5:90) na (2:219). Pia Hadithi ifuatayo inatubainishia kuharamishwa kwa kamari:

> *Abdullah bin Amr ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha ulevi, michezo ya bahati nasibu, kamari ya karata, na gobairah (aina ya pombe) na anasema: "Kila ulevi ni haram". (Abu Daud).*

Hadithi hii inatubainishia kuwa aina zote za kamari-gudugudu, pata-potea, karata, bahati nasibu, nakadhalika, ni haramu na kwa hiyo pato lolote litakalo tokana na kamari ni pato haramu.

Ni muhimu kufahamu kuwa uharamu wa kamari hauishii kwa watu wawili au kikundi cha watu wachache bali hata kama kamari hiyo itachezwa kitaifa, itabakia kuwa haramu tu.

Kwa hiyo bahati nasibu ya taifa, Bima ya Kimataifa, na michezo yote ya kamari iliyotolewa kibali na taifa, yote ni haramu mbele ya Allah na yeyote atakayeshiriki kwa namna yoyote katika michezo hiyo ya kamari atakuwa ameshiriki katika haramu na kipato chochote atakachokipata kutokana na ushiriki wake huo kitakuwa ni kipato cha haramu. Katika aya tulizozirejea hapo juu (5:90 -91) kamari imeharamishwa kwa sababu kuu tatu:

**Kwanza**, ni uchafu, kamari imeitwa "**rijsi**". Kamari imeitwa uchafu kwa sababu pesa anazozipata mtu kwa kamari ni za dhulma na haramu. Kufumba na kufumbua mtu amepata maelfu ya pesa bila jasho lolote. Hivyo ni dhulma na ni haramu.

**Pili**, kamari inajenga chuki na uadui. Hii ni kwa sababu yule aliyeliwa pesa zake kwa maelfu kwa njia hii ya dhulma huwa ana mfundo mkubwa moyoni na anamchukia sana yule aliyechukua pesa zake hata kama ajidai kuwa hajali, ukweli ni kuwa pesa zake zitamuuma sana. Na mara kadhaa wacheza kamari wameishia kupigana na hata kuuana.

(iv) Kipato chochote kinachotokana na utengenezaji wa sanamu na picha za watu na wanyama ni kipato haramu.Rejea katika Hadithi zilizotolewa chini ya "Biashara haramu".

(v) Kipato chochote kutokana na umalaya, ngoma na muziki wa aina yoyote ni kipato haramu. Kama inavyobainika katika Hadithi ifuatayo:

> *Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah ameharamisha kipato kutokana na mauzo ya mbwa, na kipato kutokana na kuimba kwa wasichana (singing girls) (Sharhi Sunnat).*

(vi) Kipato chochote kutokana na utabiri, ramli, na upigaji bao ni kipato haramu, na yote hayo ni kazi ya shetani katika Qur'an Allah (s.w.) ametuasa:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡخَمۡرُ وَٱلۡمَيۡسِرُ وَٱلۡأَنصَابُ
وَٱلۡأَزۡلَٰمُ رِجۡسٞ مِّنۡ عَمَلِ ٱلشَّيۡطَٰنِ فَٱجۡتَنِبُوهُ لَعَلَّكُمۡ
تُفۡلِحُونَ ٩٠

*Enyi mlioamini! Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu, na kutazamia kwa mishale ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo); (yote haya) ni uchafu (na ni) katika kazi ya shetani. Basi jiepusheni navyo ili mpate kufaulu" (5:90)*

Kutokana na aya hii upigaji ramli na utazamiaji wa aina yoyote ni haramu na kipato chake kitakachopatikana na kazi hiyo ni haramu pia. Utabiri wa aina yoyote ni haramu, hali kadhalika kipato kinachotokana na kazi hiyo ya utabiri ni haramu. Abu Bakar aliwahi kujitapisha baada ya kugundua kuwa amelishwa kutokana na malipo ya utabiri. Pia kipato kutokana na uchawi ni kipato haramu.

***(vii) Hongo (Rushwa)***

Utoaji na upokeaji wa rushwa ni haramu na pato lolote lililotokana na rushwa ni pato haramu. Mtoaji na mpokeaji wa rushwa wote wamelaaniwa na Allah na Mtume wake kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Abdullah bin Amr ameeleza kuwa Mtume wa Allah amemlaani mpokeaji rushwa na mtoaji rushwa katika kutoa hukumu. (Abu Daud, Ibn Majah).*

Hongo au rushwa ni kiasi chochote anachopokea muhudumu (mfanyakazi) zaidi kuliko malipo yake ya haki katika kutoa huduma alizoajiriwa kwazo. Kwa maana nyingine, mtu akipokea malipo yoyote, hata yawe madogo kiasi gani ambayo ni ziada ya mshahara wake katika kufanya kazi ile ile na katika kiwango kile kile cha kazi aliyoajiriwa kwayo, atakuwa amepokea rushwa. Turejee kwa makini Hadithi ifuatayo:

*Abu Humaid as-Sayyid ameeleza Mtume (s.a.w.) alimteua mtu katika kabila la Azd aliyekuwa akiitwa Ibnul Luthiyyah kama, mkusanyaji wa zakat, Aliporudi Madina, alisema: "Hii ni kwa ajili yenu na*

*hivi ni vyangu (nilivyopokea) kama zawadi Kisha Mtume (s.a.w.) alitoa hutuba baada ya kumhimidi na kumtukuza Allah akasema: Jambo lingine ni kwamba nimewateua baadhi ya watu miongoni mwenu kufanya (kuongoza) shughuli ambazo Allah amenipa mamlaka kwazo. Mmoja wao anakuja na kusema: 'Hii ni kwa ajili yenu na hii ni zawadi niliyopewa. Kwa nini basi asibakie katika nyumba ya baba yake au katika nyumba ya mama yake na kuona kuwa angalipewa zawadi au hangelipewa? Kwa yule ambaye mikononi mwake uko uhai wangu hapana yoyote atakayechukua kitu chochote kutokana na zakati awe siku ya Kiyama hakutokea huku amebeba kitu hicho mabegani mwake. Kama alichukua punda atakuwa analia humo begani; kama alichukua mbuzi atakuwa analia (mee mee) humo begani. Kisha Mtume (s.a.w.) aliinua mikono yake mpaka tukaona weupe wa makwapani na akasema: "Ee Allah! Nimefikisha ujumbe)? Ee Allah! Nimefikisha ujumbe)?" (Bukhari na Muslim).*

Hadithi hii inatuonesha kuwa mkusanyaji hakuwa na haki ya kuchukua zawadi katika kukusanya mali ambayo ndiyo kazi aliyoteuliwa kwayo. Swali liliLoulizwa ni: Je, angalikuwa nyumbani au asingalitoka kukusanya zakat, angaliletewa zawadi hizo? Jibu ni kwamba asingeletewa zawadi hizo nyumbani kwake. Kwa hiyo zawadi zinazopatikana kwa namna hiyo si zawadi bali ni rushwa au hongo. Hadithi hii inatupa fundisho kubwa juu ya upokeaji zawadi makazini. Mara nyingi watu hupokea rushwa kwa jina la "zawadi". Hadithi hii imetuwekea mpaka unaotenganisha rushwa na zawadi. Kitu cha ziada ya malipo ya kazi au ziada ya mshahara kitabainika kuwa zawadi au hongo (rushwa) kutokana na jibu la swali lifuatalo: Je, kama afisa (mfanyakazi) asingelikuwa katika nafasi ya kazi aliyonayo au katika cheo alicho nacho,

angalipata zawadi hiyo au asingelipata? Kama jibu ni "*asingalipata*" basi afisa huyo au mfanyakazi huyo akipokea zawadi ajuwe amepokea hongo. Kama afisa au mfanyakazi huyo amepewa zawadi isiyohusiana na nafasi yake ya kazi; na angaliweza kupata zawadi hiyo hata kama angalikuwa hana kazi au angalikuwa mahali pengine, basi zawadi hiyo itakuwa ni zawadi kweli na itakuwa halali kwake.

Madhara ya rushwa yako wazi. **Kwanza**, mwenye kupokea rushwa (hongo) anapokea chumo la haramu ambalo litamfanya asikubaliwe ibada zake zote. **Pili**, Mla rushwa hawezi kumsaidia mtu asiyejiweza. Kila mara watawahudumia wale wenye kitu cha kutoa hongo kwa namna nyingine mnyonge asiye na uwezo wa kutoa chochote hatapata huduma muhimu za maisha anazostahiki kupata. **Tatu**, mla rushwa hawezi kuheshimiwa au kuaminiwa katika jamii kwa shughuli yoyote ile.

**Suala la omba-omba**

Tukiliangalia suala la omba-omba kwa upana kidogo, ambalo hivi sasa linaongelewa katika vikao mbalimbali vya kitaifa na kimataifa, tutaona kuwa ni Uislamu pekee unaotoa namna bora ya kulishughulikia suala hili. Omba omba ni kitendo kibaya sana kikiwa kimefanywa na mtu binafsi au taifa na kinashusha hadhi ya mtu binafsi na hadhi ya taifa kwa ujumla. Hivyo Uislamu ambao ndio njia sahihi pekee ya maisha, hauwezi kamwe ukapalilia omba omba na wala Zaka na sadaka kazi yake si kupalilia omba-omba, bali kinyume chake zaka na sadaka ni miongoni mwa silaha zinazotumiwa kutokomeza omba omba. Uislamu unawashutumu vikali omba omba kama tunavyojifunza katika Hadithi ifuatayo:

> *Hubshi bin Junadah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Kuomba-omba si halali kwa mwenye uwezo wala kwa mwenye uzima wa afya na mwenye*

*nguvu (za kufanya kazi) ila kwa mwenye kupigwa ufakiri na mwenye deni kubwa (asiloweza kulilipa). Na yule anayeomba watu ili ajiongezee mali yake atakuwa na mkwaruzo usoni mwake katika siku ya Kiyama na atayala kwa ulafi mkubwa mawe ya moto kutoka motoni. Kwa hiyo anayetaka, mwache aombe kidogo, na mwache aombe kingi. (Tirmidh)*

Wanaoruhusiwa kuomba kwa mujibu wa Hadith ni:

(i) Mtu aliyesimama kumdhamini mtu mwingine ili kuleta suluhu kati ya wagomvi wawili. huyu anaruhusiwa kuomba hata akiwa tajiri. Kwa mnasaba huu, waumini wa misikitini, madarasa, na shughuli mbali mbali za Kiislamu wanaruhusiwa kuomba michango ya Waislamu ili kufanikisha shughuli hizo.

(ii) Mtu aliyepata ajali na kuharibikiwa kabisa na vitu vyake vyote kama vile ajali ya moto, mafuriko, nakadhalika.

(iii) Mtu ambaye amepigwa na ufakiri na amekosa kabisa mahitaji muhimu ya maisha kama vile chakula, malazi na makazi, lakini mtu akiwa na angalau chakula cha siku moja na malazi mkononi mwake haruhusiwi kuomba kama tunavyofahamishwa katika Hadithi zifuatazo:

*Abdullah bin Mas'ud ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: Anayeomba omba watu na ilhali ana mahitaji muhimu ya maisha atakuja siku ya Kiyama na mikwaruzo, vidonda au majeraha usoni mwake. Iliulizwa: Ee Mtume wa Allah! Ni kiasi gani kinachomtosha mtu? Akajibu: Dirham 50 au thamani yake. (Abu Daud, Tirmidh, Nisai, Ibn Majah).*

*Sahl bin Haohaliyya ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema:Yeyote yule anayeomba na ilihali anajitosheleza kwa mahitaji muhimu, anaomba moto (Jahannam). Nufaili ambaye ni miongoni mwa*

*wasimulizi wa Hadithi hii katika sehemu nyingine aliuliza: Ni yupi mwenye uwezo ambaye kuomba ni haramu? Alijibu (Mtume s.a.w.): Yule mwenye uwezo wa kupata chakula cha asubuhi na usiku. Mahali pengine amesema: Yule mwenye chakula cha siku moja (usiku na mchana) (Abu Daud).*

Hivyo ikibidi mtu aombe, basi aombe kwa sababu hizo tatu zilizotajwa katika Hadithi hii. Kuomba omba bila ya sababu za msingi kumeharamishwa kwa sababu kuu tatu zifuatazo:

(i)Kuomba omba kunamfanya mtu apoteze moyoni mwake ile hali ya kumtegemea Allah (s.w.) na atajenga moyoni mwake hali ya kulalamika juu ya neema za Allah zilizomzunguka kila mahali. Kwa msingi huu hatima ya kuomba omba ni kumfanya mja awategemee wengine kwa mahitajio yake badala ya kumtegemea Allah (s.w.) na kumfanya ashindwe kushukuru neema za Allah (s.w.).

(ii) Kuomba omba humfanya mtu awe mnyonge na ajidhalilishe kwa wengine ambapo Muislamu anatakiwa ajidhalilishe kwa Allah (s.w.) peke yake.

(iii) Vile vile kuomba omba kumekatazwa kwa sababu kunamuweka yule anayeombwa katika hali ngumu. Wakati mwingine anayeombwa hali yake si nzuri vile vile lakini kwa kuombwa hulazimika kutoa jambo ambalo linaweza kumuathiri yeye na wale anaowaangalia.

Uislamu haukuishia kwenye kukemea tu tabia ya omba omba bali umetoa njia za kutatua tatizo hili kama ifuatavyo:

(i)Kuwasaidia wale wote wenye matatizo na dhiki mbali mbali kwa kuwapa Sadaqa na zakati kabla hawajaomba.

(ii)Njia ya pili, ya kukomesha kuomba omba ni kujitegemea kwa kufanya kazi kwa kutumia juhudi na maarifa.

### *7. Mfumo wa benki*

Mabenki ni taasisi za fedha ambazo ni muhimu sana katika uchumi. Benki husaidia uchumi kwa kutoa huduma kuu zifuatazo:

**Kwanza**, Benki hutoa huduma ya kuhifadhi akiba za watu na kuhifadhi mali zenye thamani kubwa kama vile dhahabu, na mfano wake.

**Pili**, kutokana na akiba inazozikusanya, benki hujikuta kila wakati ina fedha nyingi zisizo na shughuli yoyote. Benki hukopesha fedha hizi kwa watu wanaozihitajia ili ziwe mtaji wa kuendeleza biashara, viwanda, kilimo na sekta nyingine mbali mbali za uchumi na utoaji huduma.

**Tatu**, benki hutoa huduma ya kurahisisha malipo kwa njia ya hundi *(cheque)* kuwalipa Wafanyakazi kupitia benki zao au kwa hundi, huwaepusha walipaji na hatari ya kuibiwa.

**Nne**, pia benki hutoa huduma ya kutoa malipo ya mbali popote pale penye matawi yake nchini au ulimwenguni. Huduma hii ni muhimu sana kwani huwapunguzia watu mzigo wa kusafiri na fedha nyingi mkononi.

Badala yake benki huidhinisha malipo kwa simu au kwa njia yoyote ya mawasiliano ya haraka katika tawi la Benki hiyo popote lilipo nchini au ulimwenguni kupitia kwenye *Account* ya huyo anayestahiki kulipwa.

Huduma hizi muhimu na nyinginezo nyingi ambazo hatukuzitaja hapa zinatudhihirishia umuhimu wa kuwepo taasisi hii ya fedha katika jamii.

Hivyo ni dhahiri kwamba Uislamu ukiwa ni mfumo kamili wa maisha unaojitegemea kwa kila kitu, hautarajiwi ukapinga au ukaharamisha kuwepo kwa mabenki katika jamii.Bali Uislamu unaharamisha mabenki yanayoendeshwa kwa kipato cha riba.

**Mabenki ya Riba**

Mabenki ya kitwaghuti (yasiyokuwa ya Kiislamu) sehemu kubwa ya kipato chake hutokana na riba.

Mabenki ya Riba hukopesha watu wenye miradi mbali mbali ya uchumi na kuwatoza riba kubwa katika mfumo wa malimbikizo *(compound interest)*. Sehemu ndogo ya riba inayokusanywa na Benki za Riba, hutumiwa katika kuwalipa wateja walioweka akiba zao ambao ndio hasa matajiri walioifanya Benki iwepo.

Ni kutokana na unyonyaji wa namna hii utakuta, wakati wakulima na Wafanyakazi wa ngazi za chini ambao ndio wanaovuja jasho ili kuchangia riba, hawajimudu katika kujipatia chakula, mavazi, na makazi bora, wenye mabenki wanagawa *“bonus”* kwa wafanya kazi wao na wao wenyewe wanaponda starehe na anasa zilizopindukia kutokana na riba ambayo hawakuitoleo jasho lolote.

**8. Tatizo la Riba**

Riba ni kupata chochote kile cha ziada kutoka katika mkopo au mtaji bila kushiriki katika faida au hasara. Mwenyezi Mungu anatufahamisha katika Qur’an:

ٱلَّذِينَ يَأۡكُلُونَ ٱلرِّبَوٰاْ لَا يَقُومُونَ إِلَّا كَمَا يَقُومُ ٱلَّذِى يَتَخَبَّطُهُ ٱلشَّيۡطَٰنُ مِنَ ٱلۡمَسِّۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمۡ قَالُوٓاْ إِنَّمَا ٱلۡبَيۡعُ مِثۡلُ ٱلرِّبَوٰاْۗ وَأَحَلَّ ٱللَّهُ ٱلۡبَيۡعَ وَحَرَّمَ ٱلرِّبَوٰاْۚ

*Wale wanaokula riba hawasimami ila kama anavyosimama yule ambaye shetani kamzuga kwa kumsawaa; haya ni kwa sababu wamesema, Biashara ni kama riba, hali Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na kuiharamisha riba.(2:275)*

يَمۡحَقُ ٱللَّهُ ٱلرِّبَوٰاْ وَيُرۡبِى ٱلصَّدَقَٰتِۗ

*Mwenyezi Mungu huyafutia (baraka mali ya) riba; na kuyatia baraka (mali iliyotolewa) sadaka (2:276).*

**Madhara ya riba katika jamii**

(i) Riba inachafua nafsi ya Tajiri na uchumi wake. Tajiri ambaye hayuko tayari kukukopesha mali yake pasi na riba, kamwe hawezi kutoa mali yake bure kuwasaidia wanyonge na wenye dhiki. Tajiri asiye tayari kutoa mali yake kuwasaidia wenziwe wenye dhiki na shida katika jamii huwa mchoyo, bahili, mpupiaji mali, asiyetosheka na utajiri alionao, mfujaji, muonevu na dhalimu. Tajiri mwenye moyo wa namna hii hata kama atajiita Muislamu hawezi kamwe kuchunga mipaka ya halali na haramu katika kuchuma!

(ii) Riba inamkandamiza Mnyonge mwenye dhiki. Wanyonge na wenye dhiki katika jamii inayoendesha uchumi wake katika misingi ya riba, hawapati msaada wowote wa bure kutoka kwa matajiri kwa kiasi ambacho wengi wa wale wasiojiweza kabisa kujitosheleza kwa

mahitaji muhimu ya maisha yao kwa namna duni sana - wengi hujipatia chakula chao kutoka katika mapipa ya taka (watoto wa mtaani), wengi hujisitiri kwa masalio yaliyookotezwa hapa na pale na wengi makazi yao ni stesheni na sokoni. Hawa, kisaikolojia, hujiona ni watu duni wasio na maana yoyote katika jamii na huwaona matajiri na watu wenye uwezo kuwa ndio wenye maana. Na hapa ndipo inapojengeka chuki baina ya wasionacho kuwachukia walio nacho.

(iii) Riba inaharibu uchumi wa jamii na maendeleo yake. Riba na msingi wake wa unyonyaji imma ikitozwa na tajiri mmoja au kikundi cha matajiri, imefanywa msingi wa uchumi wa taifa au wa kimataifa. Kwa bahati mbaya kutokana na mazoea tuliyonayo juu ya vyombo vya uchumi vya kitaifa na kimataifa vinavyoendeshwa katika misingi ya Riba kama vile mabenki ya taifa na shirika la Bima la Kimataifa, baadhi ya watu wamediriki kuhalalisha Riba ya mabenki na Bima. Kuhalalisha huku kwa riba ya mabenki na Bima aidha kumetokana na uzoefu wa uchumi haramu katika jamii zetu au umetokana na kushindwa kuona ubaya wa riba kitaifa au kimataifa.

Waislamu hatuna budi kukumbuka kuwa alichokiharamisha Allah (s.w) kinakuwa ni haramu katika wingi wake na katika uchache wake. Tukichukua mfano wa pombe Mtume (s.a.w.) amesema:

> *Kinacholewesha kikiwa kingi ni haramu pia hata kikiwa kichache.*
> *(Tirmidh, Abu Daud, Ibn Majah).*

Kwa hiyo kilicho haramishwa kwa mtu binafsi, pia ni haramu kwa taifa na ni haramu kwa mataifa yote ulimwenguni. Kwa upande mwingine jambo la haramu litakapotendwa kitaifa litakuwa na athari mbaya zaidi kwa

jamii kuliko likitendwa katika kiwango cha mtu binafsi, hali kadhalika jambo baya likitendwa kimataifa huwa na athari kubwa na mbaya zaidi kwa jamii ya mwanadamu kuliko likitendwa katika kiwango cha kitaifa.

(iv) Riba ni mali ya dhulma inayonyakuliwa na matajiri kutoka kwa wanyonge kwa njia moja au nyingine kiuchumi, pia riba inaukandamiza na kuudidimiza uchumi wa kitaifa au kimataifa. Mali ya riba kwa kuwa ni mali inayopatikana bila jasho na bila hata ya kushiriki katika mashaka ya uchumi, huwafanya matajiri na wenye uwezo wa kuendesha miradi mbali mbali ya kiuchumi wakae tu bila kazi wakingojea fedha zao zizae katika mabenki ambazo wana kila uhakika wa kuzipata hata itokee gharka ya namna gani. Kwa hiyo kutokana na riba, jamii huwakosa watu wenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mali ambao wangaliweza kuendesha miradi mbali mbali ya kiuchumi ambayo ingaliinua uchumi wa taifa na wa kimataifa kwa ujumla.

Wataalam wa uchumi wanakiri kuwa riba inaporomosha uchumi. Wamegundua kuwa kadiri kiwango cha riba kinavyokuwa kikubwa ndivyo uchumi unavyozidi kushuka kwa sababu matajiri huona kuwa wanapata faida kubwa zaidi na kwa njia nyepesi isiyotoa jasho lolote wakiweka fedha zao benki kuliko kuziingiza katika miradi ya kiuchumi. Hivyo utaona kuwa riba hupunguza uzalishaji na huongeza gharama za uzalishaji.

## Uharamu wa Riba katika Uislamu

**Kwanza**, Uislamu umeharamisha riba kwa sababu ni dhulma (unyonyaji).Ukichukua mkopo wa riba uliochukuliwa kwa madhumuni ya kukidhi haja ya

matumizi ya lazima ya nyumbani, utozaji wa riba unakiuka lengo la Allah la kuumba (kuleta) mali kwa wanadamu. Utaratibu aliouweka Allah ni kwamba kwa kuwa mali ameileta kwa wanaadamu wote:

هُوَ ٱلَّذِى خَلَقَ لَكُم مَّا فِى ٱلْأَرْضِ جَمِيعًا

*"Yeye (Allah) Ndiye aliyekuumbieni vyote vilivyomo katika ardhi..." (2:29).*

Ni lazima matajiri (wenye mali) wawapatie wanyonge na wenye dhiki mahitaji yao muhimu ya maisha.

**Pili**, riba imeharamishwa katika Uislamu kwa sababu inahamisha mali kutoka kwa maskini au wanyonge na kuipeleka kwa tajiri ambayo huzidi kuondoa usawa katika mgawanyo wa mali. Hii ni kinyume na mahitaji ya jamii. Uislamu unataka kila mtu apate mahitaji muhimu ya maisha. Hivyo wale walio na ziada ya mahitaji muhimu ya maisha wanatakiwa wawape wasionacho kabisa au wale waliopungukiwa kwa upendo na udugu. Riba inakanusha kabisa msimamo huu.

**Tatu**, riba imeharamishwa katika Uislamu kwa sababu hufanya kundi la watu katika jamii liishi kivivu bila ya kufanya shughuli yoyote ya uzalishaji, likitegemea kuishi kwa riba kutokana na mali zao walizozikusanya katika mabenki, bima, na vyombo vingine vya riba. Jamii inakosa mchango wa watu hawa katika uzalishaji na si hivyo tu, bali watu hawa wanakuwa mzigo na bughudha katika jamii. Ufasiki (uharibifu) wa aina zote katika ardhi hufanywa na kundi hili.

**Ufumbuzi wa tatizo la riba**

Riba imeenea na kuzoeleka duniani kwa kiasi ambacho watu wengi wanadhani kuwa bila riba hakuna

shughuli yoyote ya uchumi inayowezekana. Riba imechukuliwa kuwa kama motisha (faida) kwa mwenye kuruhusu fedha zake zitumiwe na mtu mwingine. Hivyo mikopo kutoka kwa watu, makampuni, mabenki, mashirika ya bima n.k. haipatikani bila riba. Hivi sasa mikopo karibu yote duniani haitolewi bila riba. Mikopo hii kwa kawaida imegawanywa katika makundi mawili:

(a) Mikopo ya muda mfupi
(b) Mikopo ya muda mrefu

Tatizo hasa la riba linaonekana katika aina ya pili ya mikopo (yaani mikopo ya muda mrefu) Hii ni kwa sababu kiasi cha riba huongezeka mwaka hadi mwaka pengine kuzidi hata fedha zilizokopeshwa mwanzoni. Aidha katika mikopo hii, baya zaidi ni kuingizwa kwa rahani na hatari iliyopo ya mkopeshwaji kunyang'anywa mali aliyoweka rahani pindi atakaposhindwa kulipa deni kwa muda uliopangwa. Uislamu ukifuatwa vilivyo, tatizo hili haliwezi kujitokeza kwani mwenye fedha analazimishwa kufanya moja kati ya yafuatayo kwa mwenye kuhitaji fedha hizo:

(a)Kumkopesha bila riba kwa muda watakaokubaliana. (Ama kwa kuweka au kutoweka rahani mali yake).

(b)Kushirikiana katika mtaji na kugawana gharama za uendeshaji, faida na hasara.

***(a) Kukopesha bila riba***

Uislamu ni mfumo kamili wa maisha alioufuma Allah (s.w.) na ni muhali kwa Allah (s.w.) kuwalazimisha wanaadamu kufanya jambo wasiloliweza. Amekataza riba na kuruhusu biashara kwa sababu anafahamu kuwa riba inaweza kuepukika na biashara kufuatwa. Aidha uislamu unawaruhusu watu kukopeshana. Mtu anaweza kumkopesha mwingine fedha ama kwa kutumia (matumizi

ya kawaida katika maisha), au kwa kumsaidia mtaji kufanyia biashara. Kwa hali yoyote itakavyokuwa mwenye kukopesha (mtoa fedha) analazimika kudai kiasi kile kile alichotoa kwa muda waliokubaliana bila ya kudai nyongeza yoyote. Sheria iliyopo katika Uislamu katika kukopeshana ni deni hilo kuandikwa (hata kama ni dogo) mbele ya mashahidi waadilifu. Allah (s.w.) hata hivyo ametoa ruhusa ya kukopeshana bila mwandishi kwa njia ya kuweka vitu rahani. Anayathibitisha haya Mwenyezi Mungu pale anaposema:

> *"Na kama hamkupata mwandishi basi (mdai) apewe (astakabadhishwe) (kitu kiwe) rahani mikononi mwake. Na kama mmoja wenu amewekewa amana na mwenzake basi aliyeaminiwa airudishe amana ya mwenzake, na amche Mwenyezi Mungu Mola wake. Wala msifiche ushahidi (japo juu ya nafsi zenu) Na atakayeficha basi hakika moyo wake ni wenye kuingia dhambini. Na Mwenyezi Mungu huyajua mnayoyatenda."* (2:282).

***(b) Ushirika katika biashara***

Uislamu unaruhusu watu kufanya biashara kwa shirika maadamu wanachunga sheria zilizowekwa (za Uislamu). Ushirikiano katika biashara unaweza kuwa wa watu wawili au zaidi. Mara nyingi wanaoshirikiana huchangia katika mtaji wa biashara yao. Pindi watu wakikubaliana kufanya biashara kwa shirika Uislamu unawalazimisha kushirikiana vile vile katika gharama, faida au hasara itakayopatikana. Hii hutegemea kiasi gani kila mshirika amechangia katika biashara hiyo. Ushirikiano mwingine wowote usiokuwa katika mtaji utategemea makubaliano ya washirika. Hebu tutazame ni kwa jinsi gani ushirika katika mtaji wa biashara unavyoweza kutumika badala ya mikopo ya rahani yenye riba.

(i)Mikopo inayopatikana kwa rahani (Mortgages). Kupata mkopo kwa kitu rahani si haramu katika Uislamu

kama ilivyokwishabainishwa katika Qur'an. Hata Mtume Muhammad (s.a.w.) aliwahi kufanya hivyo kama tunavyofahamishwa katika Hadithi ifuatayo:

*Bi Aisha (r.a) amesimulia kuwa: Mtume (s.a.w.) alinunua vyakula kwa mkopo kwa muda maalum na aliweka rahani (armour) zake kwa ajili hiyo (Bukhari).*

Wanyama wafugwao vile vile wanaweza kuwekwa rahani kwa ajili ya mkopo. Wanyama hawa wanaweza wakatumika hata kama bado wapo rahani. Hadithi ifuatayo inatuthibitishia hayo:

*Abu Hurairah (r.a) amesimulia: Mtume wa Allah amesema: "Mnyama aliyewekwa rahani anaweza kutumika kuendeshwa maadamu analishwa na maziwa ya mnyama atoaye maziwa yanaweza yakanyewa kulingana na kiasi mtu anagharimika juu yake. Yule anayemwendesha mnyama au kunywa maziwa yake hana budi kugharimia mahitaji ya mnyama huyo". (Bukhari).*

Kinyume na utaratibu huo hivi sasa rahani hutumika katika kupata mikopo ya muda mrefu. Mikopo hii huweza kutolewa na makampuni ya bima au makampuni ya akiba. Kitu kinachowekwa rahani huhesabiwa kama dhamana ya mkopo uliotolewa. Kwa kawaida kitu kinachowekwa rahani ni kile ambacho kinaeleweka kuwa kina uwezo wa kuzalisha mathalani nyumba au mashine. Mkopo hulipwa na riba. Kama aliyekopeshwa atashindwa kutoa riba au malipo ya fedha za mkopo basi mkopeshaji huhesabiwa kuwa ana haki ya kuchukuwa mali ya dhulma iliyo bayana kwa aliyekopeshwa.

***(c) Ushirika katika mtaji badala ya mikopo ya rahani yenye riba***

Mtu anaweza kupata fedha kwa njia hii bila kutoa riba. Njia hii inawezekana tu kwa kuwafanya watu

wengine wawe wanashirika katika mali/kitu ambacho kingewekwa rahani kwa kuchangia katika thamani ya kitu hicho kwa njia ya kununua hisa *(shared equity).* Watu hawa wataridhia iwapo watafahamu hisa walizonazo katika mali/kitu hicho. Iwapo kwa mfano kitu hicho ni nyumba kodi itakayopatikana ni lazima igawanywe kwa wenye hisa wote (baada ya kutoa gharama za uendeshaji). Mwenye nyumba au mwenye nyumba mtarajiwa *(the owner to be)* atakubaliana na washiriki hao kununua hisa zao hatua kwa hatua mpaka hisa zote zitakapokuwa zake (yani nyumba itakapokuwa mali yake). Njia hii hutekelezwa kwa kufuata hatua zifuatazo:

(i) Makisio ya thamani ya kitu na idadi ya hisa. Kitu ambacho kilifikiriwa kuwekwa rahani ili kupata mikopo hufanyiwa utafiti wa bei ambayo ingeweza kuuzwa.Hii huchukuliwa kama thamani ya kuridhisha ya kitu hicho. Ni thamani hii ndiyo itakayogawanywa kwa watakaokuwa na hisa (akiwemo atakayekuwa mwenye nyumba) Thamani ya kila hisa huamuliwa na huyo mwenye kutafuta fedha kwa wengine.

Thamani ya kitu na thamani ya kila hisa ndivyo vitakavyoonesha idadi ya hisa. Iwapo thamani ya nyumba, mathalani ni shilingi 2,000,000 na thamani ya hisa moja ni shilingi 100,000 idadi ya hisa itakuwa $\frac{2000000}{100000} = 20$

(ii) Kutafuta mtaji wa mwanzo wa atakayekuwa mwenye mali. Atakayekuwa mwenye mali lazima afahamu kiasi cha mtaji au hisa atakazokuwa nazo mwanzoni kabla ya kutoza hisa nyingine kwa wengine.

(iii) Kufahamu idadi ya hisa za washirika wengine. Idadi ya hisa za washirika wengine katika mali inapatikana kwa kugawa thamani ya hisa zote kwa thamani ya hisa moja.

(iv) Kufahamu mapato (kabla ya kutoa gharama) na mapato halisi (baada ya kutoa gharama za uendeshaji). wa mali. Mapato ya mali ambayo ilikusudiwa kuwekwa rahani kwa ajili ya kupata mkopo lazima yafahamike. Mapato kwa ajili ya nyumba kwa kawaida huwa ni kodi ya nyumba *(rental charge).* Thamani ya mapato hayo *(gross rental value)* si yote yanayogawanywa kwa wenye hisa katika mali. Kuna umuhimu wa kutoa gharama zote za uendeshaji.

(v) Mapato yaliyobaki baada ya kutoa gharama za uendeshaji, hugawanywa kwa wenye hisa kulingana na idadi ya hisa mtu alizonazo katika mali ile.

Itaonekana wazi kuwa njia hii haihusu riba kwa namna yoyote ile. Tofauti zinazojitokeza kati ya njia hii na ile ya kukopa kwa kuweka vitu rahani ni:

1) Mali humilikiwa na wenye hisa wote mpaka hapo atakayekuwa mmilikaji atakapomaliza kununua hisa za wengine wote.

2) Wenye hisa wote wana haki ya kugawana (kulingana na hisa mtu alizo nazo) mapato yanayotokana na mali hiyo na pia wana wajibu wa kushiriki katika gharama zote za uendeshaji.

**Mali yenye kuchangiwa mtaji kwa hisa**

Mtu akishaamua kuuza hisa *(share)* kwa watu wengine kwa ajili ya mali fulani katika sheria ya Kiislamu anapoteza umilikaji wa mali wa mtu mmoja. Kuuza hisa kwa wengine kwa maana nyingine ni kukaribisha watu wengine kushiriki katika umilikaji wa mali ile. Nafasi ya mtu katika kumiliki mali hiyo itategemea idadi ya hisa alizonazo katika mali ile. Wenye hisa inabidi washirikiane katika faida na hasara pamoja na gharama za uendeshaji.

***Faida anazopata atakayekuwa mwenye kumiliki mali***

Zipo faida kadhaa ambazo atakayekuwa mwenye kumiliki mali huzipata kwa kufuata ushirika katika biashara, mtaji na faida *(Shared Equity and rental)* badala ya kupata mikopo ya biashara yenye riba. Faida kubwa atakayopata ni fadhila za Allah (s.w.) kwa kule kuepuka kwake kutoa riba kwa mkopo atakaopata. Tunajifunza katika Hadithi za Mtume (s.a.w.) kuwa laana ya Allah (s.w.) huwafikia wote wanaohusika na riba (mtoaji, mpokeaji, shahidi). Hata hivyo kuna faida nyingine ambazo anaweza kuzipata:

(i) Atakayekuwa mwenye kumiliki mali kwa kutochukuwa mkopo wenye masharti ya riba hujiepusha kabisa na hatari ya kunyang'anywa mali yake (aliyoweka rahani) akishindwa kutimiza masharti yake.

(ii) Fedha ambayo angeitoa kama riba kwa ajili ya mkopo atabaki nayo na kutumia kwa shughuli nyingine kuendeshea maisha yake.

(iii) Atakuwa na uhakika wa kupata sehemu halali ya faida inayotokana na mali hiyo (kama ipo). Kadhalika kama ikitokea hasara haitamlazimu kubeba mzigo wote wa hasara kwani ushirika katika biashara huhusisha vile vile umuhimu wa kugawana hasara itokeapo.

**Faida kwa wenye kununua hisa**

Mwenye kununua hisa huchangia katika mtaji. Naye huepuka ghadhabu za Allah (s.w.) za utoaji mkopo kwa riba. Zaidi ya haya hupata faida zifuatazo:

(i) Hupata sehemu ya faida itokanayo na mali hiyo kulingana na mchango wake kwenye biashara (idadi ya hisa alizonazo).

(ii) Huwa na sauti kwenye mali kwani naye pia ni mwenye kumiliki mali ile mpaka atakapouza hisa zake. Isitoshe hutoa kiwango kidogo kujipatia haki ya kumiliki ukilinganisha na mtaji mzima.

Kwa ujumla jamii nzima itanufaika kwa kuacha mfumo wa mikopo kwa riba na kuhimiza watu kufanya ushirika katika biashara. Ilivyo waliokopeshana kwa riba hawawi katika uhusiano mzuri kiroho. Aliyekopeshwa ilimbidi kufanya hivyo kutokana na shida aliyokuwa nayo. Kutoa kwake riba anakufanya kwa kuwa anafahamu hatari za kutofanya hivyo (kupoteza mali yake) ingawa kitendo hicho kinamuuma sana rohoni. Hivyo urafiki kati ya mkopeshaji na mkopeshwaji huwa ni wa kinafiki. Jambo hili ni wazi sana katika jamii ya dunia ya sasa. Hebu fikiria athari za mikopo hii kwa nchi masikini duniani. Ni mara nyingi nchi masikini zimekuwa zikipiga kelele aidha kupunguziwa au kufutiwa kabisa baadhi ya madeni yao. Sehemu kubwa ya madeni hayo ni limbikizo la riba la miaka mingi.

Hivyo Uislamu unapiga vita riba kutokana na madhara yake kibinafsi, kitaifa na kimataifa. Aidha Uislamu unahimiza ushirikiano katika biashara kama ufumbuzi wa tatizo la riba.

**Benki za Kiislamu**

Benki za Kiislamu ambazo hutoa huduma kama benki nyingine zinaendeshwa katika msingi wa biashara na sio ule wa riba. Benki za Kiislamu badala ya kukopesha kwa riba, hutumia rasilimali zake kwa zenyewe kujihusisha katika uzalishaji kwa kufuata misingi inayokubalika katika Uislamu. Miongoni mwa misingi inayokubalika kwa Muislamu au Benki ya Kiislamu kuingiza fedha zake katika miradi ya biashara au uzalishaji ni hii ifuatayo:

***(i) Mudharabah***

Mudharabah ni makubaliano kati ya watu wawili au zaidi ambapo mmoja au zaidi kati ya hao anatoa mtaji na mwingine hushiriki kwa ukamilifu katika kuendesha na kuongoza mradi wa uchumi. Faida itakayopatikana katika mradi huo itagawanywa kulingana na makubaliano yao. Hasara itakayotokana na mradi huo itakuwa ni ya mwenye kutoa mtaji. Wengine hawatoi chochote kusaidia hasara kwa sababu wameshatoa mchango wao wa hasara hiyo kwa jasho walilolitoa katika shughuli ambayo haikuzaa matunda bali hasara.

Benki za Kiislamu zinaingiza fedha zake katika miradi ya uchumi kwa njia hii ya Mudharabah ambapo benki hutoa mtaji kwa ajili ya miradi mbali mbali ya uchumi kwa mapatano ya kupata kiasi (asilimia) fulani cha faida itakayopatikana na kuwa tayari kulipa hasara itakayopatikana.

***(ii) Musharikah***

Musharikah ni ushiriki kati ya watu wawili ambapo, tofauti na *Mudharabah* wote wawili wanachangia mtaji na kushiriki katika uendeshaji wa shughuli ya kiuchumi, lakini si lazima watoe hisa sawa sawa, kwa makubaliano ya kugawana faida na hasara kulingana na kiasi cha hisa alichotoa kila mmoja wao. Kwa mtindo huu wa "Musharikah" Benki ya Kiislamu inaingia katika kuchangia mtaji, kuendesha na kusimamia mradi wa uchumi na watagawana (faida au hasara) kulingana na kiasi cha mtaji kila mmoja alichotoa.

***(iii) Ijara-Uara wa Iktina***

Huu ni utaratibu mwingine unaokubalika kisheria ambapo mtu au benki inatumia fedha zake katika kukodi vitu kama vile magari, majumba, ardhi, na kadhalika, ambavyo vikifanyiwa kazi huzalisha mali na kutoa faida.

Benki za Kiislamu hujipatia faida kubwa kutokana na mtindo huu.

***(iv) Murabah***

Huu ni utaratibu unaotumiwa katika kununua bidhaa kwa wingi kwa ajili ya kuwauzia wafanya biashara ambao waliofikiana kuwa bidhaa hizo zinunuliwe kwa ajili yao. Benki kutokana na uwezo wake inapanga na wafanya biashara kuwa inunue bidhaa nyingi kutoka ndani na nje ya nchi kwa jina lake kisha iwauzie wafanyabiashara hao kwa bei itakayoipatia benki faida. Pia benki kwa mtindo huu inaweza kununua mazao ya wakulima na kuyauza kwa walaji kwa faida.

***(v) Muqaradha***

Mtindo huu wa Muqaradha humruhusu mtu au benki kununua "share" au "bonds" katika kampuni ya uzalishaji kwa mapatano ya kugawana faida au hasara kulingana na kiasi cha "share".

Kwa kufuata mitindo hii katika kuingiza fedha zake katika miradi ya uchumi, Benki za Kiislamu hupata faida kubwa hata zaidi ya kipato cha riba kinachopatikana katika benki za riba. Benki za Kiislamu nazo hugawa faida inayopatikana kwa wateja wake walioweka fedha zao kwenye benki.

**Uzuri wa benki za Kiislamu**

Pamoja na benki za Kiislamu kutoa huduma zinazotolewa na kila benki kama tulivyoziorodhesha huko nyuma, kuna faida za ziada zinazopatikana kutokana na benki hizi kama ifuatavyo:

**Kwanza** benki za Kiislamu huiokoa jamii na uchumi wake na madhara yote yanayosababishwa na riba.

**Pili**, Benki za Kiislamu huwaingiza katika uchumi na kuwainua hata wale ambao hawana hata rasilimali yoyote kwa mtindo wa Mudharabah. Hivyo ni kwamba, benki zinazoendeshwa kwa mikopo ya riba, haziwezi kukopesha fedha zake kwa mtu yeyote asiye na rasilimali yenye thamani sawa au zaidi ya mkopo ili atakaposhindwa kulipa ifilisiwe rasilimali hiyo. Kwa mtindo huu wa mikopo ya riba, ni matajiri tu wanaopata mikopo ya benki na masikini wasio na rasilimali yoyote huachwa hivyo hivyo na umasikini wao bila ya msaada kutoka benki wa kuwainua kiuchumi.

**Tatu**, benki za Kiislamu huinua uchumi wa jamii, kutokana na umakini na tahadhari kubwa zinazochukua katika kuchagua na kuendesha miradi mbali mbali ya uchumi. Kwa kuwa benki zenyewe zinajiingiza katika uchumi, zinahakikisha kuwa miradi zitakazoichagua ni ile yenye uwezo mkubwa wa kuzalisha faida kubwa na yenye uwezekano mdogo wa kusababisha hasara.

## Zoezi la Nne

1. Uchumi ni nini?

2.Toa ufafanuzi mfupi namna Uislamu unavyoeleza dhana ya;

(a) Mafanikio
(b) Umiliki wa mali
(c) bidhaa
(d) Matumizi

3. Soma kwa makini Qur'an (9:105),(5:1) na (6:165), kisha toa mafunzo ya kiuchumi.

4. Nukuu aya za Qur'an zinazoonesha umuhimu wa uchumi, kisha bainisha mafunzo yake kwa muhtasari.

5. Katika uchumi wa Kiislamu, serikali ya Kiislamu inawajibu gani kwa wananchi na raia wake?

6. Taja mambo matatu yanayopaswa kuzingatiwa katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa.

7. Bainisha biashara haramu zisizostahiki Muislamu kuzifanya kibidhaa na njia au kiutaratibu.

8. Mfumo wa Uchumi wa Kiislamu ni Rehema kwa walimwengu wote.

Thibitisha neema hii kwa kuonesha namna Qur'an inavyoondoa dhiki na ukata wa kiuchumi katika jamii kupitia mgawanyo wake wa mali.

9. Soma kwa mazingatio Qur'an *89:19,104:2,90:6, 68:12, 89:17-18, 70:19-25.* kwa mujibu wa Qur'an:

(a) Wajibu wa kusimamia Haki za masikini na mafukara kuwezeshwa kujikimu kiuchumi katika jamii, Allah (sw) amewakabidhi akina nani?

(b) Ni akina nani wenye jukumu la kuondoa Omba-omba katika jamii, ambao pia wanadhima ya kujibu mbele ya Allah (sw) kwa kuwepo na kushamiri tatizo hilo katika jamii.

(c) Je, katika jamii ambayo waumini wamewaachia khatamu matwaghuti wenye mioyo ya uchoyo, unyimifu, ubakhili, kuhodhi, husda, na ubinafsi wa kutojali wengine; yafaa waumini kutowaangalia Omba-omba, ambao ni “madhuluman”?.

10. (a) Onesha tafauti zilizopo baina ya biashara na riba.
(b) Riba ina madhara gani katika jamii?

11. Onesha kwa ufupi misingi ya uendeshaji benki ya Kiislamu pasina riba.

## Sura ya Tano

# SIASA

### Maana ya siasa

Siasa ni sayansi ya uendeshaji mambo ya kijamii. Dhana kuu za siasa ni utawala (mamlaka), itikadi, matashi na maamuzi.Hivyo tunapoitizama siasa hatunabudi kuzingatia kuwa ni mfumo wa utawala, itiqadi, matashi na maamuzi ya mtu au kikundi cha watu au ufunuo kutoka kwa Allah (s.w).

Kumbukumbu za kihistoria zinatufahamisha kwamba siasa ilianza pale wanaadamu walipoanza kuishi pamoja kama kijiji, mji, taifa hadi kufikia mataifa. Hivyo siasa ni jambo kongwe kama ilivyo historia ya mwanaadamu mwenyewe.

Katika jamii ya mwanaadamu kuna mfumo mikuu miwili ya siasa.

1. Mifumo ya siasa iliyobuniwa na wanadamu – siasa za kitwaghutii.
2. Mfumo wa siasa uliowekwa na Mwenyezi Mungu – siasa ya Kiislamu.

### 1. Mifumo ya siasa za kitwaghuti

Kwa mtazamo wa Kiislamu, masuala ya kijamii yenye kufuata mitindo na mipangilio iliyobuniwa na watu ndiyo yanayofahamika kama siasa za kitwaghuti. Kihistoria siasa hizo zimepita katika vipindi mbali mbali hadi hivi leo. Vipindi hivyo ni pamoja na:

(i) Ujima.
(ii) Utumwa.
(iii) Umwinyi.
(iv) Ubepari.

(v) Ujamaa na Ukomunisti.
(vi) Demokrasia.

***(i) Ujima***

Nadharia za kitwaghutii zinamuangalia mwanaadamu kama mnyama ambaye katika kipindi cha ujima (cha awali) hakutofautiana na wanyama wengine. Yeye pia aliishi mtini, akaenda kwa miguu na mikono kwa pamoja. Hakutofautiana sana na nyani alipokuwa katika hali ya usokwe-mtu. Kutokana na mabadiliko ya kimazingira baadhi ya wanyama, miongoni mwao akiwemo sokwe-mtu, walitoka katika hali ya kuishi mitini, wakateremka chini. Hapo ndipo yalipotokea "mabadiliko" ya maumbile ya miili yao kulingana na mazingira mapya. Lakini kutokana na uhasama uliokuwepo katika mazingira hayo mapya, kwani misitu na wanyama wakali walienea kote, mtu wa mwanzo hakuweza kuishi peke yake kiubinafsi. Hali hizo za kimazingira zilimlazimisha mtu wa mwanzo aishi kwa ushirikiano na wenziwe ili aweze kupambana na mazingira hayo makali. Hapo ndipo ilipoanza siasa kwa mujibu wa nadharia hii.

***(ii) Mfumo wa siasa za utumwa***

Mfumo wa siasa za kitumwa unafuatia ujima katika siasa za kitwaghutii. Ni mfumo wa siasa za kitabaka ambapo watu huishi kwa jasho la watu wengine wanaomilikiwa kama bidhaa. Watu hao wenye fursa za mali au hadhi katika jamii huishi kwa kuwatumikisha wengine. Katika mfumo huu, utawala uko mikononi mwa matajiri ambao huendesha siasa za kuwatumikisha wengine na wao kuishi maisha ya raha. Chini ya mfumo huu wa siasa, uzalishaji mali umewekwa migongoni mwa watu wa tabaka la chini la watwana.

Mfumo huu wa kitumwa ulianza kuyumba kwa migongano mbalimbali. Watumwa walianza kujizatiti na

kupinga vikali sana utumwa wao. Watu ambao hapo awali walinyang'anywa mali zao na mabwana wenye watumwa waliungana pamoja na watumwa katika mapambano ya kuufuta utumwa:

***(iii) Mfumo wa siasa za Ukabaila***

Siasa za Ukabaila ambazo zilifuatia baada ya siasa za kitumwa nazo vile vile zilikuwa na minyororo yake. Katika mfumo huu tabaka la Kikabaila hutawala njia zote za kijamii. Njia za kiuchumi hutawaliwa kwa kukodisha mashamba halafu kutoa fungu kubwa kwa mwenye shamba wakati wa mavuno. Wazalishaji kwenye mashamba hayo chini ya mfumo huu, tofauti na utumwa, hulipwa posho kidogo kama malipo ya kazi nzito walizotumikishwa. Kwa mtazamo wa Kitwaghuti juu ya historia ya mfumo huu, inadaiwa kuwa taasisi za dini pia zimetumika "kuhalalisha" ubwana na utwana! Mfumo wa siasa za Ukabaila ulisita kuendelea baada ya wanyonywaji kujiunga pamoja dhidi ya wanyonyaji.

***(iv) Mfumo wa siasa za kibepari***

Siasa za kibepari ni moja ya mifumo ya Kitwaghuti iliyokita mizizi katika jamii nyingi. Katika mfumo huu kila kitu kinachowezekana kufanywa ili "kuzalisha" pesa hufanywa. Wachache walio na fursa za mali na hadhi ndiyo huendesha masuala yote ya jamii na kundi kubwa la wanajamii huishi kwa kuuza nguvu, vipaji na taaluma zao kwa wachache hao, na wale wasio na chochote hulazimika kufanya vitendo vyovyote ili mradi wapate pesa.

***(v) Mfumo wa siasa za Kijamaa (Kikomunist)***

Katika mfumo huu uliodhaniwa na waasisi wake kuwa ungelimkomboa mwanaadamu na kuleta "**usawa wa sare**", chama ndicho hushika hatamu zote na "huwakilisha matakwa ya walio wengi" katika jamii. Aidha hudaiwa kuwa jamii chini ya mfumo huu wa siasa watu huwa huru

kabisa na kuwa na "demokrasia" halisi. Hata hivyo historia inaonesha kuwa chini ya mfumo huu wa siasa, jamii hupumbazwa na kudumazwa kwa njia mbalimbali. Kwa kuwa chama hushika hatamu za maongozi, ni kamati ya watu wachache tu ndani ya chama hicho ndio inayoendesha masuala yote ya utawala Hudhibiti kila kitu kwa kuimarisha ulinzi wa siri ambao hupenyezwa kila eneo la jamii. Huendesha propaganda dhidi ya wale wote wenye fikra tofauti na zao. Njia zote za uchumi huwa chini ya kikundi hicho cha watu kwa sura ya "mali ya umma". Katika Tasnifu (thesis) yake ya shahada ya udaktari wa falsafa mwaka 1946, Dk. Rafiuddiin, aliandika juu ya kuporomoka kwa siasa hii kama ifuatavyo:

> *"Marxism (Communism), like every wrong ideal, contains the germs of its own dissolution and must break up sooner or later"*[1]
>
> *Umarx (ukomonist), kama ilivyo kwa itikadi yoyote ile ya urongo, umebeba sumu inayoumaliza , hivyo lazima uporomoke hivi karibuni au baadae".*

Hali iliendelea kuwa ngumu katika nchi zilizokuwa viranja wa siasa hii na hadi kufikia mwaka 1989 miaka 70 ya mapinduzi hayo ya kikomonist, Urusi ilisambaratika na huo ukawa ndio mwisho wa siasa hiyo.

### *(vi) Mfumo wa siasa za kidemokrasia*

Demokrasia ikiwa na maana ya maamuzi ya wengi katika kuweka mamlaka waitakayo ni mfumo wa maisha uliobuniwa Uyunani (Ugiriki). Wataalamu wa mambo ya siasa wanafahamisha kuwa neno *Democracy* ni muungano wa maneno mawili yenye kuleta maana moja; *Demos-nguvu* ya raia na *cracy* ni "utawala", yaani utawala unaotokana na maamuzi ya wengi miongoni mwa raia.

Hivi leo Demokrasia hufahamika kama ni utawala wa watu uliowekwa na watu kwa ajili ya watu *(The government of the people by the people for the people).* Au ni uhuru wa kujiamulia mambo vile mtu apendavyo! Kutokana na tafsiri hiyo, kisiasa, kuna aina tofauti za miundo ya demokrasia; zipo demokrasia za chama kimoja, demokrasia za vyama viwili, demokrasia ya vyama vingi, demokrasia ya kiliberali ambayo ni demokrasia ya moja kwa *moja (direct democracy)* na demokrasia ya uwakilishi *(representative democracy)*, nakadhalika.

**2. Mfumo wa siasa ya Kiislamu**

Mfumo wa siasa ya Kiislamu ni utaratibu na muongozo wa masuala ya jamii ambao misingi yake ni vitabu vya Allah (s.w) na Sunnah za Mitume wake tangu Mtume wa kwanza, Adam (a.s) hadi Mtume wa Mwisho, Muhammad (s.a.w). Ni mfumo uliowekwa na Allah (s.w) kupitia kwa Mitume wake wote. Mitume wote walikuja kusimamisha mfumo wa maisha aliouridhia Allah (Dini ya Allah). Kuhusu Mtume Muhammad (s.a.w) tunafahamishwa katika Qur-an:

هُوَ ٱلَّذِيٓ أَرۡسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلۡهُدَىٰ وَدِينِ ٱلۡحَقِّ لِيُظۡهِرَهُۥ
عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوۡ كَرِهَ ٱلۡمُشۡرِكُونَ ٣٣

*"Yeye (Allah) ndiye aliyemleta Mtume wake (Nabii Muhammad) kwa uongofu na kwa dini ya haki ili aijaalie kushinda dini zote, ijapokuwa watachukia washirikina". (9:33, 61:9)*

Kwa ujumla, mitume wote waliwalingania watu wao kutambua kuwa mwenye haki ya kutoa mwongozo na kuweka utawala juu ya wanaadamu ni Allah (s.w) pekee.

Pia waliwalingania watu wao kuwa kufuata maongozi yoyote yale ya kijamii (siasa), kinyume na Allah (s.w) ni shirk. Hivyo, wale wote wanaoendesha masuala ya kijamii kwa kutumia taratibu na miongozo iliyoasisiwa na watu wanamshirikisha Allah (s.w) katika siasa na ni wazushi tu kama Mwenyewe Allah (s.w) anavyotutahadharisha:

وَإِن تُطِعۡ أَكۡثَرَ مَن فِى ٱلۡأَرۡضِ يُضِلُّوكَ عَن سَبِيلِ ٱللَّهِۚ

إِن يَتَّبِعُونَ إِلَّا ٱلظَّنَّ وَإِنۡ هُمۡ إِلَّا يَخۡرُصُونَ ﴿١١٦﴾

*Na kama ukiwatii wengi katika (hawa) waliomo ulimwenguni watakupoteza na njia ya Mwenyezi Mungu. Hawafuati ila dhana tu, na hawakuwa ila ni wenye kuzua (tu basi).” (6:116).*

**Dhana ya Dola**

Dola ni eneo la ardhi lenye mkusanyiko wa watu walio huru chini ya utawala mmoja wenye uwezo wa kujitosheleza kwa mahitaji muhimu na kulinda mipaka ya eneo lake. Eneo hili la ardhi huitwa nchi na wakazi wake ndio wazawa au wananchi wenye haki na eneo hili. Katika ulimwengu huu kuna aina kuu mbili za Dola. Dola za kitwaghutii na Dola za Kiislamu.

Tutaangalia kwa muhutasari miundo na uendeshaji wa dola hizi ili tuweze kulinganisha na kutofautisha mifumo ya utawala iliyowekwa na wanaadamu na ule uliowekwa na Muumba.

**Dola za Kitwaghuti**

**1. Muundo na Uendeshaji wake**

Chombo kikuu cha **kwanza** katika dola za kitwaghuti ni **serikali**. Kazi kuu ya serikali ni kutawala kwa kutumia

nguvu kuhakikisha kuwa jamii husika inafuata mwenendo unaotakiwa na serikali. Serikali inaundwa na sehemu tatu – Kiongozi Mkuu wa Dola au Rais. Baraza la Mawaziri na Majeshi. Kiongozi Mkuu wa Dola amekuwa ndiye mtendaji mkuu na muamrishaji mkuu wa majeshi (Amir Jeshi Mkuu). Katika uhusiano na Dola nyingine, kiongozi mkuu ndiye msemaji mkuu kwa niaba ya Dola yake. Kiongozi huyu mkuu wa dola huwa juu ya sheri**a** na hawezi kushitakiwa kwa kosa lolote analolitenda wakati wa utendaji kazi wake kama kiongozi mkuu wa dola

Majeshi ya serikali za kitwaghuti ndio nguvu ya dola. Majeshi hutumika kulinda, kutetea, na kuhakikisha matakwa na maslahi ya serikali yanapatikana. Majeshi vile vile hutumika katika kulinda mipaka na mamlaka ya dola. Wakati mwingine hutumika kuvamia nchi nyingine ili kupanua mipaka ya dola. Majeshi pia hutumiwa katika kusimamia utekelezaji wa sheria na amri zote zinazotakiwa na serikali. Majeshi yenyewe hugawanyika katika sehemu tofauti kiutendaji. Kuna jeshi la polisi lenye vikosi vya ulinzi wa kawaida kwa usalama wa raia, vikosi vya kutuliza fujo, vikosi vya usalama barabarani, na kadhalika, hivi vyote hushughulikia usalama wa raia tu. Kuna jeshi la ulinzi linaloshughulika na ulinzi wa mipaka ya dola kwa ujumla likiwa na vikosi vya nchi kavu, vikosi vya anga na vikosi vya majini. Kuna jeshi la magereza linaloshughulika na wahalifu wote wanaovunja sheria.

Pamoja na majeshi zipo idara au vitengo maalumu vya usalama vilivyo chini ya ofisi ya mkuu wa dola ambavyo hujishughulisha na utafiti wa habari muhimu kiutawala (Intelligence bureau) ambavyo ndani ya mipaka ya dola huchunguza kwa mbinu mbali mbali kutafuta hisia na minong’ono ya wananchi jinsi wanavyoitazama serikali na mipango yao dhidi yake.

Kwa ujumla Idara ya usalama hujishughulisha na maeneo yafuatayo:

(1) Kupeleleza mambo mbali mbali kisha kuiarifu serikali sambamba na kupendekeza au kushauri hatua muafaka za kuchukuliwa.

(2) Kukusanya habari na taarifa muhimu zinazohitajika na serikali kiusalama.

(3) Kuingilia kati shughuli za idara au mashirika mengine ya upelelezi na ujasusi.

(4) Kueneza na kushinikiza sera na matakwa ya serikali kwa njia mbali mbali za siri vikiwamo vitisho (intimidation), upotoshaji wa habari au kueneza habari zisizo zenyewe (disinformation), udhibiti wa habari, urubunifu, kufitinisha na kufarakanisha wapinzani, kuendesha propaganda na kuwadhibiti wapinzani wa kisiasa, kujipenyeza au kutumia watendaji (double agents) ndani ya makundi ya watu, taasisi au jumuiya ili kufahamu mipango yao ili waweze kuivuruga. Vile vile katika serikali kuna sehemu ya utawala (Administration) iliyoundwa kutokana na msururu mrefu wa urasimu. Warasimu hao waliogawanywa katika wizara, idara, na vitengo mbalimbali, husimamia shughuli za kila siku za serikali. Wanakuwa na mamlaka ya kutoa amri na maelekezo ya mara kwa mara. Mbali na kuwa na serikali kuu, Dola huwa pia na serikali za majimbo (mikoa), serikali za wilaya, miji, na za mitaa. Kila serikali inakuwa na kiongozi wake mkuu k.v. mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya, n.k.

Chombo kikuu cha **pili** cha dola ya kitwaghutii ni **Bunge**. Bunge nalo huwa na sehemu mbili. **Bunge** kwa maana ya wabunge tu na **Bunge Kuu** kwa maana ya wabunge na kiongozi mkuu wa dola (Rais). Kazi ya Bunge ni kutunga sheria na kudhibiti mwenendo wa serikali. Hata hivyo katika mfumo wa serikali iliyochini ya Rais (Presidential form of government) sheria zinazopitishwa na Bunge haziwi sheria mpaka akubali Rais na kuidhinisha kwa saini yake.

Vile vile bunge lina kazi ya kudhibiti mwenendo wa serikali kwa kujadili na kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya serikali (Budget).

Chombo kikuu cha **tatu** cha Dola ni **Mahakama**. Kazi kuu ya mahakama katika mfumo wa kitwaghutii ni kueleza na kufafanua utekelezaji wa sheria. Kuonesha namna ya kuwajibika na kuadhibu pale inapolazimu. Kwa maana nyingine mahakama inayokazi ya kutoa au kusimamia utoaji wa haki. Mahakama zinaweza kuwa na mpangilio wa kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu kama vile mahakama za mwanzo, mahakama ya wilaya, mahakama za mikoa, mahakama kuu na mahakama za Rufaa.

Kwa ujumla vyombo vyote vilivyoorodheshwa husimamiwa moja kwa moja na Dola na huwajibika kwa dola. Vipo baadhi ya vyombo ambavyo sio mali ya Dola lakini hutumiwa na dola katika kutekeleza shughuli zake kama vile **vyombo vya Kijasusi na vyombo vya Itikadi**.

**Vyombo vya Kijasusi**

Katika mataifa makubwa ya kisekula, mbali ya vitengo vya ndani vya upelelezi huwepo pia mashirika ya kijasusi yanayofanya ujasusi nchi nyingine kwa manufaa ya mataifa hayo. Mataifa hayo yana idara za usalama na mashirika ya ujasusi.

Nchi za Marekani na Israil ni maarufu katika shughuli hii ya ujasusi. Taifa la Marekani, kwa mfano, mbali ya shirika lake la ndani la upelelezi FBI *(Federal Bureau Investigation)* pia ina mashirika mengine kama CIA *(Central Intelligence Agency)*, NSA *(National Security Agency)* na DIA *(Defence Intelligence Agency)*. Taifa la Israel lina mashirika mawili makubwa ya kijasusi, shirika la *Shin-Bet* likijishughulisha na upelelezi wa ndani ya Israel na shirika Ia *Mossad linajishughulisha na "n*je" ya Israel. Uingereza ina vitengo vikuu viwili. Kitengo cha usalama (M15) ambacho hushirikiana na idara maalum ya polisi iliyo chini ya ofisi ya waziri Mkuu vikiwajibika na usalama wa ndani. Pia kuna shirika la kijasusi la secret Intelligence Service (SIS) au M16, hili liko chini ya wizara ya mambo ya Nje. Secret Intelligence Service hufanya ujasusi nje ya Uingereza kulinda maslahi ya nchi hiyo. Ufaransa nayo ina shirika liitwalo Service Documentation Exterieure Contre Espionage (SDECE). Na Ujerumani ina kitengo kama hicho kiitwacho Bundes Nachristen Dienst (BND).

***Vyombo vya Itikadi***

Katika dola za kisekula pamoja na kuwepo vyombo vya mabavu pia huwepo vyombo vya itikadi. Baadhi ya vyombo hivi huweza "kusimamiwa moja kwa moja na dola, wakati vingine huwa nje ya mamlaka hiyo.

Katika suala la itikadi chombo ambacho hupewa umuhimu wa "pekee" ni elimu. Elimu hutolewa ama na dola yenyewe au na taasisi zilizosajiliwa. Kazi moja ya dola ni kutoa au kusimamia utoaji na uendeshaji wa elimu na maarifa. Huunda, kutengeneza au kujenga itikadi na kuifanya iwe rasmi. Hulazimisha itikadi hiyo ikubalike na kufuatwa na watu wote. Japo itikadi hiyo hupingwa na jamii nzima, lakini ukweli ni kwamba itikadi inayotawala na kuongoza dola siku zote ni itikadi ya tabaka linalotawala

Itikadi hii hutumika kutawala matabaka yanayotawaliwa katika kipindi cha "**amani na utulivu**". Mara nyingi utii na unyenyekevu wa raia huwa ni wa woga kutokana na vitisho na mabavu ya watawala kwamba wote wanaokwenda, wanaoongea na wanaotenda kinyume cha itikadi rasmi hushughulikiwa na vyombo vya dola

Vyombo vya itikadi ni pamoja na shule na vyuo, dini, vyama vya siasa, miungano ya namna mbali mbali na vyombo vya habari. Pamoja na mengine vyombo vyote hivi huelimisha watu kuhusu itikadi, sera au dira ya tabaka linalotawala huwashawishi watu waikubali na kuifuata. Hujitahidi kuihalalisha kuwa ni sahihi na nzuri kuliko itikadi nyingine. Tabaka linalotawala huandaa mitaala ambayo katika ufundishaji hutumika kwenye Mashule; Vyuo, Vyuo Vikuu na Taasisi za elimu, mkazo mkubwa ukiwa kuifikisha itikadi ya watawala kwa wananchi, tangu wakiwa na umri mdogo kabisa hadi wanapokuwa watu wazima wenye uwezo wa kufahamu, kufikiri, kuchambua, kutathmini, kulinganisha, kuchanganua na kufikia, au kutoa "uamuzi huria". Shule na vyuo huwalea watu wa umri mbali mbali na kutoa daraja mbali mbali za Wataalamu na wanafikara ambao hutazamiwa watende kulingana na matakwa ya Watawala.

Katika mfumo wa kisekula (hasa wa kijahilia) Dini na taasisi zake kama makanisa, misikiti, shule na vyuo mbali na kueneza "imani ya dini", pia hutumika kueneza itikadi ya tabaka linalotawala hufundisha waumini wao kutii dola, kufuata itikadi yake na kuwa waaminifu kwa kiongozi anayetawala

## Dosari za Dola za Kitwaghuti

Historia inatuonesha kuwa pamoja na umuhimu wa uongozi au serikali katika jamii, si kila serikali iliyoweza kuwashikamanisha wanaadamu pamoja na kuwaelekeza katika lengo la maisha yao. Dola yoyote iliyowekwa na

kuendeshwa kwa kufuata matashi ya binaadamu imekuwa ikiwafarakanisha binaadamu na kuwagawa katika matabaka mbali mbali.

Matabaka ya waungwana na watwana, matajiri na maskini, wenye nguvu na wanyonge, wageni na wazawa, watawala na watawaliwa, na kadhalika. Katika kipindi cha historia ya mwanaadamu, watu wa matabaka ya juu daima wamekuwa wakiwanyonya na kuwakandamiza watu wa matabaka ya chini kwa kutumia hila mbali mbali.

**2. Muundo wa Dola ya Kiislamu na Uendeshaji wake**

Kwa mujibu wa mafundisho ya Uislamu, mwanaadamu analazimika kuishi maisha ya kijamii ambayo humtaka ahusiane na kushirikiana na watu wengine ili aweze kufikia lengo la kuumbwa kwake na kuletwa hapa duniani. Ili wanaadamu waweze kushirikiana na kuliendea lengo la maisha yao kwa pamoja hapana budi kuwa na serikali au uongozi madhubuti.

Adam (a.s) alipokuwa peponi (bustanini) pamoja na mkewe, alikuwa kiongozi. Aliposhushwa hapa duniani aliongoza familia yake (kizazi chake) kwa mwongozo utokao kwa Allah (s.w) kama tunavyofahamishwa katika Qur-an:

قُلْنَا ٱهْبِطُوا۟ مِنْهَا جَمِيعًا ۖ فَإِمَّا يَأْتِيَنَّكُم مِّنِّى هُدًى فَمَن

تَبِعَ هُدَاىَ فَلَا خَوْفٌ عَلَيْهِمْ وَلَا هُمْ يَحْزَنُونَ ﴿٣٨﴾

*Tukasema: "Shukeni humo nyote; na kama ukikufikieni uwongozi utokao kwangu, basi watakaofuata uwongozi wangu huo haitakuwa khofu juu yao wala hawatahuzunika.(2:38)*

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ النَّارِ ۖ
هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٣٩﴾

*Lakini wenye kukufuru na kuyakadhibisha maneno yetu, hao ndio watakaokuwa watu wa Motoni, humo watakaa milele." (2:39)*

Katika sehemu hii tutaangalia dhana ya utawala katika Uislamu na muundo wa Dola ya Kiislamu na uendeshaji wake.

**Dhana ya Utawala katika Uislamu**

Wataalamu wa siasa (Political scientists) wanautazama utawala kama "uwezo wa juu kabisa wa kuamuru, kuongoza na kudhibiti vyote vilivyo ndani ya mipaka ya Dola usio wajibika kwa yeyote yule ndani ya mipaka hiyo." Kwa mtazamo huo mtu au kikundi cha watu (chama, taasisi, n.k.) kinaposhika utawala, basi neno au tamko la mtu huyo au kikundi hicho huwa ni amri au sheria ya kutiiwa bila hiari.

Kwa hiyo, kwa namna dhana ya utawala ilivyo, hakuna mwanaadamu mwenye sifa, uwezo na haki ya kushika nafasi ya utawala" Ni kwa msingi huu Qur-an imetoa msisitizo na maelezo yaliyo wazi kabisa kuwa utawala ni haki na milki ya Allah (s.w) pekee kwa sababu yeye:

لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴿٢٣﴾

*Haulizwi (Mwenyezi Mungu) anayoyafanya (kwani yote ni ya haki) lakini wao (viumbe) wataulizwa. (21:23)*

قُلۡ مَنۢ بِيَدِهِۦ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيۡءٖ وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيۡهِ إِن كُنتُمۡ تَعۡلَمُونَ ﴿٨٨﴾

*Sema: "Ni nani mkononi Mwake umo ufalme wa kila kitu, Naye, ndiye, alindaye, na hakilindwi (chochote) kinyume Naye, kama mnajua (jambo nambieni hili)."* (23:88)

Yeye, Allah (s.w), peke yake ndiye Muumba wa vyote na ndiye mtawala halisi wa ulimwengu na vyote vilivyomo. Si haki ya kiuumbe yeyote yule awaye kuamrisha, kutiiwa au kuongoza kinyume na Allah (s.w).

### Vyombo vya Dola ya Kiislamu

Serikali ndiyo taasisikuu katika dola ya Kiislamu, nayo imegawanywa katika sehemu kuu tatu: Yaani Bunge (Shuura), Urasimu (mamlaka ya utendaji) na Mahakama.

### *Kazi za Bunge la Kiislamu*

Bunge la Kiislamu, tofauti na mabunge ya mifumo mingine, ni chombo cha **Mshawara** na ufafanuzi wa masuala mbali mbali ya dola. Bunge la Kiislamu si chombo cha kutunga sheria kinyume na zile zilizomo ndani ya Qur'an na Sunnah:

وَمَا كَانَ لِمُؤۡمِنٖ وَلَا مُؤۡمِنَةٍ إِذَا قَضَى ٱللَّهُ وَرَسُولُهُۥٓ أَمۡرًا أَن يَكُونَ لَهُمُ ٱلۡخِيَرَةُ مِنۡ أَمۡرِهِمۡۗ وَمَن يَعۡصِ ٱللَّهَ وَرَسُولَهُۥ فَقَدۡ ضَلَّ ضَلَٰلٗا مُّبِينٗا ﴿٣٦﴾

*"Haiwi kwa mwanamume aliyeamini wala kwa mwanamke aliyeamini, Mwenyezi Mungu na Mtume Wake*

*wanapokata shauri, wawe na hiari katika shauri lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, hakika amepotea upotofu (upotevu) ulio wazi (kabisa) ". (33:36).*

إِنَّآ أَنزَلۡنَا ٱلتَّوۡرَىٰةَ فِيهَا هُدٗى وَنُورٞۚ يَحۡكُمُ بِهَا ٱلنَّبِيُّونَ
ٱلَّذِينَ أَسۡلَمُواْ لِلَّذِينَ هَادُواْ وَٱلرَّبَّٰنِيُّونَ وَٱلۡأَحۡبَارُ بِمَا
ٱسۡتُحۡفِظُواْ مِن كِتَٰبِ ٱللَّهِ وَكَانُواْ عَلَيۡهِ شُهَدَآءَۚ فَلَا
تَخۡشَوُاْ ٱلنَّاسَ وَٱخۡشَوۡنِ وَلَا تَشۡتَرُواْ بِـَٔايَٰتِي ثَمَنٗا
قَلِيلٗاۚ وَمَن لَّمۡ يَحۡكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ
ٱلۡكَٰفِرُونَ ٤٤

*"Hakika tuliteremsha Taurati yenye uwongozi na nuru; ambayo kwayo Manabii waliojisalimisha (kwa Mwenyezi Mungu) waliwahukumu Mayahudi: na watawa na maulamaa pia (walihukumu kwa hiyo Taurati), kwa sababu walitakiwa kuhifadhi Kitabu (hicho) cha Mwenyezi Mungu; nao walikuwa mashahidi juu yake. Basi (nyinyi Waislamu) msiwaogope watu, bali niogopeni (mimi). Wala msibadilishe Aya zangu kwa thamani chache (ya duniani). Na wasiohukumu kwa yale aliyoteremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio makafiri." (5:44).*

Pamoja na hivyo, Bunge la Kiislamu hufanya kazi zifuatazo:

(i) Pale ambapo Qur'an na Sunnah zimeweka maelezo na hukumu wazi, bunge la Kiislamu halina uwezo wa kufanya vinginevyo bali kuyaweka

maelezo hayo kulingana na mazingira, kutoa tafsiri na ufafanuzi wa kina na kuweka kanuni na maelekezo yatakayohimiza utekelezaji wa hukumu hizo.

(ii) Pale ambapo Qur' an na Sunnah zina maelezo yenye tafsiri zaidi ya moja, wajibu wa bunge ndani ya dola ya Kiislamu ni kuchagua moja ya tafsiri hizo na kuiidhinisha kutumika kijamii kama rejea iliyokubalika.

(iii) Pale ambapo hukumu (Qur'an na Sunna) haziko wazi, kazi ya bunge ni kujadili na kupitisha fat-wa ya kufuatwa na jamii. Msingi utakaozingatiwa katika majadiliano, ni ule usemao kuwa jambo lolote lile ambalo halikuharamishwa basi ni halali.

(iv) Kutoa *Fat'wa* kuhusiana na hali za dharura zinazojitokeza kisiasa, kiuchumi n.k.

***Kazi za Warasimu (Ulul-Amri)***

Wenye mamlaka *(Ulul-Amri)* katika dola ya Kiislamu ni wasimamizi wa utekelezaji wa maamrisho na makatazo ya Allah (s.w.), kazi yao kubwa ni kuiandaa jamii kuyapokea, kuyakubali, kuyatii na kuyatekeleza maamrisho hayo katika maisha ya kila siku.

Utaratibu huu wa Urasimu wa dola ya Kiislamu unatofautiana na ule wa dola za kitwaghutii ambao huwafanya Warasimu kuwa waheshimiwa na watawala. Amri ya Allah juu utii kwa viongozi ni:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ وَأُوْلِى ٱلْأَمْرِ مِنكُمْۖ فَإِن تَنَـٰزَعْتُمْ فِى شَىْءٍ فَرُدُّوهُ إِلَى ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلْيَوْمِ ٱلْأَخِرِۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lo lote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Kufanya hivyo ni bora kwenu na kuna matokeo mazuri(4:59).*

Utii kwa wenye mamlaka ndani ya dola ya Kiislamu hutanguliza sharti la wao kwanza *(Ulul-Amri)* kuwa watiifu kwa Allah (s.w.) na Mtume wake. Kinyume na hivyo, Qur'an ina maelekezo yafuatayo:

وَلَا تُطِيعُوٓاْ أَمْرَ ٱلْمُسْرِفِينَ ﴿١٥١﴾ ٱلَّذِينَ يُفْسِدُونَ فِى ٱلْأَرْضِ وَلَا يُصْلِحُونَ ﴿١٥٢﴾

*"Wala msitii amri za wale maasi, (wenye kupindukia mipaka ya Mungu). " Ambao wanafanya uharibifu tu katika ardhi wala hawaitengenezi. " (26:151-152)*

### *Kazi za Mahakama*

Wajibu wa Mahakama katika dola ya Kiislamu ni kufafanua, kusimamia na kuhakikisha hukumu na sheria za Allah zinatekelezwa ili kulinda haki; kuzuia maovu,

ufisadi na dhulma katika jamii:

وَأَنزَلۡنَآ إِلَيۡكَ ٱلۡكِتَٰبَ بِٱلۡحَقِّ مُصَدِّقٗا لِّمَا بَيۡنَ يَدَيۡهِ مِنَ
ٱلۡكِتَٰبِ وَمُهَيۡمِنًا عَلَيۡهِۖ فَٱحۡكُم بَيۡنَهُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُۖ
وَلَا تَتَّبِعۡ أَهۡوَآءَهُمۡ عَمَّا جَآءَكَ مِنَ ٱلۡحَقِّۚ لِكُلّٖ جَعَلۡنَا
مِنكُمۡ شِرۡعَةٗ وَمِنۡهَاجٗاۚ وَلَوۡ شَآءَ ٱللَّهُ لَجَعَلَكُمۡ أُمَّةٗ
وَٰحِدَةٗ وَلَٰكِن لِّيَبۡلُوَكُمۡ فِي مَآ ءَاتَىٰكُمۡۖ فَٱسۡتَبِقُواْ
ٱلۡخَيۡرَٰتِۚ إِلَى ٱللَّهِ مَرۡجِعُكُمۡ جَمِيعٗا فَيُنَبِّئُكُم بِمَا
كُنتُمۡ فِيهِ تَخۡتَلِفُونَ ٤٨

*Na tumekuteremshia Kitabu kwa (ajili ya kubainisha) haki, kinachosadikisha vitabu vilivyokuwa kabla yake, na kuvihukumia (kama haya ndiyo yaliyoharibiwa au ndiyo yaliyoasalimika). Basi wahukumu baina yao kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao kwa kuacha haki iliyokufikia. Na kila (umma) katika nyinyi (binadamu) tumeujaalia sheria yake na njia yake. Na kama Mwenyezi Mungu angalitaka angekufanyeni kundi moja (Ia kufuata sheria moja), lakini anataka kukujaribuni kwa hayo aliyokupeni. Basi shindaneni kuyafikilia mambo ya kheri. Nyinyi nyote marudio yenu ni kwa Mwenyezi Mungu; naye atakwambieni (yote) yale*

*mliyokuwa mkikhitilafiana.(5:48)*

وَأَنِ ٱحْكُم بَيْنَهُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَآءَهُمْ

*Na wahukumu baina yao kwa yale aliyokuteremshia Mwenyezi Mungu, wala usifuate matamanio yao...(5:49)*

أَفَحُكْمَ ٱلْجَٰهِلِيَّةِ يَبْغُونَ ۚ وَمَنْ أَحْسَنُ مِنَ ٱللَّهِ حُكْمًا
لِّقَوْمٍ يُوقِنُونَ ﴿٥٠﴾

*Je, wao wanataka hukumu za Kitwaghuti? Na nani aliye mwema zaidi katika hukumu kuliko Mwenyezi Mungu; (yanafahamika haya) kwa watu wenye yakini." (5:50).*

Kuhukumu kinyume na hukumu za Allah (s.w.) ni kuleta dhulma katika jamii. Ni kwa msingi huu Allah (s.w.) anatuasa:

وَمَن لَّمْ يَحْكُم بِمَآ أَنزَلَ ٱللَّهُ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلظَّٰلِمُونَ

"*... Na wasio hukumu kwa yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, basi hao ndio madhalimu*". (5:45).

**Uraia katika Dola ya Kiislamu**

Dola ya Kiislamu ina raia wa aina mbili ndani ya mipaka yake:
(1) Waislamu (2) Dhimmi. Qur'an inafahamisha ifuatavyo:

إِنَّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ وَهَاجَرُوا۟ وَجَٰهَدُوا۟ بِأَمْوَٰلِهِمْ وَأَنفُسِهِمْ
فِى سَبِيلِ ٱللَّهِ وَٱلَّذِينَ ءَاوَوا۟ وَّنَصَرُوٓا۟ أُو۟لَٰٓئِكَ بَعْضُهُمْ

أَوْلِيَآءُ بَعْضٍۚ وَٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ وَلَمْ يُهَاجِرُواْ مَا لَكُم مِّن
وَلَـٰيَتِهِم مِّن شَيْءٍ حَتَّىٰ يُهَاجِرُواْۚ وَإِنِ ٱسْتَنصَرُوكُمْ
فِي ٱلدِّينِ فَعَلَيْكُمُ ٱلنَّصْرُ إِلَّا عَلَىٰ قَوْمِۭ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُم
مِّيثَـٰقٌۗ وَٱللَّهُ بِمَا تَعْمَلُونَ بَصِيرٌ ﴿٧٢﴾

*Hakika wale walioamini na wakahama na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao; (Nao ni wale Muhajiri -Waislamu wa Makka). Na wale waliowapa (Muhajiri) mahala pa kukaa (Nao ni Ansari) na wakainusuru (dini ya Mungu); hao ndio marafiki, wao kwa wao (katika kurithiana na mengineyo). Na wale walioamini, lakini hawakuhama, ninyi hamna haki ya kurithiana nao (wala ya mengineyo) hata kidogo mpaka wahame katika nchi ya kikafiri waje wakae nchi moja na nyinyi). Lakini wakiomba msaada kwenu katika dini, basi ni juu yenu kuwasaidia, isipokuwa juu ya watu ambao kuna mapatano baina yenu na wao, (hapo msiwasaidie wao mkapigana na waitifaki wenu. Lakini jitahidini kupatanisha). Na Mwenyezi Mungu anayaona (yote) mnayoyatenda. (8: 72).*

Kutokana na aya hii, sifa za kustahiki uraia ndani ya Dola ya Kiislamu ni Uislamu na asili au uzawa ndani ya mipaka ya Dola Kiislamu. Muislamu yoyote yule hata kama ni mhamiaji ni raia anaetambulika na kukubalika na Dola bila ya kujali rangi, taifa au lugha yake. Dola ya Kiislamu inawatambua Waislamu wote kama ni raia zake na wote hao ni ndugu:

إِنَّمَا ٱلۡمُؤۡمِنُونَ إِخۡوَةٞ فَأَصۡلِحُواْ بَيۡنَ أَخَوَيۡكُمۡۚ
وَٱتَّقُواْ ٱللَّهَ لَعَلَّكُمۡ تُرۡحَمُونَ ١٠

*Kwa hakika Waislamu wote ni ndugu; basi patanisheni baina ya ndugu zenu, na Mcheni Mwenyezi Mungu (msipuuze jambo la kupatanisha) ili mrehemewe. " (49:10).*

Kuhusiana na wale ambao si Waislamu lakini ni wazawa ndani ya mipaka ya Dola ya Kiislamu, uraia wao utatambuliwa iwapo watakubali kutii maamrisho ya Dola. Raia hawa watiifu kwa Dola katika sheria ya Kiislamu huitwa dhimmi na hustahiki hupata haki zote kama raia.

**Msonge wa Uongozi katika Dola ya Kiislamu**

Msonge wa uongozi katika Dola ya Kiislamu umebainishwa wazi katika Qur'an na kufasiriwa vyema na Mtume Muhammad (s.a.w) katika Dola ya Kiislamu aliyoiunda. Hebu turejee aya zifuatazo:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوٓاْ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَأَطِيعُواْ ٱلرَّسُولَ
وَأُوْلِي ٱلۡأَمۡرِ مِنكُمۡۖ فَإِن تَنَٰزَعۡتُمۡ فِي شَيۡءٖ فَرُدُّوهُ إِلَى
ٱللَّهِ وَٱلرَّسُولِ إِن كُنتُمۡ تُؤۡمِنُونَ بِٱللَّهِ وَٱلۡيَوۡمِ ٱلۡأٓخِرِۚ
ذَٰلِكَ خَيۡرٞ وَأَحۡسَنُ تَأۡوِيلًا ٥٩

*Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu walio katika' nyie. Na kama mkikhitilafiana juu ya jambo lolote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume; ikiwa mnamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hiyo ndiyo kheri na ina matokeo bora kabisa.(4:59)*

Katika aya hii tunajifunza kuwa aliye juu na anayestahiki kupewa utii wa kwanza au anayestahiki kupwekeshwa kwa utii ni Allah (s.w.), kisha hufuatia Mtume wake ndipo hufuatia viongozi wa jamii *(Warasimu)* wa ngazi mbalimbali. Viongozi hawa wa jamii, kwa mujibu wa aya hii, watastahiki kutiiwa tu pindi watakapokuwa ni Waislamu wanaoongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah.

## Msonge wa uongozi katika Uislamu

Msonge wa uongozi katika jamii yoyote ya Kiislamu.

| **Msonge wa uongozi katika jamii yoyote ya Kiislamu.** | **Msonge wa uongozi katika Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume.** |
|---|---|
| 1. Allah (s.w.) Qur'an) | 1. Allah (s.w.) |
| 2. Mtume (s.a.w.) (Sunnah) | 2. Mtume Muhammad (s.a.w.) |
| 3. Majlis Shura (Bunge) | 3. Shura (Sekretariati ya Mtume) |
| 4. Viongozi wa Jamii wa ngazi zote (Msonge wa uongozi utatiririka kuanzia Taifani hadi kwenye familia | 4. Viongozi wa Mikoa na viongozi wengine katika ngazi na nyanja mbali mbali. |
| 5. Raia (wenye mchanganyiko wa Waislamu na wasiokuwa Waislamu) | 5.Raia (wenye mchanganyiko wa Mayahudi, Wakristo na W ashirikina) |

**Kwa nini Utii uelekezwe kwanza kwa Allah (s.w.)?**

Allah (s.w.) anastahiki kupewa nafasi ya kwanza na ya juu ya Utii wa mwanaadamu kwa sababu yeye ndiye Muumba na Mmiliki pekee wa mbingu na ardhi na vyote vilivyomo - vidogo na vikubwa na vinavyoonekana na visivyoonekana. Yeye ndiye Mfalme wa kweli mwenye uwezo juu ya kila kitu asiyehitajia msaidizi au mshirika yeyote katika kuuendesha ufalme wake. Ufafanuzi wa ufalme wake tunaupata katika Qur'an. Hebu tuzingatie aya zifuatazo:

إِنَّ رَبَّكُمُ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ
ثُمَّ ٱسْتَوَىٰ عَلَى ٱلْعَرْشِ يُغْشِى ٱلَّيْلَ ٱلنَّهَارَ يَطْلُبُهُۥ حَثِيثًا
وَٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ وَٱلنُّجُومَ مُسَخَّرَٰتٍۭ بِأَمْرِهِۦٓ ۗ أَلَا
لَهُ ٱلْخَلْقُ وَٱلْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٥٤﴾

*Hakika Mola wenu ni Allah aliyeziumba mbingu na ardhi kwa nyakati sita. Kisha akatawalia juu ya arshi Yake. Huufunika usiku kwa mchana ufuatiao upesi upesi; (na huufunika mchana kwa usiku ufuatiao upesi upesi). Na ameliumba jua, mwezi na nyota (Na vyote) vimetiishwa kwa amri Yake. Fahamuni! Kuumba (ni kwa Allah) na amri zote ni zake. Ametukuka kweli kweli Allah, Mfalme (Rabbi) wa walimwengu wote. (7:54)*

ٱلَّذِى لَهُۥ مُلْكُ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ وَلَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ
يَكُن لَّهُۥ شَرِيكٌ فِى ٱلْمُلْكِ وَخَلَقَ كُلَّ شَىْءٍ فَقَدَّرَهُۥ
تَقْدِيرًا ﴿٢﴾

*(Mwenyezi Mungu) ambaye ni wake (pekee) ufalme wa mbingu na ardhi, wala hakuzaa mtoto wala hana mshirika katika ufalme (wake) na ameumba kila kitu na akakikadiria kipimo (chake)(25:2).*

Allah (s.w.) amekiumba kila kitu kwa lengo na akakiwekea utaratibu (sheria madhubuti utakaokiwezesha kuwepo, kubakia na kufikia lengo lake. Hivyo ili kitu chochote kibakie hakina hiari ya kutii sheria za Allah (s.w.) alizokiwekea. Hizi ni sheria za maumbile (natural laws) ambazo hata miili yetu inazitii bila hiari. Allah (s.w) anatutanabahisha:

أَفَغَيْرَ دِينِ ٱللَّهِ يَبْغُونَ وَلَهُۥٓ أَسْلَمَ مَن فِى ٱلسَّمَـٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضِ طَوْعًا وَكَرْهًا وَإِلَيْهِ يُرْجَعُونَ ﴿٨٣﴾

*Je! wanataka dini isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, na hali kila kilichomo mbinguni na ardhini kinamtii yeye kipende kisipende? Na kwake watarejeshwa wote. (3:83)*

Aya hii inamtanabahisha mwanaadamu kuwa pamoja na kwamba amepewa uhuru na uwezo wa kujiamulia utaratibu wa maisha na kujiwekea sharia zitakazo muongoza katika kuendesha maisha yake ya kijamii, kwanini asitumie uhuru huo kwa busara kwa kuamua kufuata utaratibu au sheria za kuendesha maisha ya kijamii alizoziweka Allah (s.w.) ambazo zinalandana na sheria za maumbile zinazofuatwa na kila kilichomo mbinguni na ardhini pamoja na mwili wake wenyewe Je, mwanaadamu atakapo amua kutii utaratibu wa maisha kinyume na ule aliomuwekea Muumba wake; Maisha ya upinzani yatamfikisha wapi kama si katika matatizo ya kijamii ya kila namna na maangamivu? Mwanaadamu

mwenye akili na busara ni yule anayemtii Muumba wake ipasavyo kwa kuitikia wito wake ufuatao:

فَأَقِمْ وَجْهَكَ لِلدِّينِ حَنِيفًا ۚ فِطْرَتَ ٱللَّهِ ٱلَّتِى فَطَرَ ٱلنَّاسَ
عَلَيْهَا ۚ لَا تَبْدِيلَ لِخَلْقِ ٱللَّهِ ۚ ذَٰلِكَ ٱلدِّينُ ٱلْقَيِّمُ وَلَٰكِنَّ
أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٠﴾

*Basi uelekeze uso wako katika dini iliyo sawa sawa - ndilo umbile Mwenyezi Mungu alilowaumbia watu, (yaani dini hii ya Kiislamu inawafikiana bara bara na umbo la binaadamu). Hakuna mabadiliko katika maumbile ya viumbe vya Mwenyezi Mungu. Hivyo ndiyo dini ilivyo haki, lakini watu wengi hawajui. (30:30)*

**Kwa nini Mtume (s.a.w) achukue nafasi ya pili ya utii?**

Ilivyo ni kwamba, Allah (s.w.) katika utaratibu wake wenye hikima, hawasiliani na kila mwanaadamu bali amewateua wajumbe wake miongoni mwa wanaadamu kufikisha ujumbe wake kwa wanaadamu wote na kuwafundisha kwa matendo namna ya kuutekeleza ujumbe huo katika kuendesha maisha yao ya kila siku kwa mtu binafsi na kwa jamii kwa ujumla.

Wajumbe hawa ni Mitume ambao walifunuliwa na Allah (s.w.) namna ya kuiongoza jamii katika njia anayoiridhia. Ambayo ndiyo pekee inayomfikisha mwanaadamu katika lengo la kuumbwa kwake kwa furaha na amani. Mitume wa Allah (s.w.) wamethibitishwa kwa walimwengu na mwenyewe Allah (s.w) kwa kuwaambatanisha na dalili mbalimbali na pia amewateremshia vitabu kutoka kwake ambavyo ni mwongozo kamili wa maisha ya mwanaadamu na ni vyenye kutoa hukumu baina ya watu kwa uadilifu.

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِٱلْبَيِّنَٰتِ وَأَنزَلْنَا مَعَهُمُ ٱلْكِتَٰبَ وَٱلْمِيزَانَ لِيَقُومَ ٱلنَّاسُ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَأَنزَلْنَا ٱلْحَدِيدَ فِيهِ بَأْسٌ شَدِيدٌ وَمَنَٰفِعُ لِلنَّاسِ وَلِيَعْلَمَ ٱللَّهُ مَن يَنصُرُهُۥ وَرُسُلَهُۥ بِٱلْغَيْبِ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ قَوِىٌّ عَزِيزٌ ﴿٢٥﴾

*Kwa hakika tuliwapeleka Mitume wetu kwa dalili wazi wazi na tukaviteremsha vitabu na uadilifu pamoja nao, ili watu wasimamie uadilifu(57:25)*

Mitume wa Allah (s.w.) ni tofauti na viongozi wa kawaida ambao huongoza kwa kutumia fikra na jitihada za kibinaadamu ambazo mara zote huathiriwa na udhaifu mwingi alionao. Mwanaadamu wa kawaida anaathiriwa sana na mazingira yake, matashi yake na ufinyu wa elimu yake. Kutokana na udhaifu huu si lazima kila atakaloamua, liwe sahihi na lenye manufaa kwa jamii. Lakini Mitume hawaongozi kwa fikra na matashi yao, bali huongoza kwa ufunuo (Wahyi) kutoka kwa Allah (s.w.) ambaye ni mjuzi wa kila kitu mwenye habari ya mambo yote. Allah (s.w.) anatuthibitishia hili katika Qur'an:

وَٱلنَّجْمِ إِذَا هَوَىٰ ﴿١﴾ مَا ضَلَّ صَاحِبُكُمْ وَمَا غَوَىٰ ﴿٢﴾ وَمَا يَنطِقُ عَنِ ٱلْهَوَىٰٓ ﴿٣﴾

*Naapa kwa nyota zinapoanguka kwamba mtu wenu (huyu Nabii Muhammad) hakupotea wala hakukosa, wala hasemi kwa matamanio (ya nafsi Yake). Hayakuwa haya anayosema ila ni Wahyi (ufunuo) uliofunuliwa (kwake). Amemfundisha (Malaika) mwenye nguvu sana. (53:1-5).*

Hivyo mwanaadamu hawezi kufuata njia ya uongofu anayoiridhia Allah (s.w.) ambayo ndiyo pekee yenye kumuwezesha kupata furaha na amani katika maisha yake hapa ulimwenguni pasina na kumtii Mtume wa Allah (s. w.). Qur' an inatubainishia:

مَّن يُطِعِ ٱلرَّسُولَ فَقَدۡ أَطَاعَ ٱللَّهَۖ

*Mwenye kumtii Mtume amemtii Allah…". (4:80)*

قُلۡ إِن كُنتُمۡ تُحِبُّونَ ٱللَّهَ فَٱتَّبِعُونِي يُحۡبِبۡكُمُ ٱللَّهُ وَيَغۡفِرۡ
لَكُمۡ ذُنُوبَكُمۡۚ وَٱللَّهُ غَفُورٞ رَّحِيمٞ ٣١

*Sema (ewe Muhammad): ikiwa nyinyi mnampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni (hapo) Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakughufirieni dhambi zenu. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye maghfira mwenye rehema.*

قُلۡ أَطِيعُواْ ٱللَّهَ وَٱلرَّسُولَۖ فَإِن تَوَلَّوۡاْ فَإِنَّ ٱللَّهَ لَا وَٱللَّهُ
غَفُورٞ رَّحِيمٞ ٣١

*Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume (wake). Na kama mkikengeuka (Mwenyezi Mungu atakutieni adabu). Kwani Mwenyezi Mungu hawapendi Makafiri. (3:31-32)*

**Masharti ya kuwatii viongozi (Ulul-amri)**

Viongozi au wenye mamlaka *(Ulul-amr)* waliokusudiwa katika Qur'an (4:59) ni viongozi wa aina zote na wa ngazi zote katika fani zote za jamii ambao huielekeza na kuiongoza jamii kwenye kuliendea lengo la maisha. Qur'an haituamrishi kumtii kila kiongozi au kila mwenye mamlaka juu yetu kwa sababu si kila kiongozi anawaongoza vyema walio chini yake na kuwaelekeza kwenye kufikia

lengo la maisha yao. Kuna viongozi wengine wanawatoa watu wao kwenye maisha ya furaha na amani na kuwatumbukiza kwenye maisha ya matatizo na huzuni. Viongozi tunaoamrishwa na Allah (s.w.) kuwa tuwatii ni wale tu Waislamu ambao ni wacha Mungu wanaoongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Viongozi hawa tulioamrishwa kuwatii hawako juu ya sheria bali nao wako sawa na wale wanaowaongoza. Wako tayari kukosolewa na kurejeshwa kwenye Qur'an na Sunnah endapo watateleza kidogo katika kufanyakazi yao. Viongozi wa namna hii ndio pekee tunaoamrishwa tuwatii kwani ndio pekee wanaotuongoza katika njia iliyonyooka:

ٱللَّهُ وَلِيُّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُخْرِجُهُم مِّنَ ٱلظُّلُمَـٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۖ

*Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini Huwatoa katika giza na kuwaingiza katika nuru (2:257)*

Kinyume chake, Waislamu tumeamrishwa tusiwatii viongozi wanaoongoza kwa miongozo mingine kinyume na Qur'an na Sunnah. Inasisitizwa katika Qur'an:

وَلَا تُطِعِ ٱلْكَـٰفِرِينَ وَٱلْمُنَـٰفِقِينَ وَدَعْ أَذَىٰهُمْ وَتَوَكَّلْ

عَلَى ٱللَّهِ ۚ وَكَفَىٰ بِٱللَّهِ وَكِيلًا ﴿٤٨﴾

*Na usiwatii makafiri na wanafiki wala usijali udhia wao, na mtegemee Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi. (33:48)*

وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ ٱلْحَيَوٰةِ ٱلدُّنْيَا ۖ وَلَا

تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُۥ عَن ذِكْرِنَا وَٱتَّبَعَ هَوَىٰهُ وَكَانَ

أَمْرُهُۥ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

*"… Wala usiwatii wale ambao tumezighafilisha nyoyo zao wakafuata matamanio yao, na mambo yao yakawa yamepita mipaka (yaani makafiri). (18:28)*

Tukiwatii viongozi hawa kinyume na mwongozo wa Allah (s.w.) tutakuwa tumewafanya miungu yetu na kuangukia kwenye shirk. Tumekatazwa kuwatii hawa kwa sababu watatuelekeza kwenye maovu na kuacha maadili mema ili tu wakidhi matashi ya nafsi zao.

وَإِن جَٰهَدَاكَ عَلَىٰٓ أَن تُشْرِكَ بِى مَا لَيْسَ لَكَ بِهِۦ
عِلْمٌ فَلَا تُطِعْهُمَا ۖ وَصَاحِبْهُمَا فِى ٱلدُّنْيَا مَعْرُوفًا ۖ
وَٱتَّبِعْ سَبِيلَ مَنْ أَنَابَ إِلَىَّ ۚ ثُمَّ إِلَىَّ مَرْجِعُكُمْ
فَأُنَبِّئُكُم بِمَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٥﴾

*Na (wazazi wako) wakikushurutisha kunishirikisha na (yale) ambayo huna elimu nayo, usiwatii lakini kaa nao kwa wema hapa duniani. Shika njia ya wale wanaoelekea kwangu kisha marejeo yenu ni kwangu, hapo nitakuambieni mliyokuwa mkiyatenda. (31: 15)*

Pia Mtume (s.a.w.) ametukataza kuwatii viongozi wanaotuelekeza kwenye uovu kama tunavyojifunza katika Hadith zifuatazo:

*Ibn Umar (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.* w.) *amesema: Muislamu analazimika kumsikiliza na kumtii kiongozi kwa lolote lile atakalomuamrisha, likiwa linampendeza au linamchukiza alimradi hamuamrishi kufanya kitendo kiovu. Atakapo amrishwa kufanya kitendo kiovu, hakuna kumsikiliza wala kumtii" (Bukhari na Muslim) Ali (r.a) ameeleza kuwa Mtume (s.a.* w.) *amesema:Hapana utii kwenye uovu (dhambi). Hakika utii ni wa matendo mazuri tu" (Bukhari na Muslim)*

Tukiwatii viongozi hawa watatutoa kwenye maisha ya nuru, wema na uadilifu na kutuingiza kwenye maisha ya giza la uovu na utapeli ambayo daima huidumaza na kuihilikisha jamii. Allah (s.w.) anatutanabahisha kwa kusema:

وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ أَوْلِيَآؤُهُمُ ٱلطَّـٰغُوتُ يُخْرِجُونَهُم
مِّنَ ٱلنُّورِ إِلَى ٱلظُّلُمَـٰتِ ۗ أُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ
هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

*" Na waliokufuru walinzi (viongozi) wao ni Matwaghuti (wachupaji mipaka ya Allah). Huwatoa katika nuru na kuwaingiza katika giza. Hao ndio watu wa motoni, humo watakaa milele. " (2:257)*

Matwaghuti ni wachupaji mipaka ya Allah (s.w.). Wale wote wanaoiongoza jamii kwa miongozo inayochupa mipaka ya Allah (s.w.) au inayopingana na Qur'an na Sunnah. Pia Allah (s.w.) anawatanabahisha Waislamu juu ya viongozi hawa walio kataa mwongozo wake:

وَلَا يَزَالُونَ يُقَـٰتِلُونَكُمْ حَتَّىٰ يَرُدُّوكُمْ عَن دِينِكُمْ
إِنِ ٱسْتَطَـٰعُوا۟ ۚ وَمَن يَرْتَدِدْ مِنكُمْ عَن دِينِهِۦ فَيَمُتْ
وَهُوَ كَافِرٌ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ حَبِطَتْ أَعْمَـٰلُهُمْ فِى ٱلدُّنْيَا
وَٱلْـَٔاخِرَةِ ۖ وَأُو۟لَـٰٓئِكَ أَصْحَـٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَـٰلِدُونَ ﴿٢١٧﴾

*" Wala (Makafiri) hawataacha kupigana nanyi mpaka wakutoeni katika dini yenu kama wakiweza. Na watakaotoka katika dini yao katika nyinyi, kisha wakafa hali ya kuwa makafiri, basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na Akhera. Na ndio watu wa Motoni; humo watakaa milele" (2:217)*

Ni haramu kwa Waislamu wa kweli kweli kumtii yeyote kinyume na Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Kumtii yeyote kinyume na Allah (s.w.) ni kumfanya huyo unayemtii kuwa Mungu wako kama tunavyofahamishwa katika Qur'an:

ٱتَّخَذُوٓا۟ أَحْبَارَهُمْ وَرُهْبَـٰنَهُمْ أَرْبَابًا مِّن دُونِ ٱللَّهِ

*Wamewafanya wanavyuoni wao na watawa wao kuwa ni Miungu badala ya Mwenyezi Mungu (9:31)*

Katika aya hii Mayahudi na Wakristo wanashutumiwa kuwa waliwafanya viongozi wao Miungu badala ya Allah (s.w.). Mtume (s.a.w.) katika kufafanua aya hii anatufahamisha kuwa Mayahudi na Wakristo hawashutumiwi hivyo kwa kuwaita au kuitakidi kuwa viongozi wao ni Miungu, bali walishutumiwa hivyo kwa kuwa walikuwa wakiwatii kinyume na maamrisho na makatazo ya Allah (s.w.)

**Sifa za anayestahiki kuwa kiongozi**

Kiongozi wa Kiislamu hachaguliwi kwa kuomba kura na kuwahonga wapiga kura kama wachaguliwavyo viongozi wa Kitwaghutii. Mtume (s.a.w.) amekataza asichaguliwe kuwa kiongozi yule anayeomba uongozi:

*Abdul-Rahman bin Samurah (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Usiombe uongozi kwa sababu utakapopewa uongozi kwa kuomba utaachiwa*

*peke yako jukumu la uongozi, na kama umepewa bila ya kuomba, utasaidiwa katika uongozi huo" (Bukhari na Muslim)*

Yeye mwenyewe Mtume (s.aw.) alikataa kuwachagua wale walioomba uongozi miongoni mwa masahaba zake kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Abu Mussa ameeleza: "Tulikwenda kwa Mtume (s.a.w.), mimi pamoja na binamu zangu. Mmoja wao akasema: "Ee Mtume wa Mwenyezi Mungu! Nifanye niwe gavana wa nchi ambamo Allah (s.w.) amekupa mamlaka juu yake. Na yule mwingine naye akamuomba hivyo hivyo. Akasema Mtume wa Allah, "Hatumchagui kwenye uongozi huu yeyote anayeomba wala hachaguliwi yule aliye mroho wa uongozi. "*

*Katika riwaya nyingine alisema Mtume: "Hatuwachagui kwenye nafasi zetu za uongozi wale wanaotaka uongozi" (Bukhari na Muslim)*

Muislamu wa kweli anafahamu vyema kuwa uongozi ni amana nzito na mtihani mkubwa. Hawezi kamwe kuomba uongozi, sembuse kuufanyia kampeni na kuununua kwa hongo! Mtume (s.a.w.) anathibitisha hivyo katika Hadith ifuatayo:

*Abu Hurairah ameeleza kuwa Mtume wa Allah amesema: "Utawaona watu hawapendi kabisa kazi ya uongozi mpaka uchaguzi utakapo waangukia (kwa kubebeshwa)". (Bukhari na Muslim)*

Katika jamii ya Kiislamu atachaguliwa kuwa kiongozi mtu mwenye sifa zifuatazo:

**Kwanza**, awe Muislamu Mcha-Mungu. Hii ni tabia anayotakiwa asifike nayo kila Muislamu wa kweli. Mcha-

Mungu ni yule anayeishi kwa kuchunga mipaka ya Allah (s.w.) kwa kujitahidi kwa jitihada zake zote kufuata maamrisho yote ya Allah (s.w.) na kuacha makatazo Yake yote. Anafanya hivyo kwa sababu anahofia adhabu kali ya Allah (s.w.) isiyo na kifani endapo atatenda kinyume na maamrisho Yake na pia ana matarajio ya kupata radhi ya Allah (s.w.) na malipo makubwa yasiyo na kifani endapo ataishi maisha ya kutii maamrisho Yake yote. Kiongozi Mcha-Mungu kwa vyovyote vile atakuwa muadilifu katika kazi yake.

**Pili**, awe mjuzi wa Qur'an na Sunnah na mwenye ujuzi na uzoefu wa kazi anayotakiwa aifanye katika eneo lake la uongozi. Ujuzi wa kutosha wa Qur'an na Hadith ni muhimu sana kwani ndio mwongozo anaotarajiwa kuutumia katika uongozi wake.

Ujuzi wa kazi ya uongozi ni muhimu pia kwani pamoja na ucha-Mungu wa mtu na ujuzi wa Qur'an na Hadith, hataweza kuongoza vizuri iwapo hana ujuzi na uzoefu wa uongozi. Umuhimu wa sifa ya elimu kuwa nayo kiongozi umebainishwa katika Qur'an, Taluti alipochaguliwa kuwa Mfalme wa Mayahudi:

وَقَالَ لَهُمْ نَبِيُّهُمْ إِنَّ ٱللَّهَ قَدْ بَعَثَ لَكُمْ طَالُوتَ مَلِكًا ۚ
قَالُوٓا۟ أَنَّىٰ يَكُونُ لَهُ ٱلْمُلْكُ عَلَيْنَا وَنَحْنُ أَحَقُّ بِٱلْمُلْكِ مِنْهُ
وَلَمْ يُؤْتَ سَعَةً مِّنَ ٱلْمَالِ ۚ قَالَ إِنَّ ٱللَّهَ ٱصْطَفَىٰهُ عَلَيْكُمْ
وَزَادَهُۥ بَسْطَةً فِى ٱلْعِلْمِ وَٱلْجِسْمِ ۖ وَٱللَّهُ يُؤْتِى مُلْكَهُۥ مَن
يَشَآءُ ۚ وَٱللَّهُ وَٰسِعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٤٧﴾

*Na huyo Mtume wao akawaambia: "Mwenyezi Mungu amekuchagulieni Taluti kuwa Mfalme:. Wakasema: "Vipi atakuwa na ufalme juu yetu, nahali sisi tumestahiki zaidi kupata 'ufalme kuliko yeye, naye hakupewa wasaa wa mali?" Akasema: "Mwenyezi Mungu amemchagua juu yenu na amemzidishia wasaa wa elimu na kiwiliwili. Na Mwenyezi Mungu humpa ufalme wake amtakaye. Na Mwenyezi Mungu ni mwenye wasaa, Mjuzi". (2:247)*

Tunajifunza kuwa utajiri au nasaba ya mtu siyo vitu vya msingi vya kuangaliwa katika kumchagua kiongozi bali vitu vya msingi vinavyoangaliwa ni uchaji wa mtu na elimu Yake.

**Tatu**, ambayo pia imetajwa katika aya hii ni Siha nzuri na uwezo wa kimwili: Mtu mcha-Mungu, mwenye elimu mwenye siha nzuri na mwili wenye nguvu anastahiki zaidi kuchaguliwa kuwa kiongozi kuliko mtu dhaifu.

**Nne**, ya mtu anayestahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Waislamu ni tabia njema. Mtu mwenye tabia njema ni yule anayejitahidi kwa kadri ya uwezo wake kujipamba na vipengele vyote vya tabia njema. Kwa mtazamo mwingine mtu mwenye tabia njema ni yule anayejitahidi kuiga mwenendo wa Mtume (s.a.w.) kama inavyosisitizwa katika Qur'an:

لَّقَدْ كَانَ لَكُمْ فِى رَسُولِ ٱللَّهِ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ لِّمَن كَانَ
يَرْجُوا۟ ٱللَّهَ وَٱلْيَوْمَ ٱلْـَٔاخِرَ وَذَكَرَ ٱللَّهَ كَثِيرًا ﴿٢١﴾

*Bila shaka mnao mfano mwema (ruwaza nzuri) kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa mwenye kumuogopa Mwenyezi Mungu na siku ya Mwisho na kumtaja Mwenyezi Mungu sana (33:21)*

Na mwenendo wa Mtume ulikuwa ni kufuata Qur'an vilivyo. Allah (s.w.) anamsifu Mtume wake kwa tabia njema aliyokuwa nayo:

وَإِنَّكَ لَعَلَىٰ خُلُقٍ عَظِيمٍ ﴿٤﴾

*Na bila shaka una Tabia njema kabisa (68:4)*

Pia Mtume (s.a.w.) amesisitiza ubora wa mtu mwenye tabia njema kwa kusema:

*"Mbora wenu ni yule aliye mbora kwenu kwa tabia njema" (Bukhari na Muslim)*

Hivyo, mwenye tabia njema kuliko wengine ndiye atakayestahiki kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Waislamu.

Hizi ndizo sifa anazotakiwa awe nazo kiongozi wa Kiislamu. Yeyote katika jamii ya Kiislamu atakayekuwa na sifa hizi anastahiki kuwa kiongozi wa watu bila ya kujali nasaba yake, taifa lake, rangi yake, umaarufu wake au wasaa wake wa kimali. Aliowachagua Mtume (s.a.w.) kushika nyadhifa mbalimbali katika uongozi wa serikali ya Kiislamu walikuwa Waislamu wenye tabia njema kweli kweli. Katika uchaguzi wake hakujali nasaba, taifa au rangi. Kwa mfano, alimchagua Bilal (r.a) aliyekuwa Mhabeshi kuwa Muadhini bila ya kujali manung'uniko ya baadhi ya masahaba wake. Pia alichaguliwa Zaid bin Harith ambaye hakuwa na umaarufu wowote miongoni mwa Masahaba wake kuwa Kamanda wa jeshi pamoja na manung 'uniko yaliyojitokeza mbele ya Mtume (s.a.w.).

lkitokea watu wenye sifa hizi za uongozi ni wengi kuliko nafasi za uongozi, wale walio mstari wa mbele na uzoefu wa muda mrefu katika harakati za kuupigania Uislamu watachaguliwa kwanza. Endapo bado watakuwa wengi kuliko nafasi zilizopo, watachaguliwa wale wenye umri mkubwa zaidi. Endapo bado watakuwa wengi kuliko

mahitaji, itapigwa kura na Waislamu wote, wake kwa waume, na watakaopata kura nyingi zaidi ndio watakaostahiki kuwa viongozi wa jamii.

Mfano mzuri wa kuigwa ni ule wa kuchaguliwa kwa Abu Bakr (r.a.) kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume Muhammad (s.a.w.). Baada ya maafikiano kati ya Answar na Muhajirina kuwa kutokana na uzoefu wa kazi ya kusimamisha dini ya Allah (s.w.), Muhajiriina ndio wachukue nafasi ya Ukhalifa, Abu Bakr alimpendekeza Umar (r.a) au Abu-Ubaidah (r.a.) achaguliwe kuwa Khalifa. Lakini wote wawili walikataa pendekezo hilo na kusema

> "Hapana, hatuwezi kukutangulia mbele katika jambo hili. Bila shaka wewe ni mbora kuliko Muhajiriina wote (kwa kila kitu). Ulikuwa na Mtume katika pango, Mtume alikuchagua kuongoza swala kwa niaba yake alipokuwa mgonjwa, na swala ndiyo nguzo kubwa ya dini. Ni nani mwingine anayestahiki kuchukua nafasi hii ya Ukhalifa kuliko wewe? Nyoosha mkono wako tukupe "Bai'at".

Baada ya kiongozi wa Kiislamu kuchaguliwa kwa kufuata utaratibu huu Waislamu hulazimika kutoa ahadi ya utii - Bai'at". Ahadi hii inafungamana na kiongozi; bali pia ni ahadi kwa Allah (s.w.) kama inavyobainika katika Qur'an:

إِنَّ ٱلَّذِينَ يُبَايِعُونَكَ إِنَّمَا يُبَايِعُونَ ٱللَّهَ يَدُ ٱللَّهِ فَوْقَ
أَيْدِيهِمْ ۚ فَمَن نَّكَثَ فَإِنَّمَا يَنكُثُ عَلَىٰ نَفْسِهِۦ ۖ وَمَنْ
أَوْفَىٰ بِمَا عَـٰهَدَ عَلَيْهُ ٱللَّهَ فَسَيُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١٠﴾

*Bila shaka wale waliofungamana nawe, kwa hakika wamefungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Bali avunjaye ahadi amevunja kwa kuidhuru nafsi yake, atekelezaye aliyomuahidi Mwenyezi Mungu; (Mwenyezi Mungu) atamlipa ujira mkubwa. (48:10).*

Amri ya kuwatii viongozi ipo wazi katika Qur'an (4:59). Pia msisitizo wa kuwatii viongozi unapatikana katika Hadithi ifuatayo:

*Abu Hurairah amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Atakayenitii amemtii Allah na atakayeniasi amemuasi Allah; na atakayemtii kiongozi amenitii na atakayemuasi kiongozi ameniasi " (Bukhari na Muslim)*

Kumpinga kiongozi aliyechaguliwa na watu kwa halali ni katika uasi mkubwa. Yeyote yule anayempinga (anayempiga vita) kiongozi wa halali anayewaongoza watu katika njia ya usawa, anauchu wa madaraka na anataka kuvuruga amani, utulivu na mshikamano wa jamii. Mtu wa namna hii anastahiki kuuawa kwa mujibu wa Hadith zifautazo:

*Urfajah ameeleza kuwa amesikia Mtume (s.a.* w.) *akasema: "Hivi karibuni patakuwa na upinzani na uasi. Anayetaka kuwagawanya watu walioungana muueni popote pale alipo "(Muslim)*

*Abu Said (r.a) amesimulia kuwa Mtume (s.a.* w.) *amesema: Ahadi ya utii itakapotolewa kwa Makhalifa wawili kwa wakati mmoja, muueni wa pili" (Muslim)*

Hadith zinaonesha uovu wa kupinga uongozi halali unaoendesha mambo kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Waislamu hawawajibiki kuwatii na wanaamrishwa kutowatii viongozi wanao waongoza kwenye mambo maovu.

Katika Khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w.) Abu Bakar (r.a) alisema: “Bila shaka nimechaguliwa kuwa Amir (kiongozi) wenu pamoja na kwamba mimi si mbora kuliko nyinyi. Nisaidieni nikiwa katika njia ya usawa na nikosoeni nikikosea” Waislamu walifanya hivyo. Hawakumchelea kiongozi yeyote aliyechupa mipaka ya uongozi wa Qur’an na Sunnah Waislamu wamekatazwa kuwachagua wanawake na watoto kuchukua nafasi ya uongozi wa juu katika jamii kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

> *Abu Bakar (r.a) ameleeza: Mtume (s.a.w.) alipopata habari kuwa Waajemi wamemfanya binti Mfalme kuwa kiongozi wao alisema (Mtume): Hawatafanikiwa kamwe wanaomchagua mwanamke kuwa kiongozi wao “(Baihaq , Ahamad)*

Uongozi ni jukumu kubwa ambalo watoto na wanawake hawana uwezo wa kulibeba. Historia inashuhudia matatizo yaliyotokea katika jamii mbalimbali zilizotawaliwa na wanawake na watoto. Bila shaka hekima ya watoto kukataliwa kupewa uongozi wa jamii iko wazi kwamba akili zao hazijakomaa kiasi cha kuweza kubeba dhima kubwa ya uongozi. Wanawake nao kulingana na umbile lao na dhima kubwa waliyo nayo ya uzazi na malezi ya familia, itakuwa ni kuwaonea kwa kuwapachika tena hii dhima ya uongozi wajamii. Hata hivyo wanawake wanawajibika kuwa viongozi wa jumuiya na idara za wanawake na katika kuongoza shughuli zote za huduma zitolewazo kwa wanawake tu.

**Wajibu wa kiongozi katika dola ya Kiislamu**

Mtume (s.a.w.) ametukumbusha sote kuwa kila mtu ajue kuwa ni kiongozi anayewajibika juu ya wale anaowaongoza na hapana shaka ya kuwepo maulizo ya

Allah (s.w.) juu ya uwajibikaji wake juu ya wale anaowaongoza kwa mujibu wa Hadith ifuatayo.

> *Abdullah bin Umar (r.a) amesimulia kuwa Mtume wa Allah amesema: "Kila mmoja ni mchunga (kiongozi) na kila mmoja ataulizwa juu ya wale aliowaongoza. imam(kiongozi wa jamii) ni mchunga wa watu anaowaongoza na ataulizwa juu yao. Mwanamume ni kiongozi wa familia yake na ataulizwa juu ya watu wa familia yake. Mwanamke ni malkia wa nyumba ya mume wake na watoto na ataulizwa juu yao. Mtumishi ni mchunga wa vitu vya mwajiri wake na ataulizwa juu ya vitu hivyo. Sikilizeni! Hakika kila mmoja ni mchunga (kiongozi) na ataulizwa juu ya wale aliowachunga (aliowaongoza)" (Bukhari na Muslim)*

Katika Hadith hii tunajifunza kuwa kila mtu ni kiongozi na kila kiongozi anao wajibu kwa wale anaowaongoza. Katika kipengele hiki tumejaribu kubainisha wajibu wa viongozi wa Kiislamu kama ifuatavyo:

***1. Ucha-Mungu***

Kiongozi ajitahidi kujikurubisha kwa Allah (s.w.) zaidi kwa kuzidisha swala za (Sunnah), funga za Sunnah, kutoa sadaqa kwa wingi, kuomba dua na maghfira kwa wingi ili kupata msaada wa Allah (s.w.). Kwani kazi ya uongozi ni nzito mno inayohitajia sana msaada wa Allah (s.w.). Pia kiongozi wa jamii ya Kiislamu anawajibika kuzidisha kusoma Qur'an na Hadith ili aweze kufanya kazi yake kwa kuchunga mipaka ya Qur'an na Sunnah na pia aweze kujipamba na mwenendo mwema uliosisitizwa katika Qur'an na Hadith. Kiongozi wa Kiislamu hana budi kujitahidi kuwa kiigizo kwa ucha-Mungu kwa kutekeleza maamrisho yote ya Allah (s.w.) na kujiepusha na makatazo yake yote. Ucha-Mungu ni zana muhimu sana inayomwezesha kiongozi kutekeleza wajibu wake vilivyo.

**2. *Huruma***

Kiongozi awe mnyenyekevu, mpole, mwenye huruma anaye wahurumia wale anaowaongoza na mwenye kuwapendelea lile analolipendelea katika nafsi yake. Kiongozi anatakiwa daima kuwa yeye ni mtumishi wa wale waliomuweka katika uongozi, awaheshimu kama mtumishi anavyomuheshimu bwana wake. Wakati huo huo, kiongozi anatakiwa ajiweke katika nafasi ya ulezi ambayo hana budi kuwahurumia wale anaowalea. Kiongozi wa Kiislamu daima anatakiwa azingatie usia wa Allah (s.w.) ufuatao:

وَهُوَ ٱلَّذِى جَعَلَكُمْ خَلَٰٓئِفَ ٱلْأَرْضِ وَرَفَعَ بَعْضَكُمْ فَوْقَ
بَعْضٍ دَرَجَٰتٍ لِّيَبْلُوَكُمْ فِى مَآ ءَاتَىٰكُمْ ۗ إِنَّ رَبَّكَ سَرِيعُ
ٱلْعِقَابِ وَإِنَّهُۥ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌۢ ﴿١٦٥﴾

*Naye ndiye aliyekujaalieni kuwa Makhalifa (viongozi) katika ardhi. Na amewanyanyua baadhi yenu juu ya wengine daraja kubwa kubwa ili akufanyieni mtihani kwa hayo aliyokupeni. Hakika Mola wako ni mwepesi wa kuhisabu na hakika yeye ni mwingi wa kusamehe, mwingi wa kurehemu. (6:165)*

Kutokana na aya hii tunajifunza kuwa kiongozi anatakiwa mara zote afahamu kuwa wadhifa wa uongozi alia nao ni mtihani kwake. Allah (s.w.) amemuinua daraja na kumfanya kiongozi juu ya wengine ili kumfanyia mtihani kuwa atashukuru neema hiyo aliyotunukiwa na Mola wake kwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo na kuchunga mipaka ya Allah (s.w.) katika kazi hiyo au atakufuru ajipe uungu kwa kuchupa mipaka ya Allah na kuwageuza watumwa wake wale waliomchagua na kumfanya kiongozi wao. Kiongozi anatakiwa awe msaada na rehema kwa wale anaowaongoza na wala asiwe mzigo

na tatizo kwa raia zake hao. Mtume (s.a.w.) kila alipowachagua sahaba zake kuwa viongozi wa mahala mbalimbali daima alikuwa akiwausia kuwa watu wa msaada wenye huruma na upole kwa raia zao.

### 3. *Uadilifu*

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muadilifu. Kipimo cha kiongozi mzuri ni uadilifu. Kiongozi wa Kiislamu akiwa muadilifu huwa Khalifa wa Allah (s. w.) na akiwa si muadilifu huwa Khalifa wa Shetani. Uadilifu unasisitizwa mno katika Qur' an kamatunavyojifunza katika aya ifuatayo:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ بِٱلْقِسْطِ شُهَدَآءَ لِلَّهِ وَلَوْ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمْ أَوِ ٱلْوَٰلِدَيْنِ وَٱلْأَقْرَبِينَ ۚ إِن يَكُنْ غَنِيًّا أَوْ فَقِيرًا

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamia uadilifu, mtoao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au wazazi wenu, au jamaa. Akiwa tajiri au masikini. (4: 135)*

Kiongozi muadilifu ni yule anayechunga haki za watu anaowaongoza. Yeye ni mchunga na mgawaji wa haki. Hana budi kuhakikisha kuwa yeye mwenyewe hachukui haki zake mpaka ahakikishe kuwa kila mtu amepata haki yake.

Mtume (s.a.w.) aliwaamuru wale aliowapa kazi kuwa wasivae kivazi kizuri zaidi kuliko wale wanaowaongoza na wasifunge milango yao wakati watu wanawahitajia haki zao, au wanataka kutoa madukuduku yao.'

Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa awe muaminifu na mkweli na asijilimbikizie mali kwa kutumia madaraka yake ya uongozi. Amir au kiongozi wa juu wa Serikali ya Kiislamu anatakiwa achukue mshahara au posho kutoka kwenye mfuko wa serikali *(Baitul-mali)* kiasi kile tu kinachotosheleza mahitaji muhimu ya chakula, mavazi na makazi kwa yeye mwenyewe na familia yake. Kiongozi wa Kiislamu anatakiwa akumbuke daima kuwa uongozi katika Uislamu si kitega uchumi kama ulivyo uongozi wa Kitwaghuti. Mtume Muhammad (s.a.w.) ambaye ndiye kiongozi wa Ummah huu wa mwisho na kiigizo chetu kwa mwenendo na uongozi wake bora, aliishi maisha rahisi.

Abu Bakar (r.a) alichaguliwa kushika uongozi wa Umma wa Kiislamu mara baada ya kutawafu Mtume (s.a.w.), alifuata nyayo za Mtume (s.a.w.) kwa kila kitu. Maisha Yake yalikuwa rahisi mno. Umar (r.a) aliyechaguliwa kuwa kiongozi wa serikali ya Kiislamu baada ya Abu Bakar alifuata vyema nyayo za uongozi wa Mtume (s.a.w.) na ule wa Abu Bakar. Pamoja na kuwa Umar alikuwa kiongozi wa Dola kubwa ya Kiislamu iliyoenea mashariki ya kati yote na kupanuka hadi Spain, aliishi maisha rahisi sana.

Umar (r.a) alikuwa na kawaida ya kuzunguka usiku ili kujua matatizo ya watu wake. Siku moja katika mizunguko yake alimkuta mama mmoja porini na watoto wake wanalia. Umar (r.a) alipomuuliza kwanini wako pale alimjibu kuwa giza la usiku na baridi kali imewafanya walazimike kulala pale. Alipomuuliza kwanini watoto wanalia, alimjibu kuwa wananjaa. Umar (r.a) aliondoka mbio mpaka kwenye ghala ya Baitul-mali na kuchukua mgongoni mwake gunia la unga wa ngano na mafuta ya kupikia mpaka kwa yule mama. Umar (r.a) alisaidiana naye kupika na baada ya chakula kuiva aliwaamsha watoto na kuwalisha ndipo akarejea nyumbani kwake. Matukio ya aina hii yako mengi katika historia ya ukhalifa wa Umar bin Khattab (r.a).

Kinyume chake viongozi wa Kitwaghuti, huchukua madaraka ya uongozl wanayopewa na jamii zao kama kitega uchumi chao kwa ajili ya kujinufaisha wao binafsi. Huifuja watakavyo na humpa yeyote wamtakaye kwa upendeleo mali ya jamii ambayo imepatikana kwa kukung'uta mifuko ya masikini. Muda mfupi baada ya kiongozi wa Kitwaghuti kukabidhiwa madaraka ya uongozi wa ngazi ya juu katika jamii, utamuona ana gari zuri jipya, ana nyumba nzuri mpya, na mabadiliko ya kila namna katika matumizi yake ya kimaisha pamoja na familia yake.

Kama mambo yenyewe ni haya, kwa nini watu wengine katika jamii ya Kitwaghutii wasiupupie uongozi kwa hali na mali au kwa kufa na kupona? Kwa nini mtu aliyeonja uongozi katika serikali ya Kitwaghuti asing'ang'anie kubakia humo kwa gharama yoyote ile?

Kwa nini mapinduzi ya mara kwa mara na mauaji yasitegemewe katika jamii za Kitwaghuti ambapo watu wanashindania uongozi kwa lengo la kujinufaisha wao binafsi? Haya yote ni matunda machungu yanayotarajiwa katika jamii kutokana na uongozi uliokosa uadilifu.

Kiongozi muadilifu hana budi kuhakikisha kuwa wanyonge katika jamii wanapata haki zao na wenye mali wanatoa haki za wanyonge. Abu Bakar, katika khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Khalifa wa kwanza wa Mtume (s.a.w.) alisisitiza:

> *"Mnyonge miongoni mwenu ni mwenye nguvu katika uongozi wangu mpaka apate haki zake; na mwenye nguvu miongoni mwenu atakuwa dhaifu katika uongozi wangu, mpaka akipenda Allah nichukue haki za watu anazodaiwa... "*

Vile vile ni katika uadilifu kwa kiongozi kuhakikisha kuwa kila mtu mkosaji anahukumiwa kwa mujibu wa sheria bila ya upendeleo au uonevu wowote. Kiongozi hatamchelea yeyote katika kupitisha hukumu. Katika Uislamu watu wote ni sawa mbele ya sheria na hakuna aliye juu ya sheria hata akiwa Amir (Rais) wa nchi.

**4. *Subira***

Kiongozi katika dola ya Kiislamu anatakiwa awe mwenye subira, mvumilivu na mstahimilivu. Kiongozi atekeleze wajibu wake ipasavyo na asitarajiwe kupendwa na kufurahiwa na watu wote. Waumini wa kweli tu ndio watakaomfurahia na kumsaidia atakapowaongoza kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah. Lakini wanafiki, wenye husda, wapenda vyeo na sifa na maadui wote wa Uislamu hawawezi kamwe kumfurahia kiongozi wa Kiislamu.

Kiongozi wa Kiislamu hana budi kukumbuka kuwa anafanya kazi ile ile ya Mtume (s.a.w.). Arejee historia ajikumbushe maudhi na vitimbi vya kila namna alivyofanyiwa Mtume wa Allah na makafiri wa Makkah na Mayahudi na wanafiki wa Madina. Kisha katika uongozi wake anapokumbana na matatizo ya kutukanwa, kusingiziwa, kuupuzwa n.k. ajiulize: "Je haya yaliyonifikia yanaweza kulinganishwa na yale yaliyomfikia Mtume wa Allah".

Pia kiongozi wa Kiislamu anayejitahidi kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Qur'an na Sunnah, hana budi kukumbuka kuwa malipo ya kazi yake yapo kwa Allah (s.w.) na ndiye pekee anayewajibika kumuogopa na kutaka radhi yake.

**Vyombo vya dola katika Uislamu**

Malengo ya vyombo vya dola *(State machineries)* katika dola ya Kiislamu yanatofautiana na yale ya serikali za

Kitwaghutii. Vyombo kama usalama, polisi, mahakama, magereza n.k., vipo katika dola zote tofauti ni malengo ya kazi na majina. Katika dola ya Kiislamu, jeshi la polisi kwa mfano, kazi yake ni kuamrisha mema na kukataza maovu na vile vile kuwakamata wale wote wanaofanya uhalifu:

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى ٱلْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ

بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۚ وَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ

ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

*Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri na wanaoamrisha mema na wakakataza maovu. Hao ndio watakaotengenekewa " (3:104)*

Magereza hali kadhalika, kazi zake si kuwaadhibu tu wahalifu bali kurekebisha tabia na mienendo yao ili wanapotoka magerezani wawe raia wema na wajute kwa makosa yao ya awali.

Kinyume na Uislamu, vyombo vya dola za Kitwaghutii malengo yake ni kama tulivyokwishaona huko nyuma, ni mabavu na kulinda maslahi ya walio madarakani. Huwaonea raia badala ya kuwasaidia, aidha badala yake kurekebisha mienendo ya wakosefu huwafanya wazame zaidi katika uhalifu, bali vyombo hivyo hufanya ukandamizaji na dhulma kwa raia. Hivyo vyombo vya dola ya Kiislamu malengo yake ni tofauti kabisa na yale ya serikali za Kitwaghuuti.

**Demokrasia katika Dola ya Kiislamu**

Pamoja na kuwepo uhuru kamili wa kuchagua viongozi kushiriki katika maamuzi ya kisiasa, kushiriki katika

kuamrisha mema na kukataza maovu ili kuhakikisha kuwepo kwa amani na utulivu, dola ya Kiislamu si ya kidemokrasia kwa mtazamo wa kitwaghuti. Maana ya serikali ya kidemokrasia kwa mtazamo wa kitwaghutii ni “Serikali ya watu inayoongozwa na watu kwa manufaa ya watu.”

Hivyo, watu kwa mtazamo wa kitwaghuti, ndio wenye kauli au mamlaka ya mwisho. Katika Uislamu mamlaka yote ni ya Allah (s.w) pekee. Viongozi na watu wote wanatakiwa wajisalimishe chini ya sheria na amri za Allah (s.w). Katika dola ya Kiislamu hapana sera ya “wengi wape” hata kama ni kinyume na haki.

Katika Uislamu “haki” itabakia haki hata kama imefuatwa na mtu mmoja au watu wachache (minority) na “dhuluma” au “batili” itabakia kuwa hivyo hata kama imesimamiwa au imeungwa mkono na watu wengi (majority).

**Tafauti ya Serikali ya Kiislamu na ile ya kidemokrasia**

| Serikali ya Kiislamu | Serikali ya kidemokrasia |
|---|---|
| 1. Watu wote wako chini ya Ufalme au utawala wa Allah (s.w.) na kila mtu ameku sudiwa awe Khalifa, wa Allah (s.w.) katika kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni. | 1. Ufalme au utawala uko chini ya watu walio wengi *(popular sovereignty).* |
| 2. Itikadi na sheria zinatoka kwa Allah (s.w.) kupitia kwa Mitume wake. Kila Muislamu anawajibika kutii sheria za Allah na kutii maelekezo ya Mtume. Hakuna aliye juu ya sheria wote wanahukumiwa sawa. | 2. Itikadi, sheria na sera hutungwa na Wananchi au wawakilishi wao katika bunge au kamati za vyama. Na kiongozi wa juu wa nchi (Rais) amepewa madaraka makubwa ya kuwa juu ya sheria. |
| 3.Dola ya Kiislamu iko kwa madhumuni ya kusimamisha ufalme wa Allah na kutafuta radhi yake. | 3. Madhumuni ya serikali ni kutosheleza mahitaji na matashi ya raia "walio wengi". |
| 4. Kwa ujumla Dola ya Kiislamu iko chini ya mamlaka ya Allah (s.w.) na Mtume wake, na huendesha mambo yake kwa kuchunga barabara mipaka ya Allah (s.w.) na Mtume wake. | 4. Dola ya kidemokrasia ina mamlaka ya mwisho na uhuru wa kuendesha mambo bila ya kuwa na yeyote aliye juu yake. |

**Serikali ya Kiislamu ni ya Ki-khalifa**

Umma wote wa Kislamu unashika nafasi ya ukhalifa wa Allah (s.w). Yaani umma wote wa Kiislamu unamwakilisha Allah (s.w) katika kusimamisha ufalme wake hapa ulimwenguni kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّـٰلِحَـٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن
قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ
بِى شَيْـًٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَـٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَـٰسِقُونَ

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia dini yao aliyowapendelea, na atawabadilishia amani baada ya khofu yao. Wawe wananiabudu, hawanishirikishi na chochote. Na watakaokufuru baada ya hayo; basi hao ndio wavunjao amri zenu. (24:55)*

Hivyo, kila mmoja anayo haki na anayo mamlaka ya kuiongoza jamii chini ya ufalme wa Allah (s.w). Kiongozi wa nchi, japo amechaguliwa na watu hana mamlaka ya kujiamulia mwenyewe mambo ya jamii. Bali uamuzi wa mwisho utapitishwa na Majlis Shura (Bunge) yenye wajumbe waliochaguliwa na watu kutokana na watu wacha-Mungu, ili wawakilishe mawazo yao kwa niaba yao.

Kushauriana katika kuongoza jamii kunasisitizwa katika Qur-an kuwa ni miongoni mwa matendo mema ya jamii yatakayo iwezesha kufaulu:

وَٱلَّذِينَ ٱسۡتَجَابُواْ لِرَبِّهِمۡ وَأَقَامُواْ ٱلصَّلَوٰةَ وَأَمۡرُهُمۡ

شُورَىٰ بَيۡنَهُمۡ وَمِمَّا رَزَقۡنَٰهُمۡ يُنفِقُونَ ﴿٣٨﴾

*Na wale waliomuitikia Mola wao (kwa kila amri zake) na wakasimamisha swala na wanashauriana katika mambo yao na wanatoa katika yale tuliyowaruzuku. (42:38).*

Pia Mtume (s.a.w) (na kwa hiyo viongozi wote) anaamrishwa na Mola wake:

وَشَاوِرۡهُمۡ فِي ٱلۡأَمۡرِۖ فَإِذَا عَزَمۡتَ فَتَوَكَّلۡ عَلَى ٱللَّهِۚ

إِنَّ ٱللَّهَ يُحِبُّ ٱلۡمُتَوَكِّلِينَ ﴿١٥٩﴾

*"... Na ushauriane nao katika mambo. Na ufungapo nia mtegemee Mwenyezi Mungu (kisha ufanye hilo ulilo azimia bila kurudia nyuma). Hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wamtegemeao." (3:159)*

Baada ya Waislamu kuamua jambo katika Shura yao, ambalo liko katika mipaka ya Allah (s.w) na Mtume wake, hawana budi kutegemeza mafanikio yake kwa Allah (s.w) na kuanza kulitekeleza kwa umoja pasi na kurudi nyuma. Kiogozi wa Dola na viongozi wengine walio chini yake, kazi yao itakuwa kusimamia utekelezaji, wao wenyewe wakiwa mfano bora, katika kutekeleza yale yaliyoamuliwa na Majlis Shura. Endapo kiongozi atafanya kinyume na maamuzi ya Shura, Umma unayo haki ya kumkatalia. Tujikumbushe tena maneno ya Abu bakar (r.a) katika khutuba yake ya kwanza baada ya kuchaguliwa kuwa Amir wa Waislamu:

*"Bila shaka mmeshanichagua kuwa Amir wenu japokuwa mimi si mbora kuliko nyinyi. Nisaidieni nikiwa katika njia ya sawa na nikosoeni nitakapokuwa nina kwenda vibaya".*

Katika Dola ya kikhalifa viongozi na wanaoongozwa wote wana nafasi sawa ya ukhalifa. Hivyo wananchi pamoja na kuwa na uhuru wa kutoa mawazo yao pia wana uhuru kamili wa kuwakosoa viongozi wao na kudai haki zao kutoka hata kwa Amir mkuu (Rais) wa nchi. Mfano mzuri wa uhuru wa kukosoa viongozi tumeupata katika uongozi wa Umar bin Khattab (r.a). Umar hakufurahishwa na tabia ya wanawake iliyozuka ya kudai mahari kiasi kikubwa sana. Hivyo akaamua kuikomesha tabia hiyo. Akasimama katika mimbari msikitini na kuamuru kuwa kuanzia wakati ule mahari isivuke dirhamu 400. Na mwanamke atakaye dai mahari yaliyozidi kiasi hicho, ziada yote itachukuliwa na kutiwa katika Baitul Maali (hazina ya dola ya Kiislamu). Papo hapo akasimama mwanamke mmoja akasema:

*"Yaa Umar! Laisa laka ahalika". Yaani "Ewe Umar! Huna mamlaka ya hilo". Akamkumbusha aya ya Qur-an:*

وَإِنْ أَرَدتُّمُ ٱسْتِبْدَالَ زَوْجٍ مَّكَانَ زَوْجٍ وَءَاتَيْتُمْ إِحْدَىٰهُنَّ قِنطَارًا فَلَا تَأْخُذُوا۟ مِنْهُ شَيْـًٔا ۚ أَتَأْخُذُونَهُۥ بُهْتَٰنًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿٢٠﴾

*Na kama mkitaka kubadilisha mke mahali pa mke, (yaani: kumwoa mke mwingine na kumwacha wa zamani) na hali mmoja wao (naye ndiye huyo atayeachwa) mmempa mrundi (tani) wa mali, basi msichukue chochote. Je, mtachukua kwa dhulma na kwa hatia iliyo wazi? (4:20)*

Aya hii inawakataza wanaume kudai mahari wanapowaacha wake zao hata kama waliwapa mali nyingi. Qintara Maana yake ni tani. Hivyo hata kama mtu ametoa mahari tani za dhahabu. Yule mwanamke akamuuliza Umar: "Kwa msingi gani wewe unataka kuwanyang'anya wanawake haki waliyopewa na Allah (s.w)? Kwa kumjibu, Umar alisema kwa unyenyekevu: "Mwanamke yu sahihi na Umar amekosea". Na akaifuta kauli yake. Je, kuna uhuru wa kukosoa viongozi uliopita huu?

**Usimamishaji Haki katika Dola ya Kiislamu**

Lengo la dola ya Kiislamu sio kutawala bali ni kuhuisha, kudumisha na kuendeleza maadili mema ambayo Allah (s.w) amemtaka mwanaadamu ajipambe kwayo; na kuzuia na kukomesha maovu ambayo Allah (s.w) amemuamrisha mwanaadamu ajitenge nayo. Yaani lengo la Dola ya Kiislamu ni kuhuisha, kudumisha na kuendeleza maadili mema ambayo huwapelekea watu katika jamii kuishi kwa furaha na amani. Na papo hapo dola ya kiilsmau iko pale kuzuia na kukomesha maovu ambayo huleta vurugu, mashaka na huzuni katika jamii. Furaha na amani inapatikana katika jamii iwapo haki inasimamishwa na udhalimu unatokomezwa. Lengo hili linaelezwa vyema katika aya ifuatayo:

ٱلَّذِينَ إِن مَّكَّنَّـٰهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ أَقَامُوا۟ ٱلصَّلَوٰةَ وَءَاتَوُا۟ ٱلزَّكَوٰةَ وَأَمَرُوا۟ بِٱلْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا۟ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۗ وَلِلَّهِ عَـٰقِبَةُ ٱلْأُمُورِ ﴿٤١﴾

*Wale ambao tukiwamakinisha (tukiwapa madaraka) katika ardhi hisimamisha swala na wakatoa Zakat na wakaamrisha yaliyo mema na wakakataza yaliyo mabaya, na marejeo ya mambo ni kwa Mwenyezi Mungu. (22:41).*

Uislamu ni Dini ya Haki na Serikali yake iko pale kusimamisha haki kama tunavyojifunza katika Qur-an:

هُوَ ٱلَّذِىٓ أَرْسَلَ رَسُولَهُۥ بِٱلْهُدَىٰ وَدِينِ ٱلْحَقِّ لِيُظْهِرَهُۥ عَلَى ٱلدِّينِ كُلِّهِۦ وَلَوْ كَرِهَ ٱلْمُشْرِكُونَ ﴿٩﴾

*Yeye (Allah (s.w) ndiye aliyemtuma Mtume wake kwa uongofu na kwa Dini ya Haki ili kuifanya ishinde dini zote ijapokuwa washirikina watachukia. (61:9)*

Uislamu ni Dini ya Haki kwa kuwa ni utaratibu wa maisha uliowekwa na Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mitume wake. Pia ni dini inayo simamia haki za binaadamu.Hawi Muislamu wa kweli yule asiyechunga haki za wengine, kuwausia wengine kusimamisha haki na kuwasaidia wengine kwa hali na mali kupata haki zao. Katika Suratul Asr, Allah (s.w) anatuhakikishia kuwa wanaadamu wako hasarani katika maisha ya duniani na akhera ila wale watakao muamini Allah na vipengele vyote vya nguzo za imani na kufanya matendo mema, na kusimamisha haki na kufanya subira ili kubakia katika haki. Kilicho iwezesha Dola ya Kiislamu wakati wa Mtume (s.a.w) na Makhalifa wane kuwa juu ya dola zote za ulimwenguni ni msimamo wake wa kusimamisha haki katika jamii kwa hali na mali.

Waislamu hawakupigana vita vyovyote ili kuwaingiza kwa nguvu watu katika Uislamu kama wanavyodai maadui wa Uislamu, bali walipigana na makabila na mataifa mbali mbali ili kutokomeza dhulma na unyonyaji wa kila aina ulioshamirishwa na watawala na kusimamisha haki kwa kuwaondoa watawala wanyonyaji na kuwaweka viongozi wa Kiislamu waliokuwa watumwa wa Allah (s.w) pekee na watumishi halisi wa watu walio waongoza. Kiongozi wa watu kuwa na ulinzi mkali au “Body-Guard” ni jambo lisiloelekewa katika mtazamo wa uongozi wa Kiislamu.

Katika dola ya Kiislamu haki za mwanaadamu zimezingatiwa kwa ukamilifu na hakuna mfano wake unaopatikana katika dola yoyote ya kitwaghutii. Dola ya Kiislamu imezigawanya haki za binaadamu katika mbeya tatu:

(a) Haki zinazomstahiki kila mwanaadamu.
(b) Haki zinazowastahiki raia katika dola ya Kiislamu.
(c) Haki zinazowastahiki wasio kuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu.

**(a) Haki zinazomstahiki kila mwanaadamu**

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kusimamia na kuhakikisha kuwa kila mwanaadamu awe Muislamu au asiwe Muislamu, awe raia au mgeni katika dola ya Kiislamu, anapata haki zifuatazo:

**(i)Haki ya Kuishi**

Kila mtu pasina ubaguzi wa aina yoyote ana haki ya kuishi na kulindiwa maisha yake. Kumuua mtu yeyote awaye ni kosa la jinai na muuaji ni lazima ahukumiwe kwa sheria ya Kiislamu. Makemeo ya Qur-an kuhusu kosa hili yanadhihirisha kwa uwazi ubaya wa kuua mtu yoyote pasi na haki:

مِنْ أَجْلِ ذَٰلِكَ كَتَبْنَا عَلَىٰ بَنِيٓ إِسْرَٰٓءِيلَ أَنَّهُۥ مَن قَتَلَ نَفْسًۢا بِغَيْرِ نَفْسٍ أَوْ فَسَادٍ فِى ٱلْأَرْضِ فَكَأَنَّمَا قَتَلَ ٱلنَّاسَ جَمِيعًا

*Kwa sababu ya hayo tukawaandikia wana wa israil ya kwamba atakayemuua mtu bila ya yeye kuua mtu, au bila ya kufanya fisadi katika nchi, basi ni kama amewaua watu wote…” (5:32)*

وَلَا تَقۡتُلُواْ ٱلنَّفۡسَ ٱلَّتِى حَرَّمَ ٱللَّهُ إِلَّا بِٱلۡحَقِّۚ

*"… Wala msimuue mtu ambaye Mwenyezi Mungu ameharamisha (kuuwa) la ikiwa (imetokea) haki (ya kuuawa)…" (6:151)*

Hukumu ya muuaji ni kuuawa kama inavyobainishwa katika Qur-an:

وَلَا تَقۡتُلُواْ ٱلنَّفۡسَ ٱلَّتِى حَرَّمَ ٱللَّهُ إِلَّا بِٱلۡحَقِّۗ وَمَن قُتِلَ مَظۡلُومًا فَقَدۡ جَعَلۡنَا لِوَلِيِّهِۦ سُلۡطَٰنًا فَلَا يُسۡرِف فِّى ٱلۡقَتۡلِۖ إِنَّهُۥ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

*Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu ameiharamisha kuuawa isipokuwa kwa haki (Akahukumu hakimu wa Kiislamu kuwa mtu amestahiki kuuawa na akatoa amri ya kuuawa). Na mwenye kuuawa kwa kudulumiwa, basi tumempa nguvu mrithi wake (juu ya muuaji huyo, akitaka ataomba kwa hakimu kuwa amuue au akitaka amtoze fidia au akitaka amsamehe). (17:33).*

**(ii) Haki ya Usalama wa Maisha**

Kila mtu katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kuokolewa au upate ulinzi utakao muweka katika hali ya usalama bila ubaguzi wa aina yoyote. Tunafahamishwa katika Qur-an kuwa:

وَمَنۡ أَحۡيَاهَا فَكَأَنَّمَآ أَحۡيَا ٱلنَّاسَ جَمِيعًاۚ

*"… Na mwenye kumwacha mtu hai (kumsaidia kuishi) ni kama amewaacha hai watu wote…" (5:32).*

Katika dola ya Kiislamu kila mtu awe mgeni au raia ana haki ya kupata mahitajio muhimu ya maisha yatakayomuwezesha kuishi na kila mtu anayo haki ya kupata hifadhi itakayomuhakikishia kuishi kwa usalama.

**(iii) Kuheshimu Utoharifu (Utakaso) wa Mwanamke**

Dola ya Kiislamu inalojukumu la kuhakikisha kuwa kila mwanamke anapata hifadhi ya kutoguswa na mwanamume yoyote awaye nje ya utaratibu wa ndoa. Kitendo cha zinaa au kishawishi chochote cha zinaa kimekatazwa katika Uislamu bila ya kujali kuwa kimefanywa na Muislamu au na asiye kuwa Muislamu au kimefanywa na raia au mgeni wa Dola ya Kiislamu. Makemeo ya Qur-an juu ya kitendo hiki ni haya yafuatayo:

وَلَا تَقْرَبُوا۟ ٱلزِّنَىٰٓ ۖ إِنَّهُۥ كَانَ فَٰحِشَةً وَسَآءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

*Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni uchafu na ni njia mbaya kabisa. (17:32).*

Uzinifu katika Uislamu ni kosa la jinai, na mzinifu yeyote anastahiki adhabu kali ya kupigwa viboko mia moja (Qur-an, 24:2) au kupondwa mawe mpaka kufa bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

**(iv) Haki ya Heshima**

Uislamu unatuamrisha kuwaheshimu wanaadamu na kuwathamini pasi na ubaguzi wowote na unatukataza kufanya jambo lolote litakalotupelekea kuwavunjia heshima. Tunaamrishwa katika Qur-an kuwa:

وَلَا تَلْمِزُوٓا۟ أَنفُسَكُمْ وَلَا تَنَابَزُوا۟ بِٱلْأَلْقَٰبِ ۖ

*....Wala msitukanane kwa kabila, wala msiitane majina mabaya...(49:11)*

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kuhakikisha kuwa kila mtu anaheshimika bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

### *(v) Haki ya Uhuru*

Ni jukumu la dola ya Kiislamu kuhakikisha kuwa mtu anakuwa huru na hawi mtumwa wa mwingine kimabavu au kifikra. Inasikitisha kuwa maadui wa Uislamu wanaun asibisha Uislamu na biashara ya watumwa. Wameunasibisha Uislamu na utumwa kwa kuwa eti walioonekana kuhusika na biashara hiyo hapa Afrika ya Mashariki ni waarabu. Wengi wa watu wasiokuwa Waislamu na hata baadhi ya Waislamu wasiojua vyema dini yao, wameuelewa Uislamu kuwa ni dini ya Waarabu. Hivyo kwa mtazamo wao huu, kila mwarabu ni Muislamu na kila alichokifanya Mwarabu kiwe kibaya au kizuri ni kitendo cha Kiislamu. Mtazamo huu ni mtazamo potofu. Uislamu ni Dini ya Allah (s.w) isiyo na ubaguzi wa aina yoyote. Uislamu ni dini ya walimwengu wote wa nyakati zote na wamataifa yote. Wote walioikubali dini hii ni ndugu (Qur-an 49:10) na Uislamu hautambui ubaguzi wowote katika mgawanyo wa haki za binaadamu.

Uislamu umekomesha utumwa wa fikra na mawazo, kwa kuwahimiza waumini wake wawe watumwa wa Allah (s.w) peke yake kwa kujinyenyekesha kwake kwa utii na kufuata vilivyo mwongozo wa maisha alio mfunulia mwanaadamu kupitia kwa Mitume wake.

Uislamu umekomesha utumwa uliokuwepo wakati wa ujahili kwa kuwahimiza Waislamu watumie mali zao kuwakomboa watumwa na katika Zakat limewekwa fungu maalumu la kuwagomboa watumwa. Katika historia ya Uislamu tunajifunza kuwa Mtume Muhammad (s.a.w) mwenyewe aliwagomboa watumwa 63 na kuwaachia huru. Mkewe Bi Aysha (r.a) aligomboa watumwa 67, Abbas (r.a) aligomboa watumwa watumwa 70, Abdullah bin Umar (r.a)

aligomboa watumwa 1000, Abdur-Rahman (r.a) aliwagomboa watumwa 30,000 na maswhaba wengine wa Mtume (s.a.w) waliwagomboa watumwa mamia kwa mamia.

Mtume (s.a.w) amekemea vikali kitendo cha kumfanya mtu huru kuwa mtumwa wa mwingine kama tunayojifunza katika Hadith ifuatayo:

> *Kuna watu wa aina tatu ambao mimi mwenyewe nitasimama kuwashitaki katika siku ya hukumu; miongoni mwa hao ni yule anayemfanya mtu huru kuwa mtumwa na kumuuza... (Bukhari, Ibn Majah).*

***(vi) Usalama na Uhuru wa Mtu binafsi***

Uislamu umeweka utaratibu kwamba, hakuna mtu atakayefungwa mpaka kwanza kosa lake lithibitishwe mbele ya mahakama ya wazi (yenye kushuhudiwa na watu). Kesi za faragha au "IN CAMERA" ni haramu katika Uislamu. Pia ni haramu kumkamata mtu kwa kumshuku tu na kumsukumiza jela bila ya kufuata utaratibu wa Mahakama na bila ya kumpa fursa ya kujitetea. Uadilifu katika kutoa hukumu, bila ubaguzi wa aina yoyote, ni jambo lililosisitizwa mno katika Qur-an:

وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ ٱلنَّاسِ أَن تَحْكُمُوا۟ بِٱلْعَدْلِ ۚ

> *"... Na mnapohukumu baina ya watu hukumuni kwa uadilifu..." (4:58)*

Katika Dola ya Kiislamu hakuna mtu atakayetiwa ndani mipaka ahukumiwe kwa uadilifu, wala hapana yeyote asiye na hatia atakaye adhibiwa au kutiwa ndani kwa makosa ya mwingine au kwa niaba ya mwingine.

### *(vii) Haki ya Kuhukumiwa kwa Uadilifu*

Jukumu kubwa la Dola ya Kiislamu ni kusimamia uadilifu. Kila mtu bila ya kujali dini yake, rangi yake, taifa lake, uraia wake, n.k. anastahiki kuhukumiwa kwa uadilifu. Uadilifu katika kutoa hukumu unasisitizwa mno katika Uislamu kama tunavyojifunza katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُونُواْ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلۡقِسۡطِۖ
وَلَا يَجۡرِمَنَّكُمۡ شَنَـَٔانُ قَوۡمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا تَعۡدِلُواْۚ ٱعۡدِلُواْ هُوَ
أَقۡرَبُ لِلتَّقۡوَىٰۖ

*Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi (wa haki) kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, muwe mkitoa shahada kwa uadilifu. Wala kuchukiana na watu kusikupelekeeni kutowafanyia uadilifu…" (5:8).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ كُونُواْ قَوَّٰمِينَ بِٱلۡقِسۡطِ شُهَدَآءَ
لِلَّهِ وَلَوۡ عَلَىٰٓ أَنفُسِكُمۡ أَوِ ٱلۡوَٰلِدَيۡنِ وَٱلۡأَقۡرَبِينَۚ إِن يَكُنۡ
غَنِيًّا أَوۡ فَقِيرٗا فَٱللَّهُ أَوۡلَىٰ بِهِمَاۖ فَلَا تَتَّبِعُواْ ٱلۡهَوَىٰٓ أَن
تَعۡدِلُواْۚ وَإِن تَلۡوُۥٓاْ أَوۡ تُعۡرِضُواْ فَإِنَّ ٱللَّهَ كَانَ بِمَا
تَعۡمَلُونَ خَبِيرٗا ١٣٥

*Enyi mlioamini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au maskini. Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi. Basi msifuate matamanio mkaacha*

*kufanya uadilifu. Na kama mkipotoa (ushahidi) au mkijitenga (na kushuhudia, Mwenyezi Mungu atakuadhibuni), na Mwenyezi Mungu anazohabari za yale mnayoyatenda. (4:135).*

***(viii)Haki ya Usawa wa Binaadamu***

Uislamu hauruhusu ubaguzi wa kabila, taifa, rangi, hadhi, kipato, ubaguzi wa aina yoyote ile. Tunafahamishwa katika Qur-an:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ إِنَّا خَلَقۡنَٰكُم مِّن ذَكَرٖ وَأُنثَىٰ وَجَعَلۡنَٰكُمۡ
شُعُوبٗا وَقَبَآئِلَ لِتَعَارَفُوٓاْۚ إِنَّ أَكۡرَمَكُمۡ عِندَ ٱللَّهِ أَتۡقَىٰكُمۡۚ إِنَّ
ٱللَّهَ عَلِيمٌ خَبِيرٞ ١٣

*Enyi watu! Kwa hakika tumekuumbeni (nyote) kwa (yule) mwanamume (mmoja – Adam) na (yule yule) mwanamke (mmoja Hawa). Na tumekufanyeni mataifa na makabila (mbali mbali) ili mjuane (tu basi). Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule amchaye Mungu zaidi katika nyinyi. Kwa yakini Mwenyezi Mungu ni Mjuzi Mwenye habari zote. (49:13)*

Mtu hawi bora kwa kuwa ni tajiri, au kuwa na hadhi kubwa katika jamii, au kwa kuwa anatokana na taifa kubwa, bali aliye bora ziadi kuliko wote ni yule mcha-Mungu mwenye tabia njema na utu kwa wanaadamu wenziwe. Mtume (s.a.w) katika kusisitiza kwake usawa wa binaadamu amesema:

*Hapana Mwarabu aliye bora zaidi kuliko asiye Mwarabu, wala asiye Mwarabu si bora zaidi kuliko Mwarabu. Pia mtu mweupe si bora kuliko mweusi, wala mtu mweusi si bora kuliko mweupe.Wote ni watoto wa Adam na adam ameumbwa kutokana na udongo (wa mfinyanzi). (Baihaqi na Bazzaaz).*

***(ix) Haki ya uhuru wa mahusiano***

Katika dola ya Kiislamu kila mtu anayo haki ya kujiunga na jumuia, chama au kikundi chochote katika kuhuisha na kuendeleza mema kwa manufaa yake na manufaa ya jamii kwa ujumla. Pia kila mmoja anayo haki ya kutojiunga au kujitoa kwenye jumuiya au chama au kikundi chochote pindi atakapoona kuwa chama hicho au jumuiya hiyo haina manufaa na wala hainufaishi umma bali huleta fitina na uadui katika jamii. Mwongozo wa kushirikiana na kushikamana umewekwa wazi katika Qur-an:

وَتَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْبِرِّ وَٱلتَّقْوَىٰ ۖ وَلَا تَعَاوَنُوا۟ عَلَى ٱلْإِثْمِ
وَٱلْعُدْوَٰنِ ۚ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۖ إِنَّ ٱللَّهَ شَدِيدُ ٱلْعِقَابِ ﴿٢﴾

*Saidianeni katika wema na ucha-Mungu wala msisaidiane katika Dhambi na uadui. Na Mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu. (5:2).*

**(b) Haki za Raia Katika dola ya Kiislamu**

Pamoja na haki za binaadamu wote kwa ujumla zinazotolewa na kusimamiwa na dola ya Kiislamu, kuna zile haki zinazo wahusu raia tu wa Dola wakiwemo Waislamu na wasiokuwa Waislamu. Hapa tutarejea haki za Msingi zifuatazo:

**(i) Haki ya Kuendesha maisha ya Binafsi**

Uislamu unatoa haki kwa kila raia kuwa asiingiliwe katika maisha yake binafsi maadam haendi kinyume na utaratibu wa kibinaadamu. Tunaamrishwa katika Qur-an kuwa:

وَلَا تَجَسَّسُوا۟

*"... Wala msipeleleze (habari za watu)..." (49:12).*

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ لَا تَدۡخُلُواْ بُيُوتًا غَيۡرَ بُيُوتِكُمۡ حَتَّىٰ تَسۡتَأۡنِسُواْ وَتُسَلِّمُواْ عَلَىٰٓ أَهۡلِهَاۚ ذَٰلِكُمۡ خَيۡرٞ لَّكُمۡ لَعَلَّكُمۡ تَذَكَّرُونَ ﴿٢٧﴾

*Enyi mlioamini! Msiingie nyumba ambazo si nyumba zenu mpaka muombe ruhusa (mpige hodi) na muwatolee Salaam waliomo humo.Hayo ni bora kwenu huenda mtakumbuka(24:27)*

فَإِن لَّمۡ تَجِدُواْ فِيهَآ أَحَدٗا فَلَا تَدۡخُلُوهَا حَتَّىٰ يُؤۡذَنَ لَكُمۡۖ وَإِن قِيلَ لَكُمُ ٱرۡجِعُواْ فَٱرۡجِعُواْۖ هُوَ أَزۡكَىٰ لَكُمۡۚ وَٱللَّهُ بِمَا تَعۡمَلُونَ عَلِيمٞ ﴿٢٨﴾

*Na kama hamtamkuta humo yoyote, basi msiingie mpaka mruhusiwe. Na mkimbiwa "Rudini" basi rudini, hili ni takaso kwenu. Na Mwenyezi Mungu anajua mnayotenda? (24:28).*

Mtume (s.a.w) amekemea vikali kuchungulia nyumba za watu kiasi cha kusema: Kama mtu atampofua macho au jicho mwenye kuchungulia nyumbani kwake, hatalaumiwa wala hatakuwa na hatia". Mtume (s.a.w) pia amekataza kusoma barua za watu.Hii ndiyo hifadhi ya maisha ya mtu binafsi inayotolewa na Uislamu. Hifadhi hii haipo katika dola za Kitwaaghuti. Ni mara ngapi twaona barua zikisomwa na kuchukuliwa kopi (photocopy) kwa kisingizio cha usalama wa taifa? Vile vile katika dola za Kitwaaghuti, simu hutegwa katika nyumba za watu ili mazungumzo yao ya siri yajulikane. Kila dola ya kitwaghuti ina askari wa siri wengi ambao kazi zao ni kupeleleza habari za watu.

### (ii) Haki ya Kupinga Udhalimu

Dola ya Kiislamu inatoa haki kwa raia wake kupinga, kuonya au kukemea kitendo cha udhalimu kitakachofanywa na dola au viongozi wake. Kila raia katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kukosoa serikali au kiongozi wa juu wa seriakli. Umar (r.a) akiwa Amir (Rais) wa dola kubwa ya Kiislamu alikosolewa hadharani na mwanamke alipotaka kuwadhulumu wanawake haki yao waliyopewa na Allah (s.w) ya kupanga kiasi cha mahari wanachokiridhia wao wenyewe. Pale pale mbele ya hadhara ya watu Umar (r.a) alikiri kuwa amekosa na akafuta amri yake.

### (iii) Haki ya Uhuru wa Kutoa Maoni na Kuamrisha Mema

Uislamu unatoa uhuru kamili kwa kila raia kutoa maoni yake yanayopelekea kwenye wema. Bali maoni ya kupelekea kwenye maovu, vurugu, fitina na uhasama katika jamii hayapewi nafasi katika Uislamu. Vile vile matumizi ya lugha mbaya ya matusi, dharau na kejeli katika kutoa maoni si jambo linalokubalika katika Uislamu.

Pamoja na kuwa kutoa maoni au mapendekezo katika serikali yanayopelekea kwenye wema ni haki ya kila raia, waumini wanawajibika kuamrisha mema na kukataza maovu katika jamii kama tunavojifunza katika aya zifuatazo:

وَلْتَكُن مِّنكُمْ أُمَّةٌ يَدْعُونَ إِلَى ٱلْخَيْرِ وَيَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ ۚ وَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٤﴾

*Na wawepo katika nyinyi watu wanaolingania kheri na wanaoamrisha mema na kukataza maovu. Na hao ndio watakaotengenekewa. (3:104).*

وَٱلْمُؤْمِنُونَ وَٱلْمُؤْمِنَٰتُ بَعْضُهُمْ أَوْلِيَآءُ بَعْضٍۢ ۚ
يَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ

*Na wanaoamini wanaume na wanaoamini wanawake ni marafiki wao kwa wao. Huyaamrisha yaliyo mema na huyakataza yaliyo mabaya…. (9:71).*

Kwa kulinganisha tabia hii ya waumini na ile ya wanafiki Qur-an inatufahamisha:

ٱلْمُنَٰفِقُونَ وَٱلْمُنَٰفِقَٰتُ بَعْضُهُم مِّنۢ بَعْضٍۢ ۚ يَأْمُرُونَ
بِٱلْمُنكَرِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمَعْرُوفِ

*Wanaume wanafiki na wanawake wanafiki, wote ni hali moja, huamrisha yaliyo mabaya na huyakataza yaliyo mazuri… (9:67).*

Katika kusisitiza wajibu wa Waislamu katika kuamrisha mema na kukataza maovu Mtume (s.a.w) amesema:

*"Miongoni mwenu atakayeona ovu hana budi kuliondoa kwa mkono wake (kutumia nguvu) iwapo anauwezo, kama hana uwezo wa) kuliondoa kwa mkono wake hana budi kuliondoa kwa ulimi wake (kulikemea); kama hana uwezo huo basi achukie na akilaani kitendo hicho kiovu moyoni mwake. Hali hii ya kuchukia ni kiwango cha chini kabisa cha imani." (Sahihi Muslim)*

**(iv) Haki ya Uhuru wa Kufuata Dini Yoyote**

Dola ya Kiislamu inatoa uhuru kamili kwa raia wake kutumia akili zao na vipaji vyao katika kuchagua dini

wanayoiona kuwa ndiyo inayostahiki kufuatwa. Uislamu umekataza watu kushuruitishwa kuingia katika dini kama tunavyojifunza katika Qur-an:

لَآ إِكۡرَاهَ فِي ٱلدِّينِۖ قَد تَّبَيَّنَ ٱلرُّشۡدُ مِنَ ٱلۡغَيِّۚ فَمَن
يَكۡفُرۡ بِٱلطَّٰغُوتِ وَيُؤۡمِنۢ بِٱللَّهِ فَقَدِ ٱسۡتَمۡسَكَ بِٱلۡعُرۡوَةِ
ٱلۡوُثۡقَىٰ لَا ٱنفِصَامَ لَهَاۗ

*Hakuna kulazimishwa (mtu kuingia) katika dini. Uongofu umekwisha pambanuka na upotofu. Basi anayemkufuru twaghuti na kumwamini Mwenyezi Mungu, bila shaka yeye ameshika kishiko chenye nguvu kisichovunjika... (2:256).*

Waislamu hawaruhusiwi kutumia nguvu yoyote katika kuwaingiza watu katika dini bali wameariwa kuwalingania watu kwenye Dini ya Allah kwa mawaidha mazuri yanayofanana na vitendo vyao na kwa hekima kama tunavyojifunza katika Qur-an:

ٱدۡعُ إِلَىٰ سَبِيلِ رَبِّكَ بِٱلۡحِكۡمَةِ وَٱلۡمَوۡعِظَةِ ٱلۡحَسَنَةِۖ
وَجَٰدِلۡهُم بِٱلَّتِي هِيَ أَحۡسَنُۚ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ أَعۡلَمُ بِمَن
ضَلَّ عَن سَبِيلِهِۦۖ وَهُوَ أَعۡلَمُ بِٱلۡمُهۡتَدِينَ ١٢٥

*Wete (waite watu) katika njia ya Mola wako kwa hikima na mauidha mema, na ujadiliane nao kwa namna iliyo bora (siyo kwa kuwatukana wao au kutukana dini yao. Kwa njia hii huwezi kumvuta mtu) Hakika Mola wako ndiye anayemjua aliyepotea katika njia yake. Naye ndiye anayewajua walioongoka. (16:125)*

**(v) Haki ya Kuabudu**

Pamoja na haki ya kufuata dini mtu anayoitaka, Uislamu vile vile umetoa uhuru kamili kwa mtu kufanya Ibada ya dini yake apendavyo. Dola ya Kiislamu inajukumu la kuhakikisha kuwa haki hii inapatikana kwa raia zake na inawajibu wa kuhakikisha kuwa Ibada na mahali pa kuabudia panaheshimiwa. Tunaonywa katika Qur-an kuwa:

وَلَا تَسُبُّوا۟ ٱلَّذِينَ يَدْعُونَ مِن دُونِ ٱللَّهِ فَيَسُبُّوا۟ ٱللَّهَ
عَدْوًۢا بِغَيْرِ عِلْمٍۢ ۗ كَذَٰلِكَ زَيَّنَّا لِكُلِّ أُمَّةٍ عَمَلَهُمْ ثُمَّ إِلَىٰ
رَبِّهِم مَّرْجِعُهُمْ فَيُنَبِّئُهُم بِمَا كَانُوا۟ يَعْمَلُونَ ﴿١٠٨﴾

*Wala msiwatukane wale wanaowaabudu kinyume cha Mwenyezi Mungu, wasije wakamtukana Mwenyezi Mungu kwa jeuri zao bila kujua. Namna hivyo tumewapambia kila watu vitendo vyao. Kisha marejeo yatakuwa kwa Mola wao. Naye atawambia (yote) waliyokuwa wakiyatenda. (6:108).*

Ifahamike wazi kuwa Uislamu haumkatazi mtu kuwa na majadiliano juu ya mambo ya dini bali umesisitiza kuwa majadiliano hayo yaendeshwe kwa utaratibu mzuri bila ya kuwa na matukano, kuzozana na vurugu nyinginezo. Mabishano na mizozano imekatazwa katika Uislamu kama tuanvyokumbushwa katika aya ifuatayo:

وَلَا تُجَـٰدِلُوٓا۟ أَهْلَ ٱلْكِتَـٰبِ إِلَّا بِٱلَّتِى هِىَ أَحْسَنُ إِلَّا ٱلَّذِينَ
ظَلَمُوا۟ مِنْهُمْ ۖ وَقُولُوٓا۟ ءَامَنَّا بِٱلَّذِىٓ أُنزِلَ إِلَيْنَا وَأُنزِلَ
إِلَيْكُمْ وَإِلَـٰهُنَا وَإِلَـٰهُكُمْ وَٰحِدٌ وَنَحْنُ لَهُۥ مُسْلِمُونَ

*Wala msibishane na watu waliopewa Kitabu (kabla yenu) ila kwa yale (majadiliano) yaliyomazuri, isipokuwa wale waliodhulumu miongoni mwao. Na semeni: "Tunaamini yaliyoteremshwa kwetu na yaliyoteremshwa kwenu, na Mu ngu wetu na Mungu wenu ni mmoja, nasi ni wenye kunyenyekea kwake." (29:46).*

Amri hii haishii tu kwa watu wa Kitabu (wakristo na Mayahudi) bali ni pamoja na wanaofuata dini nyinginezo.

**(vi) Haki ya Kuwashitaki Viongozi wa Juu wa Dola**

Katika Dola ya Kiislamu, Wafanyakazi wote wa serikali, akiwa kiongozi wa Dola au mfanyakazi wa kawaida, wote ni sawa mbele ya Sheria. Hakuna yeyote aliye juu ya sheria au asiyeguswa na sheria ya Dola. Raia yeyote katika dola ya Kiislamu anayo haki ya kutoa madai yake au mashitaka yake dhidi ya kiongozi yeyote, hata akiwa Rais wa nchi. Tunao mfano mzuri wa kuiga kwa Mtume wa Allah (s.w) kama tunavyojifunza katika Hadith ifuatayo:

*Umar (r.a) amesema: Kwa macho yangu nilimuona Mtume (s.a.w) akijilipizia kisasi dhidi yake mwenyewe. Katika vita vya Badr wakati Mtume (s.a.w) alipokuwa akinyoosha mistari ya jeshi la Waislamu alilipiga tumbo la askari mmoja, kwa bahati mbaya, katika kujaribu kumrudisha nyuma katika mstari. Yule askari akalalamika: "Ewe Mtume! Umeniumiza na fimbo yako". Mtume (s.a.w) pale pale alifunua wazi tumbo lake, akasema: "Samahani sana, unaweza kulipiza kisasi kwa kunifanyia kitendo hicho hicho nilichokufanyia'. Yule askari alitoka mbele na kulibusu tumbo la Mtume (s.a.w) na kusema: "Hicho ndicho nilichokitaka",*

Mfano mwingine tunaupata katika uongozi wa Umar (la), khalifa wa pili wa Mtume (s.a.w). Wakati wa uongozi wa Umar, Muhammad mtoto wa Amr bin al-'As, Gavana

wa Misri alimchapa (kwa maonevu) Mmisri mmoja. Yule Mmisri alifunga safari kwenda Madina kutoa malalamiko (mashtaka) yake kwa Khalifa Umar. Umar aliyapokea mashtaka na kumwita yule Gavana na mtoto wake waende Madina. Walipofika Madina, Khalifa alimpa mjeledi yule mlalamikaji wa Kimisri na akamwambia amtandike yule mtoto wa Gavana mbele yake. Baada ya kulipiza kisasi yule Mmisri alipotaka kurudisha ule mjeledi, Umar alimuamuru "Mtandike Gavana naye kiboko kimoja, kwani mtoto wake asingali kupiga kama si kiburi alichokuwa nacho kutokana na hadhi ya baba yake". Mlalamikaji alijibu: Mtu aliyenipiga nimelipiza kisasi changu kwake. Umar akasema: "Naapa kwa jina la Allah, kama ungalimtandika ('Gavana) nisingalikuzuia kufanya hivyo, umeacha kwa hiari yako mwenyewe". Kisha Khalifa wa Waumini kwa hasira alimgeukia Gavana, na kumkemea. "Ewe Amr, umeanza lini kuwafanya watu watumwa, japo wamezaliwa na mama zao wakiwa huru?"

### (vii) Haki ya Kuiendesha Dola ya Kiislamu

Wenye haki kushika hatamu ya uongozi wa dola ya Kiislamu si watu wa cheo Fulani, au wa kabila Fulani, au wa chama fulani, bali ni wale wote wanaomuamini Allah (s.w) ipasavyo na wanaoamini Ukhalifa wa mwanaadamu hapa ulimwenguni. Uislamu unatufahamisha kuwa mwanaadamu hapa ulimwenguni ni mwakilishi wa Allah (s.w), hivyo utawala wa Dola ya Kiislamu ni lazima ufuate kwa ukamilifu mwongozo wa Allah (s.w) na umshirikishe kila Muislamu kwa njia ya uwakilishi na kushauriana.

### (c) Haki za Wasiokuwa Waislamu katika Dola ya Kiislamu

Pamoja na kuona haki zinazotolewa na dola ya Kislamu kwa binaadamu wote na kwa raia zake – Waislamu na wasiokjuwa Waislamu kama ilivyobainishwa katika vipengele

(a) na (b) tunawajibika kubainisha kwa uwazi zaidi haki za wasiokuwa Waislamu katika Dola ya Kiislamu.Kuwajibika kwetu huku kunafuatiwa na kueleweka vibaya madhumuni na shabaha ya Dola ya Kiislamu kwa wasiokuwa Waislamu hasa wakristo, na hata kwa baadhi ya Waislamu wasioielewa dini yao vilivyo. Kuna shutuma nyingi dhdidi ya Dola za Kiislamu zinazotolewa na maadui wa Uislamu, hasa wakristo ambazo zinatoa picha kuwa Uislamu ni dini ya ukatili, inayoleta vurugu na fujo katika jamii. Hebu hapa tuangalie, kama mfano tu wa shutuma hizo, sehemu ya barua ndefu ya Rev. Christopher Mtikila aliyomwandikia Makamu Mwenyekiti, Halimashauri Kuu ya Chama, Dodoma (Tanzania) mnamo 1/2/1988. Katika kuonyesha ubaya wa Uislamu Rev. C. Mtikila amesema:

> *"Ubaya sana na hatari kubwa ya siasa ya Islamu kwa wale wanaoifuata kwa kila herufi, ni kule kufika mahali wanapoamua kwamba watu wote ambao si Waislamu (na hasa Wakristo) ni OUTLAWS au "State Criminals", yaani wahaini au viumbe wasiotakiwa kabisa na Mungu wao na huwaita MAKAFIRI na kadiri wanavyoendelea, ndivyo hekima ya kuwawezesha kuishi na kuchukuliana na jamii zingine alizoziumba Mungu inavyozidi kuwatoka. Asiye kubaliana na Islamu ya jinsi hiyo huwa sasa ni adui, na Islamu hiyo imeletesha mauaji ambayo wahusika kwa kuharibikiwa akili zao eti kuyaita JIHAD pamoja na ukatili wa kinyama ulionao katika SHERIA. Hushindwa kutambua kuwa Mungu wao wa mashindano, chuki, wivu, ugomvi, uadui, mauaji, unyama, uzushi, usharati, husuda n.k. ni TOFAUTI KABISA na Mungu wetu wa ukweli, Upendo, furaha, Amani, Utu wema, Uvumilivu, Fadhili, Uaminifu, Upole na Kiasi! Inabidi ndugu zetu (viongozi Waislamu) mzinduke na kutambua kuwa mwapotea kwani: Islamu hiyo ni adui kabisa wa siasa yetu kwa vile humo kuna Ubwana na Utwana, na hata wewe, ndugu Makamu Mwenyekiti, unaitwa KAFIRI kwa vile u mweusi au wa asili ya Kiafrika na siyo ya Kiarabu!"*

Hizi ndizo fikra za Wakristo walio wengi juu ya dola ya Kiislamu.Pamoja na sababu nyingine, fikra hizi zimejitokeza kwa Wakristo na maadui wengi wa Uislamu kutokana na sababu kubwa mbili zifuatazo:

**Kwanza**, kutoufahamu Uislamu na matunda yanayoletwa na Uislamu katika jamii endapo misingi ya Uislamu itafuatwa vilivyo.

**Pili**, husda na chuki iliyopandikizwa kwa Wakristo na viongozi wao ili wauchukie Uislamu ambao endapo wataachwa huru kujifunza wataupenda na uwezekano wa wengi kusilimu. Pia viongozi wa Makanisa wanaogopa kuulizwa maswali na wafuasi wao ambayo wakiyajibu vilivyo watakuwa wanathibitisha kuwa Uislamu ni dini ya haki kutoka kwa Mwenyezi Mungu na Ukristo ni dini iliyozuliwa tu na watu.

Hakuna muumini wa kweli wa Mungu wa haki atakayeufahamu Uislamu vilivyo aache kuwa Muislamu. Kila Wakristo walipopata mwanya wa kuufahamu vizuri Ukristo wao na Uislamu, wameamua kwa moyo mkunjufu kusilimu na kuwa Waislamu wa kweli.

Kuhusu sababu hii ya pili ya kuuchukia Uislamu kwa husda, kwa kuwa Uislamu ni dini ya kweli yenye hoja madhubuti zinazompelekea kuielewa upesi kila mwenye kuitaka, na kwa kuwa Qur-an inabainisha kwa uwazi ni wapi Wakristo na Mayahudi walipoacha njia ya uongofu na kupotea, hatuna msaada wowote wa kuwasaidia ndugu zetu hawa kwani huo ni uamuzi wao wenyewe. Pia, hatustushwi na chuki zao kama zilivyojionyesha katika barua ya Rev. C. Mtikila kwani hayo ndio mategemeo yetu kwao kama Allah (s.w) anavyotutahadharisha katika Qur-an:

يَـٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ لَا تَتَّخِذُوا۟ بِطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لَا
يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُّوا۟ مَا عَنِتُّمْ قَدْ بَدَتِ ٱلْبَغْضَآءُ مِنْ
أَفْوَٰهِهِمْ وَمَا تُخْفِى صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ ۚ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ
ٱلْـَٔايَـٰتِ ۖ إِن كُنتُمْ تَعْقِلُونَ ﴿١١٨﴾

*Enyi mlioamini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasiokuwa katika nyinyi: "hao hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yale yanayokudhuruni. Bughudha (yao juu yenu) inadhihirika katika midomo yao. Na yanayofichwa na vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekubainishieni dalili (zote) ikiwa nyinyi ni watu wa kufahamu.(3:118)*

Endapo fikra hizi mbaya dhidi ya Uislamu na dola ya Kiislamu zimetokea kutokana na kutoufahamu Uislamu vilivyo, tunachukua fursa hii kuwaelimisha Wakristo na wengineo wasio Waislamu na hata Waislamu ambao hawajapata fursa ya kuifahamu dini yao vizuri, kuwa Uislamu ni Dini ya Haki na dola ya Kiislamu lengo lake kuu ni kusimamisha Haki katika jamii kwa kuhakikisha kuwa kila mtu anapata haki yake bila ya kujali dini yake. Ili kuhakikisha hili linafanyika, Uislamu umetoa msisitizo maalumu kuhusu haki za wasio kuwa Waislamu katika dola ya Kiislamu kama ifuatavyo:

**(i) Haki ya Ulinzi wa maisha na Mali**

Damu ya Dhimmi ni takatifu kama ilivyo damu ya Muislamu. Muislamu akimuua dhimmi adhabu yake ni sawa na ile ya kumuua Muislamu. Muislamu mmoja

alimuua dhimmi wakati wa Mtume (s.a.w). Mtume (s.a.w) alimuhukumu kuuawa akasema:

*"Ni jukumu langu kusimamia haki za wanyonge".*

Wakati wa Ukhalifa wa Umar (r.a), Muislamu mmoja alimuua dhimmi. Khalifa aliamuru muuaji akamatwe apelekwe kwa jamaa wa marehemu. Hili lilifanyika na warithi wa marehemu walimuua.

Vile vile mali ya dhimmi katika dola ya Kiislamu ni takatifu kama ilivyo takatifu mali ya Muislamu. Muislamu akiiba mali ya Dhimmi atahukumiwa kukatwa mkono kama kawaida.

Khalifa wa nne wa Mtume (s.a.w) baada ya kumuhukumu Muislamu mmoja kuuawa na warithi wa dhimmi aliyemuua, alisisitiza:

> *Yeyote aliye Dhimmi wetu damu yake ni takatifu kama damu yetu na mali yake ni takatifu kama mali yetu.*

**(ii)Dhimmi na sheria ya jinai**

Katika dola ya Kiislamu hukumu za makosa ya jinai (penal laws) zinawahusu madhimmi sawa na zinavyowahusu Waislamu. Makosa ya jinai ni makosa yanayoathiri jamii nzima na mhalifu atakuwa anaidhulumu jamii nzima. Kwa hiyo dhimmi akiiba atakatwa kiganja chake cha mkono wa kulia, akizini atatandikwa viboko 100 au kupigwa mawe mpaka kufa endapo amewahi kuoa au kuolewa.

Ila dhimmi hataadhibiwa kwa kosa la ulevi kama atakavyoadhibiwa akilewa Muislamu kwa kutandikwa viboko 40.

**(iii) Dhimmi na Sheria za Madai (Civil Laws)**

Katika dola ya Kiislamu hukumu za madai ni sawa kwa Waislamu na wasio kuwa Waislamu. Kila mwenye kudaiwa atahukumiwa na sheria kutoa haki ya mdai bila ya ubaguzi wa dini.

Pia yale yote yaliyoharamishwa kwa Waislamu katika uchumi, pia sheria inayakataza kwa madhimmi. Kwa mfano riba na Kamari ni haramu kwa Waislamu na imekatazwa pia kwa wasiokuwa Waislamu kwani riba na kamari huiathiri jamii nzima.

Bali madhimmi wanaruhusiwa kulewa na kula nguruwe. Pia wana uhuru wa kutengeneza pombe na kufuga nguruwe katika maeneo yao ambamo hawaishi Waislamu. Hawaruhusiwi kufanya hivyo katika maeneo ya Waislamu wala hawaruhusiwi kutengeneza na kuuza pombe, kufuga na na kuuza nguruwe katika sehemu za umma zinazotumiwa na wote.

Muislamu akimuingilia dhimmi katika eneo lake ambapo anaruhusiwa na sheria kutengeneza pombe na kufuga nguruwe, kwa kuiharibu [pombe yake au kuwaua nguruwe wake atawajibika kulipa vitu hivyo mbele ya sheria ya Kiislamu.

**(iv)Haki ya Heshima**

Kumvunjia heshima dhimmi kwa kumtukana, kumuita jina baya, kumdharau, kumuadhiri, kumteta, n.k. ni makosa makubwa sana mbele ya Allah kama ilivyo makosa makubwa kumfanyia Muislamu.

Heshima ni haki inayomstahiki kila mwanaadamu pasi na ubaguzi wa aina yoyote. Ni dhima ya Serikali ya Kiislamu kulinda heshima ya kila mtu.

### (v) Sheria ya Mtu Binafsi (Personal Law)

Katika serikali ya Kiislamu, mambo yote yanayohusu imani ya mtu binafsi huhukumiwa kulingana na imani ya dini yake. Kama jambo lililoharamishwa kwa Waislamu si haramu kulingana na imani ya dhimmi, serikali itaendelea kumruhusu kulitenda jambo hilo. Kwa mfano kuoa bila ya kutoa mahari au kufunga ndoa wakati wa kipindi cha eda ni haramu kwa Waislamu lakini kama katika imani ya dini ya dhimmi haya hayakukatazwa, basi mahakama ya Kiislamu haitamkataza dhimmi huyo kuoa pasi na kutoa mahari au kuoa wakati wa eda. Kwa ufupi, katika yale mambo yanayohusu imani za dini nyingine na ambayo hayaathiri jamii kwa ujumla, kama vile ndoa, talaka na mirathi, sheria ya Kiislamu imetoa haki ya madhimmi kuhukumiwa kulingana na imani za dini zao.

### (vi) Haki ya Kuabudu na Kupewa Heshima Mahali pa Kuabudia

Katika dola ya Kiislamu, madhimmi wana uhuru kamili wa kuabudu kulingana na dini yao inavyowataka. Pia Waislamu wameamrishwa kuheshimu dini za wengine – wasizitukane wala kuonyesha dharau ya aina yoyote – (Qur-an 6:108). Vile vile Waislamu wamekatazwa kujiingiza katika mabishano yasiyo na msingi na watu wa dini nyingine, (Qur-an 29:46).

### (vii) Haki ya Kusamehewa Kushiriki Jihad

Dhimmi katika serikali ya Kiislamu wamesamehewa kupigana vita kwa sababu ulinzi wa serikali dhidi ya maadui zake ni jukumu la Waislamu tu. Inakuwa hivyo kwa sababu ni wale tu wanaokubaliana na itikadi ya dola ya Kiislamu, ndio tu watakaoipigania dola kwa moyo mkunjufu wa kufa na kupona.

Pia ni waumini tu wa Kiislamu watakaoweza kuchunga kwa ukamilifu mipaka ya Uislamu iliyowekwa kuhusiana

na vita vya jihadi. Dhimmi wanalazimika kutoa Jizya (kodi maalum) kama malipo ya ulinzi wanaopewa na Uislamu. Dola ya Kiislamu ikishindwa kutoa ulinzi kwa nchi ya Dhimmi iliyojisalimisha kwa dola ya Kiislamu, nchi hiyo ya Dhimmi haitalazimika kutoa Jizya.

### (viii)Nafasi ya Dhimmi Katika Kuendeleza Dola ya Kiislamu

Kwa kuwa serikali ya Kiislamu inaendeshwa kwa misingi ya itiqadi ya Dini ya Kiislamu, wenye kustahiki kuongoza serikali ni wale tu wenye imani thabiti juu ya itikadi ya Kiislamu.Hawa pekee ndio watakaoweza kuiongoza Dola kwa uadilifu mpaka kufikia lengo lake kuu la kusimamisha haki na kuiwezesha jamii kuishi kwa furaha na amani.

Watu wenye itikadi nyingne wanayo haki kamili ya kuchangia maendeleo ya serikali na wakipenda watashirikishwa katika sekta mbali mbali za kitaalamu na zisizokuwa za kitaalam lakini hawatapewa kazi ya uongozi katika sekta yoyote au katika ngazi yoyote ya uongozi wa dola.

Uongozi ni dhimma ya Waislamu kama tunavyojifunza katika aya ifuatayo:

وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ
لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ ٱلَّذِينَ مِن
قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ
وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا

*Mwenyezi Mungu amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa atawafanya makhalifa katika ardhi kama alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini atawasimamishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya khofu yao… (24:55)*

Waislamu wa vitendo wamepewa haki hii kwa sababu ndio pekee, kutokana na imani yao thabiti juu ya Allah (s.w) na malipo ya Akhera, watakaoweza kusimama kidete kutetea haki za watu na kuhakikisha kuwa jamii inahuisha na kuendeleza mema na inaepukana na maovu. Waislamu hawapewi kazi hii ya uongozi kwa upendeleo, bali wamepewa kazi hii kwa kuwa wanao uwezo wa kuifanya kama Allah (s.w) anavyowatukuza katika Qur-an:

كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَأْمُرُونَ بِٱلْمَعْرُوفِ وَتَنْهَوْنَ عَنِ ٱلْمُنكَرِ وَتُؤْمِنُونَ بِٱللَّهِ ۗ وَلَوْ ءَامَنَ أَهْلُ ٱلْكِتَـٰبِ لَكَانَ خَيْرًا لَّهُم ۚ مِّنْهُمُ ٱلْمُؤْمِنُونَ وَأَكْثَرُهُمُ ٱلْفَـٰسِقُونَ ﴿١١٠﴾

*Nyinyi ndio umma bora kuliko umma zote zilizodhihirishwa watu (ulimwenguni) – mnaamrisha yaliyo mema na mnakataza yaliyo maovu, na mnamwamini Mwenyezi Mungu. Na kama wale waliopewa kitabu wangaliamini ingalikuwa bora kwao… (3:110)*

Waislamu wakiacha kuchukua dhima hii ya uongozi wa jamii na badala yake watu wengine wasiomwamini Allah ipasavyo na malipo ya akhera, wakaichukua kazi

hii ya uongozi wa jamii na kuifanya kwa kufuata matashi yao kinyume na matashi ya Mwenyezi Mungu, jamii itatumbukia katika giza la huzuni na majuto kama ilivyo hivi sasa katika ulimwengu huu wa Kitwaghuti kama tunavyojifunza katika Qur-an:

ٱللَّهُ وَلِيُّ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ يُخْرِجُهُم مِّنَ ٱلظُّلُمَٰتِ إِلَى ٱلنُّورِ ۖ وَٱلَّذِينَ كَفَرُوٓا۟ أَوْلِيَآؤُهُمُ ٱلطَّٰغُوتُ يُخْرِجُونَهُم مِّنَ ٱلنُّورِ إِلَى ٱلظُّلُمَٰتِ ۗ أُو۟لَٰٓئِكَ أَصْحَٰبُ ٱلنَّارِ ۖ هُمْ فِيهَا خَٰلِدُونَ ﴿٢٥٧﴾

*"Mwenyezi Mungu ni mlinzi (kiongozi) wa wale walioamini. Huwatoa katika* ***giza*** *na kuwaingiza katika* ***nuru****. Lakini waliokufuru, walinzi (viongozi) wao ni* ***matwaghuti****. Huwatoa katika* ***nuru*** *na kuwaingiza katika* ***giza****. Hao ndio watu wa motoni humo watakaa milele". (2:257).*

---

Utukufu ni wako (Allah)! Hatuna elimu isipokuwa
ile uliyotufundisha, bila shaka
wewe (Allah) ndiye
Mjuzi na ndiye
Mwenye hikima
(2:32)

## Zoezi la Tano

1. (a) Nini maana ya Siasa
(b) Taja tanzu za mfumo wa siasa za kitwaghuti

2. Linganisha na kutafautisha baina ya mfumo wa Siasa za Kidemocrasia na mfumo wa Siasa wa Kiislamu

3. (a) Eleza maana ya Dola.
(b) Onesha msonge wa utendaji katika dola ya kitwaghuuti

4. Soma kwa makini Qur'an 27:48-49, 8:30,9:40.
(a) Ni chombo kipi kinachohusika na hila hizi katika dola la kitwaghuuti?
(b) Ni mambo gani yanayofanya chombo hiki kufikia malengo yake?

5. Kuna tafauti gani kati ya kazi za bunge,mahamaka, na polisi katika dola ya kitwaghuuti na kazi za vyombo hivyo katika dola ya Kiislamu.

6. Eleza, ni mfumo upi wa Dola, kati ya ule wa kitwaghuti na wa kiislamu ambao ni muhimu, na bora kwa jamii kuufuata

7. Taja na kufafanua misingi ya utii katika maongozi ya dola ya Kiislamu na sababu zake.

8. Bainisha sifa na vigezo vya kumstahikisha mtu kuwa kiongozi wa Kiislamu.

9.Taja, eleza na kuthibisha kwa Qur'an, njia za kumpata mtu atakaye kabidhiwa dhima ya kuwa kiongozi atakaye ongoza Waislamu na jamii katika kutekeleza wajibu na majukumu yao kulingana na lengo halisi la maisha.

9. Bainisha tafauti nne katika ya serikali ya Kiislamu na ile ya Kidemokrasia.

10. (a) Taja aina za raia katika Dola ya Kiislamu

(b) Onesha kwa ushahidi wa Qur'an na Sunnah, haki inazopasa kusimamia serikali ya kiislamu kwa raia zake.